

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIA NO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 26 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Taasisi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2004 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Marine Parks and Reserves Unit for the year ended 30th June, 2004*).

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Kazi za Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo kwa Mwaka 2004/2005 (*The Annual Report on the Activities of the University College of Lands and Architectural Studies for the year 2004/2005*).

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):**

Maoni ya kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha Uliopita pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI  
YA UPINZANI - KWA WIZARA YA USALAMA WA RAIA:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha Uliopita pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara Hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Kabla sijamwita Katibu ili tuingie hatua inayofuata. Kama kawaida tuna wageni hapa. Kwanza, wapo vijana watatu ambao ni watoto wa Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Naibu Waziri wa Usalama wa Raia. Wa kwanza ni Aboud Mohamed, ndiye Mkubwa, wale pale, Aboud yule, halafu yupo Ahmed Mohamed Aboud na Ali Mohamed Aboud. Inasemekana kwamba mmoja wao anaandaliwa kuwa Mwanasiasa. (*Makofi/Kicheko*)

Pia wageni wa Mheshimiwa Martha M. Mlata, ambao ni Madiwani saba (7) kutoka Tarafa za Ndago kule Wilaya ya Iramba, Singida. Madiwani wale pale. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofi*)

Naona Vijana kutoka shule fulani lakini haikutangazwa ni shule ipi, lakini walimu na wanafunzi tunapenda kuwakaribisha sana muone jinsi Bunge lenu linavyofanya kazi ya Demokrasia. Karibuni sana.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 280

**Boma La Utete**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA aliuliza:-**

Kwa kuwa Boma la Utete lina miaka zaidi ya 80; na kwa kuwa Boma hilo limejengwa na Wajerumani lakini sasa limeachwa kabisa kwa miaka mingi bila kufanyiwa ukarabati wa kutosha, limekuwa chafu sana kiasi cha kutia aibu:-

- (a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, kuacha kulifanyia ukarabati unaostahili mara kwa mara ni kuidhalilisha Wizara husika na kuyashushia hadhi Makao Makuu ya Wilaya?
- (b) Je, Serikali itakuwa tayari kuahidi kuanza ukarabati huo mara moja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Boma la Utete lina miaka mingi na lilijengwa wakati wa ukoloni na hivi sasa linahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa.

Hata hivyo Serikali kupitia Bajeti za Mikoa imekuwa ikitenga fedha kidogo kidogo kulingana na uwezo wa fedha uliopo ili Maboma ya Wakuu wa Wilaya nchini yaweze kufanyiwa ukarabati ikiwa ni pamoja na Boma la Utete.

Hivyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua heshima na hadhi ya maboma ya Wakuu wa Wilaya kwamba ndiyo Makao Makuu ya Wilaya na kamwe suala la kudhalilisha Wizara halipo.

Mheshimiwa Spika, tathmni iliyofanywa na Ofisi yangu mwaka 2004 inaonyesha kuwa baadhi ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya ni chakavu na nyingine kutokuwa na thamani za kutosha ikiwa ni pamoja na Boma la Utete. Serikali inatambua umuhimu wa kulifanyia ukarabati boma hilo ili watumishi waweze kufanya kazi katika mazingira yanayofaa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuweka mazingira bora ya utendaji kazi, imeamua kuanza mara moja ukarabati wa Boma la Utete. Kazi hiyo inakadiria kugharimu Serikali jumla ya shilingi milioni 300. Katika Mwaka wa Fedha 2006/2007 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 90 ili kuanza awamu ya kwanza ya ukarabati huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda watumishi wake wote wawe na mazingira mazuri ya kazi, hivyo itaendelea kufanya ukarabati majengo kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Boma la Utete halikujengwa kiholela, limejengwa katika uwanja wa vita vya Maji Maji ambako Kamanda wa Kijerumani aliuawa pale na Majugumbi Mzuzuri-jamii ya Mheshimiwa Dito. Sasa, *it's an Icon of resistance*. Pale ni Waswahili wanatetea heshima ya Mswahili pale. Ninaomba Serikali ilitazame Boma lile kwa heshima; na kwa kuwa imekubali kukarabati. Je, Serikali safari hii itatumia *Contractor* makini? Kwa kawaida huletewa *Contractor briefcase type*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani pengine jambo jema

kwa Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, ilikuwa kuishukuru Serikali kwa uamuzi wake mzuri sana wa kuanza kukarabati Boma.

Mheshimiwa Spika, Boma lile kwa bahati nzuri mimi nimelitembelea mara mbili najua hali yake na nilichochea sana katika kujaribu kufanya uamuzi wa haraka ili kuweza kulibadilisha lifanane na Maboma mengine.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tumedhamiria kufanya marekebisho ya msingi kabisa. Lakini nataka Mheshimiwa ajue kwamba masuala ya wakandarasi bado yatasimamiwa na Mkoa wa Pwani. Kwa hiyo mimi naomba Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia ashirikiane na Mkuu wa Mkoa na timu yake pale waweze kupata mkandarasi mzuri ili aweze kufanya kazi ile vizuri na kwa matarajio ya Watanzania.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Pwani una Wilaya mbazo zimetimiza takriban miaka 100 na bado ziko nyuma kimaendeleo. Je, Serikali ina mpango gani katika kuinua na kwasaidia wananchi wa Wilaya hizo na wao waeze kupata maendeleo ambayo imepita zaidi ya miaka ya uhuru wetu?

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya, halihusiani na ile Ngome ya Utete. Kwa hiyo tunaendelea.

Na. 281

### **Ukosefu wa Waganga na Wauguzi**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Singida katika baadhi ya vijiji wamejitlea kujenga Zahanati kwa kushirikiana na Mfuko wa *TASAF* ili kusogea karibu huduma za matibabu; na kwa kuwa tangu Zahanati hizo zikamilike, bado hazifanyi kazi kwa kukosa Waganga na Wauguzi:-

- (a) Je, Serikali itapeleka lini Waganga na Wauguzi katika Zahanati za vijiji vya Wilaya ya Manyoni vya Mpapa, Mvumi, Chikombo, Hika na Mpandagani?
- (b) Je, kwa Serikali kutokupeleka Waganga katika Zahanati kwa takriban miezi kumi (10) haioni kwamba inadumaza moyo wa kujitolea kwenye miradi ya maendeleo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Wilaya ya Manyoni wakishirikiana na Mfuko wa *TASAF* wamejenga jumla ya Zahanati kumi na nne (14). Kutokana na uhaba wa watumishi waliopo katika Sekta ya Afya haikuwa rahisi kuhamisha watumishi kutoaka Zahanati zilizopo kwenda kufanya kazi katika Zahanati mpya zilizojegwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika mwaka wa fedha 2005/2006 Idara ya Afya Manyoni iliidhinishiwa Ikama ya Watumishi 298. Kati ya nafasi hizo, nafasi za ajira mpya za Waganga ni nne na 13 zilikuwa za Wauguzi. Mwaka 2006/2007 Ikama iliyopitishwa na Idara ya Afya, Waganga 23 na Wauguzi 17. Hivyo nafasi za ajira za Waganga ni 27 na nafasi za Wauguzi ni 30. Hivi sasa, Serikali imeamua kuajiri watumishi katika sekta ya Afya moja kwa moja kwa wale watakaohitimu vyuo na bila kufanya usaili. Hivyo ni matumaini yetu kuwa Zahanati zilizojengwa kwa nguvu za wananchi Wilayni Manyoni katika vijiji vya Mpapa, Mvumi, Chikombo, Hika na Mpandagani vitapata wataalam wanaohitajika. Nashauri Halmashauri ya Manyoni ifuate utaratibu unaotumika wa kupeleka maombi yote haya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili ipatiwe wataalam wanaowahitaji kulingana na Ikama iliyopo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika kipengele (a) Halmashauri ya Manyoni mwaka 2005/2006 iliomba kuidhinishiwa Ikama ya watumishi kwa Zahanati mpya zilizopo ikiwa ni khatua ya kwanza ya kupata vibali vya ajira. Hivyo Serikali haikufanya makusudi kuchelewa kupeleka Waganga katika Zahanati husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu, kwanza niwapongeze wananchi wa Manyoni kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujenga Zahanati hizo, pia niwaombe wananchi hao wasivunjike moyo kushiriki katika shughuli za maendeleo yao pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu uliopo sasa wa ajira kwa Sekta ya Afya kama nilivyosema tatizo hilo naamini litapungua.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa vile afya ya wananchi ni muhimu kwa uhai wao na pia kwa uchumi wa taifa letu, Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuwafundisha Waganga hawa pamoja na Manesi ili kukidhi haja za Zahanati zinazojengwa na wananchi wetu kwa wingi zaidi kwa kufuata Mfumo wa Wizara ya Elimu inavyofundisha walimu wake?

(b) Kwa kuwa tatizo hili limekuwa ni kubwa hasa kwa Mkoa wa Singida, Waganga wengi na Wauguzi hawaendi kwa jinsi ilivyotakiwa. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba iweke Mfumo mpya ili Serikali za Vijiji ziweze kupendekeza majina ya vijana ambao watapelekwa kuchukua mafunzo kwa ajili ya mkataba ili waweze kudumu katika Zahanati hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, natambua wazi kwamba afya ni muhimu kwa taifa letu kiuchumi na kwa kutambua hilo Serikali sasa hivi inaaazma ya kuongeza idadi ya Wauguzi na Waganga katika Vyuo vyake. Kwa hiyo ni mpango mzuri tu ambao unafanywa na Serikali ili kuongeza hiyo idadi kama tulivyofanya kwenye mpango wa MMEM wa kuongeza walimu wengi.

Kuhusu swali lake la pili kwamba Waganga, Wauguzi wanaopangwa katika Hospitali za Singida au Zahanati za Singida, hawaendi huko: Nafikiri kwa utaratibu wa sasa ambapo wanafunzi kutoka Vyuni wale wahitimu kutoka Vyuni wanapangwa moja kwa moja kwenye Wilaya husika bila kufanya usaili, nafikiri huo urasimu ukipungua, hao wafanyakazi wataenda moja kwa moja kwenye vituo vyao bila kupitia sehemu nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lake la kusema kwamba Serikali za vijiji zipendekeze majina ya vijana ambao wanahitimu kidato cha nne au kidato cha sita ili waweze kupelekwa kwenye mafunzo, mimi nafikiri tunachukua wanafunzi kwenda vyuni kulingana na *qualification* zao. Kama wanafunzi hao watakuwa wame-meet vile vigezo ambavyo vimewekwa na Wizara ya Afya, nafikiri Wizara ya Afya haina kipingamizi, mradi hao vijana wawe na *qualification* zinazohitajika. (*Makofi*)

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza Swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TASAF* inajihuisha sana na kuchangia elimu, Zahanati na vitu vingine katika vijiji; na kwa kuwa wananchi wamehimizwa kuchangia sehemu ambayo *TASAF* inachangia; Ningependa tu njue *TASAF* kama mradi katika nchi nzima kwa mwaka huu wa Fedha wana shilingi ngapi, ili wananchi waanze kujipanga *ku-match* hizo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Nadhani kwa kuwa linauliza takwimu za kiasi cha fedha, pengine tungefaidika zaidi kama Mheshimiwa angeliuliza kwa maandishi ili lijibiwe mahsusii.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Zahanati zilizojengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi hukosa Waganga na Wauguzi hivyo kukosa kufanya kazi nalo ni tatizo sugu katika Wilaya ya Namtumbo.

Je, Serikali inawaeleza nini wanachi wa vijiji vya Matepwende, Milonji, Ntonya na vingine vilivyojenga Zahanati na vikakosa Waganga na Wauguzi vya Wilaya ya Namtumbo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ningependa kwanza kuungana na Naibu Waziri kwa kuwashukuru na kuwapongeza wananchi ambao wamejenga Zahanati kwa njia ya kujitolea wakiwemo wa Namtumbo, Manyoni na ningependa kutambua vile vile kwamba Urambo wamejenga Zahanati 15 na Njombe Zahanati 28. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli maswali yanayohusu uhaba wa watenda kazi wa Afya yanajirudia mara kwa mara na nimewahi kusema hapa Bungeni mikakati ambayo tunaipanga ili kujaribu kupunguza kero hiyo na ningeomba wabunge wenzangu wangoje hotuba nitakayotoa hapa siku ya jumatatu. Ahsante. (*Makofî*)

Na. 282

### **Uwindaji wa Wanyama**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi hiki cha ukame tumeshuhudia wanyama wengi wa kila aina hasa wale wanaotegemea nayasi (majani) wakifa kwa wingi kutokana na uhaba wa majani na maji:-

- (a) Je, Serikali kwa kuona hali hiyo ambayo imesababisha upungufu mkubwa wa wanyama, kwa nini isisimamishe uwindaji wa wanyama, kwani wnayama hao tayari wamepungua kwa sehemu kubwa kutokana na ukame?
- (b) Je, Serikali itachukua hatua gani ili kujua wanyamaporil walioathirika na kupungua zaidi ili waondolewe kabisa kwenye mgao wa uwindaji wanaopewa waindaji?

#### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mbunge wa Loliondo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kiwango cha ukame uliotokea mwaka 2006 ni cha kawaida kwa mtazamo wa mwenendo wa mifumo ya Ikolojia (*Ecosystem Dynamics*) na hakiwezi kusababisha kupungua kwa wanyamaporil kiasi cha kusababisha kusimamisha uwindaji.

Mbali na mtizamo huu, uzoefu pia unaonyesha kuwa janga kama hili linapotokea na kuua wanyama wengi, wanayamaporil wana uwezo mkubwa wa kuzaliana na kurejea kwenye viwango vya idadi yao ya awali katika muda mfupi baada ya hali ya kawaida kurejea.

Aidha, kuwepo kwa shughuli za uwindaji katika maeneo ya kuwinda kuna imarisha ulinzi wa maeneo hayo na kupunguza kasi ya ujangili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itafanya tathmini ya madhara yaliyosababishwa na ukame nchini mwaka 2006 ili kubaini kiwango cha athari za ukame huo kwa wanyamaporil. Tathmini hiyo itahusisha sensa zitakazoendeshwa na Taasisi ya Utafiti Tanzania (*TAWIRI*) pamoja na taarifa kutoka kwa Maafisa wa Wanyamaporil wa sehemu mbali mbali nchini.

Aidha, wakati suala la tathmini ya athari ya ukame kwa wanyama linasubiri kufanyika, Wizara yangu kwa sasa imechukua hatua za tahadhari katika kupanga viwango vya kuwinda wanyama (*quota*) katika msimu wa uwindaji wa 2006 ambao ulianza tarehe 1 Julai, 2006. Mgao wa wanyama (*quota*) umepunguzwa kwa kati ya asilimia 10 hadi 50 kwa baadhi ya spishi; Mfano Nyati, Simba na Mbuni wamepunguzwa kwa kiwango cha asilimia 10. wanyama wengine ambao idadi yao ni ndogo kama vioe Choroa (*Oryx*), Swalatwiga na Nzohe wamepunuzwa kwa asilimia 50.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Je, anakubaliana nami kwamba uwindaji huu bila kujua idadi ya

wanayama inawea kusababisha hatari ya aina fulani ya wanyama kumalizika kama Vifaru walivyoisha mpaka Serikali ikaenda kununua Kifaru Afrika Kusini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kwa kuwa wawindaji hawa wanapowinda katika vitalu vyao na hivyo vitalu viko ndani ya vijiji na wanaambiwa wasaidie vijiji vilivyomo ndani ya vitalu vyao, lakini hakuna sheria yoyote inayowabana wasaidie, ni hiari, wakitaka kusaidia, wasaidie, wasipotaka, itakuwa sio lazima. Je, Serikali itaweka Sheria ya kuwabana hawa wawindaji waweze kusaidia vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi, nimeeleza kuwa pamoja na kwamba tathmini hajafanyika na tunategemea kufanya tathmini hiyo mwaka huu, viwango vyao uwindaji tayari vimepunguzwa. Kuna wanayama ambao viwango vyao vimepunguzwa kwa asilimia 10 na hii inategemea uwingi wa wanyama, wale wanyama ambao ni wengi, asilimia imekuwa ni 10, lakini kwa wanyama ambao ni wachache sana, asilimia imepunguzwa kwa kiwango cha 50. Hii kwa vyovyote itadhibiti kutopunguza wanyama kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili: Hawa wenye makampuni ya uwindaji wanapoomba, masharti wanayopewa, mojawapo ni kusaidia vijiji ambavyo viko karibu na maeneo yao ya kuwinda. Wanawasaidia katika miradi yao ya maendeleo. Lakini vile makampuni hayo yanasadid kwa asilimia 25 katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Labda ningweza kutoa mfano; Wilaya ya Longido kwa kuwa ndio tu hivi karibuni imeundwa kuwa Wilaya hapo mwanzo ilikuwa pamoja na Wilaya ya Monduli.

Katika miaka mitano mfululizo, tangu mwaka 2001/2002 mpaka mwaka 2005/2006 Halmashauri ya Wilaya hiyo iliweza kupata jumla ya shilingi 231,942,031/= kutoka katika kampuni hizi za uwindaji. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Michael L. Laizer kwamba makampuni haya kwa kweli yanasadid. (*Makof*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kumipa nafasi niulize swali moja la nyongeza na nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Katika majibu yake ameeleza kwamba kuna baadhi ya wanyama ambao *quota* yao ya uwindaji wa kitaalii imepunguzwa kwa nusu kwa mfano Choroa au Swalatwiga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanyama hawa ni adimu sana, ni wachache sana, kwa mfano, Swalatwiga wanapatikana kwenye Jimbo la Mheshimiwa Michael L. Laizer peke yake Tanzania nzima na wanaelekea kwisha. Kwa nini basi wasiondolewe kabisa katika *quota* badala ya kupunguza nusu? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wako wanyama ambao ni wachache sana na pia wako wanyama ambao wako hatarini kutoweka. Wanyama hawa tusipokuwa waangalifu wanaweza wakatoweka.

Sasa huwa tunachukua tahadhari kubwa, kwa mfano wale wanyama ambao wako hatarini kutoweka huwa kwa kweli hawahuishwi katika biashara hiyo ya uwindaji wa utalii, ila tu wanahuishwa wanapokuwa ni wanyama waharibifu. Hapo tu ndipo watakapokuwa wanauawa. Lakini kwa hawa ambao ni wachache sana tathmini itafanyika, tutaona matokeo ya tathmini hiyo, halafu hatua zinazostahili zitachukuliwa. (*Makofisi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema anasubiri tathmini na tafiti mbalimbali juu ya wanyama ambao wameongezeka au wamepungua ili wasiwindwe, lakini kwa kuwa katika swalii la muuliza swalii amesema kuwa kuna athari za ukame na kwa kuwa katika Wilaya yangu ya Nzega wapo wanyama waharibifu wanaoitwa tembo ambao hutoka Kigoma kupitia Kahama, Urambo hadi Nzega na taarifa nilizonazo sasa hivi wapo wengi kama 200 hivi wanaharibu mazao na mali za binadamu. Je, hao nao wanangoja taarifa kutoka kwa watafiti? Maana inaonekana wameishakuwa wengi na hawaruhusiwi kuwindwa au kuuawa. (*Makofisi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Wizara inayo taarifa ya kwamba Nzega wameingia tembo wengi na wanafanya uharibifu na hatua zimekwishachukuliwa. Mpaka jana tarehe 25 Julai askari wa kutoka Halmashauri ya Wilaya wanaohusika na Kikosi cha Kuzuia Ujangili wamekwenda katika tukio, lakini vile vile Wizara imechukua hatua ya kuagiza kikosi dhidi ya ujangili kutoka Tabora nao watakwenda.

Lakini hali ikiendelea kuwa mbaya tumepanga kwamba Kikosi cha Kuzuia Ujangili cha Muyowosi kipo tayari (*standby*). Ikiwa hali ya tembo hao itaendelea hivyo hivyo, kikosi hicho kitakwenda kusaidia kuweka nguvu ili kuwaua hao tembo waharibifu. (*Makofisi*)

**SPIKA:** Ni bahati njema kwao kwamba tembo hawafuatilii mjadala huu ulioko Bungeni hivi sasa. (*Kicheko*)

Na. 283

### **Tatizo la Malazi katika Kampasi nyingi za Vyuo Vikuu**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** atauliza: -

Kwa kuwa Vyuo Vikuu hapa nchini vina maeneo makubwa yaliyo wazi na kwa kuwa vyuo hivi vinakabiliwa na tatizo kubwa la huduma ya malazi kwa wanafunzi wao jambo linalopelekea wanafunzi wengi kuishi nje ya chuo (*off campus*) kwenye hosteli na wengine kupanga mitaani: -

- (a) Je, Serikali inatambua adha kubwa wanayoipata wanafunzi wa *off campus* hasa waliopanga mitaani, jambo linaloathiri *performance* yao katika masomo?
- (b) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge ni gharama kiasi gani zinazotumiwa na vyuo hivi kupanga nyumba za watu binafsi na hosteli kwa ajili ya wanafunzi kwa mwaka?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hosteli za kutosha kwenye maeneo ya wazi ya vyuo hivi ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, uzoefu wa vyuo vyetu vikuu vitatu vya Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo unaonyesha kuwa, hakuna uhusiano moja kwa moja kati ya kuishi nje ya chuo na utendaji wa masomo wa wanafunzi kimasomo. Mwanafunzi anaweza kukaa nje ya chuo na akafanya vizuri kuliko yule anayekaa kwenye mabweni na hosteli za vyuo. Karibu nusu ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanakaa nje ya chuo na hakujatokea malalamiko yoyote yanayohusiana na utendaji wa wanafunzi hao kimasomo.

(b) Mheshimiwa Spika, vyuo nilivyovitaja awali vimeduwa vikifanya juhudzi za makusudi kuwasaidia wanafunzi wanaoishi nje ya vyuo ili wapate makazi bora yenye hadhi na mazingira mazuri ya kusomea. Mathalan, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilitumia jumla ya Shilingi 258,283,400 kwa mwaka wa masomo 2005/2006 kwa kulipa kodi ya pango kwa wanafunzi waliohitaji huduma hiyo, fedha ambazo hurejeshwa chuoni na wanafunzi. Suala hili linafanywa kwa kuweka saini au mkataba kati ya wanafunzi, chuo, pamoja na wamiliki wa nyumba nje ya chuo. Kipengele kimojawapo katika makubaliano hayo ni kwamba, mwanafunzi akubali kukilipa chuo kodi hiyo ambayo tayari inakuwa imeishalipwa na chuo kwa mmiliki wa nyumba husika na wanatumia pesa yao ya posho wanayokopeshwa au vinginevyo kulipa hiyo fedha.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Mzumbe kiliwapangishia wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa mwaka kwa masomo 2005/2006 kwa *semester* moja tu ya siku 97 na gharama zake zilikuwa ni Shilingi 5,092,500. *Semester* ya pili wanafunzi wote walirudi chuoni.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeingia mkataba na baadhi ya wamiliki wa nyumba binafsi kwa ajili ya makazi ya wanafunzi na kulipa kodi kwa niaba ya wanafunzi wanaokubali

kulipa kodi inayohitajika na mwenye nyumba kwa awamu. Kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wao huwasaidia wanafunzi kwa kuwatafutia sehemu ambayo ni nzuri kwa kupanga. Hata hivyo, wapo wanafunzi wachache ambao hujitafutia nafasi za kuishi nje ya chuo kwa sababu zao binafsi mbalimbali. Kwa mfano, wanafunzi wa kike ambao wamejifungua inabidi wakae nje ya chuo kwani ni lazima wawe na mtu au watu wa kuwasaidia kulea watoto wao wachanga.

(c) Msimamo wa Serikali juu ya ujenzi wa hosteli kama ulivyoainishwa katika Sera ya Elimu ya Juu ni kuweka mazingira mazuri yatakayowawezesha wawekezaji kujihusisha na ujenzi huo. Serikali inawashauri na kuwahimiza wadau mbalimbali wa elimu ambao wako tayari kuwekeza katika kujenga au kuwapatia nyumba za kuishi wanafunzi kama ambavyo *NSSF* imefanya kwa kujenga hosteli za Mabibo kwa wanafunzi wa Chuo kikuu cha Dar es salaam na wao wafanye hivyo. Serikali itakuwa tayari kushirikiana na wadau wanaotaka kuwekeza katika kutoa huduma za malazi au makazi kwa wanafunzi wetu. Pale inapobidi na hali ya kifedha ikiwa nzuri, Serikali itajenga hosteli katika Taasisi husika.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa kila mwaka wanafunzi wanaongezeka vyuoni kutokana na kuboreshwa kwa elimu ya *primary* na *secondary* na kwa kuwa mpango huu wa wanafunzi kukaa *off campus* siyo endelevu kwa sababu unategemea sana mpaka wawekezaji wajenge nyumba ndiyo wanafunzi wetu wapate maeneo ya kukaa, je; Serikali haioni umuhimu sasa wa kulipa suala hili umuhimu wa kutosha ili kuharakisha kuwepo kwa hosteli za kutosha ndani ya *campus* sambamba na kuhamasisha vijana kuweza kuijunga na vyuo?

(b)Kwa kuwa kila mwanafunzi anayejiunga na chuo nia yake ni kufaulu vizuri ili apate cheti kizuri na kwa kuwa uwezo wa wanafunzi unatofautiana. Je Serikali inatoa kauli gani kwa wanafunzi ambao wanakosa kabisa makazi ndani ya *campus* wakalazimika kukaa nje na hivyo kuweza kuharibu *performance* yao ya masomo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema, Serikali haina mpango wa kujenga hosteli kwa sababu, tukubaliane kwamba wanafunzi wa Chuo Kikuu umri wao ni zaidi ya miaka 20 na hatutegemei kwamba tuanze kuwaandalia malazi badala ya madarasa. Niliwahi kusema kwamba, ni vema kuwa na madarasa ya kutosha kwa sababu wanafunzi watahitaji kusoma ndani ya madarasa, lakini mahali pa kuishi wanafunzi hao wanaweza wakajitafutia wenyewe na wanafanya hivyo na tumesema hakuna uhusiano kati ya kuishi

nje ya chuo na kufaulu mitihani. Wengi wetu hapa tumeishi nje ya chuo, hasa akinamama ambao unakuta wanapata watoto na hao wanafaulu sana. Tukiweza, tunaweza kujenga hosteli na kwa taarifa katika Bajeti ya mwaka huu Chuo Kikuu cha Sokoine wamepewa Shilingi bilion 4.8 kwa ajili ya kujenga hosteli kwa sababu tuchukulie kwamba Sokoine wanafunzi wengi wanatoka nje ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, chuo kinajitahidi kuwatafutia wanachuo mahali ambapo mazingira ya kupanga ni mazuri. Hiyo yote ni juhudi ya Serikali, lakini zaidi tuna-*encourage* wawekezaji binafsi kwa sababu watakapokuwa wamewekeza kwenye hosteli katika maeneo ya chuo watapata pesa, watapangisha mpaka pesa yao itakapokwisha baadaye watatuachia yale majengo.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka kuuliza swalii moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mionganii mwa vyuo ambavyo vimeathirika sana na uhaba wa majengo ni Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*), kiasi kwamba hata wawekezaji ambao Mheshimiwa Waziri anawazungumzia kwamba wanaweza wakaweka majengo pale ni kama haiwezekani kwa sababu ya ukosefu wa nafasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta eneo jingine kwa ajili ya chuo hiki ili hata hao wawekezaji wakipatikana waweze kuwekeza kwenye eneo hilo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Chuo cha Usimamizi wa Fedha *IFM*, kiutawala kipo chini ya Wizara ya Fedha, kwa hiyo nafikiri watakuwa na mipango mizuri ya kuweza kuwapatia ardhi ya kuweza kujenga hosteli. Ninaelewa matatizo yaliyopo katika chuo hiki. Sisi tunahusiana na kile chuo kwa upande wa wanafunzi, lakini kwa upande wa utawala hiki chuo kipo chini ya Wizara ya Fedha.

Na. 284

### **Ujenzi wa Majengo ya Makao Makuu ya Benki Kuu**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imejenga majengo mapya aina ya minara pacha (*twins towers*) kwa ajili ya Ofisi za Benki Kuu ya Tanzania ili kupunguza gharama za upangaji katika majengo mengine kwa ajili ya kuendeshea shughuli zake na kwa kuwa ujenzi huo umegharimu fedha nyingi kwa lengo la kuyafanya majengo hayo yawe na hadhi kulingana na chombo chenyewe (*BOT*) kilivyo: -

- (a) Je, ujenzi huo umegharimu jumla ya fedha kiasi gani hadi sasa kwa majengo hayo yanayoonekana kuwa ni aghali sana ikilinganishwa na hali ya uchumi wa nchi?
- (b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika kwa ajili ya ujenzi pekee, samani pekee na usalama na mawasiliano?
- (c) Je, ni utaratibu gani uliotumika kumpata mkandarasi wa kujenga majengo hayo na je, kuna ongezeko la fedha kutokana na makisio ya awali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO) alijibu: -**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tarehe 3 Aprili mwaka huu wakati wa majumuisho ya Muswada wa Benki Kuu ya Tanzania, 2006 katika Bunge lako Tukufu, ujenzi wa Makao Makuu ya Benki Kuu unahuusu majengo matano yaani *South Tower, North Tower, Conference Centre, East Block* ambalo ni jengo la kuegesha magari na *North Block*. Zaidi ya majengo haya matano kuna pia mradi wa *basement* ambako ziko *strong rooms*. Gharama za ujenzi huo ni Shilingi bilioni 184.

(b) Mheshimiwa Spika, Benki Kuu hivi sasa iko mbioni kukamilisha ununuzi wa samani kukidhi mahitaji ya majengo yake, ununuzi ambaeo umepangiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 3.5. Aidha, gharama za usalama na mawasiliano kwa majengo yote mapya na matawi yote itafikia karibu Dola milioni 44.5.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa zabuni (*tender*) wa kumpata Mkandarasi ulifanywa na Bodi ya Tenda ya Benki Kuu ikisaidiwa na wataalam (*consultants*) na ikiripoti kwa Bodi ya Benki Kuu. Zabuni zilipotangazwa mwaka 2000 makampuni mengi ya ujenzi yalijitokeza wakati wa *pre-qualification*. Hatimaye makampuni manne yalipendekezwa nayo ni *Grinekker Construction, Group Five, Skanska Hensen* na *Veidekei*. Skanska ilikuwa ndiyo kampuni iliyoshinda zabuni, lakini baadaye kampuni hiyo ilijitoa kutokana na maamuzi ya makao makuu yao kuwa Skanska ijitee katika ujenzi wa majumba Afrika na itilie *mkazo* katika ujenzi wa majumba Ulaya na Amerika. Hivyo, kampuni ya pili, *Group Five*, ndiyo ikapewa tenda ya kujenga Makao Makuu ya Benki Kuu. Kumekuwa na ongezeko la gharama kutoka makadirio ya awali ambayo yalikuwa Shilingi bilioni 112 mpaka kufikia bilioni 184 kwa miradi yote kutokana na mabadiliko katika thamani ya Shilingi yetu (*exchange rate*), kuimarisha usalama na matatizo ya ubovu wa udongo na wingi wa maji mita chache tu chini ya ardhi na sehemu zote ambako zimejengwa *strong rooms*.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa haraka haraka kama nimemwelewa ni kwamba ujenzi huu sasa unagharimu zaidi ya Shilingi bilioni 244, tofauti na bajeti ya

kwanza ya Shilingi bilioni 112, ambapo kwa hesabu za haraka haraka ni kama ongezeko la asilimia 118.

(a) Je, ni utaratibu gani uliotumika na ni mamlaka yapi ambayo yaliruhusu ongezeko la gharama hizi, kitu ambacho hata Bunge lako Tukufu halikuweza kuombwa ruhusa hiyo?

(b) Mheshimiwa Spika, mradi huu inaonekana ni wa ghali sana kwa sababu kwa haraka haraka kama ni kujenga *PPF Tower*, ni kama *PPF Towers* 12 zingejengwa hapa nchini. Kama ni *Mafuta House*, basi yangejengwa majengo zaidi ya 8 kama ya *Mafuta House* hapa nchini. Sasa, nikiangalia uchumi wa nchi hii na gharama za mradi huu inaonekana haziwiani. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuruhusu kuundwe Tume Huru ya Bunge kuchunguza juu ya suala hili? (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya fedha ambazo zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa Benki Kuu ambayo kwa kweli mara nyingi sana tunasema *Twin Towers* na inaonekana kama vile ni majengo mawili, lakini kama alivyoeleza Naibu Waziri ni majengo matano ambayo yalijengwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ujenzi ulifuatwa, taratibu zote za sheria zilifuatwa katika ujenzi huu. Suala ni kwamba, fedha nyingi zimetumika katika ujenzi huu. Ni kweli fedha nyingi zimetumika, lakini nafikiri mara nyingine kufananisha vitu, kwa mfano labda vitu vinane au tisa vingeweza kufanyika. Tuangalie kwa mfano watu wanasema juu ya elimu, kwamba elimu ni ghali, lakini watu wanasema basi jaribu ujinga.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa benki hii kwa kweli umeangalia haya yote na kama tulivyoeleza ni kwamba, wakati wa ujenzi hasa katika upande wa *strong rooms* kule *basement* kulijitokeza matatizo ambayo ni matatizo ya maji kuingia katika maeneo haya, kwa hivyo ikabidi kwa kweli fedha zaidi ziweze kutumika. Fedha nyingi zimetumika, lakini nafikiri kwamba suala zima ambalo Tanzania tunapaswa kuangalia ni suala la uimara wa ujenzi huu kwa sababu Benki Kuu ndiyo benki ambayo inaweka fedha zetu, ndiyo hasa hasa uchumi wetu.

Kwa hiyo, kitu ambacho kinaangalia uchumi wetu hatuwezi tukaweka kitu ambacho kiko hivi hivi. Ni benki ambayo inaweka fedha zetu za ndani, ni benki ambayo inaweka fedha zetu za nje, lakini ni benki ambayo Waheshimiwa Wabunge hapa hapa wamezungumzia juu ya masuala ya kununua na kuweka dhahabu.

Waheshimiwa Wabunge, ni budi tuelewe kwamba, pamoja na fedha nyingi ambazo zimetumika, lakini ilibidi fedha hizo ziweze kutumika ili kuhakikisha kwamba ujenzi huu imara pamoja na *structure* nzima ya kutoa taarifa. Kwa mfano, hivi sasa baada ya ujenzi huu ni kwamba taarifa zozote za kiusalama zitawenza kutoka kwenye benki hii kwenda kwenye matawi ya Mwanza, Arusha na Zanzibar pale ambapo kinatokea kitu chochote kile cha uhujumu kwa mfano, mara moja taarifa hizi zinaweza kupatikana. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, ilibidi kufanya hivyo lakini kwa kweli tunazungumzia uchumi wa Taifa letu. (*Makofi*)

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa ujenzi huu ni ujenzi ambao umetumia gharama kubwa. Je, Serikali ipo tayari sasa kuweza kuwafidia/kurudisha tena ule utaratibu wa wafanyakazi wa *BOT* ambao walikuwa wamepangiwa kusoma lakini walishindwa kwenda kwenye mafunzo mbalimbali kutokana na ujenzi huu?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kusema kwamba si sahihi kusema kulikuwa na watu ambao walikuwa wanakwenda kusoma halafu hawakwenda kusoma kwa sababu ya ujenzi wa Benki Kuu. Ni kwamba, kuna utaratibu wa mafunzo ya watu ambao wanakwenda kusoma kwa *training* mbalimbali ama ndani ya nchi au nje ya nchi na utaratibu huu kwa kweli unaendelea.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuiachie Kamati ya Fedha suala hili.  
Na. 285

#### **Kambi ya Vijana Sasanda**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali ilichukua hektaa 335 sawa na ekari 828 katika Kijiji cha Nyimbili, Kata ya Nyimbili katika Jimbo la Mbozi Mashariki na kulifanya kama Kambi ya Vijana ya Sasanda, lakini matumizi ya eneo hili hayaridhishi kwani yamelifanya eneo hilo lione kane limetelekezwa na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya na Serikali ya Kijiji ingependa kutumia ardhi hiyo kwa shughuli nyingine za maendeleo kama vile ujenzi wa shule na kadhalika.

- (a) Je, nini hasa nia ya kuanzisha kambi hiyo?
- (b) Kwa kuwa Serikali imeshindwa kutumia eneo hilo sawa sawa. Je, isingekuwa busara kama Serikali ingeliacha eneo hilo kwa wananchi wa Kijiji cha Nyimbili ili liweze kutumika kwa shughuli nyingine za maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA  
(MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maeleo kama ifuatavyo: -

Kambi ya Vijana Sasanda ilianzishwa katika miaka ya 1978/1979 na Uongozi wa Mkoa wa Mbeya kwa madhumuni ya kuwaweka vijana pamoja kupata mafunzo ya ukakamavu, uzalendo na shughuli za uzalishaji mali. Katika miaka ya 1980 Wizara ilianzisha mipango ya vikundi vya vijana vya kuzalisha mali kwa nchi nzima na Mkoa wa

Mbeya ukaikabidhi kambi hii kwa Wizara ili iweze kuendesha shughuli hizo Kitaifa. Kutokana na mahitaji halisi ya vijana, Wizara iliona ni vema Sasanda iandaliwe kuwa Kituo cha Vijana kitakachotoa mafunzo mbalimbali ili vijana waweze kujiajiri. Hivyo, kuanzia mwaka 1992 Sasanda kimekuwa ni Kituo cha Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kumjibu Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyoeleza hapo awali, Sasanda ni Kituo cha Maendeleo ya Vijana. Madhumuni ya kuwa na kituo hiki ni kutoa mafunzo kwa vijana waliomaliza elimu ya msingi na sekondari na ambao hawana ajira rasmi. Mafunzo haya yanalenga: -

- Kuwajengea vijana misingi ya uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi yao.

- Kuwapa vijana mafunzo ya ujuzi na utaalam katika fani mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji na ufundi.

- Kuwawezesha vijana kupata mafunzo ili ujuzi huo wakauendeleze sehemu zao za miradi na kituo hiki pia ili kiwe ni kitovu cha kutengeneza ajira kwa vijana hasa za kilimo na ufugaji na pia uongozi bora wa vikundi.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara haijatelekeza kituo cha Sasanda, bali jitihada za kupaendeleza sasa zinaimarishwa kwa ajili ya kuwafundisha vijana ikiwa ni pamoja na wale wanaotoka kijiji hicho cha Nyambili (Ukombozi) kwa kutekeleza yafuatayo: -

- Kukarabati majengo yaliyopo ambayo ni mabweni, madarasa, nyumba za watumishi na ofisi.

- Kutenga maeneo maalum ya hifadhi ya mazingira na kuendeleza upandaji miti.

- Taratibu za kupata watumishi kwa kusimamia na kuendesha mafunzo zinaendelea.

- Mitaala na programu za kutolea mafunzo katika kituo zinaboreshwaa.

- Gharama za uendeshaji wa kituo zimewekwa katika Bajeti ya Wizara ya mwaka huu wa 2006/2007.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, eneo hili lina ukubwa wa hekta 335 au ekari 828 na tunajua kwamba ardhi ndiyo raslimali pekee ambayo mwananchi hasa mkulima anaitegemea sana. Sasa kwa kuwa zaidi ya  $\frac{3}{4}$  liko wazi na halitumiki kwa shughuli zozote za maendeleo kama Mheshimiwa Waziri anavyosema, je; Serikali itakuwa tayari

kuwapa wananchi wa Mbozi eneo hili walau hata sehemu ili waweze kulitumia kwa ajili ya shughuli za maendeleo?

(b) Mheshimiwa Spika, nimeshangaa kusikia Waziri anasema kwamba eneo lile linaendelezwa, labda kama kwenye Bajeti hii kama alivyosema. Lakini kuna watumishi wasiozidi watano katika eneo lile na hawa wanalipwa mshahara bila kufanya kazi zozote. Sasa, haoni kwamba haya pia ni matumizi yasiyoridhisha ya pesa za Serikali kuendelea kuwaweka watumishi kwa zaidi ya miaka 20 bila kuendeleza hilo eneo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli lile eneo lina hekta 335 na ni kweli vile vile kwamba ukilitazama sasa hivi ni kama vile limetelekezwa, lakini kama nilivyosema, halijatelekezwa. Kama nilivyosema pia, mipango sasa kwa umuhimu ambao maendeleo ya vijana yamepewa, taratibu zinafanyika kuongeza kasi ya matumizi ya eneo hili.

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo yanatarajiwa kufanywa ni kutumia eneo hili kama shamba la mfano kwa ajili ya vijana kwa ajili ya kilimo pamoja na ufgaji. Ingawa hili eneo la hekta 335 linaonekana ni kubwa, bado sisi tunafikiri kwamba halitoshi kuwa na mashamba ya mifano kwa ajili ya vijana, hiyo ni moja. Lakini la pili, eneo hili tunatarajia litatumika vile kama sehemu ya kutoa ajira ya vijana wetu katika kilimo na katika uzalishaji. Lakini jambo la tatu ambalo nataka kusema ni kwamba, nafikiri pale ambapo Serikali imepanga matumizi ya sehemu na kwa kuwa nchi yetu bado ina maeneo makubwa sana, tuache yatumike kwa madhumuni ambayo yametarajiwa. Kwa hiyo, naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge atazame pengine aachie Wizara iendelee na Mipango yao na kutumia lile shamba kama Kituo cha Maendeleo ya Vijana.

Na. 286

### **Upungufu wa Majisafi na Salama Manispaa ya Tabora**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza: -

Kwa kuwa upatikanaji wa maji kwa matumizi ya majumbani na maofisini katika Manispaa ya Tabora hauridhishi, kwani maji yanayopatikana siyo tu hayakidhi viwango vya kuwa safi na salama, bali pia yanatoa harufu mbaya na kwa kuwa maji yapatikanayo kupitia mtandao wa mabomba wa *TUWASA* hayajafikishwa katika baadhi ya kata zilizo pembeni ya Mji wa Tabora, hali inayohatarisha afya za wakazi wa Manispaa hiyo: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na tatizo hili kubwa la upungufu wa maji safi na maji salama katika Manispaa ya Mji wa Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Manispaa ya Tabora ina wakazi wapatao 190,000 wanaoishi kwenye kata 21 ambazo saba kati ya hizo ziko pembezoni mwa Manispaa. Chanzo kikuu cha maji cha Manispaa hiyo ni bwawa la Igombe lenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 41 milioni na bwawa la Kazima lenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 1.2 milioni. Vyanzo vingine ni visima vifupi ambavyo vinahudumia kata zilizoko pembezoni mwa Manispaa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la upungufu wa maji katika Manispaa ya Tabora linasababishwa na uwezo mdogo wa mfumo wa maji uliopo. Mahitaji ya maji ni mita za ujazo 22,500 kwa siku ambapo uwezo wa mitambo ya kusafisha na kusukuma maji ni mita za ujazo 17,400 kwa siku Kituo cha Igombe mita za ujazo 15,000 na kazima 2,400. Aidha mtandao wa mabomba ya kusambaza maji katika kata saba (7) zilizoko pembezoni mwa Manispaa haujafika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upungufu wa maji katika Manispaa ya Tabora hasa wakati wa kiangazi unasababishwa na ukame. Mvua za masika huwa hazinyeshi za kutosha kujaza mabwawa hayo mawili. Kwa mfano katika mwaka 1984 na 1997 mabwawa yote hayakuja, mwaka 2000 Bwawa la Kazima lilikauka kabisa. Mwaka huu mabwawa yote hayakuja hivyo kuashiria upungufu wa maji kabla ya mvua za masika. Tatizo la harufu ya maji yanayozalishwa kutoka Bwawa la Igombe linasababishwa na kuota vimelea vya mimea iitwavyo *Algae* hasa wakati maji yakipungua sana bwawani. Vimelea hivyo vikifa ndani ya maji hutoa harufu mbaya.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za dharura za kukabiliana na tatizo la harufu kwenye maji, mamlaka ya majisafi na majitaka Tabora inatumia dawa nyingi zaidi, karibu kilo 1,100 za shabu kila siku na kufanya *flushing* kwenye mabomba ya kusambaza maji mara kwa mara. Aidha kwa mpango wa muda mrefu unaoandaliwa ni kufanya marekebisho kwenye mtambo wa kusafisha maji ili uweze kuondoa harufu hiyo mbaya.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za muda mfupi za kupunguza tatizo la maji katika kata zilizoko pembezoni mwa Manispaa, Mamlaka inatekeleza miradi ya kujenga magati (*kiosk*) na kutandaza mabomba katika vitongoji vya Itetemia na Kipalapala, pamoja na vijiji vya Itaga, Misha, Luanzari, Malolo, Mbugani na Kariakoo.

Mheshimiwa Spika, ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili la upungufu wa maji safi na salama katika muda mrefu Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya *Uswiss* kupitia Shirika lake la *Swiss Secretariat for Economic Affairs (SECO)* itagharamia mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Manispaa ya Tabora. Kazi zitakazofanyika ni ukarabati

wa miundombinu ili kupunguza upotevu wa maji na upanuzi wa mtandao wa mabomba pamoja na chanzo cha maji cha Bwawa la Igombe.

Mradi huu utaanza kutekelezwa mwaka 2006/2007 kwa gharama ya shilingi takriban bilioni 15 na utatekelezwa kwa miaka mitatu. Aidha bodi ya maji ya *TUWASA* kwa kushirikiana na *SECO*, imeshauriwa kuanza uchunguzi wa maji ardhini ili kutafuta chanzo mbadala, badala ya kutegemea mabwawa ya Igombe na Kazima tu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona nitaongeza muda mfupi kama dakika tano ili kufidia muda tulipoteza kwenye matangazo mengine.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swalii, aidha napenda kumshukuru Waziri kwa majibu mazuri. Nilikuwa nataka kupendekeza kwamba pamoja na hatua zinazochukuliwa na Wizara sasa hivi kuna mradi mkubwa wa maji kutoka *Lake Victoria* kuja Shinyanga, kuitia Kahama na kuelekea Nzega. Je, isingekuwa busara kuendeleza mradi huu mpaka Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu la Mheshimiwa Kaboyonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mradi wa Maji wa *Lake Victoria* kwenda Shinyanga na Kahama ni mradi ambaa sasa hivi unafikia hatua mbalimbali lakini hata hivyo, ningependa kusema kwamba mradi huu umeghamariwa gharama kubwa mno na isitoshe hadi sasa kwa kufuatana na gharama zilizopo hauwezi kuendelezwa zaidi ya Shinyanga na Kahama ila tu napenda kupokea pendekezo lake ili hilo pendekezo labda kwa siku za baadaye ikiwa fedha zitaruhusu basi michanganuo itanywe kwani kuna maombi mengi ambaa wanataka maji hayo yaendelee ikiwemo Nzega, Igunga basi hayo ni mapendekezo ya baadaye kufuata na fedha tutaangalia mambo gani yataendelea kufanywa katika mradi huo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa amekiri kwamba kuna upungufu mkubwa wa maji na kutokutosheleza kwa mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kukarabati visima vya maji ambavyo vinatumika hata wakati wa kiangazi kwa jina maarufu vinaitwa Kitete ambavyo kwa kweli vinatumika hata kukauka havikauki na vimejengwa tangu mwaka 1961. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka pampu za maana na za kisasa ili maji yaweze kutosheleza? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri na majibu yaliyotolewa katika swalii la msingi yanatoa ukweli juu ya hatua ambazo Serikali inachukua kupambana na tatizo la Tabora. Hali ya Tabora ni ngumu kwa sababu vyanzo vya maji ni vigumu sana kupatikana siyo Tabora Mjini tu hata katika maeneo ya Wilaya zingine. Lakini kwa ajili ya Tabora Mjini tumeshauri Bodi ya Maji ya Tabora na mimi nilikwenda kule nikashirikiana nao na

nimewashauri kwamba tuanze kutazama uwezekano wa kupata maji kutoka chini ya ardhi kama njia ya uhakika ambayo inaweza kutusaidia kupata vyanzo mbadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata zamani Dodoma ilikuwa haina maji lakini baadaye uchunguzi wa ulipofanyika leo Mji wa Dodoma unapata maji yote kutoka ardhini. Kwa hiyo, mimi nina imani ya kwamba tukichunguza vizuri tutapata vyanzo mbadala na hivyo visima alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge, ni sehemu ya maji chini ya ardhi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na yale mawili yaliyosalia tutayaongeza kwenye orodha ya kesho.

Ninayo matangazo, kwanza wale vijana wa shule na walimu ambaa niliwatambulisha bila kutaja wanatoka wapi ni wanafunzi kutoka *Kikuyu Secondary School* ya Mjini Dodoma. Karibuni sana.

Mheshimiwa Jenista Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo, saa 5.00 asubuhi chumba Na. 133.

Waheshimiwa Wabunge, yamerejea tena malalamiko kuhusu baridi humu ndani ya Ukumbi. Kwa hiyo, nawaomba mafundi waweze kulishughulikia hilo. Si kweli eeh? Basi mafundi wanajua cha kufanya kama ni baridi ama si baridi watatuweka sawa. (*Makofi*)

Kuna Wabunge wawili wameniandikia kwamba leo hii hapa wanaona askari wa polisi wengi sana. Kwa hiyo, wana hofu juu ya michango yao. Leo askari polisi wako hapa ili kusikia hoja zitakazotolewa na ninyi Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Wizara yao ambayo ni ya Usalama wa Raia. Hawa wanaokuwa na hofu itabidi Spika aendeleee kuwaangalia kwa sababu mtu anayetia hofu akiona polisi basi pengine kuna tatizo. (/*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taarifa za vyombo vyahabari tarehe 23 Julai, 2006 kule Magu wakati wa makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru, Mkuu wa Wilaya ya Magu alizozana hadharani na Mheshimiwa Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Richard Ndassa. Tukio hilo nalihesabu kuwa ni la aibu kwa Serikali na kwa Bunge pia. Hatuwezi kuliacha lipite hivi hivi. Kwa hiyo, leo hii asubuhi nimemwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumshauri aagize uchunguzi ufanyike wa tukio hili ili kubaini chanzo na undani wa mkasa huo. (*Makofi*)

Inawezekana aliyesababisha tatizo katika hafla hiyo ya makabidhiano ya mwenge akawa ni Mheshimiwa Mbunge au akawa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya (DC). Lakini ikiwa kwa mujibu wa Taarifa ni kweli DC alimkatiza Mheshimiwa Mbunge wakati akitoa

salaam za Waheshimiwa Wabunge wenzie, basi huo utakuwa utovu wa nidhamu wa hali ya juu. Waheshimiwa Wabunge, malalamiko kuhusu baadhi ya watendaji Serikalini katika ngazi mbalimbali kuwapuuza au kuwadharau Waheshimiwa Wabunge kwa maneno na kwa vitendo au kwa vyote viwili yamefikishwa kwangu na Waheshimiwa Wabunge kadhaa. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge, imefika wakati niweke wazi msimamo wangu na wa Bunge ninaloliongoza kuhusu hali hiyo. Kwa kuzingatia nafasi na hadhi ya Mbunge katika Katiba ya nchi yetu ni kosa kubwa na ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu kwa mtendaji ye yote Serikalini kufanya vitendo vya dharaa dhidi ya Mbunge. Kumdhahilisha ye yote ni sawa sawa na kulidhalilisha Bunge hili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, napenda nichukua nafasi hii kutoa tahadhari kwa watumishi wa umma wenye mwelekeo potofu usiotambua hadhi ya Mbunge au Bunge, kwamba Bunge halitakaa kimya wakati hadhi yake inaathiriwa. Inapotokea kwamba anayesababisha tatizo ni Mbunge, basi taarifa zinifiki ili taratibu zetu za kawaada za maadili ya Wabunge zichukue mkondo wake.

Waheshimiwa Wabunge, naishukuru sana Serikali kwa wakati wote imekuwa sikuvi na natumaini kwa tangazo hili tutaweka sawa mahusiano kati ya Bunge na Serikali. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Wizara ya Usalama wa Raia**

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa Bungeni mapema leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi, ili liweze kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, utangulizi napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo, za asilimia 80.2 katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Desemba 2005. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein aliyekuwa Mgombea Mwenza, kwa ushindi mkubwa waliouopata.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa ushindi mkubwa aliouopata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, ambao katika mazingira ya Zanzibar ni ushindi wa

kishindo. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo. Kuteuliwa kwake na kuthibitishwa kwa kura nyingi na Bunge hili ni ishara ya imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge juu ya utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa dhati wewe binafsi Mheshimiwa Samuel Sitta na Naibu Spika Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kutuongoza. Vile vile nampongeza Spika Mstaafu, Mheshimiwa Pius Msekwa, kwa usimamizi madhubuti wa shughuli za Bunge ambao umetuwezesha kupata jengo jipya na la kisasa. Nawapongeza pia Wenyeviti, Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa kuteuliwa kuwa wenyeviti. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wote na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kuongoza kamati hizo. (*Makofì*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi nyingi za dhati kwa Chama changu cha CCM kwa kupata viongozi wapya wa kitaifa. Nampongeza sana Mwenyekiti wa CCM Taifa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kushika wadhifa huo. Ushindi wa kura 1,812 kati ya kura 1,813 zilizopigwa ni ushindi wa kihistoria.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Frederick Tulway Sumaye kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuendeleza amani na utulivu nchini. Aidha, nawapongeza kwa kusimamia utungaji mzuri wa sera za kiuchumi zilizoweza kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuufanya uchumi wetu uwe wenye ushindani na endelevu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Yusuph Rajab Makamba kwa kuteuliwa na baadaye kuthibitishwa na NEC kuwa Katibu Mkuu wa CCM. Nampongeza Mheshimiwa Jaka Mwambi kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Bara). Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa nyadhifa walizopata, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Mheshimiwa Kidawa Salehe na Mheshimiwa Rostam Aziz.

Mheshimiwa Spika, wote hawa tunawaombea kheri, afya njema na baraka tele za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yao mapya. Napenda kuwathibitishia kuwa, mimi binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo la Tanga tunawaahidi kuwapa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali, hali ya uchumi wa nchi kwa jumla na masuala ya msingi yanayopaswa kutekelezwa mwaka ujao wa fedha wa 2006/2007. (*Makofì*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa kuyapitia na kuyachambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu tarehe 30 Mei 2006, pamoja na kuchambua masuala mbalimbali ya

Wizara ya Usalama wa Raia na kuyatolea maoni na ushauri. Michango iliyotolewa na kamati kwa ujumla imetusaidia kwa kiwango kikubwa kuiboresha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani kwa ushirikiano wa karibu, ushauri na maelekezo fasaha ambayo nimekuwa nikiyapata kutoka Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Ushauri na maelekezo yao unasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarishe utendaji kazi katika Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mhe. Rais kwa kunitua kuwa Waziri wa kwanza wa Wizara mpya ya Usalama wa Raia na kunipatia Naibu Waziri wa Usalama wa Raia Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, ambaye ameonyesha umahiri na uwezo mkubwa katika kunisaidia kusimamia shughuli za Wizara na za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa Katibu Mkuu wa Wizara Bwana Bakari Mahiza ambaye ni hazina kubwa kwa Wizara yetu kutohana na uzoefu alioupata akiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo wakati huo Jeshi la Polisi lilikuwa chini yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Inspekte Jenerali Mstaafu, Alhaj Omar Iddi Mahita, ambaye ye ye pamoja na Makamishna wake wote walifanya kazi nzuri na walijitahidi sana kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Polisi. Ninawashukuru na kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa Inspekte Jenerali mpya Ndugu Said Mwema, pamoja na Makamishna wapya ambao kwa kipindi kifupi wameweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji na kukabiliana na uhalifu nchini na hivyo kurejesha heshima ya Serikali na kuwapa imani wananchi, wageni na wawekezaji, kwamba nchi yetu bado ina amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Makamanda wote wa Polisi wa Mikoa, Vikosi na Wilaya; Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa, Vikosi na Wilaya na askari wote kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya ya kulinda amani na usalama nchini. Juhudi zao tunazitambua na kuzithamini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Usalama wa Raia ilianzishwa na Mheshimiwa Rais kwa Tangazo la Serikali Na. 1 la mwezi Januari 2006 kwa lengo la kusimamia usalama wa raia na mali zao wakiwemo wageni na wawekezaji. Kuundwa kwa Wizara hii ni kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, kama ilivyoainishwa kwenye Ibara ya 111 inayozungumzia Ulinzi na Usalama. Ilani ya Uchaguzi inataka uwezo wa Taifa wa kupambana na ujambazi na uhalifu kwa ujumla wake uongezwe na pia kuwashamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao ili kuhakikisha usalama wao na wa mali zao.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kuendeleza amani na utulivu uliopo nchini ili kuimarishe uchumi wa nchi na kuongeza kasi ya maendeleo, na hivyo kuleta maisha bora kwa kila

Mtanzania. Kunapokuwa na amani na utulivu wananchi wanaweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisasa ili kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, hali ya amani na utulivu pia itawavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye maeneo mbali mbali nchini na hivyo kuongeza nafasi za ajira na Pato la Taifa. Ni katika mazingira hayo ya amani na utulivu, mipango na mikakati ya Kitaifa kama vile Mipango ya Muda wa Kati na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), inaweza kutekelezwa na malengo ya Millenia 2015 na hatimaye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara hii mara baada ya kuunda Baraza la Mawaziri, alizitaja sababu kuu za kuundwa kwa Wizara hii kama ifuatavyo:-

- (a) Ongezeko la idadi ya watu kutoka milioni 10.3 wakati wa Uhuru mwaka 1961 hadi milioni 35 hivi sasa.
- (b) Kuongezeka kwa uhalifu na maarifa ya uhalifu, ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kufanya uhalifu.
- (c) Kukua kwa Jeshi la Polisi na shughuli za Polisi kuongezeka.
- (d) Kupunguza ukubwa wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwani ilikuwa kubwa mno, kiasi cha kupunguza umakini wa kazi. (*Makofit*)
- (e) Kumpa nafasi Waziri kushughulikia masuala yanayohusu Polisi tu ili kukabiliana na ongezeko la vitendo vya uhalifu, hasa uhalifu wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara muundo wa Wizara uliidhinishwa na Mheshimiwa Rais tarehe 18 Aprili 2006. Baadhi ya majukumu ya Wizara ya Usalama wa Raia kulingana na muundo huo ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kusimamia na kufuatilia masuala yote yanayohusu usalama wa raia na mali zao ikiwa ni pamoja na wageni kama vile watalii na wawekezaji kutoka nje.
- (b) Kuandaa Sera ya Usalama wa Raia na kusimamia utekelezaji wake.
- (c) Kuandaa mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya kukabiliana na uhalifu nchini.
- (d) Kushirikisha jamii katika kuweka mikakati ya kuzuia uhalifu kuitia utaratibu wa Polisi Jamii.

- (e) Kushughulikia malalamiko mbali mbali ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi.
- (f) Kusimamia maendeleo ya watumishi wa Wizara.
- (g) Kuzuia uhalifu wa kimataifa kwa kushirikiana na nchi jirani pamoja na Mashirika ya Kimataifa na kikanda kama vile Shirikisho la Polisi la Kimataifa (*INTERPOL*), Shirikisho la Polisi la Nchi za *SADC* (*SARPCCO*), na Shirikisho la Polisi la Nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika (*EAPCCO*).

Mheshimiwa Spika, dira ya wizara, Wizara yangu imejizatiti kutekeleza majukumu niliyoainisha hapo juu kwa kuongozwa na Dira ya Kuwa na Wizara yenye uwezo endelevu wa kuhakikisha kuwa usalama wa raia na mali zao unakuwepo. Lengo la dira hii ni kuhakikisha usalama wa raia na mali zao wakiwemo wageni kama vile watalii na wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ya uhalifu nchini, kwa ujumla idadi ya matukio ya uhalifu nchini, Tanzania Bara na Visiwani, hasa makosa makubwa ya jinai kitakwimu imeendelea kushuka kuanzia mwaka 2000 hadi kufikia Desemba 2005. Mfano, kipindi cha Januari hadi Desemba 2000, jumla ya matukio 87,973 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi nchini, ikilinganishwa na jumla ya matukio 73,555 yaliyoriipotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, idadi hiyo ilishuka zaidi mwaka 2002 ambapo jumla ya matukio 67,371 yaliripotiwa. Takwimu zinaonyesha pia kwamba, idadi ya matukio hayo yalipungua zaidi mwaka 2003 na kufikia matukio 58,516. Mwaka 2004 kulikuwepo na ongezeko kidogo la idadi ya matukio yaliyoriipotiwa Polisi ambapo jumla ya matukio 61,376 yaliripotiwa. Hata hivyo, idadi hiyo ya matukio kwa kipindi kilichoishia mwezi Desemba 2005 ilishuka sana hadi kufikia matukio 46,650, ikiwa ni upungufu wa matukio 14,726 ambao ni sawa na asilimia 24. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa katika vituo vya Polisi kuanzia Julai 2005 hadi Aprili 2006 katika mikoa yote nchini yalikuwa 48,265 ikilinganishwa na matukio 51,820 kipindi cha Julai 2004 hadi Aprili 2005. Kuna upungufu wa matukio 3,555 sawa na asilimia 6.8. Hata hivyo, bado juhudhi zaidi zinahitajika kupambana na uhalifu kote nchini, Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, makosa ya Usalama Barabarani yaliyosababisha ajali ambayo yaliripotiwa Polisi kati ya Julai 2005 hadi Aprili 2006 yalikuwa 17,062 ikilinganishwa na 14,710 katika kipindi cha Julai 2004 hadi Aprili 2005. Kuna ongezeko la makosa 2,352 sawa na asilimia 16. Kati ya Julai 2005 hadi Aprili 2006 watu waliofariki kutokana na ajali za barabarani walikuwa 1,896 na wengine 12,349 walijeruhiwa ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2004/05 ambapo watu 2,159 walifariki na wengine 16,523 walijeruhiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, idadi ya watu waliofariki ilipungua kwa watu 263 sawa na asilimia 12.2 na walijeruhiwa walipungua kwa watu 4,174 sawa na asilimia 25.3 kama

ilivyoonyeshwa hapo awali. Pamoja na takwimu hizo kuonyesha kupungua, lakini bado tatizo la ajali za barabarani ni kubwa, hivyo jitihada zaidi za Jeshi la Polisi katika kukabiliana na makosa ya usalama barabarani zinahitajika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sababu za kuwepo ajali nyingi za barabarani ni pamoja na uzembe wa madereva, ubovu wa magari, ubovu wa barabara, magari kujaza kupita kiasi, uendeshaji mbaya na wa hatari, ulevi, mwendo wa kasi, kulegeza vidhibiti mwendo, utembeaji mbaya wa waenda kwa miguu, upandaji mbaya wa pikipiki na balskeli, ukosefu wa alama za barabarani, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza hapo awali, tatizo la ajali za barabarani bado ni kubwa na linahitaji mikakati thabiti ya pamoja ya wadau wote wa sekta hii. Ajali za barabarani zinasababisha vifo kwa abiria na waenda kwa miguu, zinaacha majeruhi, vilema na wengine kubaki yatima. Ajali pia husababisha upotetu na uharibifu wa mali. Kulingana na takwimu za mwaka 2005, mikoa inayoongoza kwa kuwa na ajali nyingi za barabarani ni Dar es Salaam, Mwanza, Mjini Magharibi, Pwani, Iringa, Arusha, Tanga, Mbeya, Morogoro na Kilimanjaro kama inavyoonyesha kwenye Jedwali Namba 2(f).

Mheshimiwa Spika, matukio ya ajali mbaya za barabarani ya hivi karibuni ni yale yaliyotokea Mkoani Kagera na kuua watu 28 na Mkoani Arusha, ambapo watu 54 walipoteza maisha yao. Nachukua fursa hii kuwapa pole familia, ndugu na jamaa za marehemu, na kuwatachia wapone haraka majeruhi wote ambaa bado wamelazwa. Aidha, narudia kutoa wito kwa madereva wote, kuwa waangalifu na kufuata sheria zote za barabarani. Abiria kwa upande wao, wasikubali kabisa kupanda magari yaliyojaa na yanayokwenda mwendo wa kasi kwani ni hatari kwa maisha yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye matukio mengine ya uhalifu ambapo wananchi hutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi, Wizara yangu inaomba ushirikiano kutoka kwa abiria kwa kutoa taarifa Polisi kuhusu magari ya abiria yanayokiuka sheria za Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, Majedwali Na. 2(a) hadi 2(e) na 2(g) yanatoa mchanganuo wa makosa ya jinai kimkoa kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2005. Kwa muhtasari kwa makosa dhidi ya binadamu mikoa inayoongoza ni Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Kagera, Mwanza, Shinyanga na Arusha. Makosa dhidi ya mali, mikoa inayoongoza ni Dar es salaam, Kagera, Tanga, Morogoro, Mwanza, Mbeya, Kilimanjaro, Mara na Kigoma. Aidha kwa upande wa makosa dhidi ya maadili ya jamii, mikoa inayoongoza ni Dar es Salaam, Mwanza, Mara, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Shinyanga, na Kagera. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matukio makubwa ya uhalifu yaliyotokea nchini, ufuataa ni muhtasari wa baadhi ya matukio makubwa ya uhalifu yaliyotokea katika kipindi cha Januari hadi Julai, 2006. Matukio hayo yalileta hofu kubwa kwa wananchi kiasi cha kujenga hisia kwamba Jeshi la Polisi limeshindwa kukabiliana na wimbi la ujambazi hapa nchini na wengine walithubutu hata kusema kwamba kazi hii wapewe Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya kulinda usalama wa raia na mali zao ni yenyé taaluma maalum na wenye taaluma hiyo ni Jeshi la Polisi. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa jumla kuwa Jeshi la Polisi lina uwezo wa kuwalinda wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Januari 2006 majambazi yakiwa na silaha yalivamia Benki ya *NBC (T) LTD* Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kupora Tsh. 8,762,915, mali ya benki hiyo na kutoweka.

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Januari 2006 ilisemekana majambazi manne yakiwa na silaha yalivamia gari la Kampuni ya *BIDCO* lililokuwa na makusanyo ya fedha za mauzo Tsh. 5,775,000 na kupora kisha kutoweka. Hata hivyo, ilisemekana wakati huo kwamba majambazi hayo yalikamatwa na Polisi muda mfupi baadaye na kuuawa wakati wakirushiana risasi. Tukio hili la kuuawa watu hao lilisababisha hisia tofauti mionganoni mwa wananchi ambapo yalikuwepo madai kwamba waliouawa hawakuwa majambazi bali raia wema. Malalamiko hayo yalisababisha Mheshimiwa Rais kuunda Tume ya Jaji Kipenka Mussa ili kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, tayari Tume imewasilisha ripoti yake Serikalini, na katika uchunguzi wake ilibaini kwamba waliouawa hawakuwa majambazi bali raia wema na kupendekeza askari 15 waliohusika katika tukio hilo washtakiwe kwa mauaji. Askari 12 wamekwishakamatwa na kufikishwa mahakamani ambapo kesi yao bado inaendelea. Askari waliobakia bado wanasakwa na Jeshi la Polisi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Februari, 2006 majambazi yanayokadiriwa kufikia 10 yakiwa na silaha yalivamia Benki ya *NBC* Tawi la Ubungo na kufanikiwa kupora Tsh. 123,000,000, Dola za Kimarekani 16,128 na *Euro* 50 mali ya benki hiyo na kisha kutoweka.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Machi 2006 majambazi yakiwa na silaha yalivamia benki ya *Standard Chartered* Tawi la *Life House* na kufanikiwa kupora fedha taslimu Shilingi Milioni 300 kutoka kwa mteja ambaye alikuwa anataka kuweka fedha hizo benki.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Aprili, 2006 katika makutano ya barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Nelson Mandela, majambazi kadhaa yaliyokuwa na silaha nzito za kivita yалишамбулиа msafara wa magari ya benki ya *NMB* Tawi la *Bank House* ambayo yaliwu yanasaferisha fedha Shilingi bilioni 1 kutoka tawi la *NMB Bank House Dar es Salaam* kwenda Tawi la *NMB* Wami Morogoro. Katika tukio hilo askari mmoja kati ya askari wanenewa waliokuwa wanasindikiza fedha hizo pamoja na mfanyakazi mmoja wa benki ya *NMB* waliuawa na majambazi hayo. Askari wengine watatu, dereva na wananchi wengine wapita njia walijeruhiwa kwa risasi zilizopigwa na majambazi hayo. Fedha shilingi milioni 150 ziliporwa na majambazi hayo na Polisi waliweza kuokoa shilingi milioni 850.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kisiwani Zanzibar mwanzoni mwa mwezi Julai, 2006 yametokea matukio ya ujambazi wa kutumia silaha ambapo kiasi kikubwa cha fedha kimeibiwa na mtu mmoja kuuawa. Hali hii imesababisha hofu kubwa kwa wafanyabiashara na wananchi wa Visiwani kwa sababu siyo kawaida matukio ya aina hii kutokea huko.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Julai, 2006 eneo la Darajani Mjini Unguja, majambazi yakiwa na silaha yalivamia dukani kwa Ndugu Mohamed Nassoro na kupora fedha taslimu Sh.12,000,000 na kadi za simu zenye thamani ya Sh.5,000,000. Majambazi hayo yalifyatua risasi na kumpiga kichwani Ndugu Mohamed Bakari Mrisho na kufariki. Tarehe 6 Julai, 2006 eneo la Kisiwandui, majambazi yenye silaha yalivamia duka la *Al-Habbys* na kufanikiwa kupora fedha taslimu Sh.30,000,000 baada ya kutishia kwa silaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia matukio haya ya ujambazi kutokea kwa mfululizo, Jeshi la Polisi lilijipanga upya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama na kukamata idadi kubwa ya majambazi yaliyohusika kwenye matukio haya pamoa na silaha walizotumia. Mionganini mwa majambazi yaliyokamatwa wapo raia wa nchi jirani na raia wa humu humu nchini. Watuhumiwa wamekwishafikishwa mahakamani.

Majambazi hayo yaliweza kukamatwa kutokeana na ushirikiano wa wananchi. Kwa kuitia Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwashukuru wananchi waliota ushirikiano wao uliowezesha majambazi kukamatwa. Aidha napenda kuwapongeza askari wote walioshiriki kupambana na majambazi na kufanikisha kuokolewa kwa mali na kukamatwa kwa majambazi.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuwepo kwa uhalifu nchini, zipo sababu nyingi zinazosababisha kutokea kwa uhalifu nchini. Sababu za jumla ni kama vile kuongezeka kwa idadi ya watu nchini, tatizo la wimbi la watu kuhamia mijini toka vijijini, kupanda kwa gharama za maisha na ukosefu wa ajira, na kuongezeka kwa wakimbizi amba baadhi yao huingia na silaha kinyume cha sheria. Sababu hizo za jumla kwa namna moja au nyingine zimechangia ongezeko la vitendo vya uhalifu nchini na hasa uhalifu wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonyesha kwamba zipo sababu nyingine zinazochangia kuwepo kwa vitendo vya uhalifu kama ifuatavyo:-

(a) Utandawazi na Mageuzi katika Mfumo wa Mawasiliano, Sera ya Utandawazi imesababisha na kurahisisha mwingiliano wa watu wa mataifa mbali mbali. Wahalifu wa Kimataifa nao wametumia mwanya huu na kuweza kufanya uhalifu nje ya mipaka ya nchi zao. Aidha, mageuzi katika mfumo wa mawasiliano yamerahisisha sana na kuongeza kasi ya utendaji makosa. Wahalifu hivi sasa wanaweza kuwasiliana kwa haraka na kwa mawasiliano bora zaidi popote wanapokuwa, wakati mwingine kupita yale walionayo Polisi kwa sasa. Mfano, matumizi ya *Computer, Internet* na simu za mkononi za kisasa. Aidha, pale ambapo Polisi wanahitaji kufuata utaratibu wa kisheria na

Kidiplomasia wa kuvuka mipaka kufuutilia wahalifu, wahalifu hao hawalazimiki kufanya hivyo wanapokwepa mkono wa sheria. (*Makofi*)

(b) Uchache wa askari na nyenzo za kutendea kazi, upo uhaba mkubwa wa askari ikilinganishwa na idadi ya wananchi wanaohitaji huduma ya Polisi. Kwa upande mwingine, upo uhaba wa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya doria za miguu, magari, vifaa vya majini na vifaa vya mawasiliano. Kukosekana kwa vitendea kazi hivi kumeathiri sana uwezo wa Idara kukabiliana kikamilifu na tishio la uhalifu nchini. Mfano, imekuwa ni vigumu kuwahi kwenye baadhi ya matukio ya uhalifu kwa sababu ya ama kukosekana gari au gari kutokuwa na mafuta.

Aidha, imekuwa vigumu kukabiliana na uhalifu wa kuteka nyara magari kwenye barabara kuu kutokana na kutokuwa na magari ya kufanya doria kwenye barabara hizo (*Highway Patrol*).

(c) Kutokuwa na Mfumo wa Kisasa wa Uwekaji Kumbukumbu na Upashanaji Taarifa, Upo umuhimu wa kuwa na njia za kisasa za uwекaji kumbukumbu, mawasiliano kwa njia ya mtandao wa *Computer* na umuhimu wa kuwa na *Electronic Surveillance System* kama *Closed Circuit Televisions (CCTV)*, ambayo hunakili matukio yote ya uhalifu. Kukosekana kwa mfumo huo wa kisasa wa uwекaji kumbukumbu na mawasiliano kwa Jeshi letu kumedhoofisha kwa kiasi kikubwa jitihada za kukabiliana na uhalifu. (*Makofi*)

(d) Uhaba wa Elimu na Taaluma za Upelelezi, Uhaba wa askari wenye taaluma ya upelelezi umechangia kwa kiasi fulani kupunguza kiwango cha mafanikio ya kudhibiti uhalifu kwa baadhi ya maeneo. Ukweli ni kwamba aina, muundo na mbinu za makosa ya jinai kwa jumla hubadilika siku hadi siku.

Mbinu hizo ni matumizi ya teknolojia ya kisasa kama vile matumizi ya mifumo ya kisasa na ya haraka ya kusafirisha fedha pamoja na kujenga mtandao wa magenge ya wahalifu amba unahusisha wahalifu wa nchi za jirani.

Hali hii inahitaji kupata askari amba wamepata taaluma kuhusu mabadiliko hayo ili kuweza kukabiliana kikamilifu na matishio ya uhalifu wa kisasa na yenye sura ya Kimataifa.

(e) Udhibiti hafifu wa mipaka yetu, upo upungufu wa nyenzo na watendaji wa kutosha katika maeneo muhimu ya mipaka yetu. Matukio yaliyotokea hivi karibuni hasa ya unyang'anyi wa kutumia silaha, wizi wa magari, madawa ya kulevyta, na kadhalika, yametudhahirishia kwamba wahalifu kutoka nchi jirani wamehusika katika matukio hayo.

Hali hii inaashiria kwamba kumekuwepo na udhaifu katika kuwachunguza wageni mbalimbali wanaoingia nchini mwetu. Udhaifu huu umetokana na ama ukosefu wa vifaa muhimu na vya kisasa kama vile *detecting/screening machines*, kumbukumbu sahihi za wahalifu wa Kimataifa na upungufu wa watendaji wenye taaluma inayostahili kwenye vituo vya mipakani. (*Makofi*)

(f) Ukosefu wa vyumba/ofisi maalumu za upelelezi, tatizo la uhaba wa ofisi kwa ajili ya askari wa Upelelezi na hasa vyumba maalum vya kufanya mahojiano (*Interview Rooms*) pia linaathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika upelelezi hasa wa kesi kubwa. Hali hii inachangia kuharibika au kuchelewa na hatimaye kushindwa mahakamani katika baadhi ya kesi.

(g) Mabenki na Taasisi za Fedha kutojikinga kwa njia za kisasa, kukataa ushauri wa Polisi wa kuweka mifumo mizuri ya ulinzi inayotumia teknolojia ya kisasa katika Benki na Taasisi nyingine za fedha hapa nchini, kumechangia sana wahalifu wa ndani na nje ya nchi kufanya vitendo vya uporaji kwenye taasisi hizo kwa urahisi na kuondoka bila kugundulika na hivyo kufanya kazi ya upelelezi kuwa ngumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa kuimarisha utendaji, kuanzia mwaka 2002/2003 Serikali imekuwa ikichukua hatua za kuboresha Bajeti ya Jeshi la Polisi. Bajeti hiyo imewezesha upatikanaji wa baadhi ya vitendea kazi kama vile magari, vifaa vya mawasiliano, mashua za doria n.k na upatikanaji wa makazi ya askari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Jeshi la Polisi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo: Mwaka 2006/2007 Bajeti ya matumizi ya kawaida ya Jeshi la Polisi imeongezeka kwa asilimia 40.1 na ile ya maendeleo imeongezeka kwa asilimia 36.2 ukilinganisha na mwaka 2005/2006 ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida iliongezeka kwa asilimia 18.7 na ile ya maendeleo iliongezeka kwa asilimia 1.9. Kwa mwaka 2006/2007 Bajeti ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa pamoja imeongezeka kwa asilimia 39.8 ukilinganisha na asilimia 17.6 mwaka 2005/2006 kama inavyoonyesha kwenye Jedwali Na. 4(a). Hata hivyo kutokana na matatizo ya Jeshi la Polisi kuwa makubwa, kama yaliviyotajwa bado juhud zaidi zinahitajika kuboresha Bajeti yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuiangalia Wizara hii kwa jicho la huruma. Mheshimiwa Rais akiwa ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ameona umuhimu wa kuisaidia Wizara hii ili iweze kukabiliana na vitendo vyote vya uhalifu. Pamoja na ukweli kuwa safari bado ni ndefu, lakini namshukuru sana kwa hatua zinazochukuliwa. Aidha, namshukuru Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kuyaelewa matatizo ya Wizara yangu na kuendelea kuyapatia ufumbuzi kulingana na uwezo uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kufanya mabadiliko ya uongozi wa juu wa Jeshi la Polisi, ambapo aliteuliwa Inspeksa Jenerali mpya na Makamishna, hatua mbali mbali zimechukuliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji kama ifuatavyo:-

- (a) Kufanya mabadiliko ya Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa. Aidha, baadhi ya Wakuu wa Polisi Usalama Barabarani wa Mikoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya pia wamebadilishwa.

- (b) Kuanzishwa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ambapo Wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke zimepewa hadhi ya Mikoa Kipolisi ili kuongeza ufanisi, kwani Jiji la Dar es Salaam lilikuwa linaongoza kwa matukio ya uhalifu.
- (c) Kutangazwa hadharani namba za simu za *IGP*, Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa na Wakuu wa Upelelezi wa Wilaya kumewezesha upatikanaji wa taarifa nyingi za uhalifu kutoka kwa wananchi. Matukio mengi ya uhalifu yalizuiwa kutokea kutokana na Polisi kupata taarifa mapema.
- (d) Uwekaji wa masanduku ya maoni nje ya Vituo vya Polisi umewezesha upatikanaji wa taarifa muhimu za uhalifu.
- (e) Uhamasishaji wa wananchi kwa njia ya mazungumzo na viongozi wa Serikali za Mitaa, wananchi na vikundi binafsi vya ulinzi ili kuwaelimisha juu ya utoaji taarifa za uhalifu.
- (f) Kufanya misako ya kushtukiza na yenye malengo maalum baada ya kupata taarifa za uhalifu ili kuzuia uhalifu usitokee.
- (g) Kuwasaka wafadhili wa uhalifu, ambapo baadhi yao wanaotuhumiwa wameshafikishwa mahakamani na zoezi linaendelea.
- (h) Kila Mkoo unaendelea kuimarisha kitengo cha Intelijensia ambacho kazi yake ni kutafuta na kukusanya taarifa za uhalifu kwa nia ya kuzuia, kufuatilia, kuwatambua na kuwakamata watu wanaofanya uhalifu huo.
- (i) Kuimarisha ulinzi katika Mabenki na Maduka ya fedha nchini.
- (j) Kuwahamasisha wananchi wanaosafirisha fedha nyingi kutumia huduma ya Polisi ya kusindikiza fedha.
- (k) Kuongeza juhudu katika upelelezi wa matukio ya uhalifu yaliyotokea hasa ya ujambazi wa kutumia silaha. Jitihada hizo ambazo ziliwezesha Polisi kufika hata nchi za jirani kuwafuatilia wahalifu, zimeleta mafanikio makubwa ambapo wahalifu wengi wamekamatwa na mitandao yao kuvunjwa.
- (l) Kuimarisha doria za miguu, magari, pikipiki na operesheni mbalimbali.
- (m) Kufanya ukaguzi mara kwa mara kwenye nyumba za kulala wageni na maeneo yanayohisiwa kuwa maficho ya wahalifu.
- (n) Kuwapa askari, hasa wa upelelezi, mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwaongeza ujuzi.

- (o) Kufanya uchunguzi wa kuwabaini askari wote wa Polisi na wa vyombo vingine nya ulinzi na usalama wanaojihusisha na vitendo nya uhalifu kwa lengo la kuwachukulia hatua za kisheria.
- (p) Kusindikiza magari ya abiria kwenye maeneo ambayo ni hatari kama vile Milima ya Kitonga Mkoani Iringa, Mapori ya Bihamulo Mkoani Kagera na Mlima wa Koro (Kondoa) Mkoani Dodoma.
- (q) Kuimarisha ushirikiano wa vyombo nya dola vyote nchini na kupanga mikakati ya pamoja ya kupambana na uhalifu nchini.
- (r) Kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa na kikanda wa Kipolisi kwa kupitia *INTERPOL*, *SARPCCO*, *EAPCCO*, *EAC* na kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine kwenye ukanda wetu na hata duniani kote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya mabadiliko ya uongozi wa juu wa Jeshi la Polisi, wananchi na wadau wengine wamejenga imani na kuwa na matarajio makubwa kwa Jeshi la Polisi. Kutohana na hali hiyo, Jeshi la Polisi linajitahidi kufanya yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi wa Polisi usiojali na kuheshimu haki za raia, Polisi kushindwa kushughulikia kero za wananchi kikamilifu na ukiukwaji wa haki za binadamu ni mionganini mwa sababu zinazowafanya wananchi kukosa imani na Jeshi hilo na hivyo kuacha kutoa ushirikiano. Kufuatia hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Jeshi hivi sasa kupambana na uhalifu nchini, wananchi na wadau wengine wanatarajia huduma ya Polisi kwao itaboreshwa. Hivyo, kazi kubwa ya Jeshi la Polisi itakuwa ni kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba wahalifu ni watu waishio mionganini mwa wananchi, na kwamba waathirika wakubwa ni wananchi wenyewe, raia wapenda amani na watiifu wa sheria wanatarajia kwamba Jeshi la Polisi litashirikiana nao kwa karibu zaidi katika kukabiliana na uhalifu. Katika ushirikiano huo, Jeshi la Polisi litazingatia utunzaji wa siri za raia wema wanaotoa taarifa za kuisaidia Polisi. Askari watakaobainika kuvujisha siri za raia hao watachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanatarajia Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa ukweli, uwazi na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Pia wananchi wanatarajia Polisi kujiepusha na vitendo vyovypote nya ukiukaji wa haki za binadamu, kama vile kutumia nguvu ya ziada kwa mtuhumiwa, kuwabambikiza watu kesi, kuchelewesha upelelezi wa kesi, kuwanyima watu dhamana ya Polisi hata kwa kesi ndogo na kuepuka itikadi na ushabiki wa vyama nya siasa. Aidha, askari Polisi wanatakiwa kujiepusha na kuwakamata wananchi siku za mwisho wa wiki bila ya sababu za msingi na kuwashikilia watu hasa wafanyakishara hata pale wanapoonyesha vielelezo vyote nya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imeanza kuchukua hatua madhubuti za kuwasimamia askari kwa lengo la kupunguza vitendo hivi na wale watakaobainika kukiuka, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanatarajia askari Polisi wa ngazi zote kujiepusha na vitendo vyote vya rushwa, hasa askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani na askari wa upelelezi. Polisi wanatarajiwa kuwa mstari wa mbele kupambana na vitendo vya rushwa, na siyo kuonekana wanashiriki kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya Wizara hii ni kuwahakikishia Watanzania usalama wao pamoja na mali zao. Katika hili, matarajio ya wananchi ni Polisi kufika mapema eneo la tukio. Sanjari na hili, wananchi wanatarajia kwamba Polisi watayashughulikia matukio yote ya uhalifu kwa ufanisi kwa kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wahalifu wote wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, inapotokea askari wamechelewa kufika kwenye tukio na hakuna wahalifu wanaokamatwa kuhusiana na tukio hilo, wananchi hubaki na tafsiri tofauti, ikiwa ni pamoja na tafsiri kwamba Polisi imeshindwa kazi au Polisi nayo inashiriki katika vitendo vya uhalifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili Jeshi la Polisi liweze kukidhi matarajio ya Serikali na ya wananchi, lazima liweshehwe. Serikali kwa upande wake, italipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi vya kutosha na kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Wananchi kwa upande wao, wanatarajiwa kulipatia Jeshi la Polisi ushirikiano mkubwa, hasa wa kuwapatia taarifa sahihi na kamilifu za uhalifu na wahalifu zitakazotumika kukabiliana na uhalifu.

Wananchi pia wanatarajiwa kushiriki kikamilifu katika kutafuta mbinu za kukabiliana na uhalifu katika maeneo yao. Pande zote mbili ni lazima sio tu zinapaswa kuwa na mawasiliano mazuri bali pia zinapaswa kuaminiana kwa kiwango kikubwa katika kufanikisha azma hii. Aidha, mambo yafuatayo yanatarajiwa kufanywa na Wizara:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Usalama wa Raia inatarajia kuanza mchakato wa kuandaa Sera ya Usalama wa Raia ambayo itaongoza pamoja na mambo mengine, mahusiano ya kiutendaji kati ya Wizara na Jeshi la Polisi, wananchi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahakama, Magereza, Usalama wa Taifa, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Uhamiaji, Idara ya Forodha, Taasisi zisizo za Kiserikali, Vyuo, Sekta Binafsi, Makampuni Binafsi ya Ulinzi, pamoja na mashirikisho ya Kipolisi ya Kikanda na Kimataifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya muundo wa Wizara ya Usalama wa Raia kuidhinishwa, hatua inayofuata ni kuangalia upya muundo na mfumo wa Jeshi la Polisi. Lengo ni kuuboresha mfumo wa Jeshi la Polisi ili kuliwezesha kukabiliana na uhalifu wa sasa kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi, jamii na utamaduni nchini na duniani kwa jumla ambapo sasa sera za utandawazi zinatawala dunia.

Mheshimiwa Spika, upo mpango wa kupunguza zaidi watendaji wanaoripoti moja kwa moja kwa Inspekte Jenerali ili kutawanya madaraka katika kanda kwa ajili ya kupunguza urasimu, kuharakisha maamuzi na kubwa zaidi ni kumpa muda wa kutosha Inspekte Jenerali wa Polisi kufikiria maandalizi ya mipango ya mikakati ya kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi. Kanda ya Dar es Salaam ni kama kanda ya majaribio; itakapofanya vizuri, zitaanzishwa Kanda nyingine na Makamanda wa Mikoa wa Kanda husika wataripoti kwa Kamishna wa Kanda.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa idadi ya Makamanda wanaoripoti moja kwa moja kwa Inspekte Jenerali ni 35, ikijumuisha Makamanda wa Mikoa na Vikosi. Huu sio mfumo mzuri wa kiutendaji. Watateuliwa Wataalamu (*Consultants*) kuchambua masuala haya yote na kutupa mapendekezo ya muundo na mfumo mpya wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakusudia pia kulifanyia maboresho Jeshi la Polisi ili muundo na mfumo wake uwe imara kutoka ngazi ya Makao Makuu hadi ngazi ya Kituo cha Polisi. Hii ni pamoja na kugawa madaraka na raslimali husika Mikoani, Wilayani na Vituoni na kukasimu madaraka ya uongozi kwa watendaji bila kuathiri udhibiti ili kuongeza ufanisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sheria zinazoongoza Jeshi la Polisi zilitungwa wakati wa ukoloni. Sheria hizo zilitungwa kukidhi mahitaji ya ulinzi na usalama wa wakoloni. Baadhi ya sheria na kanuni hizo hivi sasa zimepitwa na wakati na kuhitaji marekebisho kwani hazijazingatia kikamilifu Haki za Binadamu na hata za askari wa kawaida ndani ya Jeshi lenyewe. Lengo ni kuziboresha ili ziendane na wakati na zisikwamishe kwa namna moja au nyingine utekelezaji wa majukumu ya Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taratibu, kanuni na sheria zinazokusudiwa kupitiwa upya ni Taratibu za Kudumu za Polisi (*Police General Orders (PGO)*), Kanuni za Utumishi za Jeshi la Polisi (*Police Force Service Regulations*), Muundo wa Utumishi (*Scheme of Service*), Muundo wa Kamisheni ya Polisi.

Aidha, utawasilishwa Bungeni muswada wa Sheria kwa lengo la kuibadilisha sheria ya sasa ya Jeshi la Polisi yaani *Police & Auxilliary Services Act* na kutengeneza sheria ya Polisi yaani '*Police Act*'.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa askari wanaostaafu wakilalamikia utaratibu wa malipo ya Bakshishi (*Gratuity*). Pamoja na ukweli kwamba askari huchagua kwa hiari yake kuingia utaratibu wa Pensheni au Bakshishi, inaelekea askari hapati elimu ya kutosha ili kumwezesha kuchagua vizuri utaratibu unaomfaa. Kwa utaratibu uliopo ukishachagua kuingia katika Pensheni au Bakshishi huruhusiwi tena kubadilisha. Hivyo, kanuni zinazoongoza taratibu za malipo

ya Bakshishi na Pensheni zitapitiwa upya ili kuona uwezekano wa kuweka utaratibu mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo kwenye mchakato wa kuhamisha shughuli za uendeshaji mashtaka kutoka Jeshi la Polisi na taasisi nyingine zilizokuwa zinafanya kazi hiyo na kuzipeleka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini. Ili kuweza kufanikisha mchakato huo, Idara ya Upelelezi inahitaji kufanyiwa maboresho ili iweze kuhimili mabadiliko hayo. Maboresho hayo yatakuwa na lengo la kuweka mahusiano mazuri ya kiutendaji kati ya ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maboresho hayo pia yatalenga kumpatia Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini uwezo wa kuratibu shughuli zote za upelelezi wa makosa ya jinai zinazofanywa na taasisi mbali mbali ili hatimaye iweze kuwa rahisi kupata takwimu zote na kumbukumbu sahihi za makosa ya jinai nchini.

Aidha, utaratibu huu utamwezesha Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kuandaa taratibu zinazofanana za upelelezi zitakazotumiwa na taasisi zote (*Standard Operating Procedure*).

Mheshimiwa Spika, sanjari na hayo, Wizara yangu inatarajia kuigawa Idara ya Upelelezi katika vitengo kulingana na utaalamu wa makosa mbali mbali ya jinai. Kwa mfano, vitaundwa vitengo vya Makosa dhidi ya Binadamu, Makosa dhidi ya Mali, Uhalifu wa Kimataifa (*Transnational/Cross Border Crimes*), Makosa ya Uhujumu Uchumi (*Serious Economic Crimes*). Kitengo cha Intelijensia pia kitaimarishwa ili kiweze kutoa mchango mkubwa katika uzuijaji wa uhalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba ajali za barabarani bado ni kero kubwa na tishio kwa maisha ya wananchi, na kwa kuelewa madhara ya malalamiko ya vitendo vya rushwa dhidi ya askari wa usalama barabarani, Jeshi la Polisi limeanzisha utaratibu wa usimamizi madhubuti wa askari wa usalama barabarani. Kwa sasa Wakuu wa Polisi wa Vituo na Wilaya wanakofanya kazi askari hawa watawajibika kuwasimamia moja kwa moja tofauti na zamani ambapo usimamizi ulikuwa unafanywa na Makamanda wa Kikosi hicho.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kikosi cha Usalama Barabarani hivi sasa kinafanyiwa mageuzi makubwa. Sehemu ya mageuzi hayo inahusu maandalizi ya mtaala mpya, ambapo askari watakapoenda chuoni siku zijazo, watakuwa wanajifunza pia Sheria ya Usalama Barabarani na hivyo kila askari atakuwa na elimu hiyo. Lengo ni kuwafanya askari wote kufahamu kazi za Usalama Barabarani ili pale inapolazimu kuweza kuwabdalisha bila kulazimika kuwapeleka kwanza chuoni. Hivi karibuni Makamanda wa Polisi wa Mikoa wamepewa mamlaka ya kuwabdalili askari wa Usalama Barabarani wakati wowote watakapoona inafaa bila kulazimika kuwasiliana kwanza na Makao Makuu. Hivyo, hakutakuwa na askari wa kukaa katika kikosi hicho mpaka anastaafu, bali askari hao watakuwa wakibadilishwa mara kwa mara kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatarajia kupendekeza marekebisho ya baadhi ya Sheria za Usalama Barabarani, ikiwemo Sheria ya kutoa leseni, ambapo sasa madereva wa magari makubwa, hasa magari ya abiria watalazimika kujaribiwa upya ili kupima uwezo wao wa kuendelea kubeba roho za watu. Aidha, sifa zinazotakiwa ili mtu aruhusiwe kuendesha magari ya abiria zimepitwa upya na leseni daraja C inayoruhusu madereva kuendesha magari yote, sasa itatumika kwa kuendesha magari ya abiria tu. Aidha, tunatarajia pia kubadili leseni za udereva ili zifanane na za nchi za *SADC* zenye mfano wa kadi za Benki ambazo siyo rahisi kughushiwa.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kutunga sheria ya ukaguzi wa lazima wa magari (*Mandatory Vehicle Inspection*) yanaendelea. Vile vile, faini na adhabu kwa makosa ya usalama barabarani zinatazamwa upya kwa lengo la kuziongeza ili kuwadhibiti madereva wasio waangalifu. Aidha Wizara inatarajia kupendekeza kutungwa kwa sheria zifuatazo : Sheria ya kuwashitaki wamiliki wa magari, madereva, makondakta na abiria wanaozidi kwenye magari ya abiria; Sheria ya kuwaadhibu madereva na makondakta wanaonyanya wanafunzi na watu wengine wasio na uwezo; Sheria ya kuzuia magari kuweka vioo vya giza (*tinted*) ; Sheria ya kuwazuia madereva kuendesha magari wakati wanaongea na simu za mkononi na Sheria ya kuruhusu taasisi za Serikali, Makampuni binafsi na magereji yenyu uwezo kukagua magari kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kudhibiti magari mabovu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuongezeka kwa kasi kwa tatizo la wahamiaji haramu nchini na hali ya vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na wahamiaji hao, na vile vile kwa kuelewa kwamba upo uwezekano wa biashara haramu ya watu (*Human Trafficking*) kushamiri hapa nchini, Wizara inaangalia uwezekano wa kuanzisha Kikosi Maalum ndani ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kuboresha ulinzi na usalama kwenye vituo vyote vya kuingilia nchini. Aidha Wizara inaangalia sababu zilizofanya Jeshi la Polisi kujiondoa kwenye ulinzi wa bandari zetu na kuachia Mamlaka ya Bandari jukumu hilo. Lengo ni kurudisha ulinzi wa Bandari kwa Jeshi la Polisi kwa vile huo ni mlango wa kuingilia nchini kama ilivyo Viwanja vya Ndege na Mipaka ya nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya utalii katika kuchangia Pato la Taifa na kwa kuzingatia hali ya kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu dhidi ya watalii, Wizara inaangalia uwezekano wa kuanzisha Kikosi Maalum ndani ya Jeshi la Polisi ambacho jukumu lake kubwa litakuwa ni kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii, wanaotembelea nchi yetu, Bara na Visiwani. Mawasiliano yanaendelea hivi sasa baina ya Wizara yangu na Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wengine muhimu katika suala hili. Kwa upande wa Zanzibar, Wizara yangu inaendelea na mazungumzo na Wizara ya Biashara, Uwekezaji na Utalii kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli kwamba wahalifu wa kila namna, yakiwemo majambazi yanayotumia silaha ni watu waishio mionganii mwa jamii, utaaniszisha utaratibu wa Polisi Jamii (*Community Policing*). Polisi Jamii ni utaratibu wenye lengo la kuweka mazingira ya ushirikiano wa dhati baina ya Polisi na wananchi. Katika utaratibu huu Jeshi la Polisi litasambaza huduma zake kwa jamii kwa kutumia

askari Polisi wa Kata au Shehia kwa upande wa Zanzibar. Askari huyu atapangwa katika kata/shehia kwa utaratibu wa kudumu na atakuwa kichocheo cha mabadiliko ndani ya kata/shehia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumpanga askari Polisi katika kata/shehia kama sehemu yake ya kazi, Jeshi la Polisi litakuwa na mtazamo wa muda mrefu wa kutatua matatizo ya uhalifu katika kata/shehia hiyo badala ya kusubiri kutatua tatizo moja moja kila linapojoitokeza. Aidha, kwa utaratibu huu, raia wa kawaida atakuwa na kauli katika uwekaji wa malengo ya Polisi badala ya kuwa mpokeaji tu wa maelekezo kutoka Polisi juu ya namna ya kuzuia uhalifu.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuondoa dhana iliyokuwepo kuwa Jeshi la Polisi ni chombo cha mabavu, badala yake kuwa chombo rafiki na cha utoaji huduma. Hili litawezekana kwa kuwa na taratibu zilizobuniwa makusudi kuruhusu mashauriano baina ya Polisi na wananchi. Taratibu hizi zitawawezesha wananchi kuwaarifu Polisi kuhusu kuridhika au kutoridhika kwao na huduma ya Polisi. Kwa njia hii uwajibikaji wa Polisi kwa wananchi utaongezeka. Aidha, utaratibu huu utasaidia sana kupunguza kero ya rushwa ya Polisi kwa sababu Polisi Kata/Shehia ambaye ni sehemu ya jamii ya Kata/Shehia husika inatarajiwa hataweza kuwadai rushwa wanajamii wenzake ili atoe huduma ya Polisi maana mipango yenewe ya kazi wanapanga wote.

Mheshimiwa Spika, ili utekelezaji wa utaratibu wa Polisi Jamii (*Community Policing*) uweze kufanyika kwa mafanikio, Wizara yangu inaandaa mkakati maalum kwa lengo hilo. Mkakati huo pia utaelekeza namna ambavyo Polisi Kata atashirikiana na Vikundi vya Ulinzi wa Jadi katika utekelezaji wa utaratibu wa Polisi Jamii. Suala la kutoa elimu ya Polisi Jamii kwa wananchi na Polisi wenyewe nalo litapewa kipaumbele. Elimu hii ni muhimu sana ili kuondoa migongano baina ya wananchi na Polisi ambayo inaweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa vyombo vingine vya dola katika suala zima la ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Hivyo, Wizara inakusudia kukuza na kuendeleza ushirikiano uliopo hivi sasa baina ya Jeshi la Polisi na vyombo vingine vikiwemo Idara ya Usalama wa Taifa, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania, pamoja na wadau wengine muhimu, hasa katika ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia na kufanya operesheni za pamoja.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Jeshi la Polisi kutoa ushauri wa kiusalama kwa taasisi mbalimbali za kibiashara kama vile mabenki juu ya namna bora ya kuimarisha mifumo ya ulinzi katika maeneo yao. Kwa hivi sasa Jeshi la Polisi linaendelea kuwasiliana na Benki Kuu kuhusu kuweka utaratibu wa kisheria wenye lengo la kuwalazimisha wamiliki wa benki na taasisi za fedha nchini kuweka mifumo ya kisasa ya ulinzi katika benki zao kama *CCTV Cameras* kwa lengo la kudhibiti uporaji wa fedha katika taasisi hizo. Kwa kutambua kuwepo kwa mapungufu katika zoezi la ajira ya askari Polisi, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inachambua taratibu za ajira zinazotumika sasa ili kubuni utaratibu bora zaidi wa ajira.

Mheshimiwa Spika, upandishwaji vyeo ndani ya Jeshi la Polisi unapaswa kufanyika kwa mujibu wa maelekezo yaliyopo kwenye Taratibu za Kudumu za Polisi (*Police General Orders*). Hata hivyo, kwa kuwa yamejitokeza malalamiko miaka ya hivi karibuni kuhusiana na upandishwaji vyeo hasa kwa askari wa vyeo vya chini, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inaangalia upya utaratibu uliopo, iwapo bado unafaa au umepitwa na wakati ili askari wapandishwe vyeo kulingana na sifa na utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa tatizo la msongamano wa mahabusu katika magereza yetu na kwa kutambua kwamba msongamano huo wakati mwingine unasababishwa na utendaji usioridhisha wa baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi, Makamanda wa Polisi wa Mikoa wameelekezwa kushirikiana na wenzao wa Jeshi la Magereza katika kuendesha zoezi la kukagua magereza kwa lengo la kuelewa sababu za watuhumiwa kuendelea kukaa ndani na ucheleweshaji wa kesi zao.

Mheshimiwa Spika, itakapodhihirika hakuna sababu za msingi za kuendelea kukaa magerezani, taratibu za kisheria zitafuatwa ili mahabusu hao waachiwe ama kwa dhamana au kwa kesi zao kumalizika haraka iwezekanavyo. Zoezi hili litaenda sanjari na uendeshaji wa mara kwa mara wa vikao vya Kamati za Kusukuma Kesi Nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itawasiliana na Wizara za Katiba na Sheria, na Mambo ya Ndani ya Nchi kwa lengo la kuweka utaratibu ambaa Maafisa wa Polisi, Mawakili wa Serikali wakiongozwa na Majaji Wafawidhi wa Kanda husika na Mahakimu Wakazi wataenda magerezani kuwasikiliza mahabusu na kufanya uamuzi wa haraka kwa mujibu wa sheria. Lengo ni kushirikiana na wizara hizo kupunguza msongamano wa mahabusu magerezani, hasa kwa kesi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, ujambazi wa kutumia silaha nchini bado ni tatizo kubwa ambalo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la kuzagaa silaha. Hivyo, pamoja na juhudhi na mikakati mingine, Jeshi la Polisi litazikagua, kuziorodhesha na kuzisajili upya silaha zote za kiraia nchini ili kuhakiki umiliki na matumizi yake. Zoezi kama hili pia litafanyika kwa silaha ndogo ndogo zinazomilikiwa na Taasisi/Idara za Serikali ili hatimaye ziwepo kumbukumbu za silaha zote ndogo ndogo nchini na udhibiti wake uweze kuwa rahisi.

Mheshimiwa Spika, sanjari na uhakiki huu wa miliki ya silaha na risasi, yanafanya mapitio ya Sheria ya umiliki wa silaha ili hatimaye ifanyiwe marekebisho kwa lengo la kuongeza udhibiti wa silaha na risasi. Katika marekebisho hayo, suala la utengenezaji na miliki ya Magobore litaangaliwa kwa lengo la kuyapiga marufuku. Uzoefu umeonyesha kwamba watengenezaji na wamiliki wanakiuka taratibu za utengenezaji, umiliki na matumizi ya silaha hizo. Kwa mfano, sasa hivi Magobore mengi yanayotengenezwa yanatumia risasi za kisasa kitu ambacho ni kinyume cha sheria. Vile vile sheria za Kimataifa zimekwishapiga marufuku utengenezaji na umiliki wa silaha za aina hii.

Mheshimiwa Spika, udhibiti na utaratibu wa magobore unafanywa na Halmashauri za Wilaya/Manispaa chini ya sheria ndogo ya *Arms and Ammunition Native Authorities Regulations* ilio chini ya Sheria za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Chini ya sheria hii, Halmashauri za Wilaya ndizo zinazotoa leseni za kutengeneza magobore, kuweka alama au namba kwenye magobore yanayotengenezwa na kuwatoza kodi watengenezaji na wamiliki wa magobore.

Mheshimiwa Spika, kazi hii itaenda pamoja na juhudhi za makusudi za kuendesha misako ya mara kwa mara kuhakikisha kuwa silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria zinakamatwa pamoja na wamiliki wa silaha hizo kama moja ya mikakati ya kupunguza ujambazi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuzuia uhalifu nchini, Jeshi la Polisi linataraja kujenga ubia na sekta binafsi. Lengo ni kuwahamasisha wafanya biashara wakubwa, makampuni binafsi, taasisi na mashirika mbalimbali kuchangia na kutunisha mfuko wa Ulinzi wa Umma ambao tayari umeshaanzishwa na Jeshi la Polisi. Hili limeanza kufanyika kwa Benki ya CRDB kuchangia fedha kwa ajili ya kufungua akaunti Makao Makuu ya Polisi pamoja na Mikoani kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Jeshi la Polisi limepokea michango mbalimbali ya vitendea kazi na fedha taslimu toka kwa Kampuni za Ulinzi za *Ultimate Security Ltd, Vodacom*, Kampuni ya Simu ya *Alphatel*, Umoja wa Kampuni za Ulinzi Nchini, *Riki Hill Hotel*, Kampuni ya *CMC Motors*, Kampuni ya Sigara nchini (*TCC*) pamoja na wafanyabiashara mbalimbali.

Napenda kutumia fursa hii kuyashukuru makampuni haya na watu wote waliochangia. Ninatoa wito kwa sekta binafsi kwa ujumla, kuchangia mfuko huo kwa lengo la kuunganisha nguvu za Serikali pamoja na za sekta binafsi katika kukabiliana na uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi vilivyopokelewa ni pamoja na magari, pikipiki, simu za mkononi na simu za upepo. Mawasiliano yatafanyika na taasisi zinazohusika ili kuandaa taratibu madhubuti za matumizi ya fedha zinazopatikana kwenye mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu imekuwepo dhana kwamba kazi ya kudhibiti uhalifu na ujambazi ni jukumu la Serikali au Jeshi la Polisi peke yake. Mtazamo huu siyo sahihi. Kudhibiti uhalifu na hasa wakati huu wa utandawazi ni lazima kuishirikisha sekta binafsi, wafanyabiashara na wananchi wote kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Spika, Mzee Nelson Mandela alipokuwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini aliwahi kusema na ninamnukuu:

*“The business sector could make a valuable contribution in supporting Government in combating crime and the causes of crime by transfer of knowledge and*

*the development of skills and capacity through a public - private partnership*", mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limefungua milango kwa sekta binafsi na wananchi na kuwa wazi katika kuandaa mikakati ya ushirikiano wa hali na mali baina yao ili kwa pamoja watokomeze vitendo vya uhalifu. Tayari baadhi ya Mikoa kama vile Dar es Salaam, Arusha na Mbeya imekwishajitokeza kuchangia juhudzi za Polisi. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Mikoa hiyo.

Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa mingine kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha programu ya kupambana na wahalifu na hivyo kuwa karibu na Wakuu wa Polisi wa Mikoa yao katika kubuni mikakati na kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, ili kuufanya utaratibu huu wa sekta binafsi kuchangia shughuli za Polisi uwe endelevu na wa kisheria, Wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inawasiliana na Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili waweze kushauri namna ya kuufanya mfuko huu kuwa endelevu na wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu za mkononi yanachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la matukio ya uhalifu nchini, kwa kuwa simu hizo zimerahisisha mawasiliano kufanyika wakati wowote, mahali popote na kwa haraka zaidi. Wahalifu wameweza kutumia njia hii ya mawasiliano na kufanikiwa kufanya uhalifu bila kugundulika kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekwishaanza kushauriana na Mamlaka ya Mawasiliano Nchini pamoja na makampuni yote ya simu za mkononi, ili kuhakikisha unakuwepo udhibiti wa simu zote za mkononi, ambapo wamiliki wote wa simu watasajiliwa na kuondokana na utaratibu wa sasa wa kuuza namba za simu (*line*) kiholela. Utaratibu huu una lengo la kuweka kumbukumbu za wamiliki wote wa simu ili iwe rahisi kuwapata pindi wanapohitajika.

Mheshimiwa Spika, kazi za kupambana na uhalifu na wahalifu zinahitaji kufanywa kwa uadilifu mkubwa ili kuepuka uvujaji wa taarifa. Ili lengo hili lifanikiwe unahitajika mkakati utakaohakikisha kwamba askari Polisi hawakai kituo kimoja muda mrefu na kuzoleka. Jeshi la Polisi litaendelea kufanya uhamisho mara kwa mara wa askari wote, ili kudumisha nidhamu na kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na wananchi ni mashahidi wa juhudi kubwa zinazochukuliwa na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika kuboresha maslahi ya askari na kuwapatia vitendeza kazi. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda nimshukuru pia Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kuliangalia suala la mishahara ya watumishi wa umma pamoja na Askari Polisi ambapo mishahara yao imeongezwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kipato kidogo cha askari Polisi, inawawia vigumu kukopa katika mabenki nchini kutokana na riba kuwa kubwa na kukosa dhamana za uhakika. Hivyo, askari Polisi hawana mahali popote wanapoweza kupata fedha za kujiendezea kiuchumi. Aidha, mishahara na posho wanayolipwa askari bado haikidhi hali halisi ya mahitaji yao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza ukali wa maisha kwa askari, Maduka ya Polisi yenye utaratibu wa kuwakopesha askari mahitaji muhimu (Kantini) yatafufuliwa na kusimamiwa kwa karibu ili yaweze kutoa mikopo midogo midogo na huduma nyingine muhimu kwa askari na familia zao. Aidha, Serikali itaendelea kuwadhamini askari na watumishi wengine wa Wizara kupata mikopo kutoka Benki kama vile *CRDB, NMB, AZANIA BANCOP, BENKI YA POSTA* na makampuni binafsi, kama vile *TUNAKOPESHA Limited* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga utamaduni wa askari kujiwekea akiba kwa njia ya kuweka na kukopa, inatarajiwa kuanzishwa Chama cha Kuweka na Kukopa (*SACCOS*) cha Wizara ambacho askari Polisi watajumuika na watumishi wengine kukopa kwa masharti nafuu. Mikopo hii itawasaidia askari kustaa fu kwa heshima wakiwa na makazi yao na hali nzuri ya maisha.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha maslahi ya askari, Serikali ilipandisha kiwango cha posho ya resheni kutoka Sh.28,000 kwa mwezi kuwa Sh.50,000. Aidha, askari wanaidai Serikali Sh. bilioni 8.5 zikiwa ni stahili mbali mbali kama posho za safari na kadhalika. Baada ya mazungumzo kati yangu na Wizara ya Fedha, deni hili litalipwa katika mwaka huu wa fedha ili kuondoa kero hiyo ya muda mrefu na askari hao kupata stahili zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya askari 18,000 wa Jeshi la Polisi wanaishi nje au ndani ya makambi katika mazingira ya makazi yasiyofaa. Baadhi ya askari wanaishi katika nyumba za kupanga uraiani. Hali hii huathiri utendaji wao wa kazi kwa kiasi kikubwa. Jitihada zinafanyika ili kuhakikisha kwamba askari Polisi wote wanaishi kambini katika mazingira ya kuridhisha. Wizara yangu inafanya mazungumzo na Mifuko ya Fedha ya *NSSF* na *PPF* na Wizara ya Fedha kwa lengo la kuanzisha mradi wa ujenzi wa nyumba za Polisi nchini kote. Kwa kuanzia ujenzi utafanyika Dar es Salaam na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kujali afya za askari, hivi sasa yanafanyika mazungumzo na Bima ya Afya ili askari Polisi nao wajumuishwe katika mpango huo. Awali askari Polisi hawakuwa wamejumuishwa katika Bima ya Afya kama ilivyo kwa watumishi wengine. Mawasiliano na Mfuko wa Bima ya Afya tayari yameshaanza na mweleko ni mzuri. Baada ya taratibu zote kukamilika, askari Polisi na familia zao watanufaika kutokana na kupata matibabu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Askari ni mahali ambapo askari hupata fursa ya kueleza kwa viongozi wao, matatizo mbali mbali yanayowakabili. Hivyo, Makamanda

wote wa Mikoa, Vikosi na Wilaya wameelekezwa kuhakikisha kwamba Mabaraza hayo yanafanyika ipasavyo kwa malengo yaliyokusudiwa. Kila Kamanda wa Mkao, Kikosi na Wilaya ahakikishe kwamba Baraza la Askari linafanyika walau mara moja kwa mwezi na askari wanapata fursa kamili ya kueleza matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeandaa mpango wa mafunzo kazini ambapo askari watapatiwa mafunzo na mbinu mbali mbali za utendaji kazi. Hivi sasa walimu wa mafunzo hayo wako chuoni *CCP Moshi* wakipata mafunzo ili nao waweze kuwafundisha askari wenzao waliopo kazini. Aidha, unaandalisha utaratibu ili walimu kutoka nje ya nchi waje kuwafundisha askari hapa nchini ili kupata askari wengi zaidi wenye ujuzi. Aidha, Wizara yangu imeandaa mpango wa mafunzo ya uongozi wa askari wa vyeo vya juu wakiwemo Makamanda wa Mikoa ili kuwaongezea ujuzi kuhusu dhana ya menejimenti na ufahamu wa sera za maboresho mbalimbali yanayofanyika hapa nchini.

Ili kuimarisha maendeleo ya Jeshi la Polisi Mikoani, Makamanda wa Mikoa watashirikishwa kikamilifu katika kupanga mipango na maboresho ya Mikoa yao na kushirikishwa katika mipango ya maboresho. Matarajio ni kwamba, kila Kamanda wa Mkao ataweba kuandaa na kuitetea Bajeti yake, ikiwa ni pamoja na kusimamia matumizi mazuri ya raslimali.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Jeshi la Polisi katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Kwa ujumla utekelezaji wa malengo ya mwaka 2005/2006 ulikuwa wa mafanikio. Hali halisi ya utekelezaji kwa maeneo muhimu ilikuwa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lilikadiria kukusanya mapato ya Serikali ya jumla ya Sh.4,247,940,000 kwa mwaka 2005/2006. Hadi kufikia Aprili, 2006, Jeshi lilikuwa limekusanya jumla ya Sh. 3,825,584,105 sawa na asilimia 90 ya lengo la mwaka mzima. Hadi tarehe 31 Mei, 2006 Wizara ilivuka lengo lililowekwa kwa kiasi cha Shilingi 10,563,419.21.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi liliidhinishiwa jumla ya Sh. 102,161,080,300 kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2006, jumla ya Sh. 91,860,947,158 zilikwishatumika ikiwa ni sawa na asilimia 90 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo Tsh. 58,449,119,797 ni Matumizi Mengineyo, Tsh. 30,782,827,361 ni Mishahara na Tsh. 2,629,000,000 ni za Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali zimefikiwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na uendeshaji wa ofisi kutokana na fedha zilizotengwa katika Bajeti ya 2005/2006. Baadhi ya kazi zilizotekelwa ni pamoja na:-

Ujenzi wa nyumba 124 kati ya 131 katika Kambi ya Kunduchi umekamilika. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa maabara ya kisasa ya Uchunguzi (*Forensic Laboratory*) imekamilika. Ujenzi wa awamu ya pili ulikwishaanza na bado unaendelea. Ujenzi wa Kituo cha Polisi Katesh – Hanang, upo katika hatua za mwisho. Ujenzi wa mabweni mawili Kambi ya FFU Finya Pemba umekamilika. Ukarabati

wa mabweni mawili Chuo cha Polisi Dar es Salaam umekamilika. Mashua mbili za doria zimenunuliwa kwa ajili ya ukanda wa Bahari ya Hindi. Mashua moja iko Unguja na nyingine iko Dar es Salaam. Ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa uko katika hatua mbali mbali katika mikoa ya Tabora, Ruvuma, Mwanza na Iringa. Ujenzi wa Kituo cha Polisi Morogoro upo hatua za mwisho. Ukarabati wa Chuo cha Polisi Zanzibar unaendelea. Mafunzo ya askari wapya 2000 yameendeshwa na yalimalizika tarehe 21 Aprili, 2006. Mafunzo kazini yanaendelea kufanyika. Doria na Operesheni mbalimbali za Polisi zilifanyika Kiwilaya, Kimkoa, Kitaifa na Kimataifa ambapo nchi tatu za Afrika Mashariki zilishiriki. Mawasiliano ndani ya Jeshi la Polisi yaliendelea kuimarishwa kwa ununuzi wa mitambo, simu na kadhalika. Mkutano wa Maofisa wa Polisi ulifanyika CCP Mjini Moshi kwa mafanikio makubwa, ambapo mikakati mbali mbali ya utendaji iliwekwa na sasa inaendelea kutekelezwa. Kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, Jeshi la Polisi lilifanikisha Uchaguzi Mkuu mwezi Desemba, 2005 kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juhudzi za kupambana na janga la ukimwi ndani ya Jeshi la Polisi zimeendelea kwa mwaka uliopita ikiwa ni pamoja na kuendesha semina tatu za uelimishaji zilizohusisha Maofisa, askari na wakufunzi. Juhudi hizi zitaendelezwa mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendeleza vita dhidi ya rushwa ndani na nje ya Jeshi. Mafunzo mbali mbali kwa maafisa na askari wa kawaida yameendeshwa nchi nzima ambapo wadau mbali mbali wa mapambano dhidi ya rushwa walishirikishwa. Hatua za kinidhamu zimeendelea kuchukuliwa dhidi ya askari/maofisa wanaojiingiza katika vitendo vya rushwa au kuvunja maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyotajwa, baadhi ya matatizo yaliyoathiri utekelezaji ni pamoja na haya yafuatayo:-

Ufinyu wa Bajeti kwa kiasi kikubwa umeathiri utekelezaji wa mipango mbali mbali ya Jeshi na hivyo kutofanya kazi kwa ufanisi na tija kama inavyotarajiwa.

Upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, pipipiki, vifaa vya mawasiliano, mbwa, farasi, karatasi, vifaa vya kunasia sauti, fomu mbali mbali, mfano PF.3 na kadhalika.

Upo upungufu mkubwa wa nyumba za kuishi askari. Zaidi ya askari 18,000 wanaishi nje ya Makambi katika nyumba za kupanga uraiani na wengine wanaishi katika mazingira magumu sana makambini. Upo upungufu mkubwa wa vituo vya Polisi katika wilaya mbali mbali nchini, ambapo Wilaya 24 hazina kabisa vituo vya Polisi. Aidha, katika wilaya 73 Vituo vya Polisi viro kwenye majengo chakavu, ambapo baadhi yalirithiwa kutoka kwa wakoloni. Upo upungufu wa askari unaochangwa na askari kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa kazi, kufariki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazolikabili Jeshi la Polisi ni nyingi. Ni azma ya Serikali kuendelea hatua kwa hatua kulipunguzia matatizo na kulipatia mahitaji Jeshi la Polisi ili kulijengea uwezo wa kukabiliana na uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara inatarajia kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Kuandaa Sera ya Usalama wa Raia na kusimamia utekelezaji wake. Kuandaa Muundo mpya wa Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na kutazama upya Sheria na Kanuni za Jeshi hilo. Upatikanaji wa Ofisi na Makazi kwa Kanda Maalum ya Polisi Dar es Salaam. Kuboresha mazingira ya kufanya kazi, upatikanaji wa vitendea kazi na miundombinu.

Kuwapatia askari mafunzo mbali mbali ya taaluma zao na ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Kuimarisha Vyuo vya Polisi vya Moshi, Dar es Salaam na Zanzibar na kuanza maandalizi ya ujenzi wa chuo cha *CID Dodoma*. Kwa kushirikiana na Mifuko ya Fedha nchini na Makampuni kutoka nje ya nchi, itaaniszishwa Programu ya ujenzi wa Makambi nchini kote, kwa kuanzia nyumba za Kambi ya Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam na Ziwani Zanzibar.

Jeshi la Polisi kuendelea kushiriki kikamilifu katika maboresho ya Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme*). Kuharakisha upelelezi wa kesi ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka na hivyo kupunguza msongamano wa mahabusu katika magereza. Kupambana na uhalifu kwa kubuni mbinu na mikakati ya kisasa maeneo ya mijini, vijijini, mipakani na katika maeneo ya kitalii. Kuendeleza miradi ya maendeleo katika mikoa na Wilaya na ukarabati wa majengo ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu naomba kutoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Katibu Mkuu wa Wizara ya Usalama wa Raia Bwana Bakari A. Mahiza, Inspeka Jenerali wa Polisi Bwana Said A. Mwema, Wakuu wa Idara, Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Askari na wafanyakazi wa Wizara ambao kwa ushirikiano wao wamewezesha hotuba hii kuandaliwa na kukamilika katika wakati unaotakiwa. Aidha, napenda kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Bw. Cassian Chibogoye kwa kufanikisha uchapaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani wote ambao misaada yao imeiongezea nguvu Wizara yangu katika kutekeleza baadhi ya majukumu yake. Wahisani hao ni pamoja na Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Afrika Kusini, Misri na Uingereza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa ya *INTERPOL*, *SAFER AFRICA*, *UNDP* na *EU* na wafadhili wa hapa nchini ikiwa ni pamoja na Kampuni ya Ulinzi ya *Ultimate Security Ltd*, Kampuni ya Simu ya *Alphatel*, *Vodacom*, Umoja wa Kampuni za Ulinzi hapa nchini, *Riki Hill Hotel*, *CMC Motors*, Kampuni ya Sigara (*TCC*) wafanyabiashara pamoja na wote ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara ya Usalama wa Raia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani za pekee kwa nchi wahisani za Canada, Sweden, Denmark na Belgium na Mashirika ya UNDP na WB ambao wamechangia fedha kwenye mfuko (*Basket Funding*) wa kutekeleza programu ya maboresho ya Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme*) ambapo Wizara yangu ni mdau katika sekta hiyo. (*Makofi*)

Jeshi la Polisi litanufaika na programu hii katika maeneo ya mafunzo, kuimarisha upelelezi, marekebisho ya sheria, uboreshaji mazingira ya kazi na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba kwa heshima na taadhima Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia ya jumla ya shilingi 142,908,007,300 kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 kama ifuatavyo:-.

Mishahara (PE)	Sh. 52,728,751,000/=
Matumizi Mengineyo (OC)	Sh. 82,826,000,000/=
Matumizi ya Maendeleo	Sh. 7,353,256,300/=
<b>Jumla</b>	<b>Sh.142,908,007,300/=</b>

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA :** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA) :** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni taarifa ya kwanza ya Kamati yangu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara mpya ya Usalama wa Raia mbele ya Bunge lako tukufu, napenda kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa ushindi mkubwa alioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Rais na wabunge. Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa ushindi mkubwa alioupata kwenye uchaguzi uliopita.

Nampongeza pia Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkoo uteuzi ambao ulithibitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kipekee kabisa nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili kwa kura nyingi. Aidha nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anne S. Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vile vile pongezi mahsusni kwa Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, kwa kuchaguliwa kwao katika nyadhifa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama inampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkoo kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa. Aidha naungana na wasemaji waliotangulia kuwapongeza wale wote walio teuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi. Natoa pongezi za dhati kwa waheshimiwa wafuatao:-

Mheshimiwa Luteni Mstaafu, Yusuf Rajab Makamba, kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkoo wa CCM. Mheshimiwa Kepteni Jaka Mwambi, kuwa Naibu Katibu Mkoo Tanzania Bara. Mheshimiwa Rostam Aziz, kuwa Katibu wa Uchumi na Fedha. Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, kuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi. Mheshimiwa Dr. Asha Rose-Migiro, kuwa Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, kuwa Katibu wa Oganaizesheni wa CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumponeza tena Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkoo, kwa kuunda Wizara hii Mpya na vilevile kwa jinsi anavyoshughulikia matatizo yanayolikabili Taifa letu kama vile wimbi la ujambazi, mfumko wa bei ya mafuta, baa la njaa, tatizo la umeme na mengi mengineyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wakati Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, alipokuwa akiwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007 aliliambia Bunge lako Tukufu kuwa viwango vya Mishahara kwa watumishi walio katika vyombo vya Ulinzi na Usalama, vitapanda zaidi kuliko vile vya watumishi wengine wa kawaida. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huo wa kuboresha viwango vya mishahara ya watumishi hasa katika vyombo vya Ulinzi na Usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mbunge, Waziri wa Usalama wa Raia na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Mbunge, Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, Katibu Mkoo Ndugu Bakari Mahiza pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii; kwanza kwa juhudani wanazozifanya katika Wizara hii mpya, Pili kwa kutekeleza ushauri wa Kamati hii kwa Mwaka wa Fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, Pongezi mahsusni kwa Inspekte Jenerali wa Polisi, Said Ali Mwema, kwa kuteuliwa kwake kuwa Mkoo Mpya wa Jeshi la Polisi nchini. Kutokana

na ujuzi na uzoefu wake wa muda mrefu katika Jeshi la Polisi ndani na nje ya nchi, Kamati inaamini kuwa ataendelea kutekeleza majukumu ya Jeshi hili kikamilifu na kwa uadilifu.

Vile vile Kwa niaba ya kamati yangu napenda kumpongeza Inspekte Jenerali wa Polisi Mstaafu, Omari Mahita kwa kulitumikia Taifa letu. Kamati inamtakia afya njema na maisha marefu baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuipongeza Serikali kwa kuanzisha kanda maalumu ya Dar es salaam ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kuongeza ufanisi katika kukabiliana na wimbi la uhalifu na kazi nyinginezo. Vile vile Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi kwa juhudzi za kukabiliana na wimbi la Uhalifu na kumudu kurejesha imani ya wananchi kwa Polisi pamoja na kuendelea kuulinda Usalama wa Raia na mali zao. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa juhudzi zitaongezwa zaidi hadi kuutokomeza kabisa uhalifu uliokuwa siku hadi siku.

Vile vile napenda kuwapongeza kwa dhati maafisa wa Jeshi la Polisi na askari wote kwa utiifu wao kwa Taifa letu ikiwa ni pamoja na juhudzi za kuhakikisha usalama wa raia na mali zao. Sambamba na pongezi hizi nawashukuru na kuwapongeza wananchi wote waliojitokeza kulisaidia Jeshi la polisi kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa zinazowezesha Jeshi hilo kuzuia uhalifu. Naomba kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wanachi wengine wawe tayari kulisaidia Jeshi la Polisi. Aidha naomba kuitambua michango ya wahisani ambao misaada yao imeiongezea nguvu Wizara ya Usalama wa Raia kama alivyoeleza mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2005/2006 Bajeti ya Jeshi la Polisi ilijadiliwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi japokuwa kwa sasa Bajeti hii iko chini ya Wizara ya Usalama wa Raia. Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilipokuwa ikichambua Bajeti ya Polisi kwa Mwaka uliopita ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo kadhaa ya Jeshi la Polisi. Naomba kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa sehemu kubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuona utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, Kamati yangu ilitembelea Wizara ya usalama wa Raia na kupata maeleo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Pamoja na maeleo mengine, Kamati ilielezwu kuwa:-

Sera ya Usalama inatakiwa kuwaunganisha wadau wengine wa Ulinzi na Usalama na Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa masuala ya ki-usalama.

Njia za mawasiliano ndani ya Polisi zinahitaji kuboreshwa zaidi. Maslahi ya Askari Polisi yanahitaji kuboreshwa zaidi.

Jeshi la Polisi lina upungufu mkubwa wa askari na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Mwaka uliopita, Waziri aliieleza Kamati hii kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha

2006/2007, pamoja na kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka huo. Katika makadirio hayo kamati imeelezwa kuwa Wizara ya Usalama wa Raia inaomba kuidhinishiwa jumla ya sh 142,908,007,300/-, kati ya fedha hizo, sh 135,554,751,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*OC*) na Sh. 7,353,256,300/- kwa ajili ya Miradi ya maendeleo. Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kutafakari kwa kina, taarifa ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006, kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka wa Fedha 2006/2007 kama zilivyoainishwa kwenye hotuba ya Waziri iliyowasilishwa hivi punde.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuichambua kwa kina taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuunda kitengo maalumu kitakachohusika na ulinzi wa vyombo vya fedha. Kuhusu malindo mbalimbali Kamati pia inashauri kianzishwe kitengo maalumu kitakachohusika na malindo hayo. Sambamba na hilo, askari watakaokuwa chini ya vitengo hivi wapewe mafunzo mahsusini kwa ulinzi wa namna hiyo. Pamoja na ushauri huu ni maoni ya Kamati hii kuwa ulinzi katika vyombo vya fedha utaboreka iwapo Benki kuu itakamilisha Kanuni za kuliwezesha Jeshi la Polisi kutekeleza jukumu lake la ulinzi katika vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa askari kutokana na uwiano mdogo uliopo wa askari kwa raia. Uwiano uliopo sasa ni 1:1300 ambapo uwiano wa Kimataifa ni 1:400 – 600. Kamati inaipongeza serikali kwa hatua ilizochukuwa hivi karibuni za kuajiri askari wapya na kuongeza nguvukazi katika jeshi la Polisi.

Kamati inashauri kuwa waendelee kuajiriwa askari wapya wa kutosha ili kuziba pengo hili kubwa lililopo. Aidha ni maoni ya Kamati kuwa wanafunzi wanaohitimu katika vyuo vya Elimu ya Juu na wenye taaluma mbalimbali wahamasishwe kujiunga na Polisi ili kuwa na Jeshi la Polisi la kisasa.

Mheshimiwa Spika, kuna uhusiano wa karibu sana kati ya utaratibu wa ajira ya askari na nidhamu ya askari. Kamati inashauri kwamba, utaratibu wa kuchukua vijana wanaojiunga na Jeshi la Polisi uanzie mashulenii kama ilivyokuwa mwanzoni, sambamba na kuwaajiri vijana kutoka J.K.T mara baada ya kuhitimu mafunzo. Hii itasaidia kutambua vijana wenye uwezo na nidhamu kutokana na taarifa za walimu wao juu ya uwezo, mwenendo na tabia ya kijana anayetaka kujiunga na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofanya ziara katika vyombo vya Ulinzi na Usalama Jeshi la Polisi likiwemo, ilibaini upungufu mkubwa wa makazi ya askari jambo ambalo lina athari kubwa kiutendaji ndani ya Jeshi la Polisi. Kamati inashauri kuwa Serikali iwe na mpango maalum wa kutatua tatizo hili. Aidha Mpango wa ujenzi wa maghorofa utasaidia sana kupunguza tatizo la nyumba za askari na kuboresha utendaji kwa misingi ya kiaskari. Ni maoni ya Kamati hii kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ihamasishwe kushiriki katika kutatua tatizo hili kwa kujenga maghorofa hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhamisho wa Askari, Kamati inashauri kuwa haifai kwa Askari kukaa kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu. Aidha kila mara askari anapohamishwa au kwenda likizo alipwe stahili zake zote kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi wa majini: Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi lilijadiliwa kwa kina ndani ya Kamati. Kutokana na hali ilivyo katika maeneo hayo niliyoyataja, Kamati inashauri kuwa kuna haja ya kuongeza Boti za kufanya doria katika maziwa hayo na Bahari ya Hindi. Sambamba na hilo ziongezwe boti za doria ili kupambana na uhalifu katika maeneo ya ukanda wote wa bahari. Katika kuboresha usalama baharini Kamati pia inashauri kuwa boti zilizopo ziwekwe katika hali ya kuweza kufanya kazi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa boti hizo zinapata mafuta ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili kwa kina kuhusu hali ya kisiasa Zanzibar na Pemba baada ya uchaguzi na kubaini kuwa vyombo vyta Ulinzi na Usalama vimefanya kazi nzuri ya kuhakikisha kuwa hali ya usalama kwa ujumla imerudi kuwa sawa. Naomba kutoa wito kwa Watanzania wanaishi Pemba na Zanzibar wawaone askari kama ndugu zao na walinzi wa usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati zinaonyesha kuhitajika kwa juhudhi maalumu katika kukabiliana na uhalifu unaofanywa na raia wasio waaminifu kutoka nchi jirani. Kamati inashauri kwamba vikao vyta ujirani mwema vifanyike mara kwa mara ili kupata suluhisho la kudumu katika kukabiliana na hali ya uhalifu.

Aidha ni maoni ya Kamati kuwa Ushirikiano wa kijeshi katika operesheni maalumu, unapaswa kupewa nguvu zaidi katika kukabiliana na matukio ya kiuhalifu. Kamati inampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudhi zake za kuanzisha operesheni hizi. Ni matumaini ya Kamati hii kuwa juhudhi za Mheshimiwa Waziri Mkuu zitaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitafakari kuhusu uhalifu wa mauaji unaoambatana na imani za kishirikina, pamoja na utendaji wa walinzi katika ulinzi wa jadi (Sungusungu). Ili kukabiliana na uhalifu wa aina hii, Kamati inashauri kuwa operesheni maalumu inahitajika hususan katika maeneo husika. Hii ni pamoja na kufanya upelelezi wa kina wa kuwatambua watu na maeneo ambayo uhalifu wa namna hii unatayarishwa ili kuutokomeza kabisa.

Kuhusu mapigano baina ya wafugaji na wakulima na mapigano mengine ya kikabila. Kamati pia inaipongeza Serikali kwa hatua inazozichukua kukabiliana na changamoto hiyo. Pamoja na hivyo kamati inashauri kuwa hatua ziendelee kuchukuliwa ili kulimaliza kabisa tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, haya ndiyo maeleo ya uchambuzi wa Kamati yangu kwa muhtasari. Kama yapo maeneo mengine ambayo sikuweza

kuyagusia, natumaini Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine watayazungumzia pindi watakapopata fursa ya kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa mwaka wa Fedha 2006/2007. (*Makofi*)

Aidha, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kufanya uchambuzi wao wa kina ulioiwezesha hoja hii kufikia hatua iliyopo sasa. Naomba kuwatambua Wajumbe hao ifuatavyo, Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Kanali Saleh Ali Farrah, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. John Malecela, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Benson Mpesa, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Ibrahim Muhammad Sanya na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. (*Makofi*)

Vile vile naomba kuwatambua pia sekretarieti ya Kamati hii Ndugu Elisa Mbise na Ndugu Athuman Hussein, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa hatuna budi kumshukuru Mola wetu kwa kutuwezesha kuwepo hapa na kuwa na afya njema inayotuwezesha kuwatumikia wananchi wote wa nchi hii. (*Makofi*)

Napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004, Ibara ya 43 (5) (b) (c) na 81 (1).

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi na shukrani za dhati kwako wewe binafsi pia na kwa Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuwasahau na Wenyeviti wenu kwa kazi kubwa na nzuri katika kuliendesha Bunge hili. (*Makofi*)

Nitakuwa nimekosa hekima na busara kama nitashindwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa jimbo la Mji Mkongwe, Zanzibar kwa kura nyingi mno walizonipa katika uchaguzi uliopita. Aidha, nakishukuru Chama changu cha Wananchi (*CUF*) kwa kunithea kuwa mgombea wa kitu cha Ubunge kupitia chama hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile natoa pongezi na shukrani za dhati kwa viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kazi yao kubwa ya kuiongoza kambi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na Naibu wake Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed. Hawa ndio vinara na wapishi watakaoweza kuonesha ukomavu wao wa kisiasa wakisaidiana na watendaji wote wa Wizara hii. Iwapo wataongeza chumvi au kukinyima moto chungu, wao ndio watakaobeba dhima na dhamana sio tu hapa duniani bali hata kesho mbele ya haki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, leo ni siku muhimu sio tu kwa Wizara hii lakini kwa Watanzania wote hasa kwa vile hiki ni chombo ambacho hutoa matumaini kwa raia wote walio wema wa Taifa hili pamoja na wawekezaji wa ndani na nje, wageni na watalii wanaotembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba uteuzi wa *IGP* mpya, Kamanda Said Mwema, ni wa busara kubwa na uliozingatia vigezo vyote ambavyo hutakiwa *IGP* kuwa navyo. Uteuzi huu umekuja wakati muafaka kutokana na haja ya kuwa na kiongozi wa jeshi la polisi wa aina hiyo. *IG.P* tuliyenaye amejengeka vyema kitaaluma, kimafunzo, kinidhamu sambamba na kazi zake na hata ye ye mwenyewe anaonekana ni mkakamavu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mgema mara nyingi akisifiwa sote tunaelewa matokeo yake. Hivyo mimi binafsi na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani tunamtakia autumikie umma wa Watanzania kwa kheri na mafanikio makubwa ili kurejesha matumaini mapya.

Mheshimiwa Spika, hekima na busara iwe ndiyo ngao yake kubwa asiwe na papara na vishindo vya kukimbilia vyombo vya habari kwa mambo yasiyo na msingi, kwani hilo linaweza kumgharimu au kumuumbua kutokana na hadhi na cheo chake na hasa kutokana na uzoefu tuliuona huko nyuma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wameshuhudia matokeo mbalimbali ya uhalifu katika kipindi kifupi cha nyuma na wengi wao walianza kupoteza imani kubwa walijonayo katika jeshi la polisi. Wengine walidiriki hata kusema labda inawezekana kwamba baadhi ya askari wetu wanashirikiana na majambazi katika uhalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mmoja hii ni dhana potofu, lakini kwa upande wa pili wa shilingi pia upo uwezekano wa hayo kwa vigezo vya haraka haraka hasa kutokana na taarifa ya Jaji Mussa Kipenka ya kuchunguza mauaji ya raia wasio na hatia katika Jiji la Dar es Salaam baada ya kuteuliwa kufanya hivyo na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi kwa upande wa Zanzibar ni la kutatanisha, kwa vile wimbi la ujambazi sasa limepania kuhamia huko baada ya kuona kwamba katika Jiji la Dar es Salaam hawana nafasi tena kutokana na ulinzi madhubuti uliowekwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wiki tatu zilizopita majambazi yaliweza kupora mali na fedha taslimu zenyne thamani ya mamilioni ya fedha katika Kisiwa cha Unguja na kumpotezea raia mmoja maisha yake kwa kumpiga risasi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya wafanyabiashara wote wawili waliopatwa na mkasa huo wa kuporwa mali na fedha ni kutoka katika jimbo langu. Hivyo nachukua fursa hii ya pekee kuwapa pole kwa janga hili lisiloweza kusahaulika mara moja. Nawaomba wawe watulivu na wenye subira katika kipindi hiki kigumu wakati zoezi zima la uchunguzi wa maafa hayo likiendelea chini ya jeshi la upelelezi la polisi. Ni matumaini yetu kuwa idara hii ya upelelezi itafanya uchunguzi wa kina na kwa haraka ili kubaini chanzo cha uhalifu huu na iwapo kama hauna mkono wa askari wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa mkono wa rambirambi kutokana na kifo cha Afisa wa Usalama wa Taifa, Bwana Mohamed Bakari, aliyeuawa kwa kupigwa risasi na majambazi hayo. Tunamwombea dua *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. *Amin*. Vile vile kuwataka wafiwa wa marehemu hasa mke na watoto wake kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati muafaka kwa wafanyabiashara wakubwa na walio waaminifu kupewa vibali vyta kumiliki silaha ndogo ili wawe na uwezo wa kujihami inapotokea kuvamiwa na majambazi. Kama tatizo ni utata wa kisheria, basi sheria iliyopo ifanyiwe marekebisho au itungwe sheria mpya itakayokidhi haja kutokana na hali ya ujambazi ulivyo na usivyotabirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tungeomba bandari mbili muhimu zinazotumika kupokelea abiria na bidhaa Zanzibar, kwa kutumia boti ziendazo kwa kasi, meli na majahazi zipewe ulinzi madhubuti ili kuhakikisha silaha hazipati nafasi ya kuingizwa katika Wisiwa vya Unguja na Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bandari zenyewe ni ya Malindi iliyopo Mjini Unguja na bandari ya Mkokotoni iliyoko katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Zoezi hilo lisiishie Unguja peke yake ila na katika Kisiwa cha Pemba ambako upo uwezekano wa kupenyeza silaha kutokea katika bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo ni lazima ukaguzi wa kina kwa abiria na bidhaa ufanyike katika bandari zote mbili kwa upande wa Tanzania Bara nazo ni Dar es Salaam na Tanga kabla ya kuelekea Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wafugaji hasa wa mifugo ya ng'ombe mara nyingi huvamiwa na majambazi na kunyang'anywa mifugo yao au hata kuuawa. Tabia hii imejengeka zaidi katika maeneo ya wafugaji walio karibu na mipaka yetu na nchi jirani. Hivyo Jeshi la Polisi likae na kuandaa ni mikakati gani ya kuwasaidia wafugaji hao kuondokana na kero hii ya siku nyingi. Wafugaji nao ni raia na ng'ombe zao ni mali ya Watanzania. Hivyo ulinzi usiishie mabenki na kwa wafanyabiashara peke yake, ni wakati muafaka kwa

wakulima kupatiwa ulinzi wa kudumu au hata kupatiwa silaha kwa vile majambazi hayo hutumia silaha nzito wanapovamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba kwa dhati kabisa kama wito ulivyotolewa na Jeshi la Polisi kwamba raia wote walio wema kutoa taarifa na vielelezo kamili vy a wahalifu popote pale walipo ili waweze kudhibitiwa mara moja na katika wito huu ni vyema kwa raia wote kuwa waangalifu kwa kutopeleka watu wasiohusika au kutopeleka visu au mapanga yenye rangi mbalimbali na kutaja mtu au kundi fulani la watu linahodhi silaha hizo na kuhusika na ujambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ujambazi hauna rangi wala jinsia, sio dini wala kabilia ila ni tabia mbovu tu zinazo mfanya mtu kuwa jambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu misaada kwa jeshi la polisi, Tanzania itaendelea kuheshimu misaada mbalimbali inayotolewa na wafanyabiashara wa ndani na ni vyema wakapongezwa kwa misaada yao hiyo na kuwataka waendelee kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti kwa Wizara hii, tunaomba ni vyema jeshi la polisi liwe makini na kutokaribisha misaada kutoka kwa wafanyabiashara. Tunapotoa tahadhari hii tunafikiri hakuna hata mmoja kati yetu asiyeelewa ubaya wa kukaribisha wafanyabiashara au watu binafsi kuingiza mikono yao katika jeshi la polisi. Chombo hichi kiachwe na kijitegemee kiutendaji na wengi wetu tunajua vizuri kwamba kama kupokea misaada kwa vyombo vyetu vy a ulinzi basi iwe baina ya nchi na nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo kutaepusha wafadhili kuingiza mikono yao katika vyombo kama hivi vinavyolinda sheria za nchi. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwa ni bora wafadhili hao wakaelekeza misaada hiyo katika sekta za elimu, afya na nyinginezo na kwa kufanya hivyo Serikali itapunguza bajeti za sekta hizo na kuelekezwa katika vyombo vyetu vy a kulinda sheria. Jeshi la Polisi liachwe lifanye kazi kwa kupatiwa mahitaji yao yote toka Serikalini na si vinginevyo kwa usalama wa nchi na raia wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhhibit Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka wa fedha 2002/2003 kumekuwa na ongezeko la watumishi wasiochukua mishahara yao hadi kufikia shilingi 500,636,412/=. Hili tunaomba Serikali itueleze ni kwa nini watumishi hawachukui mishahara yao au kuna watumishi hewa ambao Serikali imekuwa ikiwatengea mishahara?

Mheshimiwa Spika, aidha, katika taarifa hiyo hiyo inaonyesha upotevu wa fedha taslimu na vifaa vy a stores kwa pamoja vyenye thamani ya shilingi 2,913,644,926/=. Hapa Kambi ya Upinzani na Watanzania wote wanakuwa na mashaka kama kweli Jeshi hili la Polisi kwa upande mwengine linaweza kuupiga vita na kuutokomeza ujambazi wa kutumia taaluma ambao unasemekana kuendelea katika idara nyingi za Serikali na

mashirika ya watu binafsi na kama ni hivyo kwa nini basi jeshi lenyewe linashindwa kudhibiti wizi unaotoka katika nyumba yake?

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mabenki yetu mengi nchini kiulinzi ni dhaifu. Hivyo ni vyema wamiliki wake wakabanwa kisheria ili waimarishe ulinzi katika taasisi hizo na sio kweli kwamba wateja wao wataogopa kuona ulinzi wa kisasa umeimarika katika mabenki na kuwafanya wasiende kupata huduma katika benki hizo. Nafikiri itakuwa ni kinyume chake kwa vile wengi wa wateja watajiona wako salama zaidi na fedha zao wanapokwenda kupata huduma katika mabenki hayo yanapokuwa katika ulinzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tukubali kwamba mbali na yote niliyosema lakini askari wa jeshi la polisi wanaishi katika mazingira mabaya sana na ya kukatisha tamaa. Ni muda mrefu askari hawa wamesahauliwa na kuachwa wanatangatanga kama vile ni mayatima na sababu kubwa zinazotolewa ni kwamba hali ya uchumi ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, lakini ni vyema tukaelewa kwamba uchumi wa nchi yetu ama uwe mbaya au uwe mzuri au wenye kuimari, basi mhusika mkuu katika ulinzi wa uchumi huo ni askari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inawezekana labda baadhi ya askari wetu hujiingiza katika vitendo viovu visivyokwenda na taratibu za kazi zao kutokana na vipato vyao kuwa vidogo. Ingawa hatakiwi kufanya hivyo kisheria lakini hayo yanatokana na kutomtengenezea posho nzuri na mishahara inayokwenda sambamba na hali ya maisha na vitendea kazi vya kisasa. Ni dhahiri askari ye yeyote katika jeshi lolote, kukosa vitendea kazi ni sawa na kumchukua mvuvi ukampeleka baharini bila ya kumpatia nyavu na zana nyingine za uvuvi. Usitegemee mvuvi huyo kurudi hata na dagaa, seuze nguru au papa. Hivyo basi, tunaomba kuwe na mikakati ya kulipatia jeshi la polisi vifaa bora na vya kisasa katika suala zima la ulinzi, sambamba na posho zao na mishahara kuwa mizuri tena itakayotolewa kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa njia moja ama nyingine baadhi ya matatizo niliyoyaeleza hapo juu katika jeshi letu la polisi yamesababishwa na baadhi ya matumizi yasiyofuata sheria na mpangilio wa umuhimu wa mahitaji. Hii imeonyeshwa katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuwa kiasi cha shilingi 198,211,685/= (*nugatory expenditure*) zilitumika kienyeji tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe maelezo ya kutosha kutokana na matumizi haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, askari kubaki kambini ni haki yao na ndipo nidhamu kamili itakapoweza kupatikana. Leo hii nyumba wanazoishi askari wetu hazina viwango kamili vinavyotakiwa mwanadamu kuishi. Ni nyumba chakavu na baadhi ya nyumba hizo haziwezi tena hata kukarabatiwa. Hivyo huu ni wakati muafaka wa kujenga nyumba bora tena zikiwemo za maghorofa kwa ajili ya askari wetu. Hii itasaidia matumizi bora ya ardhi na kulinda vyema mazingira yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, askari kuishi uraiani ni moja kati ya mambo yanayoweza kumpelekeea kushawishika na kujingiza katika mambo yanayokwenda kinyume na taratibu za kazi zao. Tatizo hili la ukosefu wa nyumba za kuishi ni la nchi nzima na kwa pande zote za muungano yaani Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, uhamisho kwa askari ni jambo muhimu sana na la kuzingatiwa na zoezi hilo lifanyike kwa nchi nzima. Askari kubaki katika kituo kimoja kwa muda mrefu ni kosa lingine linaloendelea katika jeshi hili. Baadhi yao hudhani kwamba vituo ni mali zao na kujenga ufalme au udikteta hivyo hupunguza ufanisi wa kazi zao na kuna taarifa kwamba wengine hudiriki kuvitumia vituo kama vile ni vitega uchumi vyao. Uhamisho uendelee kwa ngazi zote kuanzia juu hadi chini na kwa nchi nzima kuanzia Bara hadi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, askari ingawa wamepata baadhi ya haki zao lakini bado hali ya maisha yao ni duni ukilinganisha na upandaji wa bei za bidhaa zilivyo na hili hakuna asiyeelewa. Kuongeza viwango vya posho kutoka shilingi 28,000/= na kufikia shilingi 50,000/= kwa mwezi bado ni danganya toto kutockana na kazi zao na hali ya maisha ilivyo. Kambi ya Upinzani inapendekeza kiwango hicho kipande na kufikia posho ya shilingi laki moja kwa mwezi ili upatikane ufanisi mzuri wa kazi zao za kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua madeni iliyokuwa nayo katika jeshi hili mwaka huu imetenga shilingi bilioni 8.5 ili iweze kulipa malimbikizo mbalimbali ya madeni yakiwemo ya usafiri, uhamisho na mengineyo. Lakini itakuwa ni vyema Wizara hii mbali na kutoa hundi hizo za malipo pia iambatanishe na barua za kuwaomba radhi kwa kuwacheleweshea malipo hayo kwa wakati mwafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inadhani huu ni muda mwafaka kwa *IGP* mpya kusafisha uozo uliokuwepo ndani ya jeshi hilo, kwani inaonyesha jeshi hilo lilikuwa katika mfumo usiokwenda na taratibu nzuri. Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha malipo ya posho ya shilingi 176,947,000/= yalifanyika kwa watumishi lakini hakuna uthibitisho kuwa watumishi hao walipokea. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni vipi kiasi kama hiki cha fedha za walipakodi kichezewe na watu wasio waaminifu na uchungu wa nchi yetu na hatua gani zimechukuliwa dhidi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taaluma ni kitu muhimu kwa askari wetu. Kuna tabia iliozoeleka kwamba wale wote ambao kwa sababu moja au nyingine hawakupata nafasi ya kuendelea na masomo yao ya sekondari au ya juu ndio hao wanaoajiriwa katika jeshi hili. Sio vibaya kufanya hivyo kwa kutoa ajira hiyo, lakini sasa wakati umefika kuwa na askari walio na kiwango kizuri cha elimu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema basi hasa kwa askari wa Idara ya Upelelezi kupatiwa taaluma hiyo kwa kiwango cha hali ya juu ili waweze kufanya kazi zao

kisayansi na hata kuwa na maabara za kisasa za kufanyia uchunguzi kwa baadhi ya makosa ya jinai kama nchi za wenzetu wanavyofanya. (*Makofi*)

Vile vile ni muhimu askari kupewa elimu ya sheria kutokana na raia kupata usumbufu wa kupachikiwa kesi zisizo na kichwa wala miguu, matokeo yake kesi inapopelekwa mahakamani askari huonekana hawakutumia vigezo na taratibu za kisheria na inakuwa ni usumbufu kwao na kwa raia wasio na hatia kwa vile hatimaye kesi hufutwa kutokana na kukosa ushahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi vile vile lijiandae kuwa na hospitali na madaktari wao tena wa kutosha. Hii itasaidia kuwaondolea usumbufu wakati wanapotaka kupatiwa matibabu wao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, aidha, hili litasaidia kwa watuhumiwa walio chini ya ulinzi wa polisi kupata matibabu katika hospitali hizo na hivyo kuondoa uwezekano wa kuvurugwa kwa upelelezi. Mfano mzuri wa kuigwa ni *JWTZ* na askari wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani nazo ni tishio katika nchi yetu. Ajali nyingi hipoteza maisha ya watu wetu, hivyo askari wa usalama barabarani wawe macho kwa kuyakagua magari ya abiria na kwamba yanapata vibali vilivyo halali vyta kutembea barabarani na kwa kiwango kinachohitajika. Magari mengine ni chakavu mno, matairi kukosa viwango, gari kukosa taa za kuonea au za ishara (*indicators*) au mengine kubeba abiria zaidi ya uwezo wa gari lenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano hai ni wa ajali mbili za hivi karibuni zilizotokea katika mkoa wa Arusha na Kagera na kupoteza maisha na kujueruhi watu kadhaa kutokana na uzembe wa kupakia abiria wengi kuliko uwezo wa gari lenyewe linavotakiwa kubeba kisheria.

Mheshimiwa Spika, lakini juu ya yote hayo kuna taarifa kwamba baadhi ya askari wa usalama barabarani wanakuwa na tabia ya kuomba bakhshishi, tabia hii inasemekana imeshamiri kwa kiasi fulani. Hivyo wawe makini kwa hilo kwani usalama barabarani uko chini ya dhamana yao na uchunguzi ufanywe na kwa wale watakaobainika na kujihusisha na tabia hii waondolewe haraka iwezekanavyo ili kuepusha kuambukiza wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya madereva huendesha magari ya abiria kwa mwendo wa kasi hivyo kushindwa kuyadhibiti wakati linapotokea jambo la dharura barabarani na kuwapelekea kusababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, hivi hebu tujiulize ile sheria tuliyopitisha katika Bunge lako Tukufu juu ya vidhibiti mwendo imefikia wapi? Au tukubaliane na zile taarifa zilizokuwa zikitolewa na baadhi ya watu kwamba ule ulikuwa ni mradi wa mtu binafsi ni za kweli? Sheria kama zipo zifuatwe na kama inaonekana hazisaidii basi zifutwe ili utafutwe utaratibu mwengine wa kupunguza ajali katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kiasi cha shilingi 2,708,791,960/= ambazo zilitakiwa kukusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali katika jeshi la polisi na makusanyo haya hayakufanyika kama ilivyokusudiwa. Mara nyingi Kambi ya Upinzani imelipigia kelele suala hili la faini mbalimbali zinazotozwa na askari wa usalama barabarami kutowasilishwa ofisini na hivyo kuwa chanzo cha jeshi kukosa mapato. Hivyo tunamuomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako hili ni kwa nini na atwambie wahusika wa hili wamechukuliwa hatua gani za kinidhamu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ni lazima yaboreshwe kwa kupatiwa *radio call* za kutosha kwa askari wa jeshi hili. Hii itasaidia kurahisisha mawasiliano kati ya askari au kikosi na vituo, wakati wanapotaka msaada wa ziada pindi dharura inapotokea. Sambamba na hilo lakini uwepo utaratibu mzuri wa kupatiwa simu za mikononi kwa njia ya mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, usafiri ni jambo muhimu kwa askari wengi wanaoishi uraiani. Baadhi yao hucheleva kufika kazini mapema kama inavyotakiwa na vile vile huadhirika kwa kukosa hata nauli za kuwafikisha kazini. Hivyo ni bora wakapatiwa nauli ya kwenda na kurudi kazini kutokana na hali halisi ilivy. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Wizara hii ni lazima imchukulie hatua za kinidhamu askari ye yeyote anayelazimisha kupata usafiri kwa kutumia nguvu katika magari ya abiria hasa daladala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo limeripotiwa mara nyingi katika vyombo vya habari na ni kwa nini watumishi wa Wizara za Ulinzi tu ndio wanaoripotiwa kufanya vitendo hivyo? Kwani katika nchi hii hakuna watumishi wengine wanaokwenda na kurudi kazini kwa kutumia usafiri wa umma na wa kawaida? Mbona hatujasikia mwalimu au daktari au hata watumishi wengine kufanya vitendo kama hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ajira katika jeshi hili ni vyema ikatolewa kwa vigezo vinavyotakiwa na visivyohusisha ubinafsi au itikadi za kisiasa hasa katika wakati huu wa mfumo wa vyama vingi na uangaliwe utaratibu mzuri zaidi wa kuajiri vijana kutoka pande zote mbili za Muungano, ili kuondoa manung'uniko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu bima kwa askari, suala la bima limekuwa tatizo sugu kwa jeshi hili. Hivyo mashirika mengi ya bima hukataa kuwaandikisha askari katika bima kutokana na kiwango chao cha mshahara kuwa kidogo. Ni vyema basi kama bado tatizo hilo linaendelea basi Wizara iangalie taratibu nyingine za kuwakatia bima angalau kwa baadhi ya askari kwa gherama za Wizara na kuzingatia zaidi kwa wale askari ambaa hupelekwa katika maeneo hatari hasa katika vita hii dhidi ya ujambazi na biashara ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, michezo ni muhimu katika jeshi. Tunalipongeza jeshi hili kwa kuwa na timu za mpira wa miguu, netiboli na riadha zinazoshiriki katika ngazi ya Taifa. Ni vyema basi ukaandaliwa utaratibu mzuri wa kupatiwa vifaa vya kisasa vya

michezo. Hili litasaidia kuwaweka askari wetu kuwa wakakamavu katika michezo badala ya kukaa bure na kuijingga katika mambo yasiyofaa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga kiasi kizuri cha fedha kwa ajili ya kununulia vifaa vya michezo vya kisasa na kutumika katika jeshi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, UKIMWI ni jambo lingine linalowasumbua wanadamu hapa nchini na dunia nzima kwa ujumla na kwa kuzingatia kuwa asilimia kubwa ya waathirika ni vijana, ni vizuri basi askari wakapewa mafunzo ya kina na ya mara kwa mara katika kujilinda na ugonjwa huu. Hii itasaidia kuwaweka katika tahadhari ya kuijingga katika janga hilo. Kupoteza askari aliyefundishwa na kupokea mafunzo mpaka kuwa askari kamili ni zoezi ambalo lina gharama kubwa na hivyo inakuwa ni hasara kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, dawa za kulevyaa ni hatari kubwa kwa nchi yetu. Mikakati iandaliwe sio tu kwa kuwasubiri waletaji wa dawa hizi katika viwanja vyetu vya ndege au bandarini. Ni wakati muafaka sasa kwa askari wetu wa upelelezi kuwatafuta wafanyabiashara wakubwa wanaohusika na biashara hii haramu. Sambamba na hilo Serikali itoe kiwango kizuri cha zawadi kwa wale wote watakaotoa taarifa za kweli zitakazopelekea kuwakamata na kuwapeleka katika vyombo vya sheria kwa wote watakaohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la kushangaza ambapo vifaa vya thamani ya shilingi 5,499,500/= vilivyonunuliwa na Tume ya Kudhibiti Dawa ya Kulevyaa havikuonekana katika stoo na hakukuwa na maelezo iwapo vifaa hivyo vimetumika au la. Hii ni hatari sana kutokana na umuhimu wa kitengo hiki katika Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ni wapi vifaa hivi vilipo na kama vimekwisha tumiwa ni katika utaratibu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara hii kuchukua tahadhari kubwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere na hasa kwa vile hili ni eneo nyeti na kuna taarifa kwamba baadhi ya askari wasio waaminifu hueningilia kazi za Idara ya Uhamiaji na Upekuzi mizigo.

Mheshimiwa Spika, hili ni kosa kubwa la kiutendaji hasa ukizingatia kwamba kila mmoja kati ya walinzi waliopo kiwanjani hapo wamepangiwa kazi maalum.

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika ili wale askari ambao hujidai kuwa wasindikizaji wa abiria au kuwapa msaada wa kuwapitisha maeneo ya usaili kwa pasi zao (*immigration*) au kupitisha mizigo yao kwa upande wa *customs*, wachukuliwe hatua za kupewa onyo na siyo vibaya hata kupewa uhamisho iwapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo haya hufanyika zaidi wakati ndege kutoka Dubai na India zinapowasili. Sio vyema tukakaa kimya kwani baadhi ya abiria wanaosafiri katika

ndege hizo ni wafanyabiashara haramu wa madawa ya kulevy. Ingawaje hadi sasa Kitengo cha kuzuia madawa ya kulevy kinastahili pungezi kwa kazi nzuri wanazofanya kiwanjani hapo, na tunawataka wazidishe juhud zaidi katika suala zima la kuzuia madawa ya kulevy; na wasiwe tayari kuingiliwa katika kazi zao na baadhi ya hao askari wasiohusika na kazi hizo kiwanjani hapo.

Mheshimiwa Spika, kundi hili dogo la askari waliotawaliwa na tamaa na kujifanya ndio wamiliki wa kiwanja hicho wapewe uhamisho mara moja kwa usalama wa nchi na kwa bughudha wanazopata wasafiri hasa wafanyabiashara wanapowasili nchini. Inasemekana kwamba baadhi ya askari hudai hata stakabadhi za malipo wanayofanya wafanyabiashara mara wanapomaliza kufanya malipo hayo halali kwa upande wa *custom*, kazi ambayo haiwahu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu polisi na siasa, kwa kumalizia naomba sasa niongezee mawili, matatu kuhusu taratibu nzima ya jeshi letu la polisi katika mfumo huu tulionao wa vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kwa dhati kabisa jeshi hili lisiingizwe na lisijiingize kabisa katika suala zima la siasa. Siasa ibakie katika mikono ya wanasiasa na kila mwanasiasa atakayechaguliwa kwa kupata kura halali aachwe kuongoza katika eneo lake aliloomba kupewa kura na wananchi. Hivyo basi, tukubali kwamba kila askari tena kwa vikosi vyote wasiwe na ushawishi wa nani anafaa kuongoza na nani hafai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, askari anatakiwa awe mwaminifu kwa kila kiongozi anayechaguliwa kuongoza na kuondokana na kushabikia siasa jambo ambalo linaweza kuleta chuki, fitina na hata mfarakano katika jamii. Huo ni ushauri wa bure na uliojaa busara kama ni kweli tunataka kujenga utamaduni bora wa kupishana katika madaraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo basi na tushindane kwa sera, tugombane kwa hoja na baadaye tuwaachie wananchi na hasa wapiga kura waamue ni nani anayefaa kuwaongoza na achaguliwe kwa njia ya kupiga kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuwa na tahadahri kubwa ya kutoviingiza vyombo vyetu vyote vya ulinzi katika nyanja za siasa, hasa kwa nchi kama yetu inayoamini kwamba amani ndio msingi wa maendeleo yetu, basi lazima tuheshimu ule msemo unaosema *prevention is better than cure*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwanza nikupongeze kwa leo kuwa nadhifu zaidi isivyo kawaida, hivi leo ndiyo bado Waziri Kivuli, je, ungekuwa Waziri kamili sijui ungekuwaje. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, orodha ni wachangiaji ni 25, kati yao 16 ni kutoka Zanzibar na tisa ni kutoka Bara. Sasa ningeruhusu moja kwa moja kwa jinsi orodha ilivyokuja hata mmoja wa Bara asingeongea kitu ambacho kisingekuwa tena sahihi, kwa hiyo, hawa 11 ambao pengine wataweza kusema nimepanga kwamba Waheshimiwa Wabunge saba watoke Visiwani kwa uwiano huo huo walivyoomba na wanne watoke Bara kwa mchanganyiko huo. (*Makofi*)

Sasa orodha yangu inasema Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbii, nampa heshima ya kuanza yeye atafutiwa na Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan Mbunge wa Kinondoni, halafu Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Abdallah Sumry, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, baada ya hapo ni Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu na pengine tutamfikia Mheshimiwa Emmanuel Luhahula na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa. (*Makofii*)

Kwa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, wakati huo Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, ajiandae.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii leo na mimi nichangie katika Wizara hii ya Usalama wa Raia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukupongeza wewe wa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika, kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia, pia nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa busara yake kwa kumteua Mheshimiwa Margaret Sitta, kuwa Mbunge na kuwa Waziri kwa sababu kuwepo ye ye hapa katika Bunge hili Mheshimiwa Margaret Sitta kunairahisisha ile *Standard and Speed* kuwa nzuri zaidi. (*Makofisi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza Serikali kwa kuongeza mishahara ya wananchi wote wa Tanzania, lakini pia napendekeza kabla Serikali haijaongeza mishahara ifanye utafiti kwanza wa hali halisi ya nchi na uteremkaji wa thamani ya fedha yetu ya Tanzania. Kisha hapo hapo katika nyongeza za mishahara ya raia pia ningependelea zaidi kwamba askari wapewe asilimia kubwa ili waondokane na mabalaa haya wanavoshutumiwa nayo ya kula rushwa au kutesa wananchi. (*Makofii*)

Kama Msemaji wa Upinzani alivyosema kwamba askari wana hali mbaya na wanajiingiza katika matatizo kwa sababu mishahara yao ni midogo na kwa sababu hali ya uchumi ni mbaya kwa hiyo, utakutana na askari anahangaika kupata milo yake mitatu ya kila siku. Kwa hiyo, hata katika nyongeza za mishahara hii iliypita mara hii ningependekeza basi askari labda wapewe zaidi kuliko raia wa kawaida. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo kalizungumza Msemaji wetu wa Upinzani ni juu ya makazi ya askari. Mimi nilipita Buguruni nikaonyeshwa kwamba hii nyumba anakaa afisa mmoja wa polisi wa ngazi ya juu sana, nyumba hiyo ilikuwa mbali ya sura yake mbaya huko nje ya kuwa ni nzee na chakavu, lakini madirisha pia ya nyumba ile yalikuwa yananing'inia yaani karibu ya kuanguka, ye ye mwenyewe pengine hana uwezo wa kuitengeneza nyumba ile kwa sababu mshahara wake ni mdogo lakini pia

Serikali kwa nini isiangalie nyumba kama zile hasa ya Afisa Mkuu wa Polisi, isitengenezwe ikaonekana hadhi yake inafanana fanana na pale anapoishi.

Mheshimiwa Spika, pia Buguruni mpaka leo kuna vibanda vile vyatya mabati waswahili wanaviita *full suit*, wanakaa mle polisi, sasa mimi najiuliza hawa wakitaka kwenda msalani wanakwenda wapi?

**MBUNGE FULANI:** Hawaendi!

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Hawaendi eeh! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili napenda kuwapongeza Wizara hii kwa jinsi wanavyochukua hatua za kupambana na majambazi. Wizara inastahili kusifiwa na Waziri pia wapewe nishani za kubuni mambo haya ya kupambana na majambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na majambazi nilikuwa napendekeza wawemo watu wengine wa kusaidia kupata siri ya nani ni majambazi na watu hawa ni wale Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Wenyeviti wa Kata kwa sababu hawa katika sehemu zao wanazoishi wao pia ni Wenyeviti wa Mabaraza ya Usalama.

Kwa hiyo, wao wana kazi pia ya kujua majambazi ni nani wapewe kazi hii ili nao washirikiane na Wizara kuwafunua majambazi, hawa wanaweza kutufanya kazi nzuri zaidi na ikaleta mazao.

Pili, washirikishwe pia wenye vilabu, watu wenye vilabu wanakuwa wao wanajua siri kubwa sana ya majambazi. Kuna *club* moja sitaitaja katika Bunge hili lakini Waziri akitaka aniite faragha nitamweleza jina la *club* hii, *club* hii ndiyo maficho makubwa ya majambazi ikifika saa mbili usiku *club* hii wana - *tape* taarifa ya habari inalia ile ngoma ya taarifa ya habari halafu inasema hivi sasa ni saa mbili kamili, ifuatayo ni taarifa ya habari wanai *tape* ile. Kisha wanaendesa mambo yao ya *club* ya kuuza pombe ikifika saa nane wakati wanywaji wameshachokachoka au saa sita au saa saba basi unaona mbona watu wanaanza kupungua wanaiweka ile kaseti sasa inasema ile kaseti kwenye redio hivi sasa ni saa mbili kamili. Walevi wanasema alah, kumbe baaado! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi wanavutavuta majambazi bila shaka hawa wenye *club* hii wanashirikiana na majambazi kuwaambia bwana kaeni msiondoke wananchi watakunywa hapa na ninyi mtajificha ikifika saa yao ya kwenda kufanya ujambazi wanaondokea hapa kwenye *club*.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inatisha sana na iko Dar es Salaam na kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri ningependa kumweleza iko wapi.

Lingine napenda kumpongeza Waziri katika ukurara wa 46 *paragraph* ya 89 alivyosema naomba kwa ruksa yako nim-*qoute*:-“Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itawasiliana na Wizara ya Katiba na Sheria na Mambo ya Ndani ya Nchi kwa lengo la

kuweka utaratibu ambao Maafisa wa Polisi, Mawakili wa Serikali wakiongozwa na Majaji na Wafawidhi wa Kanda husika na Mahakimu Wakazi wataenda Magereza kuwasikiliza Mahabusu.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hii itakuwa ni hatua nzuri sana hasa pale sisi tulishtuka sana wengine, Waziri wa jana alipokuwa akiwasilisha hoja yake alipokuwa akisema huku hakuna maovu yanayofanywa hasa katika kosa la kujamiiana. Lakini hawa walioambiwa hapa waende naomba Wizara hii itushirikishe na sisi Upinzani ili kwani maswali tutakayowauliza wale mahabusu kuwa je, wanafanyiwa nini huko ndani. Halafu tena dhambi zitakuja hapa zinaweza kuchukuliwa hatua na Wizara hii ili yasitokee mambo haya ya kujamiiana wanaume kwa wanaume magerezani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumze juu ya uhusiano wa raia na askari. Waziri na Naibu Waziri wote mimi nafahamu waliwahi kwenda kusoma Ulaya na kuishi huko japo kwa muda mfupi, wao wanajua uhusiano kati ya raia na askari. Raia anapofikwa na shida yoyote Ulaya mfano anapopotea njia mtu wa kwanza wa kumkimbilia ni askari lakin sisi hapa Tanzania askari hatuna uhusiano nao wa aina hiyo, askari ni mtu anayetisha, ni mtu anayekimbiwa na mtoto ukitaka kumtisha anywe dawa kwanza unamwambia nitakuitia askari sasa hivi aje kukukamata kwa sababu askari si watu wazuri maana inatoa hisia kuwa wao ni watu wabaya sana na ni watu wa kuogopwa.

Mheshimiwa Spika, hasa tukienda kule kwetu Pemba, kule kwetu Pemba askari ni *bad news*, afadhalii hapa Dar es Salaam, askari ni wazuri lakini kule kwetu Pemba narudia tena kuwa askari ni *bad news*. Laiti ingekuwa inawezekana kupendekeza kuwa askari kule Pemba sisi hatuwataki kwa sababu wanatukosesha raha kule wanapiga watu, wanaumiza watu kwa jambo lililokuwa halina maana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, askari usiku wanatembea barabarani kazi yao ni kulinda usalama, akikuona askari usiku barabarani basi atakutesa, atakuadhibu na sisi kwetu tuna mila ya kwenda Msikitini na tukirudi Msikitini mara nyingi watu hukaa barazani wakazungumza. Kukaa nje usiku mabarazani tukapiga soga au kucheza karata ni njia moja sisi kwetu Pemba ya *family planning* kwa sababu sisi hatupendi sana haya mavidonge au mambo mengine ya uzazi wa majira kwa hiyo sisi tunakaa nje kuzungumza ili ukirudi nyumbani mkeo kashalala huwezi tena kumsumbuu maana ananyonyesha mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri awaeleze hawa Askari basi kuwa kule Pemba *family planning* moja ni kukaa nje tukapiga soga, wasiwa- *harass* watu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wakati mwengine mambo mengine pia yanafanywa usiku kama uvuvi maji yanakuwa na *time* yake, siku moja kulikuwa na jamaa walikuwa wanakwenda kuvua samaki na karabai zao na nyavu zao basi askari wakawakamata wavuvi wale, sasa jamani uende saa ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri kwamba askari Pemba hatuwataki ni *bad news* dhana ya ujambazi Pemba ni dhana mpya, ni dhana mpya kabisa sisemi kwamba

hakuna Wapemba majambazi lakini ujambazi wao pengine wanafanyia Bara huku, lakini kule ujambazi haupo sasa tatizo ni nini askari kututesa?

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuchangia ni askari hawa wanaovaa nguo nyeupe tunawaita yange yange, pia nao ni *bad news*. Ukishuka Mkoani mpaka Chake Chake utasimamishwa mara 1,000 na pengine kwa kisababu kidogo wewe umechoka umelala melini unataka ufile kwako huwezi kufika unasimamishwa tu kinachotafutwa na askari hawa hatukijui.

Mheshimiwa Spika, naomba niende haraka haraka kengele ya pili isije ikanigongea.

Lakini lingine napendekeza kabisa kwamba askari hawa Mheshimiwa aliyetoa hoja sasa hivi wa Upinzani amesema juu ya afya ya askari. Napendekeza hawa askari wapelekwe mazoezi mara kwa mara, ni aibu kwa askari kuwa na kitambi na naomba Wizara hii ikimalizika humu hawa waliokuja tuwakamate pale mlangoni wakabidhiwe kwa Mheshimiwa Joel Bendera, aende akawafanyishe zoezi watoe vitambi vyao maana utamkimbiza vipi mhalifu wewe mtu una kitambi utafikiri una mimba. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho napendekeza kwamba kila siku toka nianze kuwa Mbunge naona *Serjeant At Arms* kila siku ni mwanaume, ikiwa tunataka kuwajali nao wanawake naomba atafutwe na *Serjeant At Arms* mwanamke au labda niambiwe hili Siwa ni zito sana hawezi kulibeba akamuongoza Spika akampeleka kwenye kiti chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kengele ya mwisho naomba na nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini kabla sijaanza mchango wangu ningependa kutumia nafasi hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri sana waliyoifanya wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka 2005 na kuhakikisha uchaguzi ule unafanyika kwa amani, utulivu na demokrasia ilichukua mkondo wake. Lakini pia wale walioshinda ndio ambo wanaongoza, nalishukuru sana Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue sasa nafasi hii tena kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuunda Wizara hii ya Usalama wa Raia. Lakini nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri wa Usalama wa Raia na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kushika nafasi hii, nina hakika kabisa kasi mpya imeshaanza kuonekana ndani ya Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza *IGP Said Mwema*, kwa kuteuliwa na Rais kushika wadhifa huo, lakini nimpongeze pia *DCI Robert Manumba* na Makamishna wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limekuwa na kazi kubwa sana hasa ya kupambana na majambazi ambao hapa katikati ujambazi ulikuwa umekithiri sana lakini hatua ambazo zimechukuliwa na Jeshi la Polisi katika kipindi hiki cha kupambana na uhalifu ambao ulikuwa umejitokeza kwa wingi, kwa kweli zimeonyesha matunda makubwa sana na kwa kiasi kikubwa naweza kusema kwamba wamefanikiwa kutokomeza ujambazi huo ingawa bado yapo maeneo ambayo jitihada zinatakiwa zifanyike zaidi ili kuweza kuutokomeza kabisa ujambazi na uhalifu ambao upo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo za kupambana na wahalifu lakini bado kuna maeneo hasa katika Jimbo la Kinondoni lakini nina hakika takribani labda nchi nzima bado yapo maeneo katika Jimbo la Kinondoni uporaji unaendelea na imefika mahali unaweza ukaporwa simu ya mkononi na mtu anakuonyesha bastola kwa ajili ya kupora simu ya mkononi, ama anakwenda kwenye maduka madogo madogo anaonyesha bastola kwa ajili ya kupora labda shilingi 100,000/= au 200,000=/. Kitendo hicho kinaonyesha kwamba bado zipo silaha nyingi mitaani kwa wahalifu hawa, nashauri au niombe Jeshi la Polisi lifanye jitihada za makusudi kabisa kujaribu kutafuta wamiliki haramu wa sihala hizi ambao kwa kweli ndio wanachangia kwa kiasi kikubwa kwenye ujambazi. (*Makofi*)

Lakini pia nashauri kwamba labda kuna haja ya kuimarisha vituo vyetu vidogo vya polisi yaani hizi *Police Post* nina hakika tutakopoziimarisha na wakishirikiana vizuri na Mabalozi wa Mashina, Wajumbe wa Nyumba Kumi nina hakika majambazi katika mitaa ile watapatikana. Kwa hiyo, niombe Jeshi la Polisi lijaribu sana kuwa karibu na vituo vidogo ambavyo tumevianzisha kuweka askari wa kutosha lakini pia kuweka zana zinazohitajika katika vituo vile vidogo ili kuweza kupambana na uhalifu huu mkubwa na uhalifu mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda sana nizungumzie Kituo cha Polisi cha Magomeni na kwa kweli sikumbuki ni lini kilijengwa, ninachokumbuka mimi nilizaliwa nikapata fahamu kituo kile nimekiona, nina hakika kilipojengwa wakati huo Kinondoni ilikuwa na wakazi wasiozidi 200,000 au 250,000, hivi sasa wakazi wa Kinondoni ni zaidi ya 1,200,000. Kituo kile katika eneo la Kinondoni ndicho kikubwa ukitoa kile cha *Oysterbay* ambacho tunakitegemea lakini kutohana na wingi wa watu katika Wilaya ya Kinondoni uhalifu umekuwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kituo kile kwa kweli mbali ya kuwa ni kidogo lakini kwa kweli hali yake hairidhishi, maofisi yamekuwa ni madogo, vitendea kazi hakuna, lakini bayu zaidi hata nyumba za kulala askari kwa kweli zinasikitisha. Lipo jengo moja kubwa ambalo wenyewe huwa tunaliita behewa, juu limeezekwa na bati lakini na ukuta wake pia ni wa bati wa mjini wenyewe tunaliita *full suit*. Jengo kama lile na joto la Dar es Salaam askari yule ambaye ametoka kuhangaika kupambana na wahalifu anarudi nyumbani kwake ndiyo anaingia mle ndani kuna joto la ajabu akifika anapewa ugali wa moto na mchuzi wa moto, kwa kweli sitaki kusema tunawadhalilisha, lakini kwa kweli tuangalie naona kabisa kwamba haitawafanya wafanye kazi zao vizuri. Niombe Jeshi la Polisi liangalie uwezekano wa kukitengeneza, kukarabati majengo yaliyopo katika kituo kile cha Magomeni. (*Makofi*)

Sambamba na hilo naomba Wizara pia kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni mbele ya kituo kile ambapo magari na watu tumezoea kupita ndiyo njia, hapapitiki kwa sababu pana bwawa kubwa sana la maji, inabidi tuzunguke kwa kupitia nyuma huku Mahakamani, basi tuangalie uwezekano wa kuondoa lile bwawa kwa sababu mbali ya kwamba hapapitiki lakini linazalisha mbu na kuleta maradhi. Sasa askari huyu anayekaa kwenye *full suit* bado anashambuliwa tena na mbu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kituo cha Kijitonyama ambacho kwa kweli kinachukua maeneo mengi sana ya Kijitonyama yenyele lakini na Sinza na maeneo hayo ndiyo maeneo ambayo kuna uhalifu wa hali ya juu. Uporaji wa magari mengi unatokea maeneo ya Sinza, kituo kile ndicho ambacho tunakitegemea lakini nacho pia hakina zana za kufanya kazi, hakuna nyumba za askari, likitokea tatizo askari anayefanya kazi Kijitonyama au Magomeni anaishi Kinyerezi utampataje aje asaidie kwenye matatizo ambayo yanatokea?

Kwa hiyo, ningeshauri Wizara iangalie uwezekano wa kuvikarabati vituo hivi lakini kujenga nyumba za askari najua upo mpango wa kujenga nyumba za maaskari na zipo ambazo zimejengwa Kunduchi ni mfano mzuri sana. Lakini pia tuangalie uwezekano wa kujenga nyumba katika maeneo ambayo ndiko askari wanakofanya kazi na bahati nzuri ardhi ya kutosha ipo pale tunaweza kabisa tukajenga hizo nyumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nataka kuzungumzia uonevu pamoja na kazi wanayoifanya lakini wapo wachache ndani ya Jeshi la Polisi ambao kwa kweli ama kwa makusudi ama kwa kuambiwa na watu huwa wanafanya vitendo ambavyo si vya kibinadamu na wala si katika maadili yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sana Kituo cha Msimbazi Kituo hiki kimezungukwa na wafanyabiashara wakubwa lakini kimezungukwa na halaiki kubwa ya watu wanaokwenda maeneo ya Kariakoo kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali. Kibaya zaidi wafanyabiasha wa eneo lile wamefanya kituo kile kama ndiyo ofisi zao ndogo, anaweza akamkamata mfanyakazi ama wa kwake au mwananchi yejote mwenye kipato cha chini akamwambia labda wewe juzi uliniibia au mwezi uliopita uliniibia kwa hiyo nitakuonyesha. Akaenda pale Msimbazi na kweli akasikilizwa na yule mtu ambaye ni maskini akawekwa ndani, akateswa pamoja na kwamba labda amepigwa huko anakotoka akavunjwa mguu lakini askari wa pale kwa kweli hawamsaidii yule mtuhumiwa na sana wanamsikiliza yule bwana mkubwa ambaye ni tajiri aliyekwenda kutoa taarifa ile. Naomba sana Wizara na viongozi wa Jeshi la Polisi wakiangalie kwa umakini sana kituo hiki cha Msimbazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na wahalifu wananchi wa Jimbo la Kinondoni wamejitolea kujenga vituo vidogo vya Polisi na kipo kituo ambacho kimejengwa mtaa wa Mwinyimkuu, Magomeni Mapipa lakini tumejaribu mara kwa mara kuomba askari waende kwenye kituo kile mpaka leo kituo kile bado hakijapelekewa

askari. Naomba Wizara itusaidie ili kutuo kile nacho kipate askari kwa sababu eneo lile nalo ni eneo ambalo kuna wahalifu wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia amri iliyotolewa na *IGP* kuhusu mchezo wa *pool*, nakubaliana naye lakini naogopa isije kesho akasema na ninyi mnaocheza mpira saa nne asubuhi basi na ninyi muache kwa sababu tunafuga majambazi. Ningombia tu jitihada zifanyike kuangalia kama ni kweli mchezo ule unawakaribisha majambazi kwa sababu ni mchezo ambao kwa kweli watu wanaupenda. Lakini niishauri Serikali kwamba mchezo ule na hasa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, mchezo ule basi ni vema ukaenezwa katika maeneo mengine kuliko kuwa unachezwa kwenye baa peke yake tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunazo *night club* bubu Dar es Salaam zinafanya biashara kinyume cha sheria na inawezekana hizi zikawa zinafuga majambazi, lakini polisi wamekuwa wakizachia *night club* hizi bubu zinafanya kazi usiku kucha bila kuchukua hatua yoyote na wanafahamu kwamba ni kinyume cha sheria, sitaki kuzitaja kwa sababu nafahamu wanazijua. Lakini niombe Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba tunaziondoa *night club* hizo bubu. (*Makofi*)

Mwisho kabisa ningependa kuwashauri Wizara hii kupitia Wakuu wa Jeshi la Polisi wa vituo kuhakikisha kwamba wanafanya vikao vyta mara kwa mara na wajumbe wa mashina, wajumbe wa nyumba kumi isiwe tu kuagiza kupitia vyombo vyta habari kwamba wajumbe wa nyumba kumi na mabalozi wafichue majambazi, ni vema na wao wenyewe wakashuka kwenda kuonana nao na kwa kweli wajumbe wa nyumba kumi watafurahi sana watakapofanya kikao na Wakuu wa Jeshi la Polisi na nina hakika wajumbe wale watatusaidia sana kuwfichua majambazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nisije nikagongewa kengele ya pili, nimalizie tu kwa kuwapongeza tena Jeshi la Polisi na kuwaomba wajitahidi sana kupambana na uhalifu huu na wale wenzangu wa *traffic* nao wawe makini kwani ajali zimekuwa ni nyingi sana hivi sasa, watu wanakufa sana kutokana na ajali za barabarani lakini na wao wamekuwa ni chanzo kuachia magari mabovu kuendelea kutembea barabarani lakini kuachia magari ambayo yamezidisha abiria kuendelea kufanya biashara hiyo nina hakika na wenyewe nao *traffic* wakichukua jitihada hizo basi ajali zinaweza kwa kiasi fulani zikapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitamke kwamba sasa naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ALI JUMA HAJI :** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Usalama wa Raia.

Kwanza kabla ya yote kwa vile na mimi ni mara yangu ya kwanza kuchangia sina budi kuungana na wenzangu waliotangulia kwa kuwapongeza viongozi wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura nyingi alizopata katika Uchaguzi Mkuu na

kushangaza ulimwengu mzima na kukiongoza Chama chetu cha Mapinduzi hatimaye kuwa Rais wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume na  
yeye kwa kura zake za kishindo alizopata kule Visiwani na kuchaguliwa kuwa Rais wa  
Zanzibar naye nampongeza sana. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa  
ushindi mkubwa aliopata Jimboni kwake na hatimaye kura nyingi tulizompa katika  
Bunge hili kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza  
Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, naye kwa ushindi mkubwa  
alioupata. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, pia nakupongeza wewe kwa ushindi mkubwa uliopata Jimboni kwako na pia katika Bunge hili ambalo ni kama Jimbo la pili zito ambapo unatuongoza vizuri kwa kutuelimisha hadi hivi sasa tunavyokwenda hasa wakati wa kuitishwa vifungu kwenye Kamati ya Matumzi bado unatuongoza kwa kutuelimisha. Hongera sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, pia nisisahau kumpongeza Naibu Spika na Wenyeviti wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya wakikalia kitu hicho, wanatuongoza vizuri sana, nao nawapongeza. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, nisiwe mwizi wa fadhila, kwa sababu Bunge hili linaangaliwa na wananchi kweli kweli, tukitoka nje tunaelezwa moja moja. Kwa hiyo, wananchi wangu nina hakika sasa hivi wananiangalia nao niwashukuru sana kwa kura zao nyingi walizonipa na kupata asilimia kubwa ambayo hata mtani wangu pale alipata kwa kuyumba yumba sana, kwa ushindi mkubwa walionipa wananchi wangu wa Jimbo la Chaani, nawashukuru sana nami nawaahidi nitakwenda nao vizuri katika kufanya mema Jimboni kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo na shukrani, sasa nije katika mchango wangu kwenye hotuba hii ya Wizara ya Usalama wa Raia. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ujumla katika Wizara hii kwa kutuandalia bajeti hii ambayo kwa kweli inaonyesha mwelekeo mzuri sana, endapo itatekelezwa kwa vitendo. Tunawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa kwamba Jeshi la Polisi lina kazi moja kubwa sana ya kupambana na ujambazi ambao kwa kweli ulileta tishio kubwa katika nchi yetu hii. Kwa kweli tunawapongeza kwa kazi kubwa waliyoifanya ingawa haijafikia asilimia mia moja, lakini kwa hatua kubwa waliyofikia na mpaka sasa hivi kuona kwamba nchi yetu imetulia kwa kiasi fulani ni kazi moja kubwa na wanastahili pongezi za aina yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, wengi wameshapongeza katika suala la ujambazi. Lakini mimi niende moja kwa moja katika suala la mambo ya pensheni. Katika Jeshi letu hili la Polisi, kuna taratibu zao ambazo wanaziita *PGO*. Katika *PGO* namba 48, inasema pamoja na mambo mengine, lakini askari anapotimiza miaka 12 ya

kazi anatakiwa ajaze mkataba na kuchagua katika mifumo miwili iliyopo katika ulipaji wa mambo ya pensheni na bakshishi ambao wao wanaambiwa ni kiinua mgongo.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu mmoja ni mzuri wa pensheni. Lakini mfumo huu mwininge wa bakshishi ni mbaya mno. Kwa kweli unawaumiza askari wetu na wote wanaoumia katika mfumo huu ni askari wenye vyeo nya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mfumo huu mimi naiomba Serikali kwamba uondolewe moja kwa moja, haufai kabisa. Nasema hivi kwa sababu mfumo huu unawakandamiza askari wenye vyeo nya chini tu, kwa sababu askari akishafikia cheo cha *Inspector* unamtoa moja kwa moja yaani yeche automatically anatoka katika mfumo ule na anaingia kwenye pensheni. Hii ni dhahiri kwamba mfumo huu si mzuri. Kwa sababu kama ni mzuri hata kama askari alichagua ule mfumo wa bakshishi, lakini akifikia cheo kile basi unamtoa moja kwa moja na kuingia pensheni.

Mheshimiwa Spika, sasa hii inatudhihirisha kwamba mfumo huu sio mzuri na unawakandamiza askari wenye vyeo nya chini tu. Kwa nini kama ni mzuri askari akifikia cheo kile asiendelee na yeche kubakia na kuja kulipwa katika mfumo ule aliouchagua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema mfumo ule si mzuri kwa sababu nina ushahidi mzuri. Kuna askari mmoja ambaye alifanya kazi kwa muda wa miaka 32, alianza kazi mwaka 1972 na akastaa fu mwaka 2004, kwa muda wa miaka 32 yupo katika Jeshi hili la Polisi. Kwa bahati nzuri mfumo huu mwenyewe Mheshimiwa Waziri namshukuru kwamba amekiri katika hotuba yake hii katika ukurasa 36, kipo kipengele amesema kwamba askari waliochagua mfumo huu hawakupewa elimu ya kutosha na mimi nakubaliana naye kwamba hawakupewa elimu ya kutosha. Kwa sababu kama wangepeewa elimu ya kutosha hakika mfumo huu wasingeuchagua kwa sababu umewakandamiza nya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naamini mimi hawakupewa elimu ya kutosha kwa sababu huyu askari ninayemsema hapa ambaye alifanya kazi kwa muda wa miaka 32 kachagua mfumo ule wa bakshishi. Lakini aliuchagua kwa bahati mbaya kwa sababu wao hawaambiwi bakshishi, wanaambiwa ni kiinua mgongo. Sasa mtu anaona kiinua mgongo, anaulizwa unataka kiinua mgongo au unataka pensheni. Sasa anahisi labda yale mafao ya kiinua mgongo akichagua pensheni hatoyapata. Hiyo ni moja ambayo hawakupewa elimu ya kutosha. Kwa hiyo, moja kwa moja anaamua achague bakshishi, anaambiwa ndiyo kiinua mgongo anahisi yeche atapata mafao yake ya jumla ya fedha zake afanyie shughuli zake. Lakini kumbe sivyo. Hii ni bakshishi tu.

Mheshimiwa Spika, bakshishi si haki, bakshishi ni tunuku ambayo mtu anafanyiwa kwa kufanya jambo zuri ndani ya utendaji wake wa kazi. Lakini kiinua mgongo ni haki yake. Sasa inakuwaje leo anaambiwa bakshishi? Ni bakshishi kweli, kwa sababu miaka 32 aliyo fanya kazi alilipwa kiinua mgongo hiki shilingi 1,200,000 kwa miaka 32. Hiyo ni kengele ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kweli nitaongelea kitu hiki hata kama kengele ya pili itagongwa ingawa nilikuwa na mengi ya kuchangia lakini hili linaniumiza zaidi kwa sababu kuna sehemu yininge hapa inawatoa kabisa hawa watu.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu kuna *circular* ilitoka inasema hivi, imeeleza mambo mengi lakini kwa askari waliochagua bakshishi yaani kutengenezewa kiinua mgongo. Nanukuu: "Kwa askari waliochagua bakshishi watalipwa kiinua mgongo kwa kipindi cha utumishi wa muda wa miaka 21. Miaka inayozidi haitahusishwa kwenye malipo ya kiinua mgongo, isipokuwa wataendelea kupata mishahara yao mpaka watakapofikia umri wa kustaafu kazi." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii inasikitisha sana. Huyu askari kafanya kazi kwa muda wa miaka 32, lakini kiinua mgongo chake anachotengenezewa ni kwa miaka 21. Miaka 11 yote imeachwa, hii ni haki kweli? Kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake atueleze kwa nini miaka hii inatolewa wakati ni haki yake alilitumikia Jeshi. Muda wa miaka 11 ni mingi sana kwa nini imeondolewa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu isitoshe mtu kama huyu anapewa barua nzuri sana, naomba kunukuu tena anaambiwa, kumbukumbu zinaonyesha kuwa umeingia Jeshini tarehe hiyo mwaka 1972 kwa muda wote huo umefanya kazi zako kwa bidii kubwa kabisa. Ukiangalia alivyopewa sifa za upendo, uhodari na uaminifu mkubwa halafu anasema Kamishna kule Zanzibar anamtakia mafanikio mema. Kweli anamtakia mafanikio mema, huyu mtu akishachanganyikiwa kimaisha kwa kulipwa shilingi 1,200,000. Halafu anamwandikia barua anamtakia mafanikio mema. Mimi nakataa haya si mafanikio mema bali kwa kweli alimtakia matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina wasiwasi mkubwa, Serikali sasa hivi inapambana na janga kubwa la vijana ambao wameathirika kwa dawa za kulevyta. Utaratibu huu kama hautaondolewa Serikali ijiandae kupambana tena na kundi ambalo limeshachanganyikiwa kimaisha, linakuja lile la askari wastaafu wa polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana hili suala lizingatiwe na Mheshimiwa Waziri atueleze vizuri kwa nini mfumo huu unawakandamiza askari wenye vyeo vya chini tu na wale wenye vyeo vya juu wameondolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka nakuja katika suala la uajiri ambalo hili mimi katika kutoa pongezi zangu au shukrani zangu katika matawi mbalimbali katika Jimbo langu ni kilio kikubwa tunapewa kuhusu suala hili. Kwanza, vyombo vyetu vya ulinzi tukubali kwamba ndivyo vyombo ambavyo vinachukua idadi ya kubwa ya ajira. Hii lazima tukubali. Sasa wanapokuwa wanaajiri kwa kweli utaratibu wao sio mzuri sana. Kwa sababu wao wanaleta taarifa kuitia Wilayani ama Mikoani na kule vijana wetu wanaitwa, wanakwenda, wanapimwa urefu, afya na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, sasa pale wanachukuliwa majina yanapelekwa Makao Makuu ya Polisi kule Zanzibar. Sasa huku vijana hawa wameshajijua kwamba mimi

nimeshaorodheshwa na nimeshabahatika. Lakini yale majina yakifika Makao Mkuu inaanza kazi upya. Sasa wengine hapo wanakosa nafasi, kazi inatupata sisi Wabunge kwa kweli tunakuwa kama sisi ndiyo Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu. Watu wanatuufuata majumbani mwetu, vipi kijana wangu mbona akakosa wakati huko Mkoani alishaambiwa kwamba ye ye amefanikiwa. Kule Makao Makuu ya Polisi wanapimwa tena wanaambiwa hawakupata nafasi. Pengine majina yakifika Tanzania Bara huku, Makao Makuu wanapimwa tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoomba Wizara ama Jeshi la Polisi lilete wataalam wake moja kwa moja kama pale Mkoani wakishapimwa pale tujue kwamba hao vijana wameshabahatika na wakiondoka pale wanaenda moja kwa moja kusubiri safari.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele ya pili imeishalia. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante. Natumaini jina la huyo askari mstaifu utalifikisha kwa Mheshimiwa Waziri aelewe unazungumzia nani aliyeponjwa malipo yake. (*Makofii*)

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Usalama wa Raia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu, ningependa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi. Pia nimpongeze Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume na nampongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe pamoja na Naibu Spika, kwa kura nyingi mlizopata ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naungana na wachangiaji walio tangulia kuwapongeza wale wote walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali katika Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati kabisa akinamama wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Mimi naahidi kwao kwamba nitakuwa pamoja nao kwa kuleta maendeleo ya akinamama kwenye Mkoa huo. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia bajeti ya Wizara hii. Awali ya yote kwanza napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Rais kwa kuunda Wizara hii ya Usalama wa Raia. Hii ni dalili tosha kwamba Serikali imekusudia kuliimarisha Jeshi la Polisi kwa kulinda amani na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza kwa dhati Jeshi la Polisi kwa utiifu wao kwa Taifa letu ikiwa ni pamoja na juhudhi za kuhakikisha kwamba usalama wa raia na mali zao. Sambamba na pongezi hizi nawapongeza raia wema waliojitekeza kulisaidia Jeshi la Polisi kwa utendaji wao mzuri wa kutoa taarifa zinazoliwezesha Jeshi la Polisi kuzuia uhalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi ngumu sana hasa ukitegemewa kwamba hawana vitendea kazi. Wana upungufu mkubwa wa vitendea kazi, lakini Jeshi la Polisi huweza kupambana na wahalifu au majambazi kwa kujitolea kwa roho zao zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna raia wachache ambao hawalitakii mema Jeshi la Polisi kwa kuwafanya vitendo viovu, kwa kuwapiga askari, kuwachinja askari, kuwatoboa macho askari na kuwafanya vitendo vingi tu vya kihalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina ushahidi tosha pale Zanzibar kuna afisa mmoja wa kike aliyedhalilishwa kwa kupigwa, kuvunjwa mkono, kuvunjwa miguu, akapasuliwa uso na mwingine akatobolewa jicho.

Mheshimiwa Spika, sikuona raia kuwatetea askari hawa kwenye haki za binadamu wala sikuona magazeti yakikemea au wananchi wakikemea udhalimu huo waliofanyiwa askari hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli askari hao nao ni watu na wanahitaji haki za binadamu, nao wanahitajika kama sisi au raia wema kuwatetea pale yanapowafikia na wao mabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, askari wa Zanzibar mimi nampa pongezi kubwa Kamishna wa Polisi Zanzibar, Ndugu Khalid Idd Nuizan, kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi kifupi cha kupambana na majambazi. Kwa kweli anastahili sifa ye ye pamoja na askari wote wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juu ya pongezi hizi bado jambo ndogo tu ambalo ningewaomba askari wa polisi Zanzibar wakalisisitiza au wakalitilia mkazo kule ambapo kuna mahoteli ya kitalii mpakani na bahari yetu ya Hindi. Kwa kweli kule ndiko yalipo mahoteli ya kitalii. Ningependa Serikali iongoze ulinzi wa kutosha kwani watalii ambao ndiyo wanaotuletea pato kubwa kule Zanzibar lakini wanasumbuliwa sana na majambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu makazi ya askari. Askari wetu na hasa nawazungumzia askari wa Zanzibar wana matatizo makubwa ya nyumba za kuishi, nyumba wanazoishi ni chakavu na ni mbovu kwa kweli zile nyumba hazistahili kukaa

askari wetu hao. Basi naiomba Serikali katika mpango wake wote wa kujenga nyumba nyingine za askari iione Kambi hii ya Polisi Ziwani kwa kuwajengea mazingira mazuri hao askari wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapo ndani ya kambi hiyo ya Polisi Ziwani kuna hospitali. Hospitali ile ni nzuri, ina madaktari wazuri wa fani zote za udaktari. Lakini la kusikitisha zaidi hospitali ile haina zana za kisasa na hospitali ile haina dawa. Unapofika pale saa 4.00 asubuhi unaambiwa dawa zimeshamalizika. Hii hospitali inawachukua askari wengi wanaoishi kwenye Mkoa wa Mjini Magharibi na hata wanaoishi kwenye Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali itazame hospitali lile kwa makini sana na itoe mchango mkubwa sana kwenye hospitali hii ya polisi ambayo ndiyo inayowahudumia askari hao.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu mafao ya askari pale wanapostaafu kazi. Askari hupata usumbufu mkubwa wanapostaafu wanapofuutilia mafao yao. Anakwenda na kurudi kama yupo Pemba anatoka Pemba mpaka Dar es Salaam kufuutilia mafao yake. Kama yupo Unguja anatoka Unguja mpaka Dar es Salaam anakuja kufuutilia mafao yake. Hata hayo mafao yenye akiyapata, fedha zote zinakuwa zimeshamaliza kwenye nauli ya kwenda na kurudi. Kwa hiyo, nalo hili naiomba Serikali iliangularie kwa kuwarahisishia askari kupata mafao yao hayo.

Mheshimiwa Spika, lingine askari polisi anapofariki, familia yake inapofuutilia hizo fedha, anakwenda, anarudi mpaka mfuutilaji naye anafariki bado mafao yale yanakuwa hayajapatikana. Nalo hili Serikali iliangularie na ilishughulikie kwa umakini hasa ikizingatiwa kuwa Naibu Waziri wetu wa Usalama wa Raia ni mkakamavu na ni hodari kwani anavyoyojibu maswali hapa yananitia moyo, basi kwa hali hiyo, naomba na hili alifuutilie kwa makini ili askari hawa wapate ufumbuzi wa masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie posho za askari. Posho za askari siku zote kwa askari wa Zanzibar huwa fedha zao zinachelewa. Sijui tatizo hili liko wapi? Kwani kutoka Zanzibar mpaka Dar es Salaam ni saa mbili na nusu tu na ndipo yalipo Makao Makuu ya Polisi. Lakini utaona askari wa Dar es Salaam wanapata posho tarehe 15, askari wa Zanzibar wanapata posho tarehe 29. Hili kwa kweli naomba tena Mheshimiwa Waziri au Wizara ilifuutilie kwa makini ili nao askari wa Zanzibar wapate posho zao kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda tena kumpongeza Kamishna wa Polisi Zanzibar na Jeshi lake kwa kutufanya tunalala hivi sasa kwa amani na utulivu Zanzibar. (*Makofi*)

Mhesimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani za dhati kwako kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata ushindi mkubwa wa kishindo katika ngazi ya Urais na ngazi ya Uenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri, kadhalika nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyevitii wa Bunge. Kadhalika napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi waliopata na kuweza kupata nafasi hii ya kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nazipongeza Wizara zote tulizopitisha hadi wakati huu kwa bajeti zao kwa kweli zina ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Bajeti zao zinaugusa umma, tunawatakia utekelezaji mwema kwa kila walichokipanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kadhalika napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Magharibi katika Kata ya Karema, Kata ya Ikola, Kata ya Kabungu, Kata ya Mwese, Kata ya Mishamo, Kata ya Mpanda ndogo na Kata ya Katuma kwa kura zao za kishindo walizozitoa kwa ajili ya ushindi wa Madiwani wote katika Jimbo la Mpanda Magharibi. Kadhalika kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na pia kwa Mbunge wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa nafasi walionipa nakiahidi chama pamoja na Serikali na kadhalika nawaahidi wananchi wa Mpanda Magharibi kuwatumikia kwa uaminifu na nguvu zangu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuishukuru Wizara ya Usalama wa Raia kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Kata yangu kule Ikola tayari kimefunguliwa Kituo cha Polisi eneo ambalo lilikuwa linasumbuliwa na ujambazi mara kwa mara, kadhalika napenda kuwashukuru askari wote wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi na vyombo vyote vya dola sasa hivi kwa kuungana ili kuweza kupunguza kero za ujambazi na kuleta usalama kwa raia na mali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba ya bajeti ya mwaka 2003/2004 nilifikisha malalamiko yetu juu ya vijana walitekwa nyara kule Kando ya Ziwa Tanganyika katika eneo Kaseramiaga na Kasagatogwe. Vijana hao ni Tunu Wasenka, Simon Feruzi, Maganga Sokolo, John Kilimo, Grevaz Pima, hao vijana walitekwa nyara na kupeleka upande wa pili wa Ziwa Tanganyika huko Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Walipotekwa hao vijana, walitekwa pamoja mali zilizochukuliwa sawasawa na shilingi 2,500,000 katika kipindi hicho. Vijana hao walitumiwa kwa kusoza hadi upande wa pili wa Ziwa na hadi leo hii vijana hao hawajapatiwana.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilishaifikisha katika vyombo vyote vya dola. Lakini eneo lile lilikuwa halina Serikali, halikuwa chini ya Serikali ya Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo isipokuwa lilikuwa chini ya waasi. Tulitumia taratibu namshukuru sana Mkurugenzi wa Maendeleo ya Wilaya ya Mpanda alitoa ushirikiano wa dharti Ndugu

Bandisa, akatoa fedha na wananchi wetu waliweza kuvuka upande wa pili, kwenda kupeleleza juu ya hali ya wale vijana. Lakini inasemekana walikwishahamishwa kutoka eneo lile na tayari walipelekwa kwenye sehemu za machimbo ya dhahabu na wanafanya kazi huko chini ya ulinzi.

Naiomba Serikali kupitia Wizara hii sasa ni wakati muafaka Serikali ya Jamhuri ya Kongo tayari ipo madarakani na eneo lile halipo mikononi mwa waasi naiomba Serikali yetu kupitia Wizara hii na vyombo vyote vya dola kuweza kufuatilia na kujua hatma ya vijana wetu hao walioko huko.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo taarifa ya ujambazi ulioripotiwa katika Tarafa ya Karema tangu mwaka 2000 mpaka leo umepoteza roho za watu wetu wanne waliotekwa walikuwa 46, aidha, kumi hawajulikani walipo hadi sasa. Mali zilizoporwa ni zaidi ya shilingi milioni 120. Unyeti na umuhimu wa Wizara hii kwa Taifa letu sote tunaujua hivyo basi wakati umefika sasa kwa Wizara kuweka vyombo vya kisasa katika Ziwa Tanganyika na sio kukarabati zile boti za zamani kwa sababu zile boti tulizonazo ni chakavu zinatumia mafuta mengi kiasi kwamba hatuvezi kumudu. Tunaiomba Wizara hii ichukue hatua za dhati kabisa na mwelekeo mpya Kando ya Ziwa Tanganyika kushirikiana na Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo letu kando ya Ziwa huko tunashauri zile boti chakavu zilizopo sasa kabla ya kupata boti zingine ziweze kufanyiwa matengenezo ya kweli na ziwe tayari kwa ulinzi wa mwambao wa eneo lile. Sambamba na vifaa vya majini kule Karema wananchi walijitolea kujenga Kituo cha Polisi. Kituo kile kimekamilika lakini mnamo mwezi wa Januari kabla hakijaanza kutumika upopo uliezua mabati na sasa hivi kituo hicho si salama. Kituo hicho ni eneo muhimu sana kwetu hasa ni mlango bahari wa kuingilia kutoka kwetu na kwenda upande wa pili wa Ziwa Tanganyika. Tunaiomba Wizara kwa makusudi kabisa iweze kutoa msaada wa dharura ili kituo kile kiweze kukamilika sasa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nilikuwa naiomba Wizara iweze kutusaidia gari kwa ajili ya usafiri na ulinzi kando ya Ziwa. Umbali wa kutoka Karema kuja Mpanda Mjini ni kilometra 136. Ni umbali mkubwa, unahitaji huduma na eneo lenyewe ni eneo refu, linaunganisha vijiji vya Karema yenyewe, Sumbwa, Ikola, Kasangatongwe, Kaselamiaga hadi mpakani mwa Kigoma, Lwega. Naiomba Wizara iweze kutufikiria na kuweza kutusaidia tupate usafiri wenye uhakika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kadhalika natoa ushauri Polisi ni walinzi wetu, wanajitolewa maisha yao kwa ajili ya ulinzi juu ya maeneo yetu kwa mali zetu na watu wetu. Naomba askari wetu waweze kupewa vifaa vya kisasa kwa askari kama vile *bullet proof vest, silencers* na kadhalika. Wanakwenda kwenye operesheni, wapewe vifaa kama vile *night vision, modern guns* na *guard gates* za kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli shughuli za ulinzi wa askari wetu tunapaswa kuzipongeza askari polisi wanafanya kila wawezalo na tunapaswa kuwapa moyo na kuwapa ushirikiano. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili hiyo.

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY:** Ya pili. Naunga mkono hoja mia kwa mia.  
(*Makofii*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia. Kwanza kabla sijaenda mbali naomba niseme kwamba naunga hoja mkono hotuba hii. Hotuba hii ni nzuri sana na kwa kweli kama itaweza kutekelezwa kwa vitendo basi Wizara hii ya Usalama wa Raia itakuwa imefanya kazi nzuri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Usalama wa Raia kwa kazi nzuri ambayo wameifanya juzi. Juzi nilisimama hapa nilitoa kilio changu kuhusiana na wizi wa mifugo ambaa umetokea katika Jimbo la Karagwe na ambaa mpaka sasa hivi bado unaendelea. Lakini kupitia Wizara ya Usalama wa Raia pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mwapachu, Mheshimiwa Naibu Waziri wamenisaidia kupeleka FFU jimboni Karagwe na mpaka sasa hivi wako kwenye operesheni kubwa ya kutafuta ng'ombe walioibiwa na kwa taarifa niliyotumiwa jana ni kwamba tayari ng'ombe 300 wameshapatikana. Naipongeza sana Serikali na naomba iongeze juhudhi kwa wale ambaa bado hawajapatikana basi na wenyewe waweze kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatoa pongezi za dhati kwa IGP wetu Bwana Said Mwema. Mimi namfahamu vizuri sana Bwana Said Mwema na niliposikia ametuliwa kuwa IGP kwa kweli nilisema kiti kimepata mtu. Nampongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya ya kupambana na ujambazi. Wote kwa pamoja tunastahili kumwunga mkono na kumsaidia ili aweze kufanya kazi ambayo kwa kweli ni ngumu sana ya kupambana na wimbi la ujambazi kwa hapa nchini kwetu sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia mengi amezungumza lakini pamoja na kwamba tunaye *IGP* Said Mwema na anafanya kazi nzuri kama jina lake liliyvo lakini bado kuna mapungufu makubwa sana katika Wizara hii. Wizara hii kwa kweli ina mapungufu makubwa mno. Hata tukipata *IGP* akawa mzuri namna gani bila ya kumsaidia au bila Serikali kuongeza nguvu katika Wizara hii nadhani na wenyewe watafika mahali watashindwa. Nasema hivyo kwa sababu Wizara haina magari ya kutosha, ina upungufu mkubwa sana wa magari ya kufanya kazi. Nasema hivyo vile vile kwamba Wizara ina upungufu wa pikipiki, haina pikipiki za kutosha. Wizara nadhani naamini kabisa ina upungufu vile wa askari wetu. Nadhani ni vizuri wa kuongeza askari kutokana na wimbi la ujambazi ambalo wanajitokeza hapa nchini. Vile vile katika bajeti hii mimi ningefurahi zaidi kama vituo vya polisi vingeongezewa magari ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo askari wetu wanafanya kazi nzuri sana. Mimi wakati mwingine huwa nawashangaa watu wanaowalaumu askari kwamba ni

wazembe, hawafanyi kazi. Kazi ya kupambana na mtu mwenye silaha, mwenye mtutu, risasi sio ya mchezo ni kazi ya kujitoa maisha. Askari wetu kusema kweli wanajitahidi ingawa wapo wachache kidogo wanaowaangusha. Lakini pamoja na hayo askari wetu wameendelea kupambana katika mazingira magumu hasa kupata mishahara midogo. Mshahara wa askari ni mdogo na nilikuwa nashauri kwamba askari wetu waangaliwe mishahara yao iwe inapanda mara kwa mara na kwa kiwango cha kuridhisha. Askari wanapoingia kwenye kazi kwa mfano kama ya operesheni ninayoisema huko Karagwe basi waangaliwe, wapewe posho ya mazingira magumu. Kazi ya kuingia porini kumsaka jambazi sio ya mchezo, wakitoka huko wapewe posho nzuri kwa ajili ya mazingira magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna baadhi ya askari wamekuwa hawapandishwi vyeo kwa wakati. Sasa hilo jambo ningependa kabisa kuishauri Serikali kwamba askari wetu wapandishwe vyeo kwa wakati hiyo ikiwa ni pamoja ya kuwapa motisha ya kufanya kazi zao vizuri. Ili askari wetu waweze kufanya kazi katika ulimwengu wa kisasa wanahitaji kwenda shule, wanahitaji kupata elimu ya kuweza kupambana na majambazi ambao kwa kiasi kikubwa sana wameelimika na wana mbinu za kisasa. Sasa Wizara ya Usalama wa Raia ijitahidi sana, iweke programu na mkakati mzuri wa kuweza kupeleka askari wetu shulenii waweze kusoma. Vile vile Wizara ihakikishe kwamba inakuwa na shule zao binafsi kama ilivyokuwa Wizara ya Mambo ya Ndani, Magereza wana shule zao za sekondari, ili askari wetu waweze kupata elimu kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa nikimbilie jimboni kwangu Karagwe. Jimbo la Karagwe au Wilaya ya Karagwe kwa ujumla ni Wilaya ambayo iko mpakani, imepakana na nchi ya Uganda pamoja na nchi ya Rwanda. Mipaka hii hasa ule mpaka wa Rwanda na Tanzania umekaa uchi, uko *naked*, hauna mlinzi hata mmoja. Wageni wanajiingilia wanavyotaka na kutoka wanavyotaka. Utanisamehe Mheshimiwa Spika kwa kutumia neno hilo lakini maana yangu ni kwamba mpaka wetu hauna ulinzi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Naomba usilirudie.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Sawa Mheshimiwa Spika. Nimezingatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema kwamba mpaka ule hauna ulinzi hata kidogo. Sasa utakuta raia wa kutoka nchi jirani ya Rwanda hawana *control*, wanaingia mchana wanatoka mchana, hakuna hata askari wa kuhoji kwamba wewe unatoka wapi, unaelekeea wapi. Sasa ufile wakati Serikali yetu na Wizara yetu ihakikishe kwamba inalinda mipaka yetu ili raia wa kutoka nchi jirani wasiingie ovyo ovyo. Kwa kuruhusu hivyo tunakuwa na matatizo ya kuruhusu majambazi ambao wanashambulia sana raia wetu wa Karagwe na kuifanya Karagwe iwe kama nchi ambayo haiwezi kukalika.

Mheshimiwa Spika, mmesikia matukio mengi sana. Juzi kuna watu wameuawa kwenye eneo moja linaitwa Uzuri wa Kondoo, ukiwa unatoka Karagwe Mjini unaelekeea Ngara kuna eneo linaitwa Pori la Kimisi, hilo sasa ndiyo ngome kabisa ya majambazi.

Sasa nilitaka kumwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwamba watuwekee kituo cha polisi cha kudumu, hili limekuwa ni ombi la muda mrefu. Wananchi wa Karagwe wanaomba kituo cha kudumu, sio kituo cha muda. Kituo cha Kudumu katika lile pori ambapo ndiyo ngome ya majambazi na nadhani hili sio gumu kwa sababu tuna uwezo wa kujenga kituo, tunaweza kupeleka maaskari pale, tunao uwezo kabisa wa kuhakikisha kwamba ile njia inapitika kutoka Karagwe kwenda Ngara.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karagwe inayo majimbo mawili, jimbo la Karagwe pamoja na jimbo la Kyerwa. Ni Wilaya kubwa sana lakini Wilaya ya Karagwe inacho kituo kimoja cha polisi ambacho kiko Karagwe Mjini panaitwa Kayanga. Hicho kituo kimoja kinahudumia majimbo mawili, jimbo la Karagwe pamoja na jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha sana ni kwamba kituo hicho kinalo gari moja la polisi. Sisi kule tunaita *defender*. Hiyo gari moja ndiyo inayotumika kuzunguka kusaidia kukamata majambazi au kupambana na uhalifu katika Wilaya nzima ya Karagwe. Lakini tuna vituo vingine vidogo vidogo kwa mfano Kituo cha Chabalisa, Nyakakika, Nyakasimbi, Nyakahanga, Kihanga hivyo vituo vyote vinao askari lakini askari wale hawana hata pikipiki. Kwa hiyo, inapotokea kwamba uhalifu umetokea kule Karagwe askari wetu kwa kweli wanajitahidi sana kupambana na uhalifu, isipokuwa hawana nyenzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe kupitia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ya Usalama wa Raia iangalie jimbo la Karagwe kwa namna ya pekee kama sehemu ambayo iko mpakani, kama sehemu ambayo inashambuliwa na wimbi la majambazi kuliko sehemu zozote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wasaidie Karagwe tupate magari yasiyopungua matano. Wilaya ya Karagwe tupate pikipiki za kupambana na wahalifu zisizopungua 20 na tukifanya hivyo nina hakika kabisa wananchi wa Karagwe kwa mara ya kwanza watapata usingizi. Kwa sababu ninapozungumza hapa hata mimi mwenyewe wakati nikielekeea huko huwa naenda kwa wasi wasi na wakati mwingine naomba nipate *escort*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nirudie tena kwamba naunga mkono hoja nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, na mimi niseme nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza machache kidogo kuchangia hotuba nzuri sana ya Wizara ya Usalama wa Raia. Niseme tu nawapongeza wote walioshinda kihalali kushika nafasi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu wewe na Naibu Spika, naomba kuweka rekodi sawa, wewe hukushinda kwa kura nyingi wewe ulipitishwa bila ya kupingwa. Sasa ni vizuri tuweke rekodi sawa ndani ya Bunge letu. (*Makofi*)

Sasa baada ya hapo napenda nichangie kwenye hotuba hii. Wenzangu wengi wameeleza mambo ya msingi kuhusu askari. Askari wana matatizo na matatizo yao kama hayakusemwa hapa basi hapania mahali pengine pa kusemea. Sasa utuvumilie kwa sababu kila mmoja atakayekuja anazungumza pensheni, atakayekuja anazungumza haki, anazungumza uhamisho, pesa za wafiwa ndiyo matatizo yenye hayo. Mtu anakufa anakuja Dar es Salaam, anakopa fedha anachukua fedha za urithi anakopa anarudi hakuzipata, anakopa tena mara ya pili hata akizipata inakuwa balaa kubwa. Sasa kwa nini watu kama hawa wanaokufa wasipelekewe fedha zao kwa wakati angalau ikaonesha kuwa na nyie mnajaribu kuwa-*console* wale wafiwa.

Lakini la pili ni hili walilolizungumza watu wengi hapa kuhusu pensheni. Mimi nafikiri wakati umefika wa kuletwa sheria humu Bungeni, askari hata kama wanachagua wenye hui wapate hiyo bakshishi iliyozungumzwa na Mheshimiwa aliyetangulia hapa lakini *at the end of the day* kwa sababu anaathirika, mimi nafikiri wakieleweshwa vizuri watakubali. Kwa sababu wao ni binadamu na mwisho wa siku wakiangalia maisha yao yanakuwa mabaya, hawatakuwa na tatizo katika hilo.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri basi wakati umefika wa kuletwa sheria ili iweze kuwaruhusu na wao sasa wawe wanaweza kupata pensheni ambayo itawasaidia katika maisha yao. Ebu tuwaangalie wale watu ambao wanapata pensheni kubwa na wakishaacha kazi basi hali ya maisha inakuwa mbaya. Mfikirie askari kama huyu ambaye amepata kitu kidogo kile na ikawa ndiyo mwisho wa habari kwa kweli anaweza kufa kwa kuchanganyikiwa tu. Hilo lilikuwa la kwanza kuhusu maslahi na haki ya askari na nafikiri ujumbe umefika hatuna haja ya kurudia sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilivyoiangalia hii hotuba kwa mara ya kwanza niko Bungeni hapa kipindi cha tatu. Lakini nimeiangalia hotuba hii nimeona inaonekana ipo nia ya kweli sasa ya kufanya mabadiliko katika Jeshi la Polisi. Sasa kuweka maneno mazuri haya kwenye kitabu ni hatua moja lakini kuyatekeleza ni kitu kingine. Lazima tuwaambie askari wadogo ndio wanaolalamika hawa wakubwa aliowasema Mama Maghimbî wana vitu vivilvyotoka hapa, huwezi kuwaonea kwa sababu na wao si wako karibu na jiko. Lakini mfikirie askari mdogo ambaye yuko katika kituo cha Wete, Karagwe au Mbeya ambaye unamwambia nakupandisha cheo unafikia *Serjeant*, lakini inapita mwaka mzima hajapata hiyo posho ya kuwa yeye kweli ni *Serjeant*, unamsikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni hapa Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu swalii akasema wanapeleka madeni wanayodaiwa na askari na walisema watakuwa wamepata mwanzo wa mwezi huu wa saba. Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yako mpaka sasa hivi kuna wengine ambao hajapata tena wengine ni hapo Wete tu. Sasa ikiwa Wete hayajafika, mfikirie aliyeko Bukoba atasemaje? Mimi nafikiri mbali na kusema maneno mazuri lakini mtende matendo mazuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimeshafanya kazi ya kuwasemea askari, sasa nataka kuwasema wao. Wabunge jana kama uliwasiliza wengi wanawalalamikia sana mkusanyiko wa wafungwa magerezani, mahabusu na magerezani. Yuko mwenzangu

mmoja akasema watu wengine wanagunduliwa wakifika kule kuwa wamefungwa kwa kuonewa tu.

Mheshimiaw Spika, tuna tatizo na tatizo hili ni tatizo kubwa, kwa sababu tatizo tulilonalo kuwa Idara ya Upelelezi ya Jeshi la Polisi kwa maoni yangu mimi ni dhaifu sana. Uwezo wao wa kuchunguza na wakapata ushahidi wa kosa la mtu aliyelifanya ni mdogo. Sasa sijui ni ile *capacity* maana yake *intellectually capacity* tu anayo *lack* au ana *lack of efficiency* yenyewe kuwa hataki kufanya kazi au vipi. Sasa kama ni *intellectually capacity* ni suala la Waziri ni suala la Idara nzima ya Polisi kujenga uwezo basi wa hawa watu. Wasomesheni na muwapeleke wakasome ili waweze kuelewa nini wanakifanya na wanakifanya kwa muda mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika *professional investigation* mbali na kumjua huyo *offender* lakini pia unatakiwa upunguze idadi ya watu unaowasumbua katika kumpata huyo mkosaji. Leo ikiwa itakuja taarifa ataambiwa Kamanda wa Polisi wa Dodoma labda basi namba fulani kuna mtuhumiwa wataonja joto ya jiwe, wote waliomo kwenye gari maana yake wataitwa kituo cha polisi, watashushwa, watachuchumaa na hata wakaonja buti moja moja. Sasa mimi nafikiri katika kufanya kazi, vitu kama hivi havisaidii. Watu wasisumbuliwe kwa sababu amekosa mtu mmoja na haya yanatokea kwa sababu mara nyingine wapelelezi hawa hawajui wanaanzaje. Ni suala lile nililolisema la *intellectually capacity* ambayo inahitaji kujengwa. *You have to have capacity building with this unit* kama tunataka kweli kufanya *reform* katika jeshi la polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma palikuwa na kitu walikuwa wanaita *case management flow system*. Hii ilikuwa inakusanya wadau wote wa kutoa hukumu. Polisi wanakaa pamoja, Mahakama wanakaa pamoja na watu wengine wote. Hii ilikuwa inasaidia katika kuona hili kosa lililofanywa likoje na ni nani kwa hali hii wanahuksika. Sijui kama mpango huu Mheshimiwa Spika, unaendelea na kama hauendelei basi kwa nini? Kwa sababu ulikuwa unasaidia.

Mheshimiwa Spika, lingine kule kwetu Zanzibar askari wanalamika kidogo. Wanalamika kukatwakatwa fedha hivi kuchangia michezo sijui kuchangia kitu gani. Sasa kama huu ni utaratibu katika nchi nzima, *that's fine*, lakini kama unafanyika Zanzibar kama wanavyolalamika basi ni vizuri ukaondolewa au ukafanywa ni *uniform*. Kwa sababu tunaelewa sasa hivi masuala ya michezo yanashughulikiwa na Serikali kwa ujumla sasa huna sababu wa hizo pesa chache anazozipata huyu mnyonge askari polisi unazikata unasema achangie michezo, michezo gani sasa.

Mheshimiwa Spika, kama tunataka michezo kujenga kweli kwa nini Idara haitengi fungu maalum wakasema *okay*, tunapeleka vifaa vyta michezo katika sehemu hii. Msiwachangishe watu wanyonge mkawapa nafasi ya kuwalalamikia bure tu. Ionekane wanalamika sababu ya msingi kwa sababu wanazimishwa lakini kwa vitu vidogo vidogo mimi naomba tusiviruhusu. (*Makofi*)

Halafu kuna kitu kimoja ambacho nakiona siku mimi pengine ni maendeleo lakini mimi nafikiri kiuchumi inaathiri. Zamani tulikuwa tumezoea kuwaona askari polisi

wakiwa wana gari zinazofanana fanana sana. Inawezekana zote zilikuwa *Landrover* labda wale walalahoi walikuwa wana *Landrover* za wazi na dhaifu dhaifu na wale wakubwa wao walikuwa na *Landrover* nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi kwa maendeleo ya nchi yetu labda kwa nia ya kujenga uwezo wa Jeshi la Polisi magari yanakuwa na tofauti nyingi yaani *make* mbalimbali za magari. Sasa hii *maintenance* yake inakuwa ngumu. Sisemi iondolewe, lakini nasema iangaliwe kama kuna namna ya kufanya bora zaidi katika *ku-save* fedha ya Serikali na katika kuongeza uwezo wa utendaji wa kazi basi si vibaya ikaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna suala la dawa za kulevyta. Dawa za kulevyta kila mtu anakuja hapa analalamika na mimi sisemi kuwa polisi hawafanyi kazi, wanajitahidi lakini mwisho wa siku hatuoni ufuatiliaji na kutangazwa hasa maana yake unaweza kuona kwenye *TV* leo labda mtu amekutwa na kete 50, 60 za dawa za kulevyta ameshuka kutoka nazo Pakistan kwa mfano au mahali popote. Sawa tunaziona lakini unaweza ukaambiwa huyo ni mbebaji pengine sasa huyo aliyemtuma akabebe sasa nani au kama ni yeze amepewa hukumu gani ili wananchi mtupe moyo wa kuwa mnafuatilia haya mambo, ni vizuri mkatoa taarifa za dawa za kulevyta ikiwezekana kila mwezi kwa kupitia magazeti. Watu wakaona hili suala linafuatwa. Vinginevyo watu watafikiria hili jambo liko holela holela tu kama walivyosema Wabunge wengi tu hapa. Unamwona mtu mchana ikifika jioni unamwona kalala hujui usingizi huo ni wa nini kumbe tayari ameshapakia vitu ambavyo sio vyta kawaida. Jamii inaharibika, vijana wanaendele kuathirika na wakamataji ni polisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho mwenzangu mmoja alisema hapa tena yeze alikwenda mbali zaidi akasema askari hatuwataki kule Pemba. Mimi sisemi hivyo lakini kuna msemo unasema, adhabu ya kaburi aijuae ni maiti mwenyewe au aibu ya maiti anayeijua ni yule anayemuosha. (*Makofî*)

Sasa sisi Pemba kwa bahati na nasema ni bahati mbaya kwa sababu askari wote si ni ndugu zetu jamani hakuna askari anayetoka Afrika ya Kusini hapa, hakuna askari anayetoka Uingereza hapa. Askari ni Mtanzania awe wa Pemba, Unguja, Tanga au Kagera inakuwaje sasa basi wanawafikisha watu kuwachukia ni matendo yao?

Mheshimiwa Spika, karibu na uchaguzi hapa walikuja askari wengi pale Pemba kuja kusimamia uchaguzi, mimi nikamwuliza Kamanda wa Polisi wa Mkoa vipi mambo haya? Akaniambia usiogope hawa ni *auxiliary police*. Alaah, ni *auxiliary police* wala hawatakuwa na matatizo. Nikamwambia sawa. Siku ya pili napita namkuta *auxiliary police* ana *SMG* ameibeba hapa. Sasa *auxiliary police*, lakini yeze ndiyo mwenye silaha, yule *main plice* maana *if you are talking on auxiliary* kuna *auxiliary verb* na *main verb*. Sasa yule polisi mwenyewe hana kitu lakini yule *auxiliary* huyu ndio ana silaha. Ukaenda vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya uchaguzi wenyewe tu furaha za matokeo ya uchaguzi madhara yakawapata watu. Nasema yakawapata madhara watu kwa sababu hata Jeshi la Polisi kwa bahati nzuri walileta Tume kuja kuchunguza yaliyowafika watu ingawa hiyo Tume mimi nasema humu Bungeni haikufanya kazi nzuri kwa sababu watu

wengi waliofikwa na maafa hawakuwaendea haki, labda waliamua waje wakae Wete kwenye hoteli nzuri, waje wakae Chwaka kwenye hoteli nzuri na kwa sababu wao ni wakubwa waite watu. Watu waliofikwa na mashaka hawaitwi, wanafuatwa wanaulizwa. Mtu jana ameshaibiwa, ameshapotelewa mali yake halafu wewe unamtegemea kumwita Chakechake aje, haji, anaona unakwenda kumsumbu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naamini kuwa dhamana ya ulinzi wa raia iko mikononi mwa askari polisi ndiyo Katiba inavyosema. Yeyote atakayemsaidia askari polisi kufanya kazi anamsaidia, lakini pakitokea uharibifu tunaoweza kuwajua umesababisha watakuwa ni polisi. Sasa mimi nina hakika polisi wa kawaida hawezu kuleta matatizo lakini wakubwa wao ndio wanakuwa na matatizo na ninavyoona hali sasa hivi *it comes from my heart from the top man* mpaka hawa ngazi ya Mawaziri, mimi naamini nia nzuri ipo ya kuleta mabadiliko ya kweli ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kusema tuwape muda polisi wajibadilishe na wabadilike. Tuwape muda Mawaziri waweze kuwatengenezea mustakabali na mwenendo mzuri askari polisi ili manung'uniko yasiyokuwa ya lazima mionganii mwa Watanzania yasiwepo tena. Polisi wawe ni walinzi wa kweli wa mali na usalama wa watu kuliko ndio sababu ya matatizo.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuna ugomvi na polisi, polisi tunawapenda kwa sababu tunawahitaji. Unaweza kumwona polisi ni mbaya kama ameku-*harass*, lakini wakati huo huo ukija ukiyamiwa na majambazi akikuokoa kama ilivyotokea hapo Zanzibar juzi mlinzi wetu mmoja anawazuia majambazi ameuawa ye ye ndiyo mambo yenye hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa vyote vyote inavyokuwa tunawahitaji lakini pamoja na kuwahitaji huko wanahitaji waelekezwe namna nzuri ya kufanya kazi ili raia wawapende askari na wasiwalalamikie.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na nawatakia kheri hawa rafiki zangu wawili waliopewa dhamana ya Wizara hii ya Usalama wa Raia, mimi naamini Mungu atawasaidia kufanya kazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia ni dakika chache mno haziruhusu tuendelee. Napenda kueleza tu utaratibu kwamba saa 11.00 jioni nitatoa nafasi kwa mchangiaji mmoja tu na safari hii natoa nafasi kwa Chama cha CHADEMA. Kwa hiyo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, atakuwa msemajii wa mwisho. Baada ya hapo saa 11.15 jioni nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kuanza kujibu hoja kwa robo saa na atafuatiwa na mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia saa 11.30 jioni hadi saa 12.30 jioni ni muda wa saa moja. Halafu hiyo itatupa fursa ya kuingia katika Kamati ya Matumizi kwa muda wa saa moja na robo. (*Makofi*)

Nikumbushe tu ili tusipate matatizo wakati wa Kamati. Kifungu kinachohusu Mshahara wa Waziri kinatakiwa kitumike kuhoji mambo ya sera. Ukitaka kuulizia mbwa

wa polisi, usiende kwenye kifungu cha mshahara wa Waziri kwa sababu sitakuruhusu. Ukitaka gari la kituo cha polisi siruhusu hivyo.

Waheshimiwa Wabunge mnazo takribani saa tatu za kijiandaa, yote yamo katika vitabu viwili, tusiwe tunakwama tu mshahara wa Waziri kwa kila kitu. Kama ni gari utaona sehemu ya ununuzi wa magari ya polisi basi unakwenda hapo. Huduma za mbwa wa polisi, utafika mahala kuna kifungu chake. Lakini ninyi mnasimama badala ya kuuliza sera kwa mfano. Unaweza kuuliza sera kuhusu idadi nzima ya Jeshi la Polisi kama linatosheleza kwa mazingira ya sasa. Hiyo ni sera, hiyo nairuhusu kwenye mshahara wa Waziri kwa sababu unauliza swali linalohusu sera juu ya ukubwa wa Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, naomba muende mkavitzame kitabu cha pili na cha nne, ili tunapopitisha makadirio tuweze kwenda kwenye ufanuzi ambao una upeo na upana wa kutosha kuliko kubaki pale pale penye kifungu kimoja halafu tunanyima nafasi kwa wale ambao wanataka kuulizia kuhusu maendeleo kwa mfano kitabu cha nne ili nako tuweze kupata ufanuzi.

Kabla sijafunga nilikuwa napenda kutoa taarifa tu kwamba Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, anaendelea vizuri huko London na naomba sote tuendelee kumkumbuka katika dua zetu ili aweze kurejea nyumbani salama baada ya kuwa amefanyiwa upasuaji mdogo tu. Kwa hiyo, kwa kuwa tumefika muda wa kusitisha shughuli za Bunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni. (*Makofî*)

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Naona Mtoa hoja hajaja, lakini naona Waziri, Mheshimiwa Mary Nagu ndio Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa jioni hii. Tunampongeza sana. Kila mara akina mama wakipata nafasi ya kuongoza inakuwa ni vizuri tu. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa kitinda mimba wa kuchangia hotuba hii ya usalama wa raia.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza mchangano wangu, napenda kukupongeza kwa taarifa uliyoitoa leo asubuhi ndani ya Bunge lako Tukufu na barua uliyoituma kwa Waziri Mkuu. Naamini ataifanyia kazi ili yale yote uliyoyasema, yaweze kutekelezeka na tuache kuingiliana katika kutenda kazi zetu. Nakupongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri pamoja na Naibu wake, pamoja na Watendaji wake wote walioweza kuandaa Bajeti hii na hata leo kusomwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Ninaomba basi yale yote yalioandikwa katika kitabu hicho cha hotuba yaweze kutekelezeka ili Watanzania waweze kuyapata yale waliyokuwa wanayategemea kutoka Jeshi ya Polisi na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimpongeze *IGP* kwa kazi yake nzuri aliyoweza kuifanya kwa kipindi hiki kifupi na kuweza kurudisha heshima ya Jeshi letu la Polisi, ambapo Watanzania wengi walikwishakata tamaa kwa matukio yaliyokuwa yanatokea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hili nawapongeza pamoja na Makamanda na Makamishna wote kwa ushirikiano wanaompa *IGP* na kuweza kuyatekekeleza yale yote ambayo Watanzania wanayategemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajua kabisa siku zilizopita tulikuwa na tatizo la ujambazi katika nchi yetu, lakini Jeshi letu la Polisi kwa muda mfupi, limeweza kulishughulikia tatizo hili na sasa nchi yetu inarudi kuwa na amani na wananchi wanakuwa na utulivu, kwa sababu tatizo hili liliwatia uwoga sana wananchi hasa katika mali zao na hata kupoteza maisha yao. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyokwishaifanya mpaka sasa.

Pia, napenda niwapongeze Askari wetu wa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, wamejitoa kulitumikia Taifa lao, kuwalinda Watanzania pamoja na mali zao. Lakini ninaomba Askari hawa ambao wamejitoa na wanafanya kazi katika mazingira magumu, waangaliwe kwa sababu wanapoteza maisha yao, wanaacha familia zao zikiwa hazina mzazi mmoja ambaye walikuwa wanamtegemea. Hivyo, ninaomba wale wote ambao wamepoteza maisha katika kuitetea nchi yetu na katika kupambana na hawa majambazi, basi familia zao ziangaliwe na tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. (*Makofi*)

Pia, niwapongeze wananchi kwa kuweza kutoa ushirikiano kwa Jeshi letu la Polisi na ninaomba Askari wale wanaopewa ushirikiano na wananchi kwa kutoa taarifa za Wahalifu, basi taarifa zile ziweze kutunzwa na wasiende kutoa tena taarifa hizo kwa wale wahusika. Kwa sababu ziko taarifa kwamba, wako Askari wachache ambao sio waaminifu wanashirikiana na wahalifu, wananchi wanapotoa taarifa zile hurudi kwa wahalifu wale na kuwaambia kwamba fulani katoa taarifa na hii inawakatisha tamaa wananchi kushirikiana na Jeshi letu la Polisi katika kutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema, Askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hawana vifaa na zana za kisasa na wanapokutana na majambazi hao, unakuta majambazi wana vifaa zaidi ya vile walivyonavyo Askari wetu. Kwa hiyo, tunaliomba Jeshi letu la Polisi liwapatie vifaa Askari wetu hawa na kikubwa zaidi, wawapatie *bullet proof* za kuweza kuwakinga na risasi, kwa sababu wanapopambana na majambazi, hayana huruma. Kwa hiyo, vitu hivi ni muhimu vikapatikana ili viweze kukinga maisha ya Askari wetu. Pia, ningependa mishahara na posho zao zitazamwe upya. (*Makofi*)

Lingine ni nyumba za Askari. Jana tumesikia wakati wakichangia nyumba za Magereza wanazoishi Askari hao, hazina tofauti na za Maaskari wa Jeshi la Polisi, nyumba zimechakaa hazina nafasi za kutosha, zina chumba kimoja na sebule na kutokana na mila zetu, baba, mama na watoto hawawezi ku-share chumba kimoja, hivyo

tunaomba hili suala la nyumba litazamwe, ili Askari hao wanapotoka kwenye kazi ngumu hizi, usiku kucha, basi wapate mahali pazuri pa kumpukiza ili waweze kuzifanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi upande wa pili wa Shilingi kwa sababu yale mazuri nimekwishayasema na kwenye mazuri, yako mabaya. Ningependa kuyasema sasa kama ifuatavyo: Kumekuwa na taarifa na mengine tumeshuhudia, Polisi kutumia nguvu za ziada, pale mshitakiwa anapokuwa ameshakubali kuwa chini ya ulinzi, lakini bado anaendelea kupata kipigo na hatimaye hata kupata kilema na wengine hata kusababisha vifo.

Mheshimiwa Spika, tungependa suala hili litazamwe, kama mtuhumiwa yule ameshakubali kuwa chini ya ulinzi, basi taratibu zinazotakiwa zifuatwe, sio kwa kipigo na wengine wamekuwa wakilalamika kwamba wanapofikishwa Polisi, huwa wanalazimishwa kusaini maelezo ambayo sio wao waliyoyatoa na wanakubali kusaini kwa sababu wanakuwa wamepata kipigo na kwa kuhofia usalama wao, inabidi wakubali kusaini maelezo ambayo hawakuyatoa wao na sio ya kweli.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na tatizo lingine la kuwasingizia watuhumiwa kesi za uwongo ambazo zinakaa muda mrefu katika Mahakama zetu kwa kukosa ushahidi na kesi hizi nyingine kwa sababu binafsi, watu hufunguliwa kesi hizi. Wanapofunguliwa hizo kesi, inachukua muda mrefu sana wananchi hawa wanateseka katika Mahabusu zetu na hii inachangia kuongezeka kwa watu katika Magereza ambayo jana tulisema zitafutwe njia ya kupunguza msongamano katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaamini hili likifanyiwa kazi, litaondoa msongamano ulioko katika Magereza zetu.

Mheshimiwa Spika, baya zaidi, katika kesi hizi za uwongo, nyingi zinakuwa ni zile za mada ambazo mtu anaweza kukaa Gerezani zaidi ya miaka mitano na mwisho wa yote, akipelekwa Mahakmani wanatoa taarifa kwamba upelelezi umekamilika na mshitakiwa hana hatia. Lakini muda wote aliopotezewa mshitakiwa hana hatia. Lakini muda wote aliopotezewa mshitakiwa huyu, miaka mitano amekaa Gerezani, ameshindwa kuitumikia familia yake, imeteseka, halafu mnambawambia hana hatia.

Mheshimiwa Spika, tungeomba haya yatazamwe ili Watanzania waweze kurudisha imani yao kwa Jeshi letu la Polisi. Pia kumekuwa na taarifa kwamba wanapofikishwa Watuhumiwa wale katika Kituo cha Polisi, huwa wanalazimika kuchangia gharama za usafiri na hata chakula. Mtuhumiwa anapopelekwa pale, hawapati chakula. Matokeo yake, wanawaambia ndugu zao wakanunue chakula wawalettee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu sio utendaji mzuri wa Jeshi la Polisi na kwa kuwa kuna fungu la kuwahudumia Watuhumiwa hawa, tungeomba kazi hii ifanywe na Jeshi la Polisi na sio vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la watuhumiwa hawa kupata dhamana na kama tunavyoju, dhamana ni haki ya msingi ya mtuhumiwa. Ana haki ya kupewa dhamana! Yapo makosa ambayo tunajua hayawezi kustahili kupewa dhamana kama vile kesi za silaha na mada. Lakini zile kesi nyingine zote ambazo tuna hakika zinaruhusiwa kupewa dhamana tungeomba wananchi hawa au watuhumiwa wanapofikishwa Vituo vya Polisi, basi dhamana hiyo iweze kutolewa. Kwa kufanya hivi itapunguza msongomano katika Mahabusu yetu na katika Magereza yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya yakindeka, ninaamini wananchi watarudisha matumaini katika Jeshi lao la Polisi na wataacha kuchukua hatua ambazo wanazichukua hivi sasa kwa sababu wanaowakifika Polisi, wakati mwigine haki haitendeki au wale watuhumiwa kutofanyiwa haki.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie Askari wa Usalama barabarani. Hivi karibuni tumeona ajali nyingi zimetokea katika nchi yetu. Mimi swali ninalojiuliza, ni kwanini Askari hawa wanaruhusu magari haya machakavu, unakuta tairi zimechakaa, gari ina taa moja, lakini gari hizi zinaruhusiwa kupita au kuendelea na safari. Hii inadhihirisha kabisa kwamba wako Askari wachache ambao wanajihuisha na rushwa na kuruhusu magari haya kuendelea na safari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi, Askari hawa unakuta wamesimamisha malori barabarani na kuanza kupekua magari haya. Sasa ninachojiuliza, wamechukua kazi ya *TRA* ya kupekua mizigo iliyoko ndani ya malori hayo au kazi yao ni kuhakikisha magari yanayopita barabarani yana viwango vinavyotakiwa? Ninaomba Kitengo hiki cha Usalama wa Barabarani wale wachache wanaolipaka Jeshi letu la Polisi matope wawewe kuwaangalia na kuwaondoa ili Watanzania wanaopoteza maisha yao barabarani kwa kupanda vyombo ambavyo havina viwango vya kutosha waendelee kuishi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ningependa kuliomba Jeshi la Polisi liweze kufanya usajili upya wa silaha na kazi hii ifanywe na Jeshi lenyewe wasitoe kwa watu binafsi ili tuweze kujua ni wananchi wangapi wenye silaha wanazozitumia kihalali na zile ambazo sio halali, tunaliomba Jeshi la Polisi liendelee na zoezi hilo zikamatwe ili zoezi hili la ujambazi kwa kutumia silaha kali liweze kukomeshwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi. Ahsante. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMED ALI SAID:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa na ngumu unayoifanya katika kuliongoza Bunge hili. Ni ukweli usiofichika kuwa Jeshi la Polisi linafanya kazi ngumu na nzito kabisa katika ulinzi wa watu na mali zao katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mbali na Askari hawa kufanya kazi kama hiyo, lakini pia wanaifanya katika mazingira magumu. Kwa mfano, hawana nyumba za kuishi,

mishahara yao haitoshi na pia hawana zana za kisasa. Ninaombala Serikali iwaangalie Askari wetu kwa jicho la huruma kwa kuwapatia mahitaji hayo na pia, wapatiwe mikopo ili waweze kujiendeze kimaisha.

Mheshimiwa Spika, mimi kidogo nina masikitiko kwa baadhi ya Watendaji katika Jeshi la Polisi kule Pemba na hasa katika Wilaya ya Micheweni. Inaonekana kwamba, baadhi ya askari hawa wakati wa uchaguzi wanatumiwa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mgogoni, ninao vijana wawili walioshutumiwa kuwa walifanya fujo katika Kituo cha kujiandikisha Kupiga Kura. Vijana hao walitiwa ndani kwa muda wa wiki mbili na huu ni mwezi wa Saba bado wanakwenda Mahakamani, wakirejea nyumbani bila ya ushahidi kupatikana. Huu ni usumbufu mkubwa sana, kwani vijana hawa ni maskini. Ninaliomba Jeshi la Polisi lisiingiliwe kisiasa na wanasiasia. Naomba watende haki kwa Watanzania wote.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uhamisho ni kwamba, kwa kweli Askari wanachukua kipindi kirefu katika Kituo, Wilaya au Mkoa mmoja kwa mfano Askari ambao wamehamishiwa Pemba. Wapo Askari wa Unguja au Tanzania Bara ambao wapo huko Pemba kwa kipindi kisichopungua miaka 15 mpaka 20 mfululizo bila kuhamishwa. Hivyo hivyo na walioko Unguja na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa athari ya mtu au mfanyakazi kukaa sehemu moja kwa kipindi kirefu. Jambo hili linasababisha utendaji mbaya na hivyo kutopatikana ufanisi mzuri wa kazi. Hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri alirekebishe suala hilo. Pia, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie muda halisi kutokana na taratibu zao (*PGO*) Askari anatakiwa kukaa sehemu moja kwa kipindi gani.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linachelewa sana kuwapandisha vyeo Askari wetu. Kwa mfano, yule Askari ambaye alifanya kazi kwa kipindi cha miaka 32, Askari yule alipata cheo cha Koplo mnamo mwaka 1990, yaani baada ya miaka 18 na hadi alipostaifu ana cheo hicho hicho.

Sasa tujiulize, Askari huyu alikuwa ni mtukutu ama vipi? Kama ni mtukutu, kwa nini alipewa sifa nzuri wakati alipostaifu? Ninamwomba *IGP* Saidi Mwema alienzi jina lake la Mwema kwa vitendo, kwa kuwajali sana Askari wake ili nao wamsaidie kivitendo.

Mheshimiwa Spika, suala la vizuizi barabarani ni zuri sana iwapo vizuizi hivyo vitawekwa kwa mpangilio mzuri. Lakini kuna vizuizi vingi sana katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, yaani sasa umekuwa ni utamaduni, kwani katika Vituo vyote ukitoka Mjini hadi shamba vimewekwa vizuizi hivyo bila hata kuwepo na jambo maalum.

Mheshimiwa Spika, vizuizi hivyo haviondolewi, sio usiku, sio mchana, labda akipita Kiongozi wa Juu, yaani Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waziri Kiongozi, *IGP* na wageni mashuhuri, hapo vizuizi hivyo vitaondolewa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze, ni kwa nini vizuizi hivi vinakuwa vya kudumu?

Mheshimiwa Spika, mwisho nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri ambayo kama itatekelezwa kwa vitendo, italeta mafanikio mema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti sana, kwani ndiyo inayolinda amani ya nchi na raia wake na bila amani mengine yote huharibika. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara hii mpya ili iweze kutekeleza kazi yake ya kulinda raia. Wote tumeshuhudia jinsi majambazi yalivyokamatwa kwa kipindi kifupi.

Pili, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Inspekte wa Polisi, *IGP*, Mwema, kwani anafanya kazi zake kwa umahiri na umakini mkubwa. Kuna taarifa kuwa watu wameamua kuchukua sheria mikononi mfano, kuua na kuchoma moto watuhumiwa wa wizi mbele ya Askari. Hii imekuwa inatokea kutokana na wananchi kutokuwa na imani na Jeshi la Polisi. Hii ni kwa sababu Polisi hawa wamekuwa wakishirikiana na majambazi. Tunaomba wale Polisi wote wanaofanya hivi, waache mara moja, kwani wanalipaka tope Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine, ni vyema Askari hasa wenye vyeo nya juu kama *RPC*, *OCS*, *OCD*, wasikae kwenye Kituo kwa muda mrefu, kwani kibinadamu, wanazoeana na wananchi ikiwa ni pamoja na makundi yote katika jamii ile kama majambazi, wahusika wa dawa za kulevyta na kadhalika. Kwa mantiki hii ya mahusiano mema, inakuwa ngumu sana kutoa taarifa kuhusu maovu yao.

Mheshimiwa Spika, makazi ya Polisi yawe ya peke yao, wasichanganywe na raia kwani watajenga mahusiano na wananchi na hivyo kushindwa kufanya kazi zao kwa haki.

Mheshimiwa Spika, suala la ajali za barabarani nalo linatia shaka. Kama kweli Askari (*traffic*) wetu wako makini, iweje gari la abiria 30 libebe abiria 74 halafu Askari wa barabarani wasione? Iweje abiria wapande malori halafu Askari waruhusu?

Mheshimiwa Spika, *Traffic* wengi wamekuwa wakifanya mambo ya ajabu kabisa kwa mfano, hujificha pembedi mwa barabara na baadaye hutokeza ghafla na tochi zao za kupima *speed*. Hii inaweza kusababisha ajali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, suala la kuripoti wahalifu kwa Polisi halafu unaambiwa ulete gari au uweke mafuta gari yao, ni la ajabu sana! Tunaomba kwanza Vituo nya Polisi viwe vinapewa magari na magari hayo yawe na mafuta na yawe mazima, kwani hali hii imesababisha wananchi wahisi kuwa hiyo ni mbinu ya Polisi ya kuficha wahalifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Polisi na siasa, ni jambo la kushangaza kuona Polisi wanaleta fujo na kujihusisha moja kwa moja na siasa. Tumeshuhudia jinsi Jeshi hili lilivyowataabisha wafuasi wa Vyama nya Upinzani, lakini hapo hapo wakiwalinda

sana wafuasi wa Chama Tawala. Sasa, nauliza hivi, Polisi ni sehemu ya Chama Tawala? Hata kama ni hivyo, ni kwa nini basi wasiwatendee haki wafuasi wa Vyama vy a Upinzani, kwani wote si Watanzania? Kazi ya Polisi ni nini?

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kuwapongeza sana Watendaji wote wa Wizara ya Usalama wa Raia.

**MHE. CHRISTOPHER O. SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Waziri wa Usalama wa Raia. Kipekee, nampongeza Bwana Bakari Mahiza kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Watendaji wengine wa Wizara, Mikoa na Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Saidi Mwema, Inspekte Jenerali kwa kuteuliwa kwake kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini. Tunatambua na kuthamini uwezo, uadilifu na umakini wa Inspekte Jenerali Mwema na wasaidizi wake kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi nchini. Wapiganaji wetu wameonyesha utii mkubwa kwa Taifa letu, kwani kwa muda wote wamekuwa wakiu hakikishia umma usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro, naomba niwasilishe ombi lao la kupatiwa uongozi wa ngazi ya Wilaya kwa maana ya Mkuu wa Polisi Wilaya (*OCD*) na Maafisa wengine wanaopaswa kumsaidia. Wilaya ya Simanjiro ilianzishwa rasmi mwaka 1993, lakini hadi sasa hatuna *OCD*, badala yake tumekuwa tunatumia Polisi wa Wilaya nyingine. Wananchi kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa Askari wa Jeshi la Polisi, wameamua kujenga Vituo vya kisasa vya Polisi pale Mererani, Komolo na Orkesemet ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya. Najua Kituo cha Orkesemet ambacho kinatarajiwa kuwa Ofisi ya *OCD* bado kipo kwenye hatua ya kukamilishwa, ila nashauri Serikali sasa ituletee *OCD* na kutusaidia kujenga nyumba yake.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kipindi kifupi walichochaguliwa. Hakika tumeona kazi nzuri na kubwa wanayoifanya. Natoa pongezi nyingi.

Mheshimiwa Spika, ningependa japo inachosha kusikia Kilindi kila mara, lakini ndiyo maana nipo hapa. Naomba mnivumilie. Nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kutupatia gari la Polisi jipya katika miezi hii ya karibuni. Kulingana na ukubwa wa eneo la Kilindi, gari hili limekuwa ni msaada mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie matatizo yetu kama ifuatavyo: Kwanza, ni kwa sababu ni Wilaya kwa mwaka wa nne sasa, ni vyema tukapeva *OCD* kwani hadi sasa tunasimamiwa na *OCD* wa Handeni na hii inasababisha usumbufu mkubwa kwa Askari na watuhumiwa wa Kilindi. Gharama ya mafuta kwenda kila siku Handeni ni upotevu usio na sababu, achilia mbali usumbufu kwa wananchi.

Pili, Kituo cha Polisi ni chakavu sana, kibovu kiasi kwamba hata mahabusu wanaweza kutoroka na ni hatari kwa Askari wanaolinda. Kilindi tunalo eneo lililotengwa na Halmashauri na wananchi wameanza kuchangia nguvu zao kwa kufyatua matofali. Tunaomba msaada wa Serikali.

Tatu, makazi ya Polisi ni aibu. Wanapanga mpaka kwenye nyumba za udongo. Sasa, Askari anayesimamia mazingira magumu ya usalama anakaa nyumba ambayo ukipiga teke inabomoka! Naomba sisi tuanze, Serikali mtuahidi kutupa msukumo wa kujenga *barracks*.

Nne, ni kuhusu vifaa. *Uniform* ni chakavu kiasi kwamba inadhalilisha Jeshi la Polisi na naomba wapatiwe vifaa vyta kutosha na hususan *uniform* na viatu na silaha za kutosha.

Tano, kwa sababu eneo la Kilindi ni kubwa, tunaomba tushirikiane tuone namna ya kujenga *Police Posts* angalau kila Kata, ili kuhakikisha haki inatendeka na wahalifu kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nategemea majibu mazuri na ushirikiano.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Usalama wa Raia kwa asilimia mia moja. Pia, niwapongeze wataalam wote kwa kuanza kutuleteza hotuba safi na Bajeti inayotia matumaini. Nategemea kwamba itawaweka vizuri Askari wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana marekebisho yatakayofanywa kwenye *PGO*. Lakini naomba sasa mkataba wa kiinua mgongo ikifika miaka 12 uondolewe. Kuwe na pensheni tu na wale wote ambao wamenaswa na mkataba huo wapate msamaha, wote wawe penshenia ili wafanye zile kazi vizuri. Sasa umefikia wakati wa kuwepo Kikosi cha Polisi cha Doria wanaovaa nguo za kiraia. Hivi sasa twende na wakati wa kuwafanya mitego majambazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Lakini vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Harith Bakari Mwapachu (Mbunge), kwa umahiri mkubwa alionao wa kubadili *the whole image* ya utendaji wa Polisi hapa Tanzania. Anaweza kwa kiasi kikubwa kurudisha imani ya wananchi wa Tanzania. Pamoja nae, niwapongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Mohamed Abood, *IGP* Mwema na Watendaji wote Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inawagusa wananchi moja kwa moja na ni Wizara mtambuka. Ni Wizara inayoleta matumaini au kuvunja miyo raia na ni upesi kutambulika uwezo ilionao na hajifichi kama kuna utendaji usio sahihi. Ninachoomba, wajitahidi kwa sasa hivi ni:-

- (i) Kuunda chombo cha upekuzi ndani ya Idara yenyewe ili kuwatambua Watendaji wanaoyumbisha wale Watendaji waaminifu;
- (ii) Ni wakati muafaka sasa kuangalia suala la uajiri na ingekuwa vizuri wanaaoajiriwa wakawa wanatokea kwenye Taasisi kama vile *JKU* na *JKT*;
- (iii) Watoto wa wakubwa kuajiriwa ndio chanzo cha kuleta mtafaruku kwenye Jeshi hilo kutoka Tanzania Zanzibar au hata Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, majambazi wazuri, mara nyingi wanakuwa ama Maafisa wastaafu wa Majeshi yetu kama vile Polisi, JWTZ na kadhalika, kwa maana raia wa kawaida hawezi kutumia silaha nzito nzito kama vile *SMG* na hata bastola ya kawaida na hana taaluma ya kupanga ujambazi. Haya yote yanapangwa na ama wale wastaafu wakishirikiana na majambazi, wao wakiwemo kwenye operesheni yenyewe au Askari wasio waaminifu ambao ni Maafisa fulani wakapange njama kushirikiana na majambazi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, Askari wote wastaafu kama Polisi, Jeshi, Vyombo vyta Usalama na kadhalika, wawe wanafuatilia nyendo zao kwa karibu zaidi, maskani yao na wanaoshirikiana nao, hata kama tayari wako katika mazingira ya kiraia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujambazi katika sehemu za mahoteli ya utalii, Zanzibar yaelekeea kuwa sasa mapato yao makubwa yanatokana na utalii maeneo ya Kanda za Pwani kama vile Matemwe, Pwani Mchangani, Chwaka, Urowa, Bwejuu na Jambiani, ni mahali ambapo wahalifu na majambazi wanafanya kila aina ya ujambazi.

Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, kwa vile Zanzibar tegemeo lao kubwa sasa ni utalii, basi tujitahidi kuimarisha ulinzi katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, suala la nyumba au makazi ya Askari, hili nalo linaongelewa kwa namna yake. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie makazi ya Polisi katika Mkoo wa Kaskazini Unguja, kwani nyumba ni chakavu sana, hakuna mahali pa kufanyia kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa za kulevya, Zanzibar dawa za kulevya zinaletwa na wafanyabiashara wakubwa na wanapata msaada wa Vyombo vyta Ulinzi na hasa Polisi. Ni ukweli usiofichika kwamba, wauza unga wakikamatwa na kupelekwa Polisi (vituoni) baada ya muda sio mrefu wanatolewa baada ya Wakuu wa Polisi kuwasiliana na wafanyabiashara hao. Hili nalo siyo la kujificha, tulitazame.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie machache kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Moja kwa moja, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, tatizo nililonalo na ninaamini ni kwa nchi nzima na pia ni kwa Wizara zote, ni nyumba za makazi za Maofisa wa Polisi na wengine wa Wizara nyingine. Kwa kuwa Serikali iliamua kuwauzia ma-*OCD/CID* nyumba za makazi ambazo walikuwa wanaishi kwa wadhifa wao na hivyo kuleta tatizo ambalo ninalizungumzia. Ma-*OCD/CID* waliofuata kuteuliwa au kwenda uhamisho walikuta hakuna nyumba kufuatana na utaratibu na haki zao kwani nyumba zao kwa wadhifa zimeuzwa na hivyo hazipo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutokuwa na nyumba hizi, basi inabidi wapange nyumba kwa makazi uraiani, gharama za pango ni kubwa, wengine wanalipia pango hadi au karibu ya Shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Spika, Maofisa hawa wa Polisi wako *entitled* kwa nyumba za bure. Sasa wanapolipa pango, sijui lini watarudishiwa fedha zao walizoghamaria mapango/makazi yao kazini na hivyo kuendelea kupewa posho ya makazi mpaka hapo Serikali itakapowajengea nyumba nyingine!

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. EMMANUEL J. LUAHULA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kuniwezesha niwepo na kuchangia hoja hii. Natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii mpya kwa kuwezesha hotuba hii iwasilishwe leo Bungeni. Pongezi hizi nazitoa kwa sababu mtiririko wa hotuba ni mzuri sana na hotuba itakuwa nzuri zaidi endapo itafanyiwa kazi kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, naomba nichangie katika vipengele vifuatavyo kwa kuzingatia Jimbo la Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu vitendea kazi. Wakati wa Semina *Ubungo Plaza* nilieleza tatizo hili. Vitendea kazi tunavyohitaji ni gari la upelelezi. Majibu ya Wizara walionipatia, walisema nitapata gari Bukombe. Naomba Mheshimiwa Waziri anithibitishie upatikanaji wa gari, kwani Askari wetu wa upelelezi wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la mafuta (*diesel/petrol*), Askari Polisi Bukombe hulazimika kupeleka watuhumiwa wenye kesi za Wilayani Kahama. Serikali iongeze Bajeti kwani mafuta tunayopata Bukombe hayatoshelezi. *Otherwise*, Serikali ileté Mahakama Bukombe kuondoa tatizo hili. Askari hawatoshi! Niliahidiwa kuongezewa, Serikali ifanye hivyo. Utakuta Askari *uniform* zimechakaa, tunaomba Serikali ilifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya Askari, wapo baadhi ya Askari wanadai aidha fedha zao za uhamisho au posho na madai mbalimbali. Naomba Serikali ianze utaratibu wa kutoa *warrant* za kusafiria badala ya kuwaacha waje wadai. *The government should consider Time Value for Money (TVM)*.

Mheshimiwa Spika, Polisi Bukombe hawana nyumba, kila mtu anaishi anakotaka, nidhamu haiwezi kuonekana. Serikali iangalie utaratibu wa kujenga nyumba Bukombe au warudishiwe/walipwe pesa za kukodisha nyumba.

Mheshimiwa Spika, Bukombe lipo jengo la Wilaya ambalo limechangiwa na wananchi pamoja na Serikali kwa kiasi fulani. Namshukuru *IGP Mstaafu* ambaye alichangia Sh.15,000,000/= tu. Kwa ujenzi huu, bado naomba Serikali ituunge mkono kumalizia jengo hilo. Vipo Vituo ambavyo kama mvua ikinyesha Askari lazima waende wakaegame kwa jirani. Naomba Serikali iniambie ni lini vituo hivyo vya Masumbwe vitajengwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wimbi la ujambazi, naamini Wizara inafahamu tatizo la ujambazi Bukombe. Nafikiri mambo yafuatayo yanasaababisha ujambazi. Wakimbizi toka nchi jirani Rwanda na Burundi, machimbo, msitu mkubwa kati ya Ushirombo na Runzewe na kutofahamika kwa mpaka wa Biharamulo na Bukombe.

Ushauri wangu katika hilo ni kwamba, pawepo na operesheni kali katika maeneo yaliyo karibu na msitu huu wa Kigosi/*Muyowosi Game Reserve* au msitu upande wa Halmashauri ya Wilaya ugawiwe kwa wananchi ili pakosekane sehemu ya kujificha au Idara ya Wanyamapori waweke Kambi kandokando ya barabara. Suala la mpaka Serikali itoe tamko rasmi ili kila Wilaya ilinde maeneo yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubambikizaji wa kesi, napenda kuishukuru Serikali kwa kupunguza tatizo hili Wilayani Bukombe, kwani hali sasa inatia moyo. Hata hivyo, bado wapo Askari ambaio sio waaminifu, wanasumbua wananchi kwa siri na baadhi yao Wizara ina taarifa. Naomba Serikali iwahamishe Askari kama hao wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, wenye mishahara midogo Bukombe ni Polisi, lakini cha kushangaza ni kwamba Bukombe matajiri wenye majumba makubwa ya kifahari mazuri ni Askari Polisi.

Mwisho, Wizara ifanye utaratibu wa kufuatilia mambo haya toka juu. Wahalifu kwa wananchi wakifika Polisi wanaachiwa. Tafadhali Makao Makuu ifuutilie. Serikali ifuutilie kwa karibu na niombe ifanye mawasiliano na Usalama wa Taifa. Nasema hivyo kwa sababu Bukombe wale watu ambaio kila mwananchi anajua ni majambazi, hawawezi kuchukuliwa hatua na Polisi kiasi cha kutia wasiwasii kwamba huenda baadhi ya Askari ni wahusika katika mtandao huo.

Mheshimiwa Spika, naamini wapo watu hata akiulizwa mtoto sifa za watu hao watakueleza. Inakuwaje wasikamatwe? Au kwa sababu wengine wamejificha kwenye Chama kwa kuwa na nafasi za uongozi? Naomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina tena ikisaidiana na Usalama wa Taifa, mafaili yao yanajulikana, iweje waendelee kustarehe

Bukombe na kunyima raha uongozi wangu kama *DC* na *DSO!* Naomba Serikali inilinde, kwani hata usalama wangu huwa mashakani. Lakini nasema sitanyamaza hadi Wanabukombe waishi maisha bora.

Mheshimiwa Spika, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri na watu wake wachunguze kikundi cha watu wachache wanaohusika na uhalifu katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze wewe binafsi kwa jinsi unavyoliendesa Bunge letu hili kwa hali ya juu kabisa. Pia, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP* Saidi Mwema, Kamishna wa Polisi Zanzibar, Khalidi Iddi Mwinzani na Watendaji wao wote kwa kuwasilisha hotuba yao ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 kwa ufasha wa kuonyesha dhahiri ni ya kufanya kazi kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nitumie nafasi ya pekee kwa *RPC* wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ndugu Bakari Khatibu kwa utendaji wake mzuri katika Mkoa wetu. Japokuwa ameshika nafasi hiyo kwa muda mchache sana, lakini matunda yake yameanza kuonekana kwa muda mfupi tu. Hii inaonyesha kwa kiasi gani anajali kazi yetu.

Mheshimiwa Spika, nyumba nyingi za Maaskari hasa zile za Polisi Ziwanu ziko katika hali mbaya sana kiasi ambacho haziridhishi. Naomba sana zifaniyiwe ukarabati ili nao waishi katika nyumba nzuri, wapate utulivu wa kutosha baada ya kufanya kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, Polisi ya Paje kuna Kituo kizuri cha Kazi, lakini hakina nyumba hata moja ya kuishi Askari hao ukizingatia ni eneo la utalii lenye mahoteli mengi, lakini Askari hao wote wanakaa Mjini kwa ukosefu wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendea kazi, Vituo vingi vya Polisi vina ukosefu wa vitendea kazi kama vile magari, pikipiki, *radio calls*, simu za mezani na kadhalika. Nashukuru hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 20 (b), nanukuu: “Upo uhaba mkubwa wa Askari kulinganishwa na wananchi, kwa upande mwengine upo uhaba wa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya doria za miguu, magari na vifaa vya mawasiliano.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hayo, lakini Vituo vingine wanayo magari tatizo lao ni mafuta tu, kwani lita 600 kwa Mkoa mzima kwa mwezi ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Jimbo langu, kuna *Police Post* ya Jang’ombe ambayo kwa umuhimu wak,e nimewawekea simu ya *prepaid* ili wapate mawasiliano ya simu hiyo kwa gharama zangu mwenyewe. Namba yake ni 024 – 2230917. Ninachoomba, basi angalau wapatiwe Sh.50,000/= kwa mwezi ili waweze kuweka kadi ya *prepaid* na waweze kuitumia katika kufanikisha kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, hali ya mishahara, mafao na marupurupu mengine ndani ya Jeshi hili sio nzuri kutokana na kazi zao na hali ya maisha. Ni vyema wakafikiriwa kupata nyongeza ya kukidhi kupambana na maisha. Pia, kuna hali ya kusikitisha kwa Askari wanaoingia kazini siku moja, lakini wanapoacha kazi huwa kuna tofauti ya malipo yao kwa sababu ya kiinua mgongo na pensheni. Kwa nini haibakii hii pensheni tu ambayo wengi wanaiona kuwa inawasaidia kuliko kiinua mgongo kinacholalamikiwa na wengi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwekwa mahabusu kwa muda mrefu, ni jambo linalowakera wengi katika nchi hii. Nashukuru Wizara kwa kuliona hilo katika ukurasa wa 21 (d) wa kitabu cha hotuba ya Waziri, nanukuu: "Uhaba wa Askari wenye taaluma ya upelelezi umechangia kupunguza kiwango cha mafanikio ya kudhibiti uhalifu kwa baadhi ya maeneo." Mwisho wa kunukuu. Kuwa na elimu na taaluma ndogo iwe sababu ya kuwaadhibu watuhumiwa walio ndani. Hiyo sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Jimbo langu, kuna kijana anaitwa Mzee Rashid Abdallah, amewekwa ndani tangu mwaka 2002 hadi 2005 ndio amepandishwa Mahakamani kwa tuhuma za mauaji bila ya kukusudia na mpaka hii leo bado yuko Mahabusu. Ninaombwa Wizara, kama atapatikana na hatia, basi hata huo muda aliokaa rumande pia utambuliwe kwani ni muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama barabarani, madereva wanapojuwa kuwa Askari wapo mahali fulani, huwa wanaendesha magari yao kwa uangalifu wa hali ya juu kabisa. Kitendo hicho kinaonyesha kinawakera sana Polisi walioko kwenye sehemu hizo, matokeo yake Askari huamua kujificha vichakani na huwatokea ghafla madereva na kuwasimamisha, matokeo yake wao kuwa ni vyanzo vya ajali. Je, hivi ndivyo walivyofundishwa? Ama kukaa barabarani ndio kutasaidia kupunguza ajali?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie kwa maandishi katika hotuba ya Wizara ya Usalama wa Raia ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuungana na Wizara hii kumpongeza kwa heshima na unyenyekevu mkubwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuunda Wizara hii na kwa kumteua Mheshimiwa Bakari Mwapachu (Mbunge) kuwa Waziri wa Kwanza wa Wizara hii. Pia, kwa kumteua Mheshimiwa Mohamed Abood Mohamed (Mbunge) kuwa Naibu Waziri.

Aidha, napenda kutambua na kupongeza uteuzi wa Inspekte Jenerali mpya Mheshimiwa Saidi Mwema, pamoja na teuzi zote za Wasaidizi wake katika Awamu hii ya Nne ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuwapongeza Watendaji Wakuu wote pamoja na watumishi wa Wizara hii kwa kufanikisha maandalizi ya Bejeti hii. Vile vile, napenda kuipongeza Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa mawazo na fikra zake za kuboresha utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua na kukiri kwamba Uongozi wa Awamu ya Nne wa Serikali wa Wizara hii pamoja na Jeshi la Polisi, kweli ni pambazuko jipya la uamsho mpya wa matarajio mema ya uwajibikaji makini kwa maslahi yaliyopevuka kwa vitendo vya tija kwa mustakabali amani, utulivu na maisha bora kwa Watanzania. Juhudi za Viongozi Wakuu wa Wizara na juhudi za Viongozi Wakuu wa Polisi sasa ni dhahiri za kulinda amani na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Wahenga husema, umoja ni nguvu. Ni kweli mshikamano wa Viongozi wa mamlaka ya kiraia na mamlaka ya Jeshi la Polisi kwa mfano wa Waziri na Inspeksi Jenerali wa Polisi wanapokuwa katika ziara za pamoja, hii ni sura mpya ya kujenga Jeshi la Polisi lisadikike, ni raslimali ya Serikali na ni raslimali ya mamlaka ya Umma kwa mfano ule uliozoleka kwamba Jeshi la Ulinzi wa Nchi (*TPDF*) ni Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa Wizara na kwa Mamlaka ya Jeshi la Polisi kuhusu kujengwa mfumo wa Kanuni kamilifu ya kuwa Kiongozi wa kuainisha umoja ni nguvu kati ya Viongozi wa Ridhaa ya Umma na Viongozi wa Jeshi la Polisi wa ngazi zote kama yalivyo sasa mahusiano ya kuonekana hadharani kati ya Waziri wa Usalama wa Raia na *IGP*.

Namaanisha walivyoyonekana katika Mkoa wa Mbeya na kuonekana Zanzibar wakiongea na jamii, kitendo hiki kinaibua ujio mpya ya kwamba Viongozi wa kiraia wanathaminika na kusikilizwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi. Je, Mikoani pana nini? Je, katika Wilaya kwa nini huku hapaonekani kuwepo mahusiano haya?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushika ridhaa ya Umma, napenda kutanabaisha kwamba, Viongozi wanaowakilisha Umma wana hazina ya kusadikika ndani ya jamii iliyowachagua na ni kweli Wabunge na Madiwani, tuna ushawishi wa kisaikolojia wa kuvuna ridhaa ya Umma kwa kuwapa maelekezo na kwa kupata mapokeo ya mawazo ya wananchi ya uwazi na ukweli na rutuba ya amani ya jamii. Chimbuko hili ni historia ya mila na utamaduni na desturi zetu za asilia na kijamii.

Mheshimiwa Spika, mbele ya macho ya Umma, tangu kipindi cha Jeshi la Mkoloni, sifa ya Askari ni mtu asiyecheka na kuchanganyika na Umma. Aidha, dhana hii inaelekezwa na imani ya kwamba Jeshi la Polisi ni la mapambano na ubabe wa kusukumana bila utendaji wa subira ya mawazo ya majadiliano kwa sababu kiongozi raia mbele ya Polisi hasadikiki na kuchagulika kusikilizwa awe ni chujio la kuainishwa kwa taarifa za kutendewa maamuzi ya kujenga na kulinda usalama wa raia na katika kuharakisha raia kutendewa haki zao.

Mheshimiwa Spika, nashawishika kusema, hazina ya ufanisi wa tija wa Jeshi la Polisi hivi sasa ni dhoofu kwa vipimo vya viwango vya kupata mashirikiano na Umma.

Jeshi la Polisi litambue mantiki ya umoja ni nguvu kwa kutunga kanuni za kujenga taratibu za kusadikika na kuthaminiana Viongozi wa Kijeshi na Viongozi wa Kiraia katika Mikoa na Wilaya ili Jeshi la Polisi liguse hisia na kukonga miyo kwa urafiki wa kuvuma mashirikiano thabiti yasiyo ya kutegeana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, amesema katika hotuba yake, amegusia kujengwa Polisi Jamii. Ninawapongeza sana kwa maudhui haya ya kuwepo na Polisi Jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa *IGP* ili aweze kufanikisha dhamira ya kuwepo Polisi Jamii, namwomba abadilike yeye mwenyewe kwanza. Wahenga husema: "Huwezi kusukuma gari ukiwa umekaa ndani ya gari na honi sio ufunguo wa gari." Ninamwomba *IGP* asioneokane Kitaifa na katika hafla za Kimataifa tu. Wananchi wanataka kumwona *IGP* wao Vijijini kama Rais wetu na Waziri Mkuu wetu wanavyotembelea Wilaya na baadhi ya maeneo ya Vijiji.

Mheshimiwa Spika, natoa ombi kwa *IGP* kwa kurejea kwamba, katika kipindi cha njaa, Waziri Mkuu alitembelea maeneo yaliyokumbwa sana na baa la njaa. Sasa namwomba Mheshimiwa *IGP* atembelee Mikoa yenye kusikika imekumbwa na dhuluma na dhahama ya tabia chafu za hulka na silka binafsi za Mapolisi Jamii katika Vijiji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa *IGP* Saidi Mwema, ni muungwana sana na uungwana ni vitendo. Nasikitika kusema kwamba, kuna watu hawana utu, lakini wana ubinadamu wao ndani ya Jeshi la Polisi. Je, Polisi Jamii itapokelewa vipi kwa kuwepo Polisi wa aina hii? Mfumo wa kanuni za leo ni kwamba wa kwanza kuaminika ni Askari, raia baadaye.

Pili, kuna Askari ambao sio wabaya kwa jamii, lakini ni wahalifu kwa kanuni za maadili ya Polisi na hawa jamii inawajua.

Tatu, wananchi hawana mbio za kukimbiza uongo wa Polisi ukakamatwa kwa sababu hawapigiwi kura kama wanavyopigiwa kura wala rushwa, wezi na majambazi.

Mheshimiwa Spika, ukweli wa raia hutembea mtupu mbele ya maafande. Uongo wa raia wabaya ama Polisi wabaya hutiwa vipodozi ambapo humvutia afande kuamini. Tatizo, afande ambaye bahati mbaya kasikiliza yale ya uongo wa vipodozi asikipo ya Kiongozi raia siyo afande wa ngazi za juu. Afande msikilizaji wa Kituo, huamua kwa mfano wa kwamba, koroboi haiwezi kumulikia taa ya umeme. Je, Polisi Jamii itathamini vipi kwa mfumo huu? Je, siyo kweli kanuni za Jeshi la Polisi zitazamwe upya? Je, Mheshimiwa *IGP* atasukuma gari liwake akiwa amekaa ndani ya gari? Je, Mheshimiwa *IGP* na honi ya Vyombo vyta Habari wanaielewa jamii bila kuja kuisikiliza jamii hiyo?

Mheshimiwa Spika, kupitia Kikao hiki cha Bunge hili Tukufu, namwalika Mheshimiwa *IGP* aje Jimbo la Wilaya ya Maswa kwa azma ya kujisomea jamii ina kisomo gani Vijijini. Ninamwomba katika ziara hiyo, aje aongee na Sungusungu.

Mwisho katika hili namwomba yeye tu avae vazi rasmi ili wananchi waone sura ile ile wanayoiona katika Vyombo vya Habari. Ziara hii itakidhi kuelewesha hata kanuni za Polisi kwa mantiki ya kuwa na Polisi Jamii. Pia, Mkoa wa Shinyanga kama ulivyokumbwa na baa la njaa, pia tuna baa la adui ujinga, balaa la kiu ya msako wa haki.

Mheshimiwa Spika, *IGP* amepata dhamana hii ambayo imefichua tabia yake ya kupenda wananchi wapate haki na Jeshi la Polisi lipendwe. Ukweli umedhihirika kwamba, kila jambo na mbegu yake. Namwomba aje Maswa asiwe na mashaka, kwa sababu mashaka yoyote yale ni hasara ya kutopata maarifa. Napenda kusisitiza kwamba, kufikiri ni tofauti na kuelewa na ndiyo maana pana imani za kichawi. Mengi yanasemwaa toka tupate uhuru kuhusu mauaji ya imani za kichawi. Naomba kunena tena, umoja ni nguvu pale tu binadamu tutakapokuwa wakweli zaidi ya ukweli wa fisi kutokula nyama ya fisi mwenzake, lakini binadamu humla kisogo binadamu mwenzake.

Mheshimiwa Spika, nguvu za hoja za azma ya kusimamiwa na kufuatiliwa masuala yote yanayohusu usalama wa raia na mali zao ni mikakati muafaka. Wakenya husema: “Nguvu za hoja ni jeuri ya ukweli.” Bajeti hii naiunga mkono kwa hoja walizowasilisha. Ninaombwa Wizara itafiti uwazi na ukweli wa hadhi ya Vituo vya Polisi kwa Wilaya kongwe. Maswa imechutama kwa utupu wa mfumo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua hoja ya Wizara hii kwa kusema kila ngoma ina hadithi yake. Hadithi ya ngoma hii itaanza mara atakapofika *IGP* Maswa ili ajionee malinganisho ya faraja au malinganisho ya majonzi ya watu wa Maswa ni utendaji wa watu au ni Kanuni mbovu za kuboreshwa. Naomba Mheshimiwa Waziri anithibitishie ujio wa *IGP* Maswa katika majibu yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kutoa mchango wangu katika Wizara ya Usalama wa Raia.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Nne katika utawala wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, nchi yetu imetokana na ridhaa ya wananchi wetu kuweza kuishi angalau kwa mategemeo. Hii inatokana na maamuzi ya Mheshimiwa Rais kuamua Jeshi la Polisi kulijenga upya kiuongozi, pia kimajukumu ya utendaji wa kazi zao. Mabadiliko ya kumchagua Inspekte Jenerali wa Polisi, Said Ali Mwema. Wizara imepiga hatua nzuri kwa faida ya wananchi pia kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, hakuna sifa isiyo na kasoro. Hii ina maana Jeshi la Polisi ndio chimbuko la maafa katika nchi yetu. Polisi somo lake ni sheria. Mwenye kujua sheria na akaivunja huwa mkosaji zaidi kuliko aliyekosa bila ya kujua. Hivi ndivyo ilivyo kwa raia wa kawaida anapokataa amri ya Polisi, hushitakiwa kwa madai ya kukataa amri halali ya Polisi. Jeshi la Polisi linapopewa amri haramu na Mkuu wake hutekeleza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Kisiwani Pemba, limeweza kuvunja sheria ya nchi Kikatiba, lakini hakuna kilichofanyika. Katika Nchi yetu, hukumu ya kuua ni pale Mahakama itakapoamua mshitakiwa imethibitishwa kosa lake na hukumu yake ni kifo, mtu huyu hawesi kuuliwa mpaka pale Rais atie saini ya kuuliwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeweza kutumia nguvu za ziada na kukabili baadhi ya wananchi mpaka kufa kwa kupigwa risasi na Jeshi la Polisi. Vitendo vya kufa raia kwa risasi mara nyingi hutokea wakati wa Uchaguzi nchini. La kusitikisha zaidi, vifo hivyo mara nyingi hufa Wanachama wa Chama cha Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Polisi kuua hadi leo hakuna Askari aliyepelekwa Mahakamani. Mwaka 2001 watu walipigwa risasi bila sababu.

Mheshimiwa Spika, katika Kituo cha Polisi Chakechake, Askari Polisi mmoja alichukua silaha na kuwapiga risasi Askari wenzake wawili, mmoja kati yao alikuufa, huyo ni Marehemu Nahoda. Aliyejeruhiwa, kwa jina simkumbuki pia na mwenye kutenda kosa simjui.

Mheshimiwa Spika, mwenye kufanya tendo hilo leo yuko kizuzini, kwa nini akawa kizuzini hadi leo? Hivyo wale waliooliwa kwa risasi hawakuwa raia katika nchi hii? Aliyeua Polisi ndio mwenye makosa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kudai Askari yoyote aachane na ushabiki wa kisiasa, hii sio kweli. Ushahidi wa hili ni pale Mkuu wa Polisi aliystaa fu Bwana Mahita aliposema atahakikisha Wapinzani hawatachukua nchi. Pia, alidiriki kuchukua visu na kudai ni silaha za Wapinzani. Mahita alikuwa Mkuu wa Jeshi hili, ambaye alikuwa ni mtu wa juu katika chombo hiki cha Serikali.

Mheshimiwa Spika, uko wapi ukweli wa kuwa Jeshi sio la watu wa siasa? Hivyo, Jeshi la Polisi ni haki kumkamata raia na kumlazimisha kosa? Hadi leo ndani ya Jimbo langu kuna vijana wangu sita ambaao walikamatwa na Polisi wakati wa kujianzikisha kuwa wapiga kura katika Kituo cha Kilindi - Jimbo la Chonga. Hao vijana walilazimishwa makosa na baadhi yao walishikishwa silaha na kupigwa picha ili ithibitike kuwa wao walivamia Kituo. Iko wapi haki ya raia ndani ya Polisi?

Mheshimiwa Spika, sasa ni matumaini yetu, ndani ya Jeshi la Polisi kwa uongozi wa sasa uliopo litakuwa na urafiki na raia kwa upande wa Waziri, Naibu Waziri na Mkuu wa Polisi. Nina imani kubwa yale yote yaliyotendeka hayatarejewa.

Mheshimiwa Spika, ninaitakia Wizara ufanisi mwema wa kazi zao. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia. Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wake kwa hotuba waliyotoa leo na jitihada zao za kuliongoza vyema Jeshi la Polisi wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kulipongeza Jeshi la Polisi nchini kwa mafanikio katika kazi yao ngumu ya kupambana na wimbi la ujambazi nchini. Hali

imeanza kuelekea kuwa shwari Muheza kwa kazi nzuri wanayo jitahidi kuifanya kudumisha amani na utulivu. Pamoja na hayo, napenda sasa kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuhusu hali ya usalama katika Mji wa Muheza. Hivi karibuni kumeibuka wimbi la ujambazi na mauaji ya raia katika Mji mdogo wa Muheza na maeneo ya Kata Jirani. Katika miezi miwili Juni, 2006 na Julai, 2006 mauaji kadhaa yametokea, wananchi kadhaa wameshambuliwa kwa silaha pamoja na mapanga na hata ng'ombe wameibiwa. Hali imeanza kuwa mbaya na ya kutisha ghafla!

Mheshimiwa Spika, inawezekana hali hii inachangiwa na wavamizi wengi waliozagaa katika maeneo mengi wakitafuta dhahabu huko Amani Magoroto, Mkwajuni na Kwatango. Tunashauri Jeshi la Polisi Wilaya ya Muheza lionezewe uwezo ili limudu kurejesha hali ya usalama Mji wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, pili, ni maombi ya muda mrefu ya gari katika Kituo kidogo cha Amani – Muheza. Kwa muda mrefu nimeomba gari kwa ajili ya Kituo kidogo cha Polisi Amani, kutokana na kuwepo katika eneo la mazingira maalum na muhimu. Amani iko kilomita 35 kutoka Kituo cha Makao Makuu ya Polisi Wilaya. Kituo hakina gari wala usafiri wowote, hata pikipiki. Eneo linalohudumiwa na Kituo hicho ni Tarafa nzima ya Amani yenye Kata tatu na lipo umbali wa zaidi ya kilomita 15 kutoka Kituo hicho cha Amani hadi mwisho wa Kata ya Zirai, Kijiji cha Kizerui na Bombo Majimoto kupakana na Wilaya ya Korogwe.

Mheshimiwa Spika, inakuwa vigumu kwa Askari kutembea kwa miguuu kufuatilia wimbi kubwa la uhalifu wa wachimbaji wa dhahabu, wizi na uharibifu wa maliasili ndani ya Hifadhi za Msitu wa Amani na hali ya usalama kwa watalii na wananchi. Hivyo, bado naomba wapatiwe gari kuboresha utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, tatu, umiliki wa eneo la Kituo cha Polisi na Nyumba za Askari Makao Makuu – Muheza. Eneo kilipo sasa Kituo cha Polisi na nyumba za Polisi Muheza ni mali ya Shirika la Reli. Mwaka 2004 nilianzisha hoja kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tanga na kwa kushirikisha Wizara ya Mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakati huo, kuomba umiliki wa ardhi, eneo linalotumiwa sasa kama Kituo cha Polisi na nyumba za Polisi uhamishwe kutoka Shirika la Reli na kuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani wakati huo ambapo sasa ni Wizara ya Usalama wa Raia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara hii mpya iendelee kufuatilia pendeleko hilo kwa manufaa ya Jeshi la Polisi Muheza kuendelea kutumia eneo hilo ambalo linaweza kuuzwa kwa wawekezaji wengine katika mpango unaoendelea kwa nia ya kukodisha au kubinafsisha Shirika la Reli Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Nne, pongezi kwa ujenzi wa Kituo kipywa cha Polisi. Naipongeza Wizara kwa kuamua kujenga Kituo kipywa cha Polisi cha Wilaya ya Muheza. Hali ya Kituo cha zamani licha ya kuwa katika eneo la mmiliki wa Shirika la Reli, kilikuwa na bado kipo katika hali mbaya sana. Pamoja na ujenzi huo, napenda kuishauri Wizara ya Usalama wa Raia kukamilisha ujenzi wa Kituo hicho, kujenga

nyumba mpya za Askari na pia kukarabati nyumba zilizopo sasa ili kuongeza nafasi ya makazi kwa Askari wa Muheza na familia zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI A. KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza wewe, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia na Serikali ya Awamu ya Nne kwa usimamizi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Mungu aibariki Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, hali ya uajiri katika Jeshi la Polisi haitoshi, kwani wanaoajiriwa ni vijana wachache kulingana na hali ya vijana wengi kutoweza kujiunga na Jeshi la Polisi na wanao uwezo kielimu. Lakini kutokana na uchache wa nafasi, hawawezi kuajiriwa. Inabidi kusubiri na kupitiliza masharti ya umri unaotakiwa kwa ajira ya Jeshi la Polisi na vijana hao wengine huharibika kimazingira kuwa wahuni, walevi kwa madawa ya kulevyta hata kujihusisha na ujambazi. Kwa hiyo, naiomba Serikali na kwa usimamizi wa Waziri kuongeza nafasi za ajira. Polisi pia iwachukue vijana wa Darasa la Saba sio kuanzia *Form Four* ili kupunguza kero ya uhuni kwa vijana na pia kuwasaidia wazazi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina kazi kubwa sana kuweka usalama wa raia. Kwa hiyo, bila usalama wa raia, maisha bora kwa kila Mtanzania hakuna na Tanzania kila mtu anatakiwa apate maisha bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali iipe uwezo Wizara hili ili Jeshi la Polisi liweze kuleta amani na utulivu katika nchi yetu kwa kupatiwa mahitaji, kama Jeshi linaloendana na Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyeo vya Jeshi la Polisi, naomba sana na kwa heshima, vyeo vitolewe kwa Askari kwa wakati na kwa sifa na kwa viwango vizuri bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, Askari wanapostaafu, wapate mafao yao mapema bila usumbufu kwa kiwango cha kuendana na hali ya dunia inavyoendana na wakati, kwani kuna sababu gani wasipate haraka mafao yao au kuna nini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Rais wetu kwa kumteua Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu kuwa Waziri na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed kuwa Naibu wake. Pia, uteuzi wa Katibu Mkuu Ndugu Bakari Mahiza na *inspector General* wa Polisi Ndugu Said Mwema. Ninayo imani kubwa kuwa timu hii itafanya kazi zake vizuri sana. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa jinsi wanavyokabiliana na majambazi katika ari mpya. Ninazidi kushauri kwamba, *IGP* aendelee kuwashirikisha zaidi wananchi na pale inapowezekana, wawapatie kifuta jasho kwa taarifa za siri wanazozipata Mitaani na kuziwasilisha kwenye vyombo vinavyohusika. Ninashauri kuwa, idadi ya makachero iongozwe na ijumuushe hata baadhi ya wahalifu waliostaafu lakini mitandao wanajua.

Mheshimiwa Spika, akinamama wanaweza kutusaidia zaidi kwenye suala la kuwafichua majambazi. Idadi yao iongezwe kwenye ukachero. Mafunzo ya hali ya juu yatolewa ili kukabiliana na wimbi hili la wakorofsi. Kila inapowezekana, ni vizuri baadhi ya viongozi wa mitandao ya ujambazi wawe wanapigwa picha na kusambazwa kwenye vyombo vingi vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa zaidi ya miaka kumi, nimekuwa nikiomba Wizara isaidie ujenzi wa Ofisi ya Polisi - Manispaa ya Sumbawanga. Mji huu hauna "*Central Police Station*" yenye jengo linalofanana na jina lenyewe. Angalieni Ofisi zote za Miji Mikuu ya Mikoa, mwone kama kuna jengo lililo na hadhi ya uduni kama jengo la Polisi (Manispaa ya Sumbawanga).

Mheshimiwa Spika, naona aibu kusimama mbele ya Wabunge wenzangu na kulalamika kwa jambo hili ambalo kwa miaka zaidi ya kumi, nimekuwa nikilalama nalo. Mimi kama kiongozi wa siku nyingi, nisingependa nikaonyesha tabia ya kutokomaa. Naelewa Mheshimiwa Waziri na *Inspector General* Bwana Said Mwema watanielewa na kuwaomba waone namna ya kushughulikia matatizo hayo pamoja na hali nzima ya maisha ya Askari wangu wa Sumbawanga na wa Mkoa mzima wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa leo niyaseme hayo machache na nimwombe Mheshimiwa Waziri atueleze, nini mipango ya Wizara kwa Manispaa ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kuliomba Jeshi zima la Polisi liendele na moto ule ule ambao wameuanzisha katika kutekeleza agizo la Rais kuhusu majambazi, tuendeleze usemi usemao "*help the Police to help you.*"

**MHE. DR. WILLRBOD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Moja, kupandishwa vyeo Maaskari. Maaskari wetu wa ngazi za chini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kuna malalamiko mengi kuhusu upandishwaji vyeo na nafasi za masomo zaidi hutolewa kwa upendeleo.

Ni imani yangu kuwa wakati utaratibu huu unatazamwa upya, utaratibu wa wazi utawekwa kuondoa kero hii. Malalamiko hayo, yanaongezea katika kuwapunguzia vijana wetu morali hata kuwaingiza katika vishawishi ikiwemo rushwa ndogo ndogo.

Pili, kuna malalamiko toka kwa vijana wetu waliopambana na majambazi na hata kutunukiwa Cheti cha Sifa ya Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania *PF 160*. Lakini wala hawakutunukiwa zawadi na wala kupandishwa vyeo. Haya nazungumzia Askari wetu aliyekuwa Arusha na sasa kahamishiwa Mkoa mwingine.

Kwa vile Wizara inazo kumbukumbu ya waliotunukiwa hati hiyo, ningependa kufahamu kati ya 2000 – Juni, 2006 ni Askari wangapi walitunukiwa hati hizo? Walipewa zawadi gani na wangapi walipandishwa vyeo? Ni imani yangu nitapata jibu kamili bila kuhitaji kutumia vifungu wakati wa Kamati ya Matumizi.

Tatu, ujambazi, wizi, uhalifu mwingi unafanyika kwa kutumia magari. Pamoja na kuwa majambazi hubadili namba za magari hayo, utaratibu wetu wa kuandikisha magari hayo hautusaidii sana katika kutambua uhalifu kwa vile namba za magari zote zinatolewa Dar es Salaam. Wenzetu wanatumia kwa mfano “T”, inaonyesha nchi, lakini Mkao ilikoandikishwa gari nao utaonekana mathalani T..... Do... Ni kwa nini katika mabadiliko yanayowasilishwa na Wizara hii, utaratibu wa uandikishaji wa magari usitazamwe upya?

Nne, natanguliza shukrani za dhati kabisa.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa ngazi zote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kwa hatua mbalimbali katika uandaaji wa hotuba hii. Ni hotuba nzuri inayotia matumaini kwa usalama wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pongozi zangu zingine ni kwa Jeshi la Polisi kwa jumla kwa mafanikio mengi na muhimu katika kupambana na ujambazi uliokuwa unaelekeea kukithiri. Mafanikio haya yamerejesha heshima na hadhi halali ya Jeshi hili. Ninashauri heshima na hadhi hizi zisiruhusiwe kupotea. Ninaamini kwa heshima na hadhi hii, wananchi wataendelea kushirikiana na Jeshi hili ili kulifanya liweze kutekeleza majukumu yake kwa wepesi zaidi. Ninawapongeza na kuwatachia kila kheri katika shughuli zao zote za kulinda na kuhifadhi usalama wa raia.

Mheshimiwa Spika, moja ya vitendea kazi muhimu kwa Jeshi hili ni wananchi wenywewe. Hivyo, ninashauri vitendo vyote vinavyosababisha mpasuko katika Jeshi hili na wananchi, vingekwepwa na Jeshi hili. Vitendo hivyo ni pamoja na rushwa na unyanyasaji wa aina yoyote wa kauli na vitendo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili pamoja na wananchi ni wadau wa msingi wa usalama wa raia na Taifa kwa jumla. Makundi yote hayo yanatakiwa kufanya kazi kwa pamoja. Maelezo yangu yanaunga mkono kipengele cha 53 cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na matarajio ya wananchi kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya, napenda nitoe shukrani zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba na Kwimba kwa jumla kwa kumhamisha

Mkuu wa Kituo cha Polisi Ngudu. Wananchi wengi wa Kwimba wameipokea taarifa hiyo kwa furaha kubwa bila hata kufahamu ni nani anakuja kuchukua nafasi yake. Mkuu wa Kituo hicho alikuwa kero sana kwa wananchi wa Kwimba. Walikuwa wakimwona kama siyo msimamizi wa usalama wao, ila ni mtu aliyejkuwa amekuja kujitajirisha tu. Mtandao wake wa Wakuu wa Vituo vidogo vya Polisi kama kile cha Hungumalwa ulikuwa wa manufaa kwake zaidi kuliko raia. Nazidi kuomba Wakuu wa Vituo vidogo hivyo wangebadilishwa.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba, ili Jeshi hili liwe karibu na wananchi, Jeshi hili lingelifanya kazi karibu na Sungusungu. Mimi ninaamini kuwa matokeo mazuri yanaweza kupatikana. Hivyo Jeshi la Polisi liangalie upya mtazamo wake kwa Sungusungu. Kinachohitajika ni kutoa elimu kuhusu uwezo, umuhimu na mipaka ya Sungusungu. Ni vyema kukawa na utaratibu wa kudumu wa uongozi wa Polisi ngazi ya Wilaya kukutana mara kwa mara na Viongozi wa Sungusungu ili kurekebisha na kubainisha tofauti na umuhimu wa umoja wao.

Mheshimiwa Spika, pili, mawasiliano. Kuhusiana na wageni ndani ya nchi, ninashauri utaratibu uliokuwepo miaka ya nyuma urejeshwe, hata kama utarejeshwa na marekebisho yatakayolinda na kuheshimu haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kila mtu ana haki ya kwenda na kuishi mahali popote ili mradi asivunje sheria, lakini ni muhimu kukawa na utaratibu wa kufahamu mtu anakwenda wapi na kwa muda gani na kufanya nini. Hivyo, ninashauri kila mtu apokeaye mgeni, kwanza awe na uhakika naye ni nani na ikiwezekana afahamu shughuli anayotaka kuifanya na kwa kipindi cha muda gani. Hili sio jambo geni. Kila tuendapo hotelini na *guest house* huwa tunajaza vitabu. Kinachopungua ni taarifa hizo zipelekwe wapi baadaye, kwa mawazo yangu.

Mheshimiwa Spika, Vijijini, taarifa hizo zingelipelekwa kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kata. Kwani moja ya kazi zao ni ulinzi na usalama. Taarifa hiyo inayopelekwa na mwenyeji inatakiwa pia ipelekwe kwa Viongozi wa Jeshi la Jadi/Sungusungu. *VEO* na *WEO* wanatakiwa hatimaye kuzifikishe taarifa hizo kwa *DC/OCD* na hasa kwa wageni wanaokaa muda mrefu na wanaotiliwa mashaka.

Mheshimiwa Spika, Mijini, taarifa hizo zipelekwe kwenye Vituo vya Polisi vilivyo karibu. Polisi nao pale wanapokuwa na mashaka waweze kufuutilia kitendo hiki kitapunguza uzururaji. Aidha, mwenyeji anayeshindwa kutoa taarifa, mgeni akipatikana na hatia naye atuhumiwe. Utaratibu huo ulikuwepo, ulipotelea wapi?

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uhalifu, uhalifu ukikithiri, unarudisha nyuma maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, inabidi kila raia ahushishwe kulinda usalama. Ni bora muamue kuweka Polisi jamii, hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, ni maoni yangu kuwa Polisi Kata/ Sheria washirikiane moja kwa moja na Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji, Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji awe na daftari la kuandika wananchi wote wanaoishi kwenye eneo lake. Hii ilikuwepo, lakini Serikali

haijaiwekea nguvu. Kwa hiyo, ni bora irudishwe ili wageni wanapoingia kwenye eneo itakuwa rahisi Serikali kujua. Mwenyekiti apewe uwezo wa kuangalia nyumba/kaya zake mara kwa mara na kuripoti atakapoona ingia na toka ya wageni kwenye eneo lake, ni kazi ngumu lakini uhakika wowote ni gharama.

Pili, Wizara iamue kuwa na jamii mara kwa mara, kwani hata Wazungu wa unga watajulikana kwa urahisi wa biashara za magendo. Silaha zote ziorodheshwe na Mwenyekiti, ajue watu wake wanaomiliki silaha kwa eneo lake. Vijana wetu waangaliwe kwa ukaribu sana wanapokuwa kwenye makundi au vijiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama barabarani, kwa vile ajali zinaletwa na mwendo mkali na madereva kutokujua kwamba wanabebe roho za watu ni vizuri kutekeleza yatafuatayo kwa maoni yangu.

Moja, magari yote ya abiria (mabasi) viti vyote viwe na mikanda, wananchi wote wafundishwe kufunga mikanda na lazima mabasi yote na Taxi ziwe na mikanda. Raia yejote (abiria) ambaye hatafunga mkanda yeeye ndiye wa kulipa faini.

Pili, askari (trafiki) wahakikishe abiria waliosimama wateremshwe wao, kwa sababu, kama abiria hawatakubali kusimama, basi magari hayawezi kuongeza abiria. Kwa hiyo, wao ndio wawajibishwe. Tatu, abiria wafundishwe kumkemea dereva anapoendesha gari kwa kasi. Nne, maoni yangu kuhusu magari mabovu, yote yafutiwe leseni ya kuwa barabarani na dereva atakayekubali kuendesha gari bovu na yeeye anyanganywe leseni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upelelezi wa kesi, siku hizi hakuna siri ya kuendesha upelelezi wa kesi, kwani rushwa imekithiri. Usikatae basi kwani Jeshi la Polisi linasemwa vibaya midomoni mwa wananchi. Serikali ifanye bidii kuongeza maslahi ya Jeshi hili, kwani kesi zote zinaanza kwa Jeshi hili kupelekewa malalamiko na wao kuchukua hatua ndipo kesi iende Mahakamani. Sasa wao wanapeleleza, wanaleta mpango wa kupeleleza kinyumentume baada ya kupewa rushwa na mhusika wa kosa.

Chuki zinazojengwa na Jeshi la Polisi kwa watu ambao eti wamekosana na wao hutafuta njia ya kumkomesha, kwa kumbambikiza kesi ya uongo na hata kumlazimisha kwa kumwekea bangi au unga ndani ya surualiyake. Hivi ni vibaya sana, kunaangamiza jamii, njama na kujenga jamii ya watu wakorofii.

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya sana na watu ambao ni mashuhuri, ndio wanaomiliki majambazi na silaha kubwa kubwa na kuzikodisha. Mfanyabiashara anauza vitu vidogo sana na mkitaka kumpeleleza ni jambo ndogo sana, kwani biashara zake anazilipia VAT. Ukiangalia VAT anayolipa utajua anafanya biashara ya faida gani, lakini muda mfupi anatajirika na kuwa na majumba makubwa makubwa. Je, fedha hizo amezipata wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madawa ya kulevyaa, vijana wetu wanaangamia kwa madawa haya. Zamani, madawa ya kulevyaa yalikuwa yanatumika na vijana wa Mijini.

Siku hizi hata vijana wa Mikoani na wao wanayatumia madawa haya, yanaingizwa nchini kwa kasi sana, inashangaza yanapitia wapi?

Mheshimiwa Spika, undani wa kikundi ambacho kitafanya kazi ya kufuutilia na waanze kwa upelelezi wa wafanyabiashara ambao nimeshawataja hapo juu na kuwaangalia hawa vijana kwa utaratibu ili waseme madawa wanayapata wapi. Kama tunajenga uwoga wa kutowafuutilia wafanyabiashara wanajiita wakubwa, basi Taifa la kesho litaangamia kwa madawa ya kulevyta. Hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoweza kufuutilia ujambazi wa silaha na tukaweza, basi sasa tuweke nguvu kwa madawa ya kulevyta. Namalizia kwa kuunga mkono hoja hii.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. Napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Kamanda *IGP* Mwema, Watendaji, Maafisa na Askari wake wa Tanzania, kwa kazi zao nzuri na ulinzi mzuri wa raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:- Moja, nampongeza *IGP* Mwema kwa kupandisha vyeo Makamanda wa Upelelezi wa Wilaya na kuwa wa Mikoa na wale Makamanda wa Polisi wa Wilaya kuwa wa Mikoa hasa kwa wale Makamanda wa kike.

Mheshimiwa Spika, suala la maslahi ya Askari ni tatizo sugu sana. Kwa kweli mishahara ya Askari, licha ya kuongezewa, lakini bado maslahi (mishahara) ni midogo kwa Askari wetu, tujue kuna Askari wetu hawana muda mkubwa wa kufanya kazi zao binafsi na muda mkubwa wanautumia katika kulinda usalama wa raia. Kwa hiyo, ni vyema kulipwa mishahara inayoendana na kazi nzito wanazozifanya, sio mishahara pekee, bali na posho mbalimbali zinazowahu.

Mheshimiwa Spika, suala la makazi ya Askari ni tatizo zaidi. Ni vyema Askari wajengewe nyumba za kuishi (*campus*) kwa sababu sio vyema kuishi uraiani, endapo wakikaa kwenye *campus* wanaweza kutekeleza kazi zao kwa urahisi hasa pale inapotokea dharura. Naomba Askari wa Mkoani Pemba nao wajengewe nyumba. Hivi sasa wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, vifaa bora vya kisasa kwa Askari, ni nyenzo muhimu kutokana na mabadiliko yaliyopo ya ujambazi na ukatili ulioenea nchini kama wanavyofanya majambazi, wana silaha, magari na kadhalika vya kisasa iweje Askari wawe na vifaa duni? Ni vyema Askari wapatiwe vitendea kazi vya kisasa, magari, *radio call* na kadhalika ili kuwa na mawasiliano ya uhakika na ya haraka.

Mheshimiwa Spika, michezo ni muhimu kwa Jeshi letu. Naomba wanamichezo waenziwe na watengewe fedha maalum kwa ajili ya shughuli zao za michezo. Wanamichezo wa vikosi vya Polisi wanaipatia sifa Jeshi na nchi yetu. Ni vizuri

washughulikiwe ipasavyo kama kuwapatia posho, vifaa vya michezo na magari ya kuwahudumia wakiwa na safari za kimichezo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kuongeza nyumba za Askari wa Chakechake - Pemba, nyumba ambazo ziko katika Jimbo la Wawi, Kijiji cha Mfikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waunge mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mohamed Aboud Mohamed na ponezi kwa *IGP Said Mwema* na wataalamu wote.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kama ifuatavyo: Moja, nyumba za Askari haziridhishi kwa hali ya sasa, hata mfumo wa maji machafu sio mzuri. Zitengwe fedha za kutosha ili ukarabati au ujenzi uweze kukamilika.

Pili, vitendea kazi kama vile magari, pikipiki, ningeshauri kuwepo ongezeko la pikipiki Mijini ili kuwapa urahisi wa kutimiza kazi yao kwa ufanisi kuliko ilivyo sasa na wanaweza kufanya kazi kwa kwende kwenye matukio hata Vijijini.

Tatu, maslahi ya Polisi na posho zao hususan malimbikizo ya siku za nyuma yalipwe. Nne, Sare za Polisi (*uniform*). Ningeshauri Serikali itoe angalau *pair* nne kwa kila Askari kutokana na aina ya vitambaa kwa sasa vinachuja (kutoa rangi na kupauka).

Tano, Polisi washauriwe kufuata maadili mema kwa kutoshirikiana na wahalifu ili heshima yao ibaki kama zamani.

Sita, Polisi washirikiane na vikundi vya ulinzi na raia ambavyo vinasaidia katika kupambana na uhalifu kama vile Sungusungu. Vikundi hivi vipewe elimu ya awali ili wajue mipaka yao ya kazi.

Saba, kitengo cha usalama barabarani, kwanza, ninawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia, ninawalaumu wale wachache ambao wanachafua Kitengo hiki. Wapewe vitendea kazi vya kisasa ambavyo vinaweza kumudu hali halisi ya ongezeko la magari, hususan Dar es Salaam ambako magari yao hutegemea sana taa za kuongozea magari, pale tu umeme unapokatika. Wapewe motisha kwa masaa wanayosimama na kuongoza magari kwenye maeneo meusi Dar es Salaam. Wawekewe Bima ya Maisha, kwani mara nyingi hugongwa na magari kwa bahati mbaya na kuvunjika wawapo kazini.

Nne, *TAZARA*, Kitengo hiki kimesahaulika sana, kwani mara kwa mara wanasadifira bila posho ya kujikimu na huambiwa wanaporudi ndipo waje kudai. Ushauri

wangu ni kwamba, ni vyema walipwe kabla ya kuanza safari. Kuwepo na utaratibu wa kuhamisha wale waliokaa kwa muda mrefu kwenye vituo vyao vya kazi ili kwanza kubadili mazoea na kuondokana na suala zima la kudai rushwa.

**MHE. KIUMBWA M. MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniwezesha kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi zao wanazozifanya. Wanastahili kupewa pongezi kubwa sana, kwani wanapambana na kazi ngumu sana, lakini wanajitahidi kufanya kazi kwa moyo thabiti.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wenzetu hawa jitihada zao ndio imani kwetu kwa sababu wanapambana na majambari ambao wanahujumu mali za raia wema wa Tanzania pamoja na roho za watu nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Tunguu Zanzibar, ambazo zimeuzwa kwa Polisi, lakini nyumba hizi haziridhishi hata kidogo kwa sababu ni mbovu sana, hazistahili kukaa Polisi. Hali iliyokuwepo, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani kuhusu nyumba hizo zilizoko hapo Tunguu Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA S. N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naiomba Wizara kwa heshima kubwa na taadhima na Serikali iangalie uwezekano wa kufanya ukarabati mkubwa wa nyumba pamoja na Ofisi za Polisi Mwera Zanzibar. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza magari katika Kituo cha Mwera pamoja na mafuta ya kutosha ili Polisi wafanye kazi kwa ufanisi. Serikali iangalie uwezekano wa kujenga nyumba mpya za Maaskari Mwera ili kupunguza tatizo lililopo sasa la Askari wengi kuishi uraiani.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iandae mkakati maalum wa kuwakopesha fedha au vifaa vya ujenzi ili Maaskari wawewe kujenga nyumba zao za kuishi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Spika, mimi nimeamua kutozungumza kulalamika kwa kutumia *microphone*, kwa vile ninachokerwa nacho tayari nimeanza kunong'ona na Naibu Waziri wako, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri awasiliane na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Wilaya ya Ruangwa haina Kituo cha Polisi, haina *OCD* na hakuna Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pale Mjini pana Kituo kidogo cha Polisi kwenye kijumba chakavu eneo la Shule ya Msingi Ruangwa. Wananchi hupata huduma hizo Mkoani, yaani Lindi Mjini. Kule kwenda tu, nauli hawajiwezi. Kupata dhamana haiwezekani kwa vile mtuhumiwa hana ndugu wala jamaa, yeye ni mtu wa Ruangwa umbali wa kilomita 156 kama anatoka pale Ruangwa Mjini. Ni umbali zaidi kama anatokea Mandawa, Mamichiga ambako ni pembeni. Nalalamikiwa sana kwa mahabusu waliojaa Lindi Mjini wanaotokea Ruangwa kwa machungu wananiomba kuwa nifanye mpango kwa Serikali ili tukaazime Askari hasa *OCD* na watu wake kule nchi jirani ya Msumbiji. Haijulikani ni kwa nini hakuna Kiongozi huyo kama zilivyo Idara nyininge za Serikali. Kiongozi wa pale ni mwanamke, ni mchapakazi, lakini ni trafiki mwenye Cheo cha *Sergeant*. Pilikapilika za kuwa Kamanda wa Wilaya nzima nadhani haziendani na *speed* ya mipango yenu kwa hivi sasa. *OCD* haletwi kwa kuwa nyumba hakuna, lakini viongozi wenzake wapo katika eneo hilo na yeye ni Askari anaweza kuishi hata kwenye hema.

Nne, inasemekana Ruangwa hakuna uhalifu. Sio kweli! Mbona matukio ya wizi wa kutumia silaha yameanza kujitokeza! Kuna mgodi wa Namumgo ambako kumetokea *unreported cases*.

Mheshimiwa Spika, kuna ujangili kwa vile tupo na *Selous Game Reserves*. Hakuna Askari, ndio maana hawakamatwi. Mambo ya ndani mwa Tanzania kutunza Gereza hivi karibuni, nami naomba tupate *OCD*, Ofisi yake na Mahakama. Mtume Naibu wako aje aone pia namna silaha zilivyo peupe huku zikiangaliwa na waliopo rumande. Nyumba ile siyo imara. Naomba tafadhali sana, nikirudi wataniulizia tu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Matatizo ya ujambazi katika Wilaya ya Ngara, kuna matatizo makubwa ya ujambazi katika Wilaya ya Ngara. Karibu kila wiki kuna mtu anauawa kwa kupigwa risasi na majambazi. Hii inatokana na kwamba kuna bunduki nyingi katika mikono ya Wakimbizi amba ni majambazi wakazi wa Wilaya ya Ngara wanaomba yafatayo:-

- (1) Kuboresha uwezo wa Polisi ili waweze kukabiliana na majambazi wapewe silaha na waongezewe idadi ili waweze kukabiliana na wimbi la ujambazi;
- (2) Wapewe magari ili waweze kufanya doria hasa usiku;
- (3) Wapewe *Radio-Call* na simu za mikononi ili waweze kuwasiliana na Makao Makuu ya Wilaya - Ngara; na
- (4) Wavezeshwe ili wajenge Vituo vya Polisi katika kila Kata na Vijiji ambavyo vipo mipakani ambapo uvamizi unatokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakimbizi, matatizo mengi ya ujambazi yanatokana na Wahamiaji haramaau. Mipango ifanywe iliwakimbizi wote warudishwe kwao. Hii ndiyo njia pekee ya kudhibiti ujambazi.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Usalama na Raia.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Fuoni kwa imani waliyokionyesha Chama cha Mapinduzi kwa kukiamini na kukichagua kuongoza Jimbo hilo na kwa imani hiyo imeniwezesha kuwa Mbunge wa Jimbo hilo na kwa imani hiyo, ninaahidi nitawatumikia na sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, sasa nimpongeze Waziri wa Usalama wa Raia kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo na matumaini makubwa ya maendeleo katika Jeshi letu la Polisi. Nimpongeze Naibu Waziri kwa juhudi zake anazozionyesha katika uboreshaji wa Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Watendaji wote wa Wizra wakiongozwa na Katibu Mkuu. Baada ya shukrani na pongezi, sasa nichangie katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, sina budi kulipongeza Jeshi hili la Polisi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika mazingira magumu. Pia, nimpongeze *IGP* Ndugu Mwema kwa kipindi kifupi alichokaa katika uongozi wake ambaa unaleta matumaini ya kuwakomboa Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, ndugu zetu hawa wanafanya kazi kwa uzalendo wa kuipenda nchi yao pamoja na ndugu zao na kama sio uzalendo waliokuwa nao, wasingeweza kufanikisha kazi zao kutokana na mazingira magumu walionayo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ndugu zetu hawa kwanza ni kidogo sana kulingana na ongezeko la watu pamoja na ongezeko la uhalifu. Lakini kutokana na juhudi zao za msaada wa raia wema, kazi hii wanaitekeleza ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Polisi hawana nyumba za kuishi na walizonazo ni chache na wanaishi kwa kujibana bana kwa chumba kimoja kwa kila familia. Kwa hiyo, kuna haja ya ujenzi wa Serikali kuwapatia nyumba Askari hawa au wapewe mikopo ya kujijengea nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, sehemu wanazofanya kazi pia haziridhishi, chafu, hamna samani na zilizokuwemo ni mbovu, hata karatasi za kuandikia hamna.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya kufanya kazi hawana kama vile gari, redio za mawasiliano na hata ni kidogo Askari wanafanya doria na magongo.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Jeshi la Polisi ni madogo, lakini naishukuru Serikali kwa kuliona hilo mapema. Nakuhidi kulishughulikia katika kipindi hiki cha Bajeti. Lakini hali ilikuwa mbaya sana. Kwa hiyo, ninashauri, pamoja na kupandisha mshahara, naomba na posho nyingine ziende sambamba na kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, malipo duni ya baadhi ya Askari wanaostaafu ni kero na linatia huzuni kubwa kuona Jeshi moja la nchi moja, lina matabaka kwa Askari wake wanapostaaafu.

Mheshimiwa Spika, Askari walioajiriwa siku moja na kupandisha cheo pamoja na mshahara mmoja, lakini malipo ya kustaafu yanapitana kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Askari ambao wamefikia cheo cha *S/SGT* ambao wamefanya kazi kwa muda usiopungua miaka 30 na 40 kwa mshangao wale wa kiinua mgongo wamelipwa Sh. 1,290,000/= na hawapewi mafao ya uzeeni yanayotolewa kila baada ya miezi sita na wenzao wa pensheni wamelipwa Sh. 420,000/=.

Mheshimiwa Spika, kulingana na tofauti hiyo kwa Askari wa nchi moja ni hatari kubwa sana kwa ulinzi wa Taifa kwa sababu hawa wanaostaafu ni Askari na wengine walikuwa katika sehemu nyeti kabisa wanastaafu akiwa hajafurahi au hana imani anaweza kurabudiwa na akahujumu nchi na wale ambao bado wako kazini, wakati anaona kiyama kinakuja atakuwa hana utendaji mzuri na anaweza kutoa siri ya Jeshi kwa kupata chochote, Mungu atunusuru yasitokee hayo.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameyaona hayo, namwomba aharakishe kufutwa sheria hiyo inayotumika hivi sasa ikiwezekana baada ya Bajeti hii tu alishughulikia sula hili kwa ari na kasi mpya na kutokufanya hivyo ni kuvunja haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, pia katika Jeshi la Polisi katika kumjali Askari ninamwomba Mheshimiwa Waziri anapofariki, Askari wa Polisi baada ya kushughulika na mazishi tu, basi aendelee kulipwa mshahara kwa miezi mitatu ili kuwafariji wafiwa angalau kulipia madeni aliyoayaacha Marehemu, kwani hata kama Marehemu alifanya kazi, basi siku zile alizofanya kazi halipwi na siku ile ndio mwisho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na Viongozi wengine Watendaji kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo walizonazo.

Pili, nawapongeza kwa kutayarisha Bajeti nzuri yenye mwelekeo ingawa bado haijibu matatizo yote yanayolikabili Jeshi letu la Polisi. Ni kwa msingi huo, ndio nalazimika kumchangia kwenye baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kufanya kazi majengo ya Ofisi, majengo mengi ya Ofisi za Polisi yapo katika hali mbaya sana na hapa nataka nitoe mfano wa Kituo cha Polisi kilichopo Wilayani Mbozi Mjini Vwawa. Kituo hicho kimejengwa zaidi ya miaka 45 iliyopita, kimechakaa na hakikidhi haja, ni kidogo! Kituo hicho kinatazamana na barabara kuu ya Dar es Salaam – Zambia, wageni wengi hupita hapo na kwa kweli huonyesha sura mbaya kwa nchi yetu.

Nilipouliza swali la nyongeza, katika Mkutano huu kuhusu uchakavu wa Kituo hicho, nilijibiwa kwamba Kituo kipo kwenye mpango wa kujengwa upya. Lakini kilichonisikitisha zaidi ni kwamba mpango wenyewe ni wa miaka kumi, hii ina maana kwamba, inaweza ikafika mwaka 2013 bado hakijajengwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Wizara ikiweke Kituo hiki kwenye programu yake ya ujenzi, mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, nyumba za kuishi Askari, zaidi ya asilimia 70 ya Askari Polisi wote katika nchi hawana nyumba za kuishi na hivyo kulazimika kuishi uraiani. Hali hii siyo nzuri sana, hasa ukizingatia majukumu yao hali hii ni kuhtarisha maisha ya Askari hao. Naishauri Wizara na Serikali iendelee kujenga nyumba zaidi ya Askari.

Mheshimiwa Spika, hata nyumba zilizopo za Askari zipo kwenye hali mbaya sana. Kule Mbozi, Kituo cha Polisi Vwawa kina nyumba karibu tano, hivi ambazo zilijengwa pamoja na Kituo hicho. Nyumba hizo ni chakavu sana na hazijafanyiwa matengenezo yoyote ya kuridhisha. Naishauri Wizara iwaonee huruma Askari wetu kwa kuwatengenezea nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa unaotumika na Jeshi la Polisi, nina hakika na majeshi mengine, wa kuwfukuza Askari kazi siyo nzuri. Chini ya utaratibu wa sasa, Askari anapotuhumiwa kufanya kosa, kwa mfano la wizi, hufukuzwa. Tatizo linakuja pale ambapo Askari mhusika anashinda kesi, kwa utaratibu wa sasa, bado Askari mhusika hawezikurejeshwa kazini.

Sheria au kanuni hii ni mbaya, kwani huwahukumu Askari kabla ya kumsikiliza hapa *natural justice* iko wapi? Naishauri Wizara na Serikali ilione hili kwa kurekebisha Sheria au Kanuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwendo mkali wa magari ya abiria, tunashangaa kuona kwamba pamoja na *Askari Traffic* kumekuwa barabarani kwa wingi sana, lakini bado magari ya abiria huenda mwendo mkali sana na hivyo kusababisha vifo kwa wananchi ambao hawana hatia kabisa swali la kuijiliza ni kwamba Askari hawa hufanya kazi barabarani? Au ndio rushwa hufanya kazi!! Inashangaza pia kuona Mikoa ambayo ina Askari wengi wa barabarani *traffic* kama iliyotajwa ukurasa wa 13 wa kitabu cha Bajeti ndiyo inayoongoza kwa ajali.

Mheshimiwa Spika, hapa lazima tujiulize, kulikoni? Iweje pia kwa basi ambalo kwa dhahiri kabisa linaonekana kuwa na kasoro nyingi kwa mfano kwisha kwa matairiliruhusiwe kutembea na Askari wetu wa barabarani? *Speed governor* ziliishia wapi?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali na Wizara kuwadhibiti Askari wa barabarani kwa sababu inaonekana kuwa wanachangia kutokea kwa ajali za barabarani. Aidha, Askari wa barabarani wasikae muda mrefu kwenye Kituo kimoja na pale inapobidi wabadilishwe wafanye kazi za kawaida za Polisi.

Mheshimiwa Spika, inapotokea anayeendesha gari hajui lugha ya Kiswahili na ikatokea ametenda kosa, basi huachiwa na kuambiwa aendelee na safari. Tatizo hapa ni kwamba, Askari wetu wengi hawajui Kiingereza na lugha ya dereva mhusika. Hivyo kwao inakuwa kazi sana kuongea na mkosaji huyo. Nashauri Wizara iwafundishe Askari wa barabarani japo kiingereza kidogo kitakachowawezesha kuwasiliana na madereva ambao inawezekana hawajui Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulichangia ni la kuwapima wale ambao wanaomba kupatiwa leseni za kuendesha gari. Hivi karibuni dereva wangu ambaye alikuwa na leseni “E” na ambayo baada ya mafunzo Chuo cha Taifa cha Usafirishaji Dar es Salaam alirudi Mbeya ili aombe kupatiwa leseni, alichambiwa ni kwamba apeleke gari aina ya lori tani saba mpaka 15 ili ajaribiwe! Hivi huyu mtu anayejifunza gari na pengine ambaye kwao hata gari ndogo hana, hili kubwa la tani kati ya saba mpaka 15 atalitoa wapi? Naomba Wizara itoe maelezo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ambayo Wizara imekuwa inatoa kuhusu kupandisha vyeo Askari na kwamba hili linafanyiwa kazi, nadhani bado hili linahitaji kufanyiwa kazi zaidi. Askari ambaye mimi namfahamu ambaye aliajiriwa kazi mwaka 1992 kama *PC* hadi leo bado yuko hivyo hivyo. Kulikoni? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, malipo ya madai mbalimbali Askari wa *TAZARA*, Askari wengi wa Kikosi cha *TAZARA* hawajalipwa malipo mbalimbali kama vile za safari, matibabu na kadhalika zaidi ya miaka mitatu hivi. Naomba Wizara ifuatilie maana hali hii imewakatisha tamaa Askari wengi sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii. Nampongeza Waziri wa Wizara hii pamoja na Watendaji wale wote walioshiriki kuiandaa hotuba hii na naipongeza Kamati kwa mchango wake na ikaifanya hotuba hii kuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wake kwa kuongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kiwango na *speed*.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina wajibu wa kuongeza ufanisi katika kukabiliana na wimbi la uhalifu uliotapaka nchini ili kurudisha imani ya wananchi. Raia akitembea, akilala, hana raha hata kula chakula chake kwa hofu ya maisha yake hajui ni wakati gani atauwawa au kuporwa na majambazi Vijijini na Mijini. Lazima sasa ajue

hilo ni jukumu sio Mgambo wala Sungusungu, kwani ye ye hana majambazi wao wana silaha kila aina, huyu jambazi anazipata wapi?

Bila shaka kuna baadhi ya Polisi wanashirikiana na majambazi kuwapa silaha au wanajua habari zao, kwa sababu raia anaweza akaingiliwa na majambazi na akapeleka ripoti, lakini itachukua muda mrefu hajapata jibu mpaka majambazi watafanya uhalifu na kuondoka.

Kwa hiyo, Serikali ifanye uchugnuzi wa Askari hao walikuwa hawana imani na raia wao waondoshwe mara moja, ili wasilitie Jeshi letu doa na sifa lilizonazo.

Mheshimiwa Spika, Askari wetu hawana makazi bora. Kwa hiyo, Serikali iwajengee majumba ya kuishi, kwani Askari ana kazi nzito, sio Askari aishi uraiani kwani anaweza kushawishika na akaenda kinyume na dhamana yao.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Askari wa barabarani wanapenda kupokea zawadi pindi wanapokamata makosa kwenye vyombo hivyo bila kumpeleka kunakohusika.

Kwa hiyo, Serikali iwachunguze Askari hao na pindi atakapobainika, afukuzwe kwani hao wakorofii wataitia doa Wizara hiyo.

Vilevile, Askari wana hali mbaya kwenye kazi yao, kwani wana haki ya kuongezwa posho na mshahara ili wananchi waondokane na maneno ya wananchi kwa kusema wao ni walaji wa rushwa na wale raia watakaopeleka taafira wapewe zawadi na wala wasitangazwe ili wavuta unga au majambazi au wahalifu wasije wakawapotezea maisha yao. Askari waache kumbambikia kesi aliyekuwa hana hatia kwa kupewa zawadi wala akimkamata mtu asimtese kwa kumpiga au kumuadhibu.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema kwa kuniwezesha kuwa mzima na afya kamili na kuweza kuchangia katika hoja hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi wanavyojitahidi katika kukomesha suala zima la ujambazi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili Serikali inajitahidi kwa kufanya mambo mbalimbali ya doria na katika hilo wametoa pikipiki zitumike katika doria. Lakini kwa ushauri wangu, nahisi haya mapikipiki ni hatari kwa maisha yao kwani majambazi ni hatari sana. Wakishaona wanafuatiiliwa wanaweza kuwategeshea na kuhatarisha maisha yao. Kwani nakumbuka katika miaka ya nyuma ilikuwa ikifanya doria kwa namna hiyo. Baadhi ya Askari walipoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ni kazi ngumu sana ambayo watu wanayoifanya, kwa hiyo, inabidi wawe na ujuzi wa kutosha wa kuweza kulinda raia na mali zao na vile vile wawe na ustahimilivu wa kuweza kukabiliana na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ugumu wa kazi wanatakiwa waangaliwe vizuri na Serikali hasa kupatiwa nyumba nzuri za kuishi, maisha yaboreshwe, vitendea kazi vya kileo pamoja na kivazi.

Mheshimiwa Spika, Askari wanaishi katika mazingira magumu, mishahara hailingani na kazi zao, vilevile kivazi kibovu hakina hadhi ya Askari. Kutokana na ugumu wa maisha yao, inakuwa sio rahisi kuwatendea haki raia walikuwa na hali ya chini kwa hiyo, mazingira ya rushwa yanatawala.

Mheshimiwa Spika, kujikita katika suala la viongozi wa Zanzibar ambao wakati wa uchaguzi kugeuka kuwa wanasiwa na kutumia vyeo vibaya kwa kuwaamrisha Askari kutumia nguvu za ziada Zanzibar hugeuka kama nchi ya vita, badala ya Askari kulinda ria na mali zao, basi huwapiga raia na kupora mali zao.

Mheshimiwa Spika, tuna matumaini makubwa kwa Ari hii na nguvu na kasi mpya mambo yatabadilika watu wawe na haki ya kuishi kwa amani, raia wa Zanzibar wamepoteza imani kubwa kwa Askari kwa jinsi Askari walivyojigeuza makada wa CCM. Sheria ya Vyama vya Siasa ilivytaka kutoingiza Askari katika siasa kwa sababu walijua Askari wanalipwa na Serikali iliyopo madarakani. Kwa hiyo, ni lazima wawafuate wanilotaka. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ifuate sheria. Ahsante sana na nashukuru.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, napongeza hatua za haraka zilizochukuliwa kututetea safu mpya ya mapolisi Itigi ambako huko nyuma majambazi na wahalifu walituhumiwa na wahalifu, walituhumiwa kushirikiana na Polisi kwa muda mrefu. Sasa hivi kazi ni nzuri na wananchi wana imani na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, napongeza na hususan Mheshimiwa Waziri Mwapachu na Naibu Aboud kwa kazi nzuri na mikakati mizuri waliyopanga kukabiliana na wimbi la ujambazi Dar es Salaam. Hata Kambi ya Upinzani wamekiri wazi kuwa ujambazi sasa umehama Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Nashauri mikakati hiyo hiyo ipelekwe Zanzibar iwatokomeze.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa mara nyingine katika Wizara ya Usalama wa Raia. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri na timu yao ya wataalam kwa hotuba ya Bajeti ambayo ina matumaini kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, Polisi wamekuwa wakipata lawama kubwa na wananchi kutokuwa na imani nao kwa namna ambayo Jeshi hili lilivyokuwa likilaumiwa kutaka rushwa. Naomba chombo hiki kipatiwe vitendea kazi vya kisasa na elimu zaidi ili liwe Jeshi la kisasa. Sambamba na hayo, wapatiwe nyumba bora za kisasa.

Mheshimiwa Spika, ningependa suala hili liangaliwe na kufanyiwa marekebisho. Kuna baadhi ya Vituo vya Polisi hasa Jiji la Dar es Salaam Polisi Kituo cha kazi, mfano Msimbazi Polisi, yeze mwenyewe anaishi Kituo cha Buguruni. Inapotokea Msimbazi ambako likitokea tukio na Mkuu wa Kazi akimuhitaji kwa dharura, Askari huyu hapatikani na hii huzorotesha utendaji kazi. Napendekeza kila Askari akae na kuishi katika Kituo chake ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, suala la ujambazi limekuwa ni kero. Naomba Wizara iangalie sasa jinsi ya kushirikisha wananchi, wakiwemo Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji kwa sababu majambazi wanaishi na raia na hii itasaidia kuwagundua kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia mpya katika Jiji la Dar es Salaam baadhi ya Madereva hupitisha na kuendesha magari yao wakati taa nyekundu za barabarani zikiwaka na hii husababisha ajali zisizo na lazima. Naomba hali hii idhibitiwe na Askari wa Barabarani.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua ni kwa nini wakati wa uchaguzi Mkuu Jeshi hili hutumia nguvu kubwa ya kijeshi na mateso makubwa kwa wananchi hata mahali ambapo hapana fujo, huja na kupiga mabomu na kadhalika? Naomba kuwasilisha.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana kwanza Mheshimiwa Waziri Mwapachu kwa uongozi mzuri tangu akabidhiwe Wizara hii.

Pili, nimpungeze sana Naibu Waziri kwa kazi nzuri za kujituma na ziara nyingi za kuwafikia wananchi na kusikia kero zao. Naupongeza uongozi wote wa Jeshi la Polisi kuanzia *IGP* Said Mwema na Makambanda Mikoani, kazi yao inaonekana.

Aidha, nimpungeze Jeshi kwa kuwakubalia Askari wake wanapoomba kujiendeleza hasa kozi za Walimu. Nikiwa Chuo cha Usalama Bukimba, nimepokea vijana sio chini ya 33 kuanzia mwaka 2004/2005 hadi nilipoondoka mwaka 2005 mwishoni. Idadi hii naamini inaongezeka mwaka hadi mwaka kwa vyuo vingine vikiwemo Vyuo Vikuu. Sasa swali langu ni kwamba Walimu hawa Mapolisi wanatumiwaje baada ya utaalam huo wa Ualimu kwa masomo mbalimbali? Wengine wao ni wazuri sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, Jeshi lijenge au lione jinsi ya kupata Shule ya Sekondari *specifically* kwa ajili ya kuendeleza wale wachache wasiokuwa nayo bado. Lakini pia isaidie watoto wa familia za Askari hawa na wananchi wanaoishi maeneo jirani na *barracks* hizo. Hosteli pia itafaa maana italipatia Jeshi *income* kwa matumizi yao ya maendeleo na ya kawaida. La msingi, wale Walimu wasipoteze utaalam na taaluma zao za Ualimu bure wakati wanaweza wakawafundisha wenzao na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba aliyosoma Mheshimiwa Waziri kwamba, wapo Polisi wanaojishughulisha na siasa ukurasa wa 30 na 31, tatizo hili liko hasa Zanzibar na inafika wakati tukio lolote analoripoti mtu wa CCM linachukuliwa hatua haraka haraka na yako matukio mwana-CCM anampiga Askari na Mkuu wa Kituo cha Polisi ameshindwa kuchukua hatua yoyote. Mfano halisi ni ule uliotokea Mkoani Pemba. Kwa maana hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, sio suala la kusema tu, bali alieleza Bunge lako Tukufu ni hatua gani hasa Jeshi la Polisi litachukua ili kukomesha tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, Polisi kubakia kituo kimoja kwa muda mrefu, hili ni suala lingine linaloleta usumbufu kwa raia kwa sababu Askari aliyepo Kituoni muda mrefu hujiona ni yeye tu wala hakuna wa kumzidi. Hujenga jeuri na kiburi na kujishughulisha na biashara ambazo haziwahusu. Mfano mmoja ni kule Pemba ambapo yuko Askari ambaye amekaa Kituo hicho ambacho hivi sasa ni chake, anavyojiona na kujishughulisha na biashara ya kukata miti na hivi sasa amekuwa mashuhuri kusafirisha mbao kutoka Pemba kwenda Unguja na miti yote Pemba tayari ameshaimaliza.

Mheshimiwa Spika, kutofanya upelelezi kabla ya kukamatwa mtuhumiwa, nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri pia amekiri katika hotuba yake ukurasa wa 28 kuwapa Askari hasa wa upelelezi mafunzo kwa lengo la kuwaongezea ujenzi. Kwa maana hiyo, kuna kesi nyingi sana ambazo watuhumiwa wengi wameshaswagwa rumande kwa kipindi kirefu na hatimaye watuhumiwa wanaachwa huru kwa kushinda kesi.

Mheshimiwa Spika, ni watu wachache wanaojua Sheria na kuwashitaki kwa wale waliosababisha tuhuma. Hivyo, napendelekeza kwa Mheshimiwa Waziri kwamba Askari wapewe mafunzo na kwamba wajue sio vizuri, tena haifai kumkamata mtu na kumpeleka katika vyombo vya Mahakama ikiwa bado hujafanya upelelezi wa kutosha na kwa hiyo, Wizara ya Usalama wa Raia walete Muswada hapa Bungeni utakaompa raia ye yote aliyefunguliwa kesi za kubuni, kupata fidia ya moja kwa moja bila kufungua kesi.

Mheshimiwa Spika, suala la Polisi kuwa chombo cha ukoo fulani: Kule Unguja imezoleka tena kwa muda mrefu sasa kwamba katika kila Askari 100 basi Askari 80 wanatoka katika eneo moja. Kwa maana nyingine, ajira za Uaskari zinazingatia vigezo gani hata ikasababisha asilimia kubwa kutoka Mkoa au Wilaya moja tu? Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atufanfulie kuhusu namna gani hizi ajira za Askari zinavyotolewa na ni kwa nini eneo hili la Zanzibar likawa na Askari kuanzia Bosi Mkuu mpaka ngazi za chini wanatoka eneo moja tu? Vinginevyo tutaamini ajira ya Askari inatolewa kwa ubaguzi mkubwa.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Bakari Mwapachu kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Wizara hii mpya ya usalama wa raia. Kwa kweli kuteuliwa kwake ni ishara ya uwezo aliokuwanao katika kuongoza Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Mtoni Zanzibar kwa kunichagua kwa kura nyingi na mimi nawaahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hoja ya Wizara hii, kwanza napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wameweza kuifanya kwa kipindi kidogo kuweza kupambana na ujambazi na hatimaye kuweza kupungua kwa wimbi hilo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria na Kanuni za Jeshi la Polisi, nikija kwenye kitabu cha Bajeti hii ukurasa wa 35, napenda kuipongeza sana Wizara hii kwa kutaka kuzipatia upya Sheria na Kanuni za Jeshi la Polisi kwani baadhi ya sheria hizo zimepitwa na wakati na zinahitaji marekebisho hasa kuhusu mafao ya kustaa fu pensheni na kupandishwa vyeo kwa Askari wa chini. Kama sheria hizi zitafanyiwa marekebisho, ni imani yangu kuwa Jeshi hili litakuwa zuri na Askari watakuwa na imani nalo.

Mheshimiwa Spika, wimbi la ujambazi Zanzibar, mnamo miezi ya Julai, 2006 majambazi yamevamia maduka ya wafanyabiashara na kupora fedha pamoja na kuwa jambo ambalo kwa Zanzibar sio kawaida, matokeo yake ni kusababisha hofu kubwa kwa wafanyabiashara pamoja na wananchi wa visiwani. Ushauri wangu, namwomba Mheshimiwa Waziri, ili kuondoa tatizo hili la ujambazi Zanzibar, ni kwanini watu wanaingia kiholela? Kuanzishwa utaratibu wa vitambulisho ili kuweza kujua nani aliyeingia na anatoka wapi, kwani kwa asilimia 95 ujambazi Zanzibar unafanywa na wageni kutoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Wizara hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. MWAJUMA HASAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe kuchangia katika Wizara hii. Baada ya shukrani, sasa naomba nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Usalama kwa Raia ni Wizara yenyе kuleta maslahi kwa raia, kwani mlinzi wa mali za raia ni Polisi. Sura ya Wizara hii, muda mrefu uliopita, Jeshi la Polisi mara nyingi liliacha utaratibu wake wa kikazi na kuijingiza katika shughuli za kisiasa. Hali hii ilitokana na uongozi wa Jeshi hili kuwa ulishiriki kikamilifu kisiasa.

Mheshimiwa Spika, sasa Jeshi la Polisi limekamilika na linaonesha wazi kazi zao. Muda mrefu nchi yetu iligubikwa na wimbi la majambazi kiasi ambacho wananchi hawakuwa na uhakika wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kama ni kushukuriwa, sijui nimuanze nani? Ama Rais ama Waziri ama Naibu Waziri ama Inspekte Mwema!

Mheshimiwa Spika, hali ya nchi yetu ni shwari, majambazi wamepunguzwa sana na nimatumaini yetu watatoweka kabisa. Serikali sasa inafaa iwayue Askari mzigo

mkubwa Askari wetu wamebeba mzigo ambao kwa kweli ni mkubwa. Sasa naomba mambo yafuatayo wamesaidiwa, nyumba za Askari mbovu sana, vitendea kazi havitoshi, mishahara haikidhi haja. Ni vyema Serikali, mambo haya wayape kipaumbele ili waweze kufanya kazi zao kimapenzi na kwa hamu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendo kama vile, gari, pikipiki, Askari hawana uwezo wa vitu hivi, jambo ambalo wale wanaoishi katika maeneo ya uraiani huchelewa kazini kwao. Ni vyema basi itafute mipango ya kuwaondolea kudhia hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maadili ya kazi za Polisi kuna malalamiko makubwa juu ya Askari wa Barabarani (*Traffic*) mara nyingi huwasumbua wananchi wakati wa safari zao. Kuonesha ni ishara za kupewa rushwa. Wakati umefika sasa wa Jeshi la Polisi kuwafichua wale wote wanaoleta madawa ya kulevyaa katika nchi yetu jambo ambalo hupelekea vijana wetu kuathirika kimwili. Kwa vile Jeshi la Polisi limeweza kudhibiti ujambazi katika nchi yetu na sasa itupe macho katika maeneo yanayopitisha madawa ya kulevyaa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naipongeza Wizara. Kazi njema.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndio inayobeba dhima na jukumu la usalama wa raia pamoja na mali zao. Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa katika ulinzi wa raia tena katika mazingira magumu ya kazi zao, bila hata kujali aidha wakati wa jua au mvua, mchana usiku saa zote wako kazini.

Mheshimiwa Spika, Askari wanahitaji mafao bora zaidi ili kujimudu na kujikimu na maisha, wanahitaji mishahara bora, marupurupu ya kujikimu ili kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Jeshi la Polisi wanahitaji kuwa na nyumba bora za kuishi na familia zao pamoja na vitendea kazi vya kisasa ili kukabiliana na majambazi na wahalifu.

Mheshimiwa Spika, kila kizuri hakikosi kasoro. Baadhi ya Askari wamekuwa na tabia ambayo hairidhishi hasa ya kuwatesa raia na kuwabambikia kesi ambazo hazina msingi wowote. Kwa mfano wanapomkamata mtuhumiwa, wao ndio wanajifanya Mahakimu, kwanza kumpiga kabla hata ya kumpeleka Mahakamani hata kama mtuhumiwa huyo wakati wa kumkamata alikuwa mtulivu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Askari wa Jeshi la Polisi, wamewafanya raia wasiwe na imani nao na hili naomba nipatiwe majibu. Siku ya Jumanne tarehe 30 Novemba, 2004 ilikuwa ni siku ya pili ya uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura. Mnamo saa 7.00 za mchana kikundi cha watu walichoma moto kwa kutumia *petrol* nyaraka zote na baadaye kutokea vurugu katika Kituo hicho cha Kiwani.

Katika Jimbo langu, la kushangaza, watu zaidi ya 35 walifkishwa Mahakamani. Kwa hili sina tatizo nalo, Mahakama ndio waamuzi. Swali langu: Je, wale waliohusika na kuchoma moto, mbona wao hawakuchukuliwa hatua yoyote ya kisheria? Je, wao

wana kinga au wao ni nani katika nchi hii? Mheshimiwa Waziri, naomba jawabu ili kujenga imani na Jeshi lako na raia.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Usalama Barabarani nao wanahitaji kuangaliwa, kwani inaonekana na wao wanawasumbua madereva na waendesa vyombo nya moto barabarani, kusimamisha vyombo mara kwa mara hata kama chombo hicho hakina tatizo lolote kwa nia ya kupata chochote. Ahsante.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kusema, ninaunga mkono hoja.

Aidha, ninapenda kuwapongeza Waziri wa Usalama wa Raia, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa Bajeti nzuri na kwa kazi nzuri waliyofanya tangu walipoteuliwa kuiongoza Wizara hii mpya na nyeti, takribani miezi saba iliyopita.

Mchango wangu leo hii ni kwa uchache tu na unahuhusu hususan maslahi ya Polisi. Pamoja na nyongeza ya mshahara iliyotolewa na Serikali hivi karibuni, naomba Serikali ifikirie tena na iwaongezee Polisi maslahi kwa lengo la kuwapo motisha zaidi ya kufanya kazi, lakini pia kuwaondolea kishawishi cha Rushwa. Kazi ya Polisi ni ngumu, inahitaji moyo, hivyo ni muhimu pia maslahi yakawa mazuri.

Mheshimiwa Spika, rushwa, hususan kwa Askari wa Idara ya Usalama Barabarani Mkoa wa Shinyanga imeota mizizi. Naomba Serikali na hususan *IGP* afuatilie mienendo ya Askari wa Idara hii hususan katika Wilaya ya Kahama ambayo imekuwa ni kero kwa wananchi. Vitengo hivyo vinatia doa kazi nzuri ambayo inafanywa na Polisi wa (M) na Wilaya ya Kahama ya kutokomeza ujambazi amba hapo nyuma ulikuwa umeota mizizi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mwapachu na Naibu Waziri Mohamed Abood kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa wakati huu wa wimbi la ujambazi. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Mahiza kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kusisitiza yafuatayo:-

Suala la kuwa taratibu mbili za pensheni na *gratuity* kwa Jeshi la Polisi limepitwa na wakati, nakubaliana na wazo la Serikali la kupitia upya taratibu hizi ili pawe na utaratibu mmoja tu wa Pensheni kwa Askari wote wa Polisi ili kuwapa Polisi wastaafuli haki yao ya kuishi salama na familia zao. Nashauri Serikali/Wizara iharakishe kushughulikia suala hilo.

Pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikieleza kuwa suala la chakula kwa mahabusu na usafiri kwa watuhumiwa ni wajibu wa Jeshi la Polisi. Bado yapo malalamiko kutoka kwa wananchi. Nashauri hatua zaidi zichukuliwe ndani ya Jeshi la Polisi, lakini pia Elimu kwa wananchi itolewe.

Bado *Traffic Police* wako wengi hawatimizi wajibu wao. Ajali zinazotokea zina mchango mkubwa wa *Traffic*, kwani mabasi yanapita mbele yao, wanaona jinsi

walivyojaza na wanavyoyaachia baada ya kupewa chochote. Matokeo yake ajali zinauwa watu wengi.

Inasikitisha sana kuona kuwa magari husimamishwa kila baada ya *distance* fupi na *Traffic Police* na kubwa zaidi ni kutaka kupewa chochote. Ukisafiri kwenda Mbeya, ndio utasikitika zaidi, kwani utasumbuliwa kila baada ya Kilometra tano na kumi. Naomba Jeshi la Polisi na Wizara liangalie tatizo hili kwani linakera.

Mheshimiwa Spika, Polisi Singida wanafanya kazi vizuri, lakini wanahitaji kuongezewa vitendea kazi hasa magari kwa Wilaya ya Singida Vijijini ambayo inapakana na Mkoa wa Tabora ambapko ni mbali sana, kwani yanapotokea matukio ya mauaji au uhalifu Mgangila wanachelewa kufika katika matukio.

Mheshimiwa Spika, suala la makazi kwa Polisi lisiishie Dar es Salaam pekee, bali hata Singida kuna ubaha wa nyumba kwa Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko kuhusu ucheleweshaji wa kesi kwa kuchelewa uchunguzi. Naomba hili nalo litazamwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Usalama wa Rais kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumpongeza Waziri wa Usalama wa Raia kwa hotuba yake nzuri, lakini naomba na mimi nizunguzie katika baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la usalama wa Askari Polisi. Watumishi wa Jeshi hili la Polisi ni watu wanaofanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa mfano, Polisi ni watu wanaopambana na watu wa hatari zaidi kama vibaka na majambazi yakiwamo majambazi sugo, ambao wanatumia silaha kali pamoja na mbinu za kisasa

Pili, Maaskari hawa kazi yao ni kuokota mizoga ya binadamu wanaokufa na kutupwa aidha, porini au mtoni na pengine maiti hizo zimeshachukua muda mrefu, yenye harufu mbaya sana, lakini hawana kinga ya kutosha.

Tatu, Askari hawa wanaishi katika nyumba zisizoridhisha. Aidha, nyumba zenye vyumba vidogo au *full suit* (yaani bati kwa bati).

Nne, utakuta mtu anafanya kazi ngumu na ya hatari kwa maisha yake, lakini pia kiafya, lakini hana motisha ye yeyote kitu ambacho kinamkatisha tamaa, hivyo kukosa ari ya kufanya kazi. Lakini pia inaweza kuwa ni kichocheo kwa baadhi ya Askari kuomba rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba, kuanzia sasa Askari yeote ambaye yupo kwenye doria, ingefaa wapewe sare ya kuzuia risasi (*Bullet Proof*).

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizoendelea, Askari anatakiwa wakati wote wavae *bullet proof* kujikinga na risasi za majambazi.

Mheshimiwa Spika, nguo za kuzuia kupenya risasi ni muhimu mno kwa Askari Polisi kuliko hata Bunduki yenewe. Kwa mfano bunduki anaweza kuitupa au kunyang'nywa na majambazi, lakini *bullet proof* itamsaidia kumlinda, hivyo kuokoa maisha yake. Lakini pia Askari anapata moyo wa kufanya kazi yake kwa ujasiri zaidi kwa vile anayo kinga ya kufaa.

Napendekeza kuwa, Askari wanapokwenda kuokota maiti, basi wapewe vifaa vyta kujikinga kama *gloves, gumboots* na *apron* za kuzuia kuchafua nguo zao.

Pia, nashauri Askari hawa wajengewe nyumba nzuri za kuishi. Wizara hii inaweza kupanga na Wizara ya Mambo ya Ndani ili Magereza waweze kujenga nyumba kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashauri Askari hawa wapewe posho wakati wa kufanya kazi zaidi (*Extra duty allowance*).

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili pia naomba lipatiwe vifaa vyta kutenda kazi kama magari ya kutosha ili yawawezeshe kusafiri kwa haraka inapotokea matatizo na vile vile Ofisi za Jeshi la Polisi ziboreshwe ili wahusika waweze kufanya kazi katika mazingira yanayofaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie suala la wananchi wengi kubambikiziwa kesi za kubuni.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia ya baadhi ya Askari kuwapiga watuhumiwa wa makosa mbalimbali kabla na baada ya kuwafikisha Polisi. Huu sio utaratibu wa kisheria. Ni vyema ukakomeshwa mara moja. Pia, kumekuwa na tatizo la gharama za kukamata wahalifu kurudishwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Suala la ulinzi na usalama wa raia ni jukumu la Polisi. Inashangaza sana kuona jukumu hili linachukuliwa na *KMKG, JKU, KVZ* na kadhalika. Tunaomba Waziri atupe maelezo ya kina, kwa nini suala la ulinzi linaachiwa Vikosi vyta Zanzibar ambavyo vina kazi za kulinda na kuzuia Mageuzi au kuzima moto?

Mheshimiwa Spika, Askari wana dini zao. Ni vyema wakapangiwa utaratibu mzuri wa kazi ili waweze kupata muda wa kuabudu hasa wale Askari wanaopangiwa zamu barabarani kusubiri misafara ya Viongozi.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwa maandishi katika hotuba ya Waziri wa Usalama wa Raia.

Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia kwa hotuba nzuri iliyooonesha wazi mipango mizuri ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa siku zijazo. Nampongeza pia kwa kazi nzuri ambayo Wizara imefanya ya kupambana na uhalifu. Nampongeza pia Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kulipa kipaumbele suala la usalama wa raia wa Tanzania. Hakika viongozi wetu hawa wameonyesha dhahiri kuwa wamepania kuwawezesha wananchi kiuchumi kwani ni vigumu kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi iwapo hawana uhakika na usalama wao na mali zao. Kwa hiyo, ninaamini kabisa endapo uchumi wa nchi yetu kwa upande wa mwananchi mmoja mmoja utakuwa basi umechangiwa kwa kiasi kikubwa na uhakika na usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kuliomba Jeshi la Polisi kama halijarekebisha mwenendo wake, basi lijirekebishe. Japokuwa mabadiliko ya uongozi yamefanyika, lakini bado wananchi wengi hawajakata imani nalo kabisa. Hivyo, inabidi Jeshi hili lifanye kazi ya ziada ili kubadilisha mtazamo hasi wa wananchi uliotokana na vitendo viovu vya baadhi ya Askari hasa vile vya kushiriki katika vitendo vya uhalifu ukiwemo ujambazi na rushwa.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la usalama barabarani. Katika hili, nianzie na kasi kubwa ya magari ya abiria wakati wa safari. Mwendo huu wa kasi kubwa ni hatari kwa usalama wa abiria. Nakumbuka kuna kipindi Askari walikuwa wakisimama barabarani na kifaa cha kupimia kasi ya mwendo wa gari. Lakini hivi karibuni sijaona tena hilo zoezi likifanyika na hivyo magari hukimbizwa kama vile yameibiwa. Je, ule utaratibu wa Askari kudhibiti kasi, umeishia wapi? Naomba Bunge lipewe sababu ni kwa nini kasi hii inaruhusiwa?

La pili ni ujazo wa abiria kuzidi uwezo wa gari. Naomba yafuatayo yawekwe wazi: Je, ni abiria wangapi wanaruhusiwa kuzidi idadi ya Viti? Je, wakikaa katika *corridor* ya gari na katika lile eneo la dereva bila kusimama ni sahihi?

Mheshimiwa Spika, suala la kuruhusu magari mabovu kusafiri mwendo wa mkali hali ya kuwa wamebeba abiria, ni hatari kubwa mno kwa maisha ya abiria hao. Japokuwa mkakati umetajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia kuhusu udhibiti wa magari mabovu, napenda kuiomba Wizara ianze kuchukua hatua za awali kwa haraka ili kunusuru maisha ya wananchi kutokana na ajali ambazo zingeweza kuzuulika.

Mheshimiwa Spika, lipo pia tatizo la mlalamikaji kulazimika kugharamia gharama za kumtafuta mhalifu. Kwa mfano, mtu anaweza kuamua kuiba Morogogo na kukimbilia Dar es Salaam. Cha kusikitisha ni kwamba mlalamikaji anapofanikiwa kutambua alipojificha mhalifu huyu, mlalamikaji hulazimika kugharamia nauji na

gharama zote za Askari toka Morogoro hadi kumpata mtuhumiwa zikiwemo za *taxi* na malazi katika hotel nzuri pamoja na chakula kizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba hili liangaliwe upya, kwani linakatisha tamaa, kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi na wakati huo huo linamhimiza mhalifu kuendeleza kazi yake, kwani kukamatwa sio rahisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuishauri Wizara itoe mafunzo mazuri ya mahusiano kati ya raia na Polisi. Maaskari waache kutoa lugha chafu, kuwafokea na kuwasukuma raia pale wanapokuwa wakiwashuku. Ile hali ya kumkamata mtu nguo na kumvuta au kumsukuma ni udhalilishaji. Pengine hili lingefanyika pale ambapo raia anaonekana kuwa mkorofii.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba, kuna baadhi ya Askari, sijui ni kwa sababu zipi huamua tu kumkamata mtu akiwa katika shughuli zake na kuanza kutoa lugha chafu bila hata kuomba maelezo, wakiulizwa sababu hujibu, kuwa wameagizwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza niunge mkono hoja asilimia mia moja.

Niwapongeze Waziri Mwapachu, Naibu wake Mheshimiwa Mohamed Aboud, Katibu Mkuu Mahiza, *IGP* Said Mwema na Makamisha wote wapya kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya kuliweka Taifa katika hali ya amani na usalama dhidi ya vitendo vyu ujambazi.

Mimi napenda nijielekeze sana kwenye tatizo la ongezeko la mahabusu kwenye *Police Castodies* na kwenye Magereza yetu. Nashawishika kuamini kuwa, Jeshi letu la Polisi likiweka kipaumbele katika taaluma ya *Investigation* na hasa *Criminal Investigation* kwa Polisi wote (*Plain na uniformed Police*) tutafanikisha sana zoezi la kupunguza idadi ya Mahabusu nchini. *Professional Criminal Investigation* itaondoa mtindo wa kumbakumba, yaani mtindo wa kukusanya watu kadhaa kama watuhumiwa na kuiachia sheria iwachuje.

Ni imani kubwa sana na uongozi mpya wa Jeshi la Polisi na ni matumaini yangu kuwa kifungu (f) na (i) ukurasa 62 na 63 ya kwenye kitabu cha Bajeti ya Wizara vitakuwa na maana zaidi iwapo somo hilo la *Criminal investigation* linapata kipaumbele. Naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake ambao wameandaa hotuba hii.

Pia, napenda kuwapongeza Askari wetu hawa kwa kazi kubwa wanazozifanya hasa kulinda usalama wa raia na mali zao. Askari wetu wanafanya kazi kubwa ya kupambana na majambazi na kupelekea kupata matatizo mbalimbali. Kwa hiyo, Serikali

itoe huduma nzuri kwa Askari wetu wanapopata matatizo wakiwa katika mapambano hayo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuiboresha Wizara hii kwa mishahara na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye majengo chakavu Makao Makuu ya Mkoa wa Kaskazini Uguja, majengo yake ni chakavu sana tena majengo haya hayaelekei kuitwa Makao Makuu jinsi yalivyochakaa. Ninaionba Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri, atakapotoa mgao wa kukarabati majengo chakavu, basi Makao Makuu ya Mkoa wa Kaskazini Uguja mtupe kipaumbele ili wafanya kazi wetu waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, vitenda kazi, kama vile magari, maboti na kadhalika, vitu hivi vinahitajika katika Mkoa wa Kaskazini Uguja, kwani Mkoa wa Kaskazini Uguja una mahoteli mengi ya kitalii.

Mheshimiwa Spika, Askari wanapostaifu, hucheleweshewa kupewa viinua mgongo vyao na kuwasababishia matatizo makubwa wastaifu wetu wa kimaisha.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii, Askari anapokaribia kustaaifu, basi afanyiwe mambo yote yanayostahili ili akistaifu pasiwe na usumbufu apatiwe mafao yake haraka ili aweze kukabiliana na maisha yake ya kila siku. Pensheni ni tatizo kwa wastaifu. Hivi kweli Askari akipewa kiinua mgongo akae miezi mingapi ili aweze kupewa pensheni yake? Kama Askari yuko Zanzibar: Je, aifuate wapi pensheni yake Askari huyu.

Mheshimiwa Spika, ninaombaa Mheshimiwa Waziri anipe majibu ili wastaifu wetu wamsikie.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa Askari ni tatizo katika utendaji kazi. Serikali iwaongezee kuajiri Askari ili tuweze kukomesha zaidi ujambazi nchini. Ninaunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri anijibu, kwani nimeomba kuchangia kwa kusema nimekosa. Ahsante.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanazofanya. Hivi sasa imani ya wananchi kwa Polisi imeongezeka.

Hata hivyo, ningependa kuiomba Wizara kutekeleza yafuatayo:-

1. Majengo mengi ya kuishi na Ofisi ni ya siku nyingi sana na hayalingani na hali ya sasa. Ni aibu sana kukuta Polisi wanaishi kwenye mahema au nyumba za “*Unepot*” bati tupu. Serikali ijenge nyumba za kutosha za kuishi Polisi. Vyombo vya

fedha visaidie katika kutoa fedha za mkopo kwa madhumuni hayo (mfano *NSSF, ALPF, PPF*);

2. Kuimarisha Vituo vya Polisi vilivyojengwa na raia kwa kujitolea Vijijini. Vituo hivi vipewe magari na pikipiki kuweza kusafiri kwa urahisi Vijijini. Pia, kuongeza Polisi kwenye Vituo hivi.

Hapa ningependa kutoa ombi maalum. Kituo cha Polisi, *Mvumi Mission* kipewe usafi wa hakika, maana hivi sasa hawana usafiri wa aina yoyote. Pia, naiomba Wizara kuongeza majengo ya Ofisi ya Kituo hicho.

Kuhusu ulinzi wa Mgambo, Polisi itengeneze utaratibu wa namna Polisi wanavyoweza kushirikiana na vikundi hivyo kama Mgambo na Sungusungu, maana Polisi nchini ni wachache mno.

Serikali ihakikishe kwa madeni ya aina yoyote ya nyuma wanayodai Polisi yalipwe mara moja. Polisi waishi kwenye Makambi ya Kijeshi na sio kukaa uraiani. Hii itaongeza ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa kuimarisha ulinzi wa majini na *Lake Tanganyika*, maana wananchi waishio kandokando ya Ziwa Tanganyika huporwa mara kwa mara na maharamia toka Congo. Jambo hili liangaliwe haraka.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wizi wa mifugo ni kubwa sana katika sehemu za wafugaji. Wizi umeshamiri sana. Jeshi la Polisi litengeneze mpango maalum, maana kila Kikosi cha *STPU* hakijaweza kudhibiti kikamilifu tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha Askari wetu wana vitendea kazi muhimu na vya kisasa kama Vyombo vya mawasiliano vya masafa marefu na mafupi. Kila Kituo cha Polisi kiwe na chombo cha mawasiliano ya hakika ili kuweza kuwasiliana kwa haraka na hakika. Pia, wapatiwe vyombo muhimu vya usafiri hasa kwa Vituo vidogo wapewe pikipiki.

Mwisho, napenda kuwapongeza tena Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayofanya ya kulinda raia na mali zao. Naunga hoja mkono.

**MHE. FELIX N. KIJKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara ya Usalama wa Raia katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la wimbi la wahalifu kutoka nchi jirani na hasa kwenye Mikoa yenyе Wakimbizi kama vile Kigoma, Kagera, Tabora na Rukwa. Nikizungumzia Mkoa wa Kigoma ambaо upo mpakani na nchi za Burundi na DRC, kumekuwa na matukio ya ujambazi kwenye Vijiji ikiwa ni pamoja na yale maeneo yanayozunguka Kambi. Ni dhahiri kuwa Makambi yote yanalindwa na Askari Polisi. Lakini utaratibu wa kuwabadili Askari hao kila baada ya miezi sita ni kidogo mno kwa

sababu kipimo hicho ndicho Askari anakuwa amejenga mtando wake wa kufanya kazi. Ninadhani ingekuwa vizuri Askari wakibadilishwa baada ya mwaka mmoja.

Hata hivyo, ili kukabiliana na ujambazi unaofanywa, tatizo kubwa wanalo kuwanalo Askari wanapokuwa kwenye doria, ni uhaba wa mafuta unatokana na kasma ndogo wanayoipata. Je, Waziri anaweza kutoa hofu wananchi wa mpakani kuwa katika kasma ya mwaka 2006/2007 kiasi cha mafuta kitakachotolewa kwa Vituo vya Polisi huko mpakani kitaongezwa?

Mheshimiwa Spika, Askari Polisi yuko kazini saa 24. Hata hivyo, malalamiko yaliyopo ni Askari kutokulipwa malipo ya ziada ya kazi baada ya saa za kazi. Je, Waziri mwenye dhamana anaweza kuwatoa hofu Askari kuhusu hilo ikiwa ni pamoja na kuwaongeza mshahara?

Mheshimiwa Spika, tatizo la mawasiliano ya redio kwa Vituo vidogo vya Polisi ni tatizo sugu linalochangia utendaji kuwa mbaya na hasa nyakati za usiku. Je, Waziri mwenye dhamana anaweza kuwatoa hofu wote Askari wanaofanya kazi kwa mazingira magumu kuwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007? Sasa redio zitanunuliwa ikiwa ni pamoja na kuweka mitambo ya kurefusha masafa toka zile sehemu ambazo ziko mbali.

Mheshimiwa Spika, nyumba wanazolala Askari Polisi kwenye Vituo vyote zimejengwa kama sare. Kwa maoni yangu, ni adha kubwa sana Askari mwenye familia yenye watoto kukaa kwenye nyumba yenye chumba kimoja. Hicho ni kilio cha Askari cha muda mrefu ambacho ninategemea Waziri atalizungumzia ili kuwashamasisha Askari katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Mara nyingi askari katika utendaji wao wa kila siku wamekuwa wakipambana sana na tatizo la usafiri na hasa mijini. Tatizo kubwa ni kwamba yanatumika magari yanayotumika kila siku katika ukamataji na ufuutiliaji wa matukio yanayofanywa na askari wa Upelelezi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Kikosi hiki kikawa na magari ya kufanya kazi ambayo hayatatambuliwa kwa mara moja na wahalifu.

Mheshimiwa Spika, Mahabusu yaliyopo kwenye Vituo kwa wale wahalifu wanaokamatwa ni vifinyu mno. Ninashauri, kwa makusudi kabisa vyumba vya mahabusu viongezwe ukubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri ajipange upya kuhakikisha Askari wanapelekwa kozi za mara kwa mara kwani utendaji mzuri unatokana na elimu inayokwenda sambamba na wakati. Baada ya kusema hayo, ninaomba sasa kutamka kuwa naiunga mkono hotuba hii.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kupongeza Wizara hii kwa mikakati mizuri iliyoweka ili kuhakikisha kuwa amani, ulinzi na usalama unapatikana nchini.

Kwa hiyo, pongezi ziwafikie Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Mwapachu, Naibu Waziri, Ndugu Mohamed A. Mohamed, Katibu Mkuu Bakari Mahiza, *Inspector General*, Said Mwema, Makamanda wote wa Mikoa na Wilaya na Vikosi vyake.

Mheshimiwa Spika, watajwa hapo juu walifanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kuwa, raia wa Tanzania wanaishi katika hali ya ulinzi wao na mali zao. Ahsante sana.

Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Sasa nichangie hoja.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuanzishwa kwa Kitengo cha Tangazo la Serikali Na. 1 hapo mwezi Januari, 2006 ambalo lilitangazwa na Mheshimiwa Rais Kikwete kwa lengo la kusimamia usalama wa raia na mali zao, pia ushirikishwaji wa raia katika ulinzi. Suala hili ni ukombozi mkubwa sana nchini.

Kwa hiyo, ninashauri ushirikishwaji uendelezwe hadi katika nchi za jirani zetu wa mipakani, kwani inabainika wazi kuwa baadhi ya watu kutoka nchi za jirani wanachangia uhalifu kiasi fulani. Kwa hiyo, mchango wangu hapa ni kwamba, kuwepo na ushirikishwaji wa nchi jirani zilizopo mipakani kwa kukaa nao pamoja mipakani kwa kukaa nao pamoja katika Vikao maalum na kushirikisha vitengo vifuatavyo na nchi zifuatazo, kwani jirani mbaya usimwonee haya. Nchi hizo ni Rwanda Urundi, Kenya, Uganda, Comoro, Mozambique, Zambia, Malawi na Demokrasia ya Congo.

Nchi hizo za jirani zikae na vikao vyetu kwa makusudi kabisa kwa kuandaliwa na kuwajumuisha viongozi wetu hawa: Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu *Inspector General*, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa na Wilaya, Viongozi wa *Council* na Wakuu wa Mikoa na Wilaya .

Viongozi hao hapo juu wote wakutane na Viongozi wenye vyeo kama hao wa nchi za jirani nilizozitaja wakutane pamoja katika Kikao cha pamoja hata ikibidi kila nchi kwa wakati wake ili kuzungumzia ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Vile vile, tumeshaona kuwa ujambazi mwangi unaotokea katika nchi za jirani. Kwa hiyo, ni muhimu pia kutumia vyombo vya *Interpol*, *SARPCCO*, *EAPCCO*, *EAC* katika kuwashirikisha katika suala la ulinzi wa Tanzania kama mlivyoamua kuwashirikisha ili kuimarisha ulinzi nchini. Lazima vyombo hivyo vya Kimataifa vishirikishwe ili kuimarisha ulinzi.

La pili, nzungumzie suala la matukio ya uhalifu. Sasa hivi matukio ya uhalifu huja hadi Vijijini na sio Mjini tu. Kwa hiyo, kuna haja sasa Wilaya zote ziwe na Mkuu wa Kituo cha Polisi, Ofisi za Wilaya na viongozi wote wanaohusika Wilayani, kwani mpaka leo hii, kuna Wilaya ambazo hazina Kamanda Upelelezi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano mmoja tu. Mkoani Lindi katika Wilaya Ruangwa, hakuna Ofisi, nyumba za Polisi na hakuna Mkuu wa Polisi wa Wilaya. Polisi kutoka Wilaya ya Lindi kuja kuhudumia Wilaya ya Ruangwa. Matokeo yake hapo tarehe

24 Desemba, 2005 walikuja majambazi kumi kuteka silaha zote zilizopo katika Wilaya hiyo, lakini katika purukushani za kurushiana risasi, majambazi hayo kumi yalikamatwa yote na majambazi sita wakiwa wamekufa na manne yakiwa hai. Masuala yao yapo Polisi.

Kwa hiyo, tafadhali sana kuwepo na ujenzi wa majengo ya Polisi yote yakiwemo Kituo cha Polisi, nyumba za Polisi nyumba ya kuweka silaha na vile vile kuwe na Maafisa Polisi wote wanaohitajika kwa mfano Kamanda wa Wilaya ili kudhibiti uhalifu Ruangwa Mkoani Lindi. Tusaidiane, tafadhali sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na uvuvi haramu na wahalifu kuitia majini, aidha, katika maziwa au bahari, kwa mfano Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, ulinzi katika maeneo haya ni muhimu sana. Kwa hiyo, kunahitajika boti maalum ziongezwe katika ulinzi. Katika Maziwa yaliyotajwa hapo juu, angalau yana boti, lakini katika Bahari ya Hindi Mikoa ya Lindi na Mtwara hakuna boti hata moja. Serikali iliahidi kuwa italeta boti, lakini hadi leo bado.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ilete angalau boti moja kwa Mikoa hiyo kwani, uhalifu wa uvuvi haramu na uhamiaji haramu umezidi katika Mikoa hiyo. Upo mfano mmoja, tarehe 3 Aprili, 1998 kulifanyika Operesheni Uvuvi Haramu na Jeshi la Pono. Wavuvi 300 walikamatwa na bomu Tani 151 zilikamatwa. Hii inaonyesha wazi kuwa, uhalifu wa aina hiyo upo. Sasa kuna hatari ya wavuvi hao kurudia tena, kwani tangu operesheni hiyo ifanyike mwaka huu hadi sasa bado kufanyika tena. Wala hakuna boti iliyobaki. Tunaomba tupewe boti ya ulinzi Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha Bungeni, hotuba ambayo imeonyesha mwelekeo wa kukabiliana na majambazi na kuhakikisha wananchi wanaishi katika hali ya usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba nimpongeze Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma kwa juhudhi anazofanya kuweka Mkoa wa Dodoma, tunaishi kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete na Mkuu wa Majeshi yote ya Ulinzi, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kushirikisha majeshi yote na kusimamia na kuhakikisha mizizi ya ujambazi imeng'olewa na kuwezesha wananchi kuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze machache juu ya Wizara hii. Kwanza naomba Seriakali ianzishe ujenzi wa nyumba za watumishi zilizo bora kwa kutumia wafungwa ambao ni mafundi na itasaidia kupunguza gharama za ujenzi. Vile vile wafungwa hawa wanaweza kuchoma matofali ya kusaidia kujengea nyumba.

Mheshimiwa Spika, kutohana na kazi ngumu na ni ya ku-*risk* maisha yao, kwani wao wakati mwangi hupambana na majambazi na baadhi ya Askari wamepoteza maisha yao. Naomba Serikali ieleze kwa nini Askari wasikatiwe Bima?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Askari wa vyeo vya chini mara nyingi haki zao haziwafikii wote, ni vizuri utaratibu ufanyike wa kuwawekea posho zao hizo kwenye mishahara yao. Vile vile, ningeomba Serikali ipandishe mishahara kuliko ilivyopandisha hata sasa.

Mheshimiwa Spika, kuwaendeleza Askari kielimu, tunaomba Jeshi la Polisi liwe na utaratibu wa kuwaendeleza Askari wao kielimu bila kikwazo na Jeshi liwe tayari kuwalipia maana wanapolipia wenyewe hawawezi kutohana na mshahara wanaopata Askari wa vyeo vya chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa za kulevya, dawa za kulevya ni kitu ambacho inaonekana kudhibiti imekuwa ni kikwazo pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali. Mimi ninaomba Serikali ifuatilie zaidi wanaoingiza dawa za kulevya nchini badala ya kushughulika na wauzaji wadogo wadogo ambapo wakipatikana hawa waagizaji, hawa wauzaji wadogo hawatapata hizo dawa.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba wale vijana wanaokamatwa wamemeza dawa za kulevya na hatujasikia waliowawezesha kusafiri na kwenda kuzimeza wakamatwe ni nani? Tunaomba Serikali itueleze, maana vijana hawa hawana uwezo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na uongozi wa sasa wa Jeshi kwa hotuba inayoonyesha azma na taswira (*vision*) inayoleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, Polisi ni Jeshi muhimu sana kwa kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zao na sisi wote tunawajibika kuhakikisha Jeshi hili linaimarishwa. Njia moja ya kuimarisha Jeshi hili ni kutoa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Spika, nafanya wajibu wangu wa kutoa ushauri na maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Uhusiano wa Polisi na Chama cha *UDP* Wilaya ya Bariadi ni mfano mbaya wa Polisi kutumikia siasa badala ya kutumikia raia bila upendeleo. Mifano hii inaeleza: Wakati wa Uchaguzi Mkuu 2005, kwa amri ya Kamanda wa Upelelezi, wakati huo nyumba yangu ilipigwa mabomu ya machozi na risasi zilirindima kwangu na mke wangu karibu afe kwa risasi na mabomu ya machozi bila sababu yoyote ya kutosha. Wakati huo huo Vijiji vya Ikindilo na Njwamumpenda vilipigwa mabomu bila sababu yoyote ya msingi. Mambo yote haya nilieleza Ofisi ya *Inspector General*.

Mheshimiwa Spika, Kamanda huyu wa Mkoa alikamata vijana wa *UDP* na kuhamisha mashitaka Shinyanga ili kutupa hasara ya kupeleka watuhumiwa kwa gharama kubwa. Mpaka leo vijana hawa wanakwenda Shinyanga kwa gharama kubwa na kupewa tarehe tu.

Jambo hili nimeliandikia barua na kuzungumza na Kamanda huyu ambaye sasa ni Kaimu *RPC* – Shinyanga. Naomba kesi hizi zirudishwe Bariadi na kama kuna ushahidi, basi upelekwe Bariadi.

Mheshimiwa Spika, kama kuna kitendo chochote cha uhalifu wa kukamatwa, ni uongozi wa *UDP*. Mfano wa Sapiwi, Kijiji cha Nyawikoma, mahindi ya njaa yameliwa na leo anakamatwa Mwenyekiti wa Kijiji – *UDP*.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya halaiki kule Kasori Mtendaji Kata, anayekamatwa ni Diwani na Mwenyekiti wa *UDP*.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano mingi kama kupigwa kwa Diwani wetu, Viti Maalum, Christina Salum John wa Nkoma mpaka katoa mimba kwa shinikizo la *DC* Rugarabamu, lakini hakuna uwajibishwaji wa wale wote waliohusika.

Mheshimiwa Spika, Bariadi hatutaki Wilaya hii iwe uwanja wa mapambano na Serikali unaoletwa na Viongozi wa Polisi kupendelea Chama kimoja cha Siasa.

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha haya, naomba Waziri aunde Tume huru kwenda Bariadi kuchunguza uhusiano wa Polisi na Chama cha *UDP*.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa dhamira ya Wizara pg.30, paragraph 16, basi Tume itaimarisha azma hii.

Mheshimiwa Spika, Sungusungu inaweza kuwa mwanzo mzuri wa Polisi Jamii (*Community Policing*) kama wakipata elimu ya Kipolisi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga tuna tatizo la watu kuuawa na halaiki (*Nywano*) kwa makosa madogo kama kuiba baiskeli au kopo moja la dawa ya Pamba. Sungusungu chimbuko lake ni kwa jamii kukosana imani na Polisi na Mahakama. Lakini sasa ni wakati muafaka kuliangalia upya Jeshi hili la jadi ili lisaidie Polisi katika ulinzi wa raia na mali zao katika misingi ya kufuata sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, niko tayari kushirikiana na Wizara katika kutoa elimu kwa Jeshi hili la jadi kwa misingi ya Polisi Jamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Wizara na Polisi kwa mtizamo mpya wa sasa na mafanikio yao usoni ambapo Jeshi la Polisi litakuwa kimbilio la wananchi.

Nawatachia kila la kheri na ninatoa mkono wa ushirikiano.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake baada ya kuindaa kwa umakini mkubwa yeche na Watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana, hivyo Serikali inapaswa kuwaangalia kwa makini sana Watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Askari ndiye mlinzi wa raia na mali zao, lakini Askari wetu wanafanya kazi zaio katika mazingira magumu mno.

Mheshimiwa Spika, hatari au majanga karibu yote yanayotokea nchini, Askari ndiye mtu wa mwanzo anayekabiliana nayo. Viongozi na raia, penye sherehe ama matatizo, tunahitaji Askari ili kufanikisha shughuli zetu. Ni jambo la ajabu na aibu kwa nchi yetu kwamba Askari huyu hajui anapolala wala anachokula, kwani nyumba wanazoishi ni chakavu sana na mishahara yao ni hafifu mno na hasa ukizingatia ugumu wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Askari wetu tunawafanya wawe ama ombaomba ama wala rushwa ili waweze kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara na Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma. Nyumba za Askari Wete ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, Askari yeote ni lazima aipende kazi yake ili aweze kuifanya kwa uadilifu na kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi hilo. Kwa hiyo, tumwezeshe ili asikiuke sheria na maadili ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Usalama Barabarani wana jukumu kubwa la kuhakikisha usalama wa abiria na mali zao pia (Mizigo), lakini inasikitisha kuona kwamba Askari hao mionganoni mwao hawajui hata hizo sheria wanazozitumikia.

Nasema hivi kwa sababu Askari anaweza kusimamisha gari mahali ambapo hapastahiki na mara nyingine kusababisha ajali na wengine hawawezi ama hawafahamu hata kusoma zile *stickers* zilizomo kwenye gari na kumsababishia usumbufu dereva.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nashauri kwamba vijana wanaoajiriwa waangaliwe kwamba wamefaulu ama la, na waliokwishaajiriwa, basi wapewe mafunzo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, tujiepusha na Jeshi hili kuujiingiza katika siasa. Askari wetu unapofika wakati wa kampeni za Uchaguzi hucaa sare za Chama Tawala na kushiriki kwenye Mikutano na kukaa katika maskani na kujisahau kwamba wao hawapaswi kufanya hivyo. Elimu itolewe ili kuwakumbusha.

Mheshimiwa Spika, suala la kupandishwa vyeo kwa Askari sijui ni kwa kigezo gani! Lakini kuna Askari hukaa kazini mpaka kustaafu hawajapandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuthamini elimu, lakini pia uzoefu nao unasaadid sana. Hivyo, Serikali iwaangalie wale ambaa wanastahiki tuzo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uteuzi wa Makamanda wa Mikoa na Wilaya, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri: Je, kuna kigezo gani cha uteuzi huu? Kwa sababu sina kumbukumbu nzuri, lakini sijawahi kumwona Kamanda wa Mkoa kutoka Kisiwa cha Pemba ama kufanya kazi kule au sehemu nyingine ya Tanzania. Je, ni kutokana na kwamba hawana hiyo elimu ama vipi?

Mheshimiwa Spika, ninaomba ufanuzi. Ahsante, ninashukuru.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikiwa mzima na salama.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kazi ngumu wanazozifanya hasa zile za kupambana na majambazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jukumu la ulinzi na usalama ni la Jamhuri ya Muungano na kwa kuwa vikosi vya SMZ vimeundwa kwa kazi maalum ambazo kila Kikosi kinajulikana kazi yake na sina haja ya kutaja kazi zake. Hivi inakuwaje Askari hawa wa SMZ wanaingilia kazi za Jeshi la Polisi nao wapo na ikawa hawana kazi wakafanya kazi hizo Vikosi vya SMZ. Mifano ipo minge na nitaitoa.

Moja, Bandarini Unguja na Pemba Askari Polisi wapo, lakini Askari wa Vikosi vya SMZ ndio wanaopekua mizigo na watu.

Pili, wakati wa uchaguzi kwenye *Road Block* Askari Polisi wapo wa kutosha, lakini kwa nini na Askari wa KMKM, Mafunzo na JKU wanakuwepo barabarani na wao ndio wanaoongoza kwa kupekuwa magari na watu wakati wao sio kazi yao?

Tatu, ambalo ndio kubwa zaidi, kwa nini Askari hawa wa Vikosi vya SMZ wanashirikishwa kikamilifu kwenye shughuli za Uchaguzi na wao hawahusiki na kazi hio au tuseme Askari Polisi Visiwani wameshindwa kazi zao ndio wakafanya wao? Au tuseme ni katika kukipatia Chama Tawala ushindi wa kishindo! Naomba majibu kwenye majumuisho.

Mheshimiwa Spika, au tuseme sasa sheria zimebadilika kuwa Askari wa KMKM na JKT au kazi yao kukaa barabarani na kukaa katika vyumba vya Uchaguzi, jawabu ya kuwa Askari Polisi au kidogo sio kweli, kwani nao huwa wapo, lakini hawana nguvu za kusema kwa nguvu zote, wanazo Askari wa Vikosi vya SMZ. Serikali ya Muungano ishughulikie suala hili sisi tunasema kuwa linakera sana. JKU afanye kazi zake, KMKM hivyo hivyo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Micheweni, lakini ninakaa katika Mji wa Wete. Siku ya tarehe 31 Oktoba, 2005, baada ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar, kabla ya kutolewa matokeo ya Urais wa Zanzibar Askari Polisi walikuwa wakitembea tembea katika Mji huo na baadaye Askari hao wakarejeshwa Kituoni na wakaletwa Askari wa Mafunzo, KMKM na JKU wakaanza kutesa raia bila ya sababu

yoyote wakavunja maduka wakaiba pesa, kadi za simu na vitu vya thamani na kutesa watu na baadaye kumpiga risasi na kumwua kijana mmoja Haji Seif Haji mkazi wa Bopwe Wete.

Baadaye, watu wakaenda Polisi kulalamika na Serikali wakasema hatua zitachukuliwa, lakini hakuna chochote. Walioiba waliuza vitu vya thamani hapo hapo Wete na wanajulikana waliouwa hakuna hatua ye yoyote ambayo imechukuliwa hadi hivi sasa.

Ninaiomba Serikali iseme lolote kuhusu hili ili watu wa Wete waelewe. Mheshimiwa Waziri asiache kunijibu kwa sababu ya kuchangia kwa maandishi. Naomba lielezwe kwa kina ili wananchi wasikie.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Askari hulipwa viinua mgongo baadala ya pensheni, Askari wengi wanakuwa wakilalamikia hili hebu Serikali na iwafanyie mabadiliko japo waliomba wenyewe lakini walikuwa hawajui. Ahsante.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Bakari Mwapachu, kwa hotuba yake nzuri.

Katika kuchangia hoja hii napenda kumpongeza Mkuu wa Polisi nchini, *Inspector General* Saidi Mwema kwa kuteuliwa kwake, lakini zaidi kwa kazi nzuri sana anayofanya.

Nampongeza Inspeksa Jenerali kwa kupiga marufuku mchezo wa *Pool Table* unaocchezwa na vijana wetu wakati wa kazi. Kuna baadhi yetu wanapinga agizo hili au kuihoji. Mimi naomba sana Inspeksa Jenerali aendelee kukaza kamba katika hili kwa sababu nguvu kubwa ya wananchi wetu, vijana na wengineo wameacha kabisa kazi za uzalishaji mali Vijijini, ukiacha masuala ya ujambazi na uhalifu mwingine.

*Pool table* kule Ulaya inachezwa na watu wenye fedha na ni baada ya kazi, wakati wa mapumziko, sio kama sisi kwetu, vijana maskini wanapotezea muda wa kazi. Ikitibidi Serikali itoze kodi mchezo huu hata kwa saa zilizoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, napingana na mawazo kwamba sababu ya kuongezeka kwa uhalifu kuwa ni kuongezeka idadi ya watu; kupanda kwa ghamama za maisha, au ukosefu wa ajira. Kama hizi sababu zingekuwa kweli, basi asingepatikana tajiri au watu wenye biashara zao, ajira au kazi zao kupatikana na ujambazi. Tatizo kubwa ni ukosefu wa nidhamu na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, nazidi kumpongeza *IGP* kwa kuhanikisha abiria kwenye vyombo vya usafiri. Zoezi hili tafadhali sana liendelee kwa nguvu zote. Lakini pia udhibiti wa mwendo wa kasi wa vyombo vyetu vya usafiri. na raia wanaporipoti habari ya *over speeding* Serikali (Polisi) isikilize.

Mheshimiwa Spika, naomba Kituo cha Polisi kilichojengwa na wananchi wa Galapo Jimboni kwangu kipate Polisi. Wananchi wamekwishaandaa miundombinu yote pale Galapo kwa ajili ya Kituo hicho cha Polisi. Ni Mji unaokua na biashara kubwa. Tunaomba Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti ya Usalama wa Raia imeongezeka, naomba Serikali isaidie ujenzi wa Vituo vya Bashanet, Dareda, na Gidas. Ahsante. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri na Mheshimiwa Mohamed Abud, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanya katika kutimiza majukumu mazito ya Wizara hii. Napenda kusema wazi kwamba, ninaunga mkono Wizara hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ninapenda kuuelekeza katika mambo muhimu yafuatayo ambayo ni kero sugu katika Jimbo langu na Wilaya ya Korogwe kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninashauri sana Askari wa Upelelezi katika Wilaya ya Korogwe na pengine nchi nzima, wafanye kazi yao kwa ari, nguvu na kasi mpya. Staili yao ya kufanya kazi inahitaji mabadiliko makubwa. Hivi ni kwa nini upelelezi unachukua muda mrefu sana hadi kumalizika? Korogwe kuna zaidi ya kesi 30 ambazo ninazifahamu mimi hadi leo ni zaidi ya miaka mitano, mitatu, miwili, upelelezi haujakwisha kwa sababu ambazo hazieleweki. Matokeo yake ni Mahabusu wa kesi hizo kuteseka rumande.

Zipo kesi za wizi wa ng'ombe nyingi tu ambazo wahusika wanajulikana, lakini Askari wa Upelelezi wameshindwa hadi leo hii kuamua na kupata ufumbuzi wa kudumu. Mitindo kama hiyo ndiyo vinavyofanya wananchi kuchukia Polisi au kusema Polisi wanakula rushwa. Ninashauri sana suala la Askari wa Upelelezi lipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Korogwe sasa umepata Halmashauri ya Mji (*Town Council*), lakini hali ya ulinzi na usalama ni duni. Kituo cha Polisi Kilole, Ngombezi *Old Korogwe* havina usafiri na Askari wa kutosha. Ninashauri sana Vituo hivyo vikapatiwa vitendea kazi hasa usafiri, silaha na kuboreshewa majengo yao. Nyumba za Askari wa Vituo hivyo ni mbaya sana na hata mazingira ya Ofisi zao ni mbaya. Ninaomba ziboreshwe sana. Ikumbukwe kwamba Korogwe Mjini ni *Centre* ya matukio.

Ninashauri *OCD, CO* wapelekewe Askari wenye uwezo. Ni mahali pagumu sana. Historia ya Korogwe hakuna asiyejua kwamba makabila yote 120 ya Tanzania yanaishi katika Wilaya hiyo. Hiyo ni kwa sababu ya historia ya mkonge (manamba). Kwa hiyo, wanaishi watu mchanganyiko wenye tabia tofauti. Ninaomba sana na kushauri Korogwe wawekwe Askari wenye uwezo wa juu. Huko nyuma ilikuwa hivyo kiasi cha kuonekana kwamba kila aliyepitia Korogwe hatimaye amepata cheo kikubwa, mfano, Afande

Selemani *RPC* Pwani, Afande Kova, *RPC* Mbeya, Afande Mbutu na kadhalika. Korogwe ni mahali pagumu, panahitaji kupatiwa vifaa vya kutosha na vya kisasa.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Aman Abeid Karume, kwa ushindi mkubwa walioupata kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita.

Pia natoa pongezi zangu kwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Chama Tawala, Chama Cha Mapinduzi.

Pia, nampongeza Katibu Mkoo wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Yusufu Makamba. Viongozi wote walioteuliwa/kuchaguliwa katika Awamu hii ya Nne, Mwenyezi Mungu awape afya njema.

Pia, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunateuwa mimi kuwa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Narudia kumshukuru na kusema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba mchango wangu ujielekeze kwenye suala la ujambazi. Suala la ujambazi sio geni na wala hakuna hata ya kulaumiana kwa sababu majambazi tunaishi nao, tunakula nao na kama sio mtoto wako, ni mtoto wa shangazi, mjomba baba mkubwa na na kadhalika. Hivyo sio vyema kulaumiana, kwa sababu majambazi hao hawatoki Mbinguni. La msingi, tuwape vijana wetu wa Polisi ushirikiano mwema ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi kama ilivyo hivi sasa chini ya Serikali yao inayoongozwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete yenye ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, naunga mono asilimia mia.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa, mchango wangu umo katika Taarifa ya Bunge ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo, ninachochangia ni kukumbushia mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa kwa lengo la kuimarisha maadili na misingi ya Jeshi la Polisi. Nashauri mambo yafuatayo yaboreshwe:-

1. Ajira izingatie utaratibu ufuatao:-

- (a) Waajiriwa wafanyiwe *vetting* kabla na mara baada ya kuajiriwa. Hatua hiyo itapunguza kuajiri Askari wasiokuwa na sifa sahihi.
- (b) Askari mara baada ya kuajiriwa, wawekwe Makambini.

2. Ukaguzi wa usafi wa Kambi pamoja na *kit – inspection*, hatua hiyo itaendeleza utimamu na utayari wa Askari.
3. Paredi za kila wiki zizingatiwe na kufanyika kama ilivyokuwa ikifanyika miaka ya nyuma.
4. Suala la *MESS* ya Maofisa *NGOs* na makapera zitengwe kwa ajili ya kudumisha nidhamu kati yao.
5. Zoezi la upigaji wa shabaha uendelezwe kwa Askari wa ngazi zote.
6. Kwenye jimbo la Songwe, kuna Vituo viwili vyta Polisi, kwenye Mji mdogo wa Mkwajuni na Galula ambako ni Makao Makuu ya Kata. Vituo hivyo vyote havina usafiri wa gari wala pikipiki wala baiskeli. Usafiri huo utasaidia sana kuwawezesha Askari kufanya kazi hadi kwenye Vijiji vya Ngwala, Gua, Namkukwe na Isanzu na Manda. Pili, Kituo cha Mkwajuni kina hadhi ya *Class “C”* ambapo Mkuu wa Kituo anatakiwa awe na cheo cha *Senior Inspector* nyota tatu. Aliyeko hivi sasa apandishwe cheo kutoka nyota moja awe na Cheo cha nyota tatu.
7. Kozi zifuatazo ziimarishe:-

- (a) *Charge Room Officers Course*; na
- (b) *Proficiency examinations* zirejeshwe elimu hizo hii itaimarisha uwezo na uelewa wa hali ya juu kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, asilimia mia kwa mia.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri. Aidha, nawapongeza Watendaji wote kwa uwajibikaji wao. Mchango na ushauri wangu kwa Wizara ya Usalama wa Raia ni kama ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri vijana walioajiriwa Polisi na wenye Elimu ya Juu wawe wanapandishwa vyeo na wapewe madaraka kwani watakuwa na uwezo wa kufanya kazi kitaalamu, kisasa na kwa ari mpya.

Askari wanawake warudishiwe posho ya (hifadhi ya kike) kwa maana ya (*black hand and pads*) taulo za kike. Kurudishwa kwa huduma hii kutawawezesha wanawake Mapolisi kujiona huru na sawasawa wakati wote. Naamini sio wengi na kwamba zoezi hili linawezekana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iandae *training roster* ambayo itatumika kuwaendeleza vijana/watumishi wake wakiwa kazini na hivyo kuwapandisha vyeo kwa elimu, taaluma na ujasiri au uaminifu katika utendaji wao. Suala hili litapunguza

malalamiko yaliyopo kuwa upo upendeleo katika kufadhili masomo hasa kwa wale waliopo Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, naomba *Traffic* wetu wawe makini katika kazi zao. Malalamiko ni mengi kwa wao kutokuwa wakali kwa madereva wa daladala hasa Dar es Salaam. Huwaachia madereva kupita kandokando ya barabara hasa nyakati za asubuhi na jioni kwa kuwaruhusu, madhara yake ni mengi, lakini machache ni kuharibu barabara na Kujeruhi/kugonga wenda kwa miguu kwani kule ndiko kwenye haki yao kisheria ya kupita.

Mheshimiwa Spika, naamini kero nyingine zinaweza kurekebishika. Naunga mkono hoja. Nawatakia Bajeti njema.

**MHE. JUMA H. KI LLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Usalama wa Raia kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya mwaka 2006/2007. Kadhalika, pongezi pekee kwa *Inspector General of Police (IGP)*, Saidi Mwema, kwani ameonyesha umahiri mkubwa kwa muda mfupi tangu ashike nafasi kama *IGP*.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika Wizara hii ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wanachi katika kuweka mikakati ya kuzuia uhalifu bado ni hafifu au ile ambayo inaambatana na mashaka haya yanayotolewa na ubovu wa utendaji wa Polisi wenye kwa raia. Polisi wengi wanapokuwa kazini utendaji wao sio wa kuzingatia maadili, bali unaambatana na vitisho, unyanyasaji na kadhalika. Hawa, hali hiyo basi, kumekuwepo na wigo kati ya raia na Polisi, hatua ambayo naamini imesababishwa sana na Polisi hasa kwa namna wanavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri Polisi iwe na urafiki wa karibu na wananchi kwa dhati kabisa na iwe tayari kutoa msaada unaostahili kwa raia ili raia wajenge imani na Jeshi lao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushughulikiaji wa makosa ya jinai, bado utaratibu ni mbovu, hasa kwa Idara ya Upelelezi, kwani kesi nyingi ni za kubambikiza na mara nyingi Polisi wanapokamata na kupeleka kesi Mahakamani, basi hushindwa kwa kuwa kesi hukosa ushahidi, hivyo kufutwa.

Mheshimiwa Spika, watuhumiwa wanawekwa Vituoni zaidi ya saa 48, hivyo kuvunja *Police Ordinance* ambayo inawataka Polisi kupeleka Mahakamani kesi kwa muda wa saa 48.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa rushwa, udhibiti uanzie kwa utendaji wa Askari kwa ngazi zote. Polisi wasikae Kituo kimoja kwa kipindi kirefu. Ziwepo taratibu za kuchunguza nyendo zao kwa muda wote.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu usalama barabarani. Magari ya abiria yaangaliwe tena kuhusu vidhibiti mwendo na magari yote ya abiria yasafiri kwa nyakati zilizowekwa kisheria mwisho saa 4.00 usiku. Vile vile, Idara ya *Traffic* iangaliwe kwani inanuka rushwa na imekuwa kama genge la wahuni fulani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA ABDALLA TAMIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa katika hali ya uzima.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa utendaji wao wa kazi pamoja na Watendaji wao wote.

Mheshimiwa Spika, nikianza mchango wangu, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia kwa uwasilishaji mzuri na kutoa taarifa kwa kila jambo lililotendeka.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutoa ufanuzi mzuri wa tukio lililotokea Zanzibar na pia kutoa pole kwa ndugu wa raia aliyepoteza roho yake kwa hawa majambazi. Kwa kweli kitendo hiki ni cha kuigwa, kwani Waziri hana ubaguzi, anawatendea haki wananchi wake wote. Mungu amzidishie imani.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa tukio lililotokea Zanzibar kwamba majambazi walikamatwa na pia tumeelezwa kuwa wametoa siri na maficho wanayojificha majambazi. Hii sio mara ya kwanza kukamatwa majambazi wanaotumia silaha.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri basi atutajie au atupe tathmini ya majambazi waliokamatwa wa kutumia silaha na wangapi kesi zao zimeishatolewa maamuzi na wangapi kesi zao hazijatafutiwa ufumbuzi bado na hao waliotolewa uamuzi, wamefungwa miaka mingapi kila mmoja?

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia Mheshimiwa Waziri alipitie hili Jeshi la Polisi wana tabia ya kuwapa kesi za uongo raia. Pengine wamekosana wenyewe huko Mitaani, badala yake anamngojea apatwe na tatizo dogo kisha ambadilishie kesi na kumpa kesi asiyostahili.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri atoe adhabu kali inayostahili kwa wale watakaobainika na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Usalama wa Raia - Mheshimiwa Bakari Mwapachu, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mohamed Aboud Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaaj Bajeti hii yenye mwelekeo wa kuleta ufanisi katika utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, vile vile niwapongeze sana Mheshimiwa Mwapachu na Naibu wake, Mheshimiwa Aboud kwa jinsi wanavyojitahidi kupambana na matukio mbalimbali ya ujambazi na hatimaye hali sasa inatia moyo sana ikiwa ni pamoja na adha mbalimbali, Mungu awatangulie pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuleta ufanisi wa kazi kwa Jeshi letu la Polisi, ni bora Askari wetu wasikae Kituo kimoja muda mrefu, kwani huolewa na mazingira kwa kuwa wenyeji sana na kuwa na ndugu wengi mfano baba, mjomba, baba mkwe, shangazi na kadhalika na kushindwa kuwajibisha hata kama wanayo hatia.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiojificha kuwa Askari wetu wa Usalama Barabaran bado wanapokea rushwa. Hivyo basi, naiomba Serikali itafute mbinu za kukomesha tabia hii, kwani inawasumbua sana madereva wengi na huwafanya safari zao kuwa ngumu na kukwama njiani kwa kukosa fedha. Kwa kuwa, Askari wamekuwa na Vituo vingi barabarani, naiomba Serikali iteue Vituo maalum kwa kila Mkoa na kuwapa maelekezo ya mambo muhimu ya kukagua magari kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kufanya kazi yao, barabara ya kukamata wahalifu, bali kuna dosari katika kutunza mali za mahabusu, kwani wengi wao mali zao hupotelea kwenye Vituo vya Polisi. Vile vile, naiomba Serikali kuhakikisha kuna vyumba maalum kwa ajili ya mahabusu wa kike, kwani Vituo vingi vya Polisi havina sehemu maalum kwa ajili ya mahabusu wanawake, naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, uuzaaji wa madawa ya kulevyaa umezidi sana hapa nchini. Hivyo basi, Serikali itumie nguvu nyingi kukomesha biashara hii haramu, kwani waingizaji, wauzaji na watumiaji, wanajulikana, hawajifichi tena. Hawa wenzetu wanatafuta utajiri wa haraka haraka, sasa basi, inatosha. Tukinusuru kizazi cha leo na kesho.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kufanya kazi kubwa ya kutoa vifaa vya kufanya kazi katika Jeshi hili la Polisi mfano magari, pikipiki, *radio calls* na kadhalika.

Naiomba Serikali, kwa kuwa imekwishatoa vifaa vingi kwenye Miji, Manispaa, Majaji ambayo yalikuwa yanaongoza kwa ujambazi, sasa tuelekeze pia hivi vifaa Mikoani pamoja na Singida. Vile vile, kila Kituo kiwe na Amari ya kutunza vifaa, ni muhimu sana naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wizi wa mifugo, bado lipo. Naiomba Serikali iwapeleke Askari wa kutosha wa kupambana na wizi huu wa mifugo huko huko Vijijini ikiwezekana na kila Kituo cha Polisi wawe wawili, naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, suala la ujambazi, ni kweli Serikali imejitahidi sana, bali naiomba Serikali iendelee kubuni mbinu mpya. Pia, mbinu hizi sasa ziwe siri, majambazi yasijue hapo tutajitahidi kukabiliana nayo. Vile vile, naishauri iwatumie sana Askari wadogo, kwani wana taarifa nyingi sana muhimu kuwataja wanapotoa taarifa vile vile wapewe tuzo za aina mbili zawadi, kupelekwa kozi ama kupewa cheo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ipunguze masharti ya waombaji wa kujiunga na Jeshi la Polisi mfano *Division III* iwe hadi *Division IV*, kimo sio lazima kiwe wale warefu tu, hata wafupi wapewe nafasi.

Kuhusu kustaaifu, naiomba Serikali ijitahidi kuwapeleka Askari wengi kusoma ili waweze kupanda vyeo na waweze kufikia cheo kitakachowafanya wastaaifu miaka 60. Hali hii itawasaidia Askari wengi wenye uwezo kuwepo kazini muda mrefu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nyumba za Askari, naiomba Serikali kuongeza kasi ya kujenga nyumba nyingine zenyе hadhi na maadili ya familia za Askari wetu. Hii ni kwa sababu nyingi. Ni chumba kimoja na chumba na sebule wakati Askari ana mke na watoto wa jinsia mbili. Hii itasaidia watoto wao kuwa na maadili mema wanapolala watoto wa kike kipekee na wa kiume hivyo hivyo na wazazi peke yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie upya mishahara ya Askari pamoja na posho zao, hazitosh! Kazi zao nzito sana! Huenda ndiyo sababu wanajiunga na rushwa kwa ajili ya ukata.

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. AME P. AME:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, kwa hotuba yao nzuri. Pia, nikupongeze wewe binafsi pia na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge hili kwa makini kabisa. Nami napenda kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Usalama wa Raia.

Mheshimiwa Spika, usalama wa raia na mali zao, Tanzania mashakani kutokana na ujambazi unaokithiri hapa nchini. Wizara ya Usalama wa Raia, inapopanga mipango yake ya kupambana na majambazi isitangaze kuwa itafanya hivi au vile, kwani majambazi ni watu, wana akili, wanaitumia, wana mbinu wanazitumia, wana silaha wanazitumia na pia hufanya Vikao vya kupanga mikakati ya kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, majambazi hutumia Bandari ndogo ya vichochoroni kwa kupidisha silaha za kufanya ujambazi. Mfano, Mkokoni Kaskazini Zanzibar, Matemwe, Nungwi na kadhalika, usalama wa raia, paangaliwe kwenye vipando, kama vile magari. Madereva wa magari ya abiria hupakia watu kupita kiasi na kuendesha kwa mwendo wa kasi sana na hata akikamatwa hutozwa faini ndogo tu na siku nyingine huendesha kuliko vile.

Mheshimiwa Spika, bila shaka, madereva hufanya hivyo kwa sababu ya adhabu ndogo na kwa kuwa Serikali suala hili la usalama wa raia na mali zao, hajatilia maanani hasa. Madereva wanapoua kwa uzembe, basi atahifadhiwa, watu wakishasahau, anapewa ruhusu ya kuendesha gari tena na ataendesha kuliko vile. Wizara (Serikali) ingeliweka sheria kuwa dereva atakayeua kwa uzembe, basi anyang'anywe leseni na afungwe jela miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, sio kweli kama usalama wa raia na mali zao utakuwepo nchini kama hakutakuwa na watu wenyewe nidhamu na heshima. Kuna raia ambao wanapofanya makosa na anapokamatwa na Askari wanakuwa wabishi sana na hufikia kupigana na Askari. Mtu kama huyo hashitakiwi kwa kuwa kapigana na chombo cha dola. Lakini Askari atashitakiwa hapa, sheria iangaliwe.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kuna raia wanateswa na wakimbizi na Serikali inafumbia macho wakimbizi hao kwa sababu tu ya kuheshimu sheria ya kimataifa. Kwani sheria ya kimataifa inawaruhusu hao wakimbizi kufanya hujuma huko wanakokimbilia?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Usalama wa Raia. Aidha, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Bakari Mwapachu na Naibu wake pamoja na watalaam wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye mchango wangu mdogo. Tatizo la kuwepo kwa ajali nyingi hapa nchini zinazosababisha watu kupoteza maisha kupata vilema vya kudumu kujeruhija na wengine kuadhirika kisaikolojia zimekuwa nyingi na za kutisha. Pamoja na Serikali kujitahidi sana kudhibiti vyombo vya usafiri, kufuata taratibu za usalama barabarani ili kunusuru roho za wasafiri, lakini bado tatizo hili linaendelea kutikisa Taifa hili, kwani kila leo ajali zinatokea tena za kutisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado haijapata suluhisho la kudumu kwa tatizo hili. Sasa baadhi ya malori yanatumika kubeba abiria maeneo mbalimbali, magari mengine ya wazi kama makenta, *pick up open* zinabeba abiria na pale ajali zinapotokea, basi wananchi wengi wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesema hakuna basi kupanda abiria zaidi ya *seat level*. Leo hii mabasi yanaingia kupita kawaida na wanapofika kwenye Mizani wanawashusha kabla, wanapopita kwenye *Police Post* wanawapa rushwa nao *Police* wanaruhusu basi linapita. Kwa mwendo huu hutaweza hata siku moja kuondoa tatizo hili sugu.

Sababu nyingine ni Serikali kutumia sheria za zamani kuadhibu madereva/madai yanaposababisha ajali. Hili linapelekea madereva hao kutokuumia na hivyo kuona ni kawaida tu. Dereva anasababisha ajali watu wanakufa wengi, gari inapelekwa *Police* linakuwa na makosa kibao. Siku mbili tu utamkuta dereva huyo yuko barabarani na gari hilo lipo barabarani hata waliofiwa hawajazika wahanga wa ajali hiyo. Faini inayotozwa kwa mabasi ni yanayokutwa na makosa ni ndogo sana na hivyo kuwapa rushwa wamiliki wa mabasi hayo kutoona shida yoyote kwa lile lililotokea.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majumuisho, naomba Waziri awaambie Watanzania ni hatua gani za kisheria zilizochukuliwa kwa gari lililosababisha ajali mbaya huko Arusha hivi karibuni ambalo libebe zaidi ya abiria mara tatu ya wale waliotekwa

na kuua karibu wote. Basi hilo lililokuwa bovu na pili lilikwepa *Police* na kupitia uchochoroni na hatimaye kutumbukia mtoni. Je, basi hilo bado linabeba abiria? Je, dereva wake yuko Mitaani? Je, mmiliki wa basi hilo kachukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, suala la misaada kutoka kwa wafanyabiashara kuboresha chombo cha *Police*, ni zuri ila Serikali iangalie kwa makini sana. Misaada hiyo isije kugeuka kwa wafanyabiashara hao kutumia chombo hicho kutekeleza matakwa yao binafsi kwa kisingizio cha misaada hiyo.

Nina wasiwasi sana na suala hili. Misaada hii ni vizuri ikaenda kwenye Sekta nyingine na siyo chombo hiki muhimili sana kwa Watanzania. Serikali iwe macho isije kufunikwa macho na wafanyabiashara wengi wenye uwezo wa kununua utu wa uhuru wa watu kwa pea zao.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja ya usalama wa raia kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa ushindi wa kishindo katika uchaguzi uliopita. Napenda pia nichukue fursa hii kumpongeza *IGP* Said Mwema katika shughuli zake za ufanisi wa hali ya juu tangu ateuliwe na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa huo. Hii siyo siri, kwani imani ya wananchi imerudi katika Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida, Mheshimiwa Rais alitembelea Magerezani kujiona hali halisi, baada ya hapo imejitokeza kwamba limbikizo la mahabusu lipo katika *graph* ya juu.

Hii inatokana na kumbukumbu zinazoonyesha upelelezi hafifu unaowafanya watu wasio na hatia kukaa muda mrefu bila hoja za msingi kuwepo huko.

Katika kipindi kifupi sana *IGP* amefanya mabadiliko makubwa sana na *impact* yake imeonekana kwamba ufanisi katika Jeshi hivi sasa ni mzuri sana. Hivyo, namwomba pia aiangalie Ofisi ya *DPP*, kwani zipo habari kwamba uwajibikaji katika Ofisi hiyo haviendani na kasi mpya ya uendeshaji wa shughuli nzima, hivyo hupelekea *speed* ya haki kwa watuhumiwa kukosa haki zao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Polisi hivi sasa limekua kwa kasi fulani. Haiwezekani kesi kupelekwa zaidi ya mwaka, huku mtuhumiwa akiwa mahabusu aidha bila kutoa dhamana, lakini zaidi mtuhumiwa aonekane hana hatia.

Naomba sana Jeshi la Polisi pia liekeze hivi sasa nguvu zake katika magereji bubu, kwani zipo tetesi kwamba baadhi ya magereji hutumika kuwa maficho ya magari ya wizi kwa kufuliwa na kuuzwa *spair*, hii hasa inasemekana Dar es Salaam, Arusha, Mwanza ndio Mikoa kiongozi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ndiyo kioo cha nchi yoyote. Bado naishauri Serikali kupitia Jeshi la Polisi kuongeza wapelelezi *CID* kwani ni bora kukinga kuliko kutibu. Naamini kwa taaluma aliyonayo *IGP* anaweza kulifanya zoezi kwa hili kwa ufanisi mkubwa. Naomba sana kupitia Jeshi hili kutoa mafunzo ya mara kwa mara ya ndani na nje. Hii itatoa hamasa, mwamko na uwajibikaji wa kiwango.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumesikitishwa sana na kitendo cha jambazi kuingia kituoni na kuchukua silaha. Hiki ni kitendo cha aibu, kwani Kituo ni sawa na Kambi, hivyo suala hili lichunguzwe kwa kina na hatua za kinidhamu zichukuliwe Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, bado nashauri *IGP* wetu aendelee kuwatumia Maafisa wastaifu waaminifu (wanaostahiki) awatumie kumsaidia katika shughuli zake kirahisi. Bado nashauri Jeshi lifuatilie katika kuchukua *recruit* toka uraiani wawe vijana safi. Hii itasaidia sana kupata Askari safi ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, nalishauri Jeshi sare za kikazi ziwe safi napongeza unadhifu wa *Traffic* na napongeza wapelelezi katika ngazi ya itifaki wamelijengea sifa Jeshi la Polisi. Mungu alipe uwezo Jeshi katika kulinda amani ya raia. Ahsante.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri sana na hotuba nzuri sana. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Jeshi la Polisi likamilishe ahadi yake ya kukisaidia Kituo cha Polisi PAWAGA Iringa Vijijini. Kituo kimejengwa miaka mitano iliyopita na nyumba za Askari zipo, ila tuliomba *IGP* atusaidie kuzikamilisha na ahakikishe Kituo kimeanza kazi. *IGP* aliyepita aliahidi na aliyejewa Mkuu wa Idara ya Jeshi na Utawala aliahidi na pikipiki na Waziri katika Bajeti ya 2005/2006 aliahidi.

Naomba sana sasa tufute ile historia. Wizara ipeleke watalaam wakafanye tathmini ya mahitaji na Wizara itusaidie ili mwaka huu wa fedha kianze kazi. Ni vifaa vichache sana vinahitajika. Tukumbuke Kituo kiliwekwa jiwe la msingi na Marehemu Dr. Omar A. Juma, Makamu wa Rais, miaka sita iliyopita na kilikuwa kimekamilika tayari wakati huo. Tafadhali naomba sana kero hii na ahadi hii itekelezwe kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama *RC* wa Dodoma, naomba gari la *FFU* na pikipiki za kuongozea misafara. Wakati misafara ya Viongozi hapa Dodoma ni mingi sana, inashangaza pikipiki hata moja hakuna. Mikoa ambayo hata wageni hawaendi, inazo hizo pikipiki. Gari la *FFU* huachwa nyuma wakati wa misafara, kwani haliendi kwa kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu yangu nipewe kwa maandishi. Naunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, Naibu Waziri, katibu Mkuu, Inspekte Jenerali wa Jeshi la Polisi, Makamanda, Askari na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao ambao umeongeza tija katika ulinzi wa raia na mali zao. Hali ya usalama inaridhisha na mikakati iliyowekwa inatia matumaini. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, amani katika nchi yoyote ile ina gharama kubwa. Ninaunga mkono hatua za Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu za kuliangalia Jeshi la Polisi kipekee. Ni vyema na Bunge letu Tukufu limuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa kuongeza Bajeti maalum kwa usalama wa raia, hasa baada ya mapato ya Serikali kuonyesha dalili za kuongezeka kufikia karibu Shilingi bilioni 226 mwezi uliopita.

Taratibu zinaweza kuandaliwa na Serikali, maombi yakaletwa Bungeni tukaidhinisha. Usalama wa Raia siyo jambo la kungoja mwaka mzima kama uwezo wa kifedha unaruhusu.

Mheshimiwa Spika, mifano michache ya udharura wa ulinzi wa raia ni matukio yanatokea Kanda za Ziwa. Shughuli zinazoendelea za kiuchumi katika Kanda ya Ziwa ni nyingi lakini pia takwimu zinazoonyeshwa na majedwali Na. 2 (a) hadi 2 (e) na 2 (g) katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni ushahidi wa mahitaji maalum katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga. Hata Mikoa ya Kigoma na Rukwa inaweza kuongezwa katika kundi hili.

Kwa hiyo, kunahitajika Askari wengi zaidi, vitendea kazi na mafunzo. Nashauri kianzishwe Kituo cha Askari Polisi wa anga watakaotumia helikopta kutokea Mwanza. Nchi yetu ni kubwa sana, hivyo doria ya boti na magari haitoshi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako, nawashukuru makamanda na Askari wa Kagera hususan Muleba kwa kazi nzuri sana katika mazingira magumu. Maombi maalum ya wananchi ni kupitia Askari wa nyongeza na kujengewa kituo cha Polisi Tarafa ya Nshamba yenye watu wanaokaribia 130,000. Kwa sasa kuna Askari watatu tu katika Kituo kidogo cha Nshamba. Nashukuru Jeshi la Polisi, kwani Viongozi wameahidi kuliangalia tatizo hili kulingana na uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. Aidha, ulinzi katika Ziwa Victoria unastahili kupewa uzito wa kipekee, kwani kuna watu wengi sana na matukio mengi ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA MOSES MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii kwa maoni kama ifuatavyo:-

Kwanza, vituo vingi vya Polisi vilivyopo nchini ambavyo vimejengwa na wananchi, havina silaha wala *radio call*. Askari anayekuwa zamu anakuwa hana nguvu za kuifanya kazi yake kwa umahiri kwa kukosa vitendea kazi. Nashauri kwamba, Wizara itenenge fungu la kununua vifaa hivyo kila Kituo.

Kama haiwezi, ni bora kusiwepo Vituo hivyo, kwani havina maana ya kuviweka, badala yake Askari hao wanapelekwa kwenye doria ya Mita.

Pili, Askari wahamishwe toka makazi ya raia, maana kunawafanya wazoe wahalifu na kuwaonea aibu kuwafichua na kwa kutoharibu mahusiano ya ujirani.

Tatu, Wizara itumie watoto kufichua vitendo vya ujambazi na uovu mwingine.

Nne, uwewe utaratibu wa wananchi kutoa taarifa kwa magari yanayosimama bila utaratibu kwa kusababisha ajali (daladala) yalekezwe kwa sheria kali kusimama kituoni.

Tano, Serikali (Wizara) inasema nini juu ya magari yanayo jaza sana abiria kupita uwezo wake hasa yanayotoka Mkoani Singida kwenda Dar es Salaam na kuhatarisha maisha ya wananchi hao?

Sita, Serikali (Wizara) isiwaache Maaskari waliopo Vijijini katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hotuba hii mia kwa mia na ni mategemeo yangu kutokana na namna Serikali ya Awamu hii ilivyo jitahidi kuboresha maslahi ya wafanyakazi, hasa ya ngazi ya nthini.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Wizara walio teuliwa umedhihirisha wazi kipaji alichopewa Mheshimiwa Rais kwani wote watatu ni mahiri na wanafanya kazi zao kwa uadilifu. *IGP* mwema ni ushahidi tosha wa hayo kwa kulipangua Jeshi jambo ambalo limewapa amani wananchi kwa namna ya utulivu.

Mheshimiwa Spika, lawama nyingi zinazotolewa kwa askari zinaangalia upande mmoja tu wa Shilingi Waswahili wanasema, ukichokoa chokoa pweza binadamu hamtamweza. Sasa Askari hao umeshawachokoa, wao wafanye nini?

Mfano, Meja Ayoub ameuwawa Chake Chake wakati wa kujiandikisha upigaji kura; pili, Askari Sharif wa JKU ameuwawa kikatili Piki Pemba baada ya upigaji kura; tatu, Askari wa kike wa Magereza kutekwa nyara siku ya upigaji kura.

Mheshimiwa Spika, waungwana wakiomba na mambo ya kheri hupeana. Mimi naomba kero za Askari Tunguu zimalizwe, ukarabati na pia Kituo cha U/Ukuu wajengewe nyumba za Askari.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nyumba za kuishi Askari katika Mji wa Magu Mkoani Mwanza zilijengwa mwaka 1976 (miaka 30 iliyopita). Tatizo ni kuwa makazi haya hayajapatiwa umeme. Zimefanyika jitihada na maombi mbalimbali ya kupata umeme bila mafanikio.

Mimi binafsi nibewahi kulileta suala hili kwa Viongozi wa Polisi na Kitaifa bila mafanikio. Gharama za kufikisha umeme za mwaka 2003 ni Sh.1,421,700/= tu. Kwa nini mpaka leo hii makazi haya hayajapatiwa umeme?

Askari pamoja na familia zao wananyanyasika sana wakati umeme uko nyumba jirani na gharama yake haizidi Shilingi milioni mbili. Kwa kweli mimi kama Mbunge wa Askari hawa pamoja na familia zao walionipigia kuwa kwa kipindi cha pili sasa siridhiki na hali hii. Napenda nielezwe. Umeme watapata lini?

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi mungu kwa kutujalia katika Kikao cha leo tukiwa wazima na wenye afya njema.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Napenda kumpongeza Waziri wa Usalama wa Raia pamoja na Naibu wake kwa hotuba yao iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza *IGP* Said Mwema kwa kazi nzuri ambayo ameanza kuionyesha ya kupambana na majambazi pamoja na Askari ambao wanakwenda kinyume na maadili ya kazi zao. Namtakia kazi njema.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Jeshi la Polisi ni kulinda raia na mali zao, lakini kwa bahati mbaya, wako baadhi ya Askari hao ambao wanafanya kinyume chake. Baadhi ya Askari wanatumia nafasi zao kwa kuthubutu kuwanyanyasa wananchi kwa kuwapiga, kuwakamata na kuwaweka ndani kuwabunia makosa yasiyokuwa ya kweli na hata kupora mali zao baadhi ya wakati.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linasahau wajibu wao zaidi inapofikia wakati Uchaguzi Mkuu na hasa kule Zanzibar. Unyanyasaji wa namna mbalimbali hufanyika katika Visiwa vya Unguja na Pemba, hufanywa na Jeshi hilo wakishirikiana na Vikosi vya SMZ ambavyo hutia hofu na kuwafanya wananchi waishi kwa wasiwasi mkubwa. Mambo haya yanababishwa kuwakosesha wananchi haki zao mbalimbali wakiwa wao ni raia halali wa Visiwa hivi.

Mheshimiwa Spika, udhalilishaji na unyanyasaji unaofanywa wakati wa Uchaguzi Mkuu hasa hufanywa kwa wafuasi wa Vyama vya Upinzani na hasa wafuasi wa Chama cha Wananchi (*CUF*). Hii inatokana na kuwa Chama cha CUF kina upinzani mkubwa sana kule Zanzibar dhidi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, watu kukamatwa ndani kwa muda mrefu bila kufikishwa Mahakamani, limekuwa ni jambo la kawaida wakati wa Uchaguzi Mkuu. Kufanya hivi ni kinyume na haki za binadamu na ni udhalilishaji mkubwa. Naiomba Serikali iangalia suala hili hasa inapofikia wakati wa Uchaguzi Mkuu ili nchi yetu iweze kuwa katika hali ya amani na utulivu wakati wote. Ahsante sana.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Kwa kweli bila kuficha majambazi sasa yako njia panda yakihaha kutafuta mahali pengine pa kufanyia kazi yao. Tanzania sasa siyo mahali pao. Pamoja na pongezi hizo, naomba nieleze yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kubambika kesi, ni mojawapo ya matatizo makubwa yaliyomo katika Jeshi la Polisi. Raia wengi wasio na hatia wanabambikizwa makosa kwa makusudi na Polisi wetu. Hali hii ni kinyume na maadili ya kazi yao na isivumiliwe kuendelea. Kufanya hivyo, kutawapoteza imani. Kwa wananchi na kukosa ushirikiano, naomba Wizara inieleze ni Askari wangapi wamebainika wakifanya hivi na hatua za kisheria na kinidhamu zilizochukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, suala la kushirikiana na watuhumiwa, nalo ni tatizo kubwa katika Jeshi letu la Polisi. Wananchi wengi hushikwa na butwaa kuona jinsi baadhi ya Askari Polisi wetu wanavyoshirikiana kwa ukaribu sana na watu ambao wanatuhumiwa/wanafahamika kuwa wanafanya uhalifu. Naomba kuelezwani hatua gani Wizara imechukua kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Kibara ni kikubwa kikisaidiana na Vituo vingine vidogo vidogo vinne. Lakini Kituo hiki, licha ya eneo kubwa la Jimbo na vile vile kuwa na matukio mengi ya uhalifu likiwemo wizi wa nyavu, mashine za kuvulia samaki na ujangili majini, Kituo hiki (Ofisi zilizojengwa na Serikali), gari, nyumba za Polisi na vyombo vya mawasiliano. Naomba kuelezwani lini Kituo hiki kitapewa vitendea kazi hivi ili kiweze kulinda usalama wa wana Mwibara na mali zao!

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu kwa kulinda Watanzania na mali zao. Napenda kukiri kuwa, wameanza vizuri kutekeleza majukumu yao, wananchi wa Jimbo la Rorya wanawapongeza kwa umahiri wao katika kusimamia, kufuutilia na kuimarisha utendaji kazi ya kila siku. Hongera sana.

Baada ya pongezi hizo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rorya, napenda kutoa maombi yao kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kama walivyotuma.

Kwanza, Jimbo la Rorya linapakana na Jamhuri ya Kenya katika eneo la nchi kavu na eneo la Ziwa. Lina Kata 21 na wakazi wapatao 250,000. Jimbo la Rorya linatarajiwa kuwa Wilaya kamili baada ya maombi yaliyopelekwa Serikalini kuanza kufanyiwa kazi na uamuzi wa Serikali utatolewa baadaye. Kutokana na maelezo hayo, Jimbo la Rorya linakabiliwa na vitendo vya ujambazi, wizi wa mifugo, ujambazi wa kutumia silaha na matukio ya magendo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na matukio ya uhalifu na ujambazi, Vituo vya Polisi katika Jimbo la Rorya, vinapungukiwa na vitendea kazi na hivyo kudhoofisha

juhudzi za Polisi wetu kudhibiti ujambazi. Napongeza juhudzi za Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayofanya licha ya ukosefu wa vitendea kazi. Mara nyingi Polisi wamefuatilia wahalifu kwa baiskeli au kuomba msaada wa usafiri kutoka kwa raia ambao mara nyingi raia wenye usafiri hawana mafuta kwa ajili ya magari yao.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Rarya linalo Vituo vikubwa vya Polisi. Kituo cha Utegi ambacho kiko katikati ya Jimbo na hivyo kutumika mara nyingi kufuatilia matukio ya wizi wa mifugo, mali za wananchi na magendo. Kituo hiki hakina gari, mwaka 2003 na 2004 nilimwomba *IGP* Mstaafu asaidie katika kulipatia gari kwa ajili ya doria Kituo cha Utegi. Alikubali, lakini hadi sasa gari halijapatikana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamenituma kuleta ombi lao kwa Wizara. Nafurahi kutamka kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amepokea ombi hili na ameahidi kushughulikia. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua aliyoichukua kwa kuzingatia uzito wa tatizo ambalo ni kero ya miaka mingi. Naomba Kituo cha Polisi Utegi ipatiwe usafiri.

Kituo cha Polisi hakina umeme, licha ya waya za umeme, inapata mlangoni mwa Kituo hicho. Inahitajika nguzo tatu tu kupidisha umeme katika Kituo hicho. Naomba Kituo kipatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, Askari katika Kituo hiki ni wachache. Naomba waongezwe.

Mheshimiwa Spika, hakuna nyumba hata moja iliyojengwa kwa makazi ya Polisi. Wote wanaishi uraiani, hivyo, kupunguza nidhamu na ufanisi wao. Eneo la kujenga nyumba za kuishi karibu na Kituo lipo. Naomba mpango wa mradi wa ujenzi wa nyumba za kuishi Polisi uandaliwe. Nampongeza *IGP*, Makamanda wote na Polisi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naunga mkono hoja.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hotuba hii ni nzuri na malengo na mikakati ya kuendeleza ulinzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa angalizo kwamba Wizara iendelee kumulika watumishi wabovu katika Jeshi hili. Ukiukaji wa maadili bado Vijijini wananchi wanapata taabu sana. Wanatembelewa na Askari ili kutafuta chochote, hata kama sio kesi, ili mradi mwananchi atatishwa hadi atoe kilichopo, ushirika wa Askari Vijijini na wanamgambo na Watendaji wa Vijiji na Kata ili kumdhulumu mwananchi, hasa wafugaji.

Wafugaji hao wengi hawana elimu, kutafsiri sheria au kufahamu haki zao za kikatiba ni aghalabu sana. Ni matumaini yangu kuwa Askari Polisi wana mstari wa mbele kumsaidia mwananchi na kumwelisha haki yake ya kuishi kwa amani, badala ya mara akionekana Askari, basi anaona utu umekwisha, hana usalama kabisa, badala ya kuwa na amani.

Viongozi wa Polisi, Mkoa, Wilaya, waone umuhimu wa kuwatemebelea Askari walioko katika Vituo vidogo vidogo vilivyoko Vijijini. Askari walioko huko, wanakuwa Miungu, kwani hakuna *check and balance* ya kazi zao. Viongozi wengi wanasahau Ukaguzi wa Vituo vya pembezoni. Ibueni kazi hizo ili ufanisi uonekane unafanyika. Nawatakia kheri kwa kazi.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Napenda kukupongeza sana wewe Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Naomba pia nintamke *IGP* Said Mwema kwa kazi kubwa ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Aidha, nampongeza kwa kuteuliwa kwake.

Hoja yangu ni kwamba kule Utete Rufiji, Makao Makuu ya Wilaya, yenyе umri wa miaka 100, haina Ofisi ya Polisi ya Wilaya. Makao Makuu hayo, Ofisa Mkuu wa Polisi Wilaya anajibanzabanza tu Bomani. Hakika ni aibu kubwa kwa Jeshi letu. Kwa vile, Utete sasa ina hadhi ya Mji mdogo, kuna uwingu wa matukio ya uhalifu kwa mfano, wizi, vurugu za watu wengi, ujangili kule *Selous* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Polisi wanahitaji Ofisi yao ya Wilaya pale Utete. Aidha, kuna haja ya kuwajengea nyumba za kuishi watumishi (*Police Offers Quarters*) pale Utete/Rufiji.

Maafisa Polisi wanaolinda Daraja la Mkapa, Rufiji, pale Ikwiriri wanapata adha kubwa ya kutembea kutoka Ikwiriri kwenda katika lindo, yaani daraja la Mkapa. Umbali wake yapata kilometra 10. Askari hawa hawana usafiri kabisa. Naomba Polisi Ikwiriri ipatiwe usafiri wa uhakika kwa ajili ya kwenda kulinda Daraja la Mkapa. Daraja la Mkapa limejengwa kuvuka Mto Rufiji kwa gharama kubwa sana. Serikali isione taabu kutoa usafiri, kwani gharama ya daraja hilo ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Rufiji kulitokea matukio mengi. Lakini naomba ninukuu haya matatu:-

- (i) Kuchomwa moto kwa Ofisi ya CCM ya Kata ya Umwe Tarafa ya Ikwiriri. Mpaka sasa hakuna Taarifa rasmi ya *Arrests* au *convictions* au *Acquittals*.
- (ii) Siku ya mkesha wa Uchaguzi Mkuu, kule Mohoro Rufiji Kada wa CCM alipoteza maisha na hadi sasa wananchi hawajui kumetokea nini. Maiti hajipatikana. Hakuna taarifa rasmi ya *Arrests*, *Convictions* au *Acquitals*.
- (iii) Kuna taarifa za biashara ya magendo huko Mohoro/Rufiji bidhaa aina mbalimbali huingizwa Jimbo la Rufiji bila kufuata utaratibu. Hakuna taarifa rasmi ya *arrests convictions* au *acquittals* au hata kuweka ulinzi wa kuzuia biashara hiyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja hizi ni doa katika kanzu nyeupe ya Ijumaa. Namwomba atazame matukio haya na wananchi waelezwe ukweli wa mambo.

Mwisho, nakupongeza sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, Naishukuru Wizara kwa kauli yake kwamba Kituo cha Polisi cha kisasa Wilayani Lushoto kitajengwa mwaka 2007-2008. Je, kwa kutambua kwamba maandalizi ya msingi ikiwemo michango ya nguvu za wananchi yalifanyika miaka kadhaa iliyopita, Serikali haioni umuhimu wa kuanza ujenzi huo mwaka 2006-2007 japo kwa hatua za awali za kutangaza tenda?

Vituo vya Polisi (*Police Posts*) Ibara ya 79 ya hotuba, kwa kutambua umuhimu wa Vituo vidogo vya Polisi wananchi wa Wilaya ya Lushoto wamehamasika kuchangia ujenzi wa Vituo katika maeneo yao. Wizara ina mkakati gani wa kusaidia juhudhi hizo za wananchi kwa mfano ushauri, michoro, usimamizi, vifaa na kadhalika? Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKE J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia kwa hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo wa kuhakikisha maandeleo ya Watumishi wa Wizara hiyo na usalama zaidi kwa raia wa nchi hii.

Napenda pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Katibu Mkuu na Watendaji wako wote wa Wizara hii kwa kazi yao kubwa wanayofanya kuhakikisha usalama wa raia wetu pamoja na ugumu wa mazingira wanayofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi Wilayani Mbozi lenye ukubwa upatao kilometra za mraba 6,300, lina maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na msitu wa akiba wa Msangano, Isalalo, Nyimbili kati ya Itambalila na Ntungwa, Malinga kati ya Ndalambo na Myunga, ambayo mara kwa mara huvamiwa na majambazi ambao huwapora na kuwajeruhi wasafiri na kutokana na kutokomea msituni bila kukamatwa, kutokana na kwamba katika Jimbo hili kuna Vituo viwili tu vidogo vya Polisi pale Tunduma na Kamsamba ambavyo haina hata usafiri wa kufuatilia matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Ndalambo, Msangano na Kamsamba ni Makao Makuu ya Tarafa zenyе majina hayo hayo. Ndalambo iko kilometra 80, Msangano kilometra 60 na Kamsamba iko kilometra 120 kutoka Vwawa (Mbozi) ambapo kuna Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi na kutokana na ukosefu wa mawasiliano ya simu na barabara mbovu kati ya maeneo hayo na Makao Makuu ya Wilaya, taarifa za matukio ya uhalifu huchukua hadi siku tatu kufika Wilayani na hivyo wahalifu kuendelea kufanya vitendo hivyo kama wapendavyo. Wananchi wa Tarafa hizo kwa mfano Msangano, walikwishajenga Vituo vidogo vya Polisi (*Police Post*). Tangu miaka kumi iliyopita, lakini hadi leo hakuna Askari Polisi waliopolekwa.

Mheshimiwa Spika, Jimbo hili linapakana na nchi za Zambia, Malawi na Wilaya za Ileje, Sumbawanga, Chunya na Jimbo la Mbozi Mashariki. Maeneo yote hayo ni maingilio ya watu mbalimbali ikiwa pamoja na wahalifu wa hatari.

Mheshimiwa Spika, ombi la wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi ni kwamba kufunguliwa Vituo vidogo vya Polisi Msangano, Myunga, Kapele na Chilulumo, ili kuwezesha Askari wa Vituo hivyo kufanya doria kwenye maeneo ya misitu ya Akiba ya Msangano – Isalalo, Utambalila – Ntungwa (Nyimbili), Ndalambo – Myunga na Kakozzi – Kapele na pia kupeleka taarifa za kuomba msaada Wilayani pindi matukio ya uhalifu yatokeapo maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum kuhusu Mji mdogo wa Tunduma kutokana na kuwa Kituo kikubwa cha mpaka wa Kimataifa ni kuongezwa idadi ya Askari na gari kwa ajili ya doria mpakani kwa sababu sasa hivi matukio mengi huhusisha wahalifu wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja ya Wizara ya Usalama wa Raia asilimia mia moja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa hotuba nzuri ya Waziri. Nampongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya *IGP*.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Misungwi wanaipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya ulinzi wa raia na mali zao. Kipindi hiki Jeshi la Polisi limethibitisha uwezo wake wa kupambana na wahalifu (majambazi) wananchi wa Misungwi kwa kutumia Jeshi lao la Sungusungu, wanaahidi kutoa ushirikiano na Jeshi la Polisi kupambana na wahalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo yanayowakera wananchi wa Misungwi. Misungwi ni Wilaya iliyanzishwa mwaka 1997 hadi leo hii tumekosa uongozi wa Wilaya yaani *OCD*. Huduma zetu zimebaki Kwimba kwa muda mrefu, hivyo kero hii inawafanya wananchi kupungukiwa nguvu za kupambana na majambazi.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu, baada ya kuongeza Mikoa ya Kipolisi pamoja na Kanda maalum Watendaji katika Mikoa hiyo yaani, Kinondoni *RPC* alipatikana; Ilala *RPC* alipatikana; Temeke *RPC* alipatikana. Je, Ofisi za *RPCs* hao zilitoka wapi? Hivyo, wana Misungwi wanaona kama hawatendewi haki.

Mheshimiwa Spika, mfano mwengine, Misungwi, *DED* wake hana nyumba, amepangishiwa, hivyo wanaomba wapatiwe nyumba kwa ajili ya *OCD*.

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara kwa kutupatia gari iliyohidiwa na *IGP* wa kipindi kilichopita pamoja na hayo, watumishi wa Wizara hii wanayo matatizo mengi ikiwemo nyumba za kuishi Serikali ianze kuliona jambo hilo, kwani baada ya kazi nao waweze kupumzika usemi wa kuwa ni watumishi wa masaa 24 ni pamoja na kupumzika kama ilivyo kwa Waganga.

Mheshimiwa Spika, nitahitaji kupokea jibu juu ya *OCD* katika Wilaya ya Misungwi katika majumuisho. Naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWADINI ABbas JECHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Bakari Mwapachu, Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa Mohamed Aboud, Mbunge kwa kuteuliwa na Rais kuiongoza Wizara hii. Kadhalika niwapongeze kwa juhudhi kubwa ambayo wao wameionyesha katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Jeshi la Polisi ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Hii ni kazi ngumu inayohitaji ujasiri wa hali ya juu. Siku za hivi karibuni tumeshuhudia wimbi kubwa la ujambazi nchini. Serikali imechukua hatua madhubuti kuidhibiti hali hii na kwa kweli nalipongeza Jeshi letu hili.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya wimbi hili la ujambazi limehamia Tanzania Zanzibar. Nitoe pongozi zangu kwa Waheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuchukua juhudhi ya kuzungumza na wafanyabiashara wa Zanzibar kuona ni namna gani Serikali inaweza kudhibiti mfumko wa ujambazi Zanzibar. Naiomba Wizara kuchukua juhudhi za ziada kukomesha ujambazi wa kutumia silaha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi pia linaweza ama kuimarishe au kuna demokrasia nchini. Majeshi yetu yameondolewa katika kushiriki shughuli za siasa. Wanachoruhusiwa ni kupiga kura tu. Ni dhahiri kwamba haingekuwa jambo la busara kwa majeshi yetu ama kutumika kusaidia au kuwanyima haki/fursa Chama chochote cha Siasa. Polisi pamoja na majeshi mengine yanapaswa kuwa *neutral* katika kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, katika chaguzi za nchi zilizopita, tumeshuhudia ukiukwaji mkubwa wa maadili ya Uaskari. Lakini baya zaidi, badala ya Polisi kulinda usalama wa raia na mali zao wamekuwa mstari wa mbele katika kupiga raia na kuiba ama kupora mali zao. Haya yametokeza na kwa masikitiko makubwa. Hii imewafanya baadhi ya raia kuziogopa chaguzi.

Aidha, kauli ya *IGP* aliystaafu Ndugu Mahita aliposema kuwa kwa muda wote ambao yeeye atakuwa *IGP* kamwe hatachukua madaraka katika nchi hii. Hii ni kauli potofu na ya kichochezi, ambayo ilipaswa kukemewa kwa nguvu zote. Ni kauli ambayo inaviza demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kumteua *IGP* Mwema. Kamanda Mwema anaonyesha ukomavu na uwelewa mkubwa katika kazi zake. Tuna matumaini kwamba atatumia busara zake kuhakikisha kwamba Jeshi la Polisi linatekeleza wajibu wake bila ubaguzi wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, Polisi kama mfanyakazi yeьте anahitaji mazingira mazuri ya kazi ili aweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Miongoni mwa mazingira hayo, ni kupata nyumba bora, mishahara na marupurupu mazuri, vitendea kazi, elimu na

kadhalika. Kukosekana au upungufu wa hayo kunasababisha kutetereka utendaji kazi wa Polisi.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu, kuna makazi ya Polisi maarufu *Polisi line*. Nyumba hizo zilijengwa zamani sana, ni chache, zenyenafasi finyu. Lakini kwa bahati mbaya, nyumba hizo katika siku za hivi karibuni zimekuwa zinapasuka, zinavuja sana siku za mvua na sasa asilimia kubwa ya nyumba hizo zimehamwa kwa sababu ni hatari kwa maisha ya mwanadamu.

Nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Bunge ya Ulinzi kwa kutembelea makazi hayo ya Polisi na kujionea hali halisi ilivyo. Naiomba Wizara ili kuokoa maisha ya Polisi wetu pamoja na familia zao ni vyema sasa ikachukua hatua za haraka kujenga na kuzifanyia ukarabati nyumba zote za makazi ya *Polisi line* ili kuwaondolea usumbufu wa makazi Askari wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inaboresha maslahi ya Watendaji wake. Lakini kwa sababu siku za nyuma maslahi mengi ya Jeshi la Polisi yamekuwa hayalipwi ipasavyo, kumekuwa na malimbikizo makubwa ya madai ya aina hiyo.

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa Askari Polisi wa Mkao Kaskazini Pemba kwamba madai yao kwa muda mrefu sasa hayajalipwa pamoja na kwamba ahadi kadhaa zimetolewa kwamba malipo hayo yatalipwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuyatupia macho madai ya Askari hao kutoka Mkao wangu na kuona kwamba madai yao yanalipwa haraka iwezekanavyo.

Mwisho, naiomba Wizara na Jeshi la Polisi kwa ujumla *to establish public trust and confidence*, lakini pia *to establish Community Policy*. Hatua hii itasaidia kukuza maelewano baina ya Polisi na raia na hatimaye kukuza mashirikiano yatakayosaidia utendaji katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Jeshi zima kwa jinsi walivyopambana na mwishowe kushinda wimbi la ajabu la ujambazi. Karibu wananchi tupoteze matumaini. Naomba Wizara ikaze kamba, kwa hili tuko pamoja.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa utendaji wa kila siku. Ni Wizara ngumu. Tunaona mmeepanga safu upya. Inatupa matumaini.

Mheshimiwa Spika, Askari (*Welfare*) nyumba bado vijana wetu na hata baadhi ya Maofisa wanalala katika makazi duni. Tubadilishe, tujenge makazi zaidi, nyumba zisiwe ndogo mno, zisiwe chini ya *bedroom* mbili kwa hali yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, naomba mishahara ya Askari wetu iboreshwe, kwani wanafanya kazi masaa mengi, lakini tofauti na wengine ye ye hana *overtime*. *The salary is all inclusive.*

Mheshimiwa Spika, naomba stahili za Askari, hizi zilipwe, kama vile pesa za uhamisho, safari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni vitendea kazi. Usafiri Vituo vidogo (siyo *Police Post*), mfano Wilaya ya Karagwe tuna baadhi ya Vituo kama Murongo, Kaisho, Rubwera na kadhalika. Vituo hivi vinahudumia maeneo makubwa sana. Bila usafiri ni vigumu kufuatilia masuala ya kazi. Napendekeza Vituo vipewe pikipiki angalau moja kila Kituo.

Mheshimiwa Spika, penye simu kwenye maeneo tunaomba Vituo viwe na huduma ya simu. Itawasaidia sana wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya bei ya mafuta, Vituo vya Polisi, hata vya Wilaya, napendekeza vipewe pikipiki kadhaa za kuweza kukimbia kimbia kwenye matukio haraka na kwa gharama ndogo. Hii hasa ni kwa Miji midogo nje ya Dar. Kutegemea gari moja tu, kunakwamisha mambo. Pikipiki ni rahisi. Naunga hoja mkono.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na uwezo wa kuchangia angalau machache katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Usalama wa Raia.

Mheshimiwa Spika, kazi za Askari katika jamii, kama jina la Wizara hii linavyojieleza, kwamba ni Usalama wa Raia, basi hapana budi na wale wote ambao wanafanya kazi katika Wizara hii amba wengi wao ni Askari, basi kazi yao kubwa ni kulinda Usalama wa Raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, mara nyangi hali sivyo ilivyo, maana kumekuwa na matukio kadhaa ambayo yanaashiria kwamba Askari ndio wanaharibu au kutishia usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, imedhihirika kwamba baadhi ya Askari wanajishughulisha na vitendo vya ujambazi na kwamba hata baadhi yao wanaendelea na kasi ya aina hiyo Mahakamani. Ili kukomesha hali hiyo, ni lazima Serikali ijipange na kuwa na mikakati endelevu, sio tu ya kupunguza hali ya Askari kujihusisha na vitendo vya uhalifu, bali kutokomeza kabisa hali hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ni haki za binadamu. Askari wa Jeshi la Polisi wamekuwa wanalamikiwa sana kuhusiana na suala la uvunjaji wa haki za binadamu. Katika hili, baadhi ya Askari huwa wanachukua hukumu mikononi mwao, yaani kabla ya mtuhumiwa kupatikana na makosa (hatia) na hajafanya tatizo lolote linalolazimu kuadhibiwa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sana Serikali (Wizara) iwakumbushe Jeshi lake la Polisi wajibu wake (wao) kupitia kwenye Vikao, warsha, kongamano na kupitia kwenye Semina.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria za nchi hii, Askari wote wa Tanzania hawaruhuswi kujihusisha na vitendo vyo vyote vile nya siasa. Lakini kinyume cha hivyo Askari hasa wa Jeshi la Polisi, baadhi yao wanajihusisha sana na vitendo nya siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hao wanaojihusisha na siasa wanategemea upande wa Chama Tawala, basi kwa makusudi sheria inapuuzwa, lakini pale inapotokea Askari kujihusisha na siasa za upinzani, basi Askari (wa Jeshi la Polisi) huyu hunyanyaswa, kupewa uhamisho kutoka alipo kwenda pengine au kuadhibiwa kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali kupitia Vikao vyao kuwakumbusha Askari (Jeshi la Polisi) kutojihusisha na siasa kama sheria za nchi hii zinavyooleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya Askari (Jeshi la Polisi) bado yapo malalamiko mengi kuhusiana na maslahi ya Askari hasa wa Jeshi la Polisi na kutoekana na kazi zao za kila leo. Ni vyema maslahi ya Askari wa Jeshi la Polisi yaangaliwe upya, ikiwezekana mishahara na posho zinazohusika na kazi zao.

Mheshimiwa Spika, suala la nyumba za Polisi, ni tatizo sugu karibu katika Wilaya na Mikoa yote nchini. Kumejitokeza malalamiko mengi pamoja na madai juu ya uhaba wa nyumba za Polisi. Serikali imekuwa inaeleza kuongezeka kwa juhudi ya kuwapatia Polisi nyumba za makazi , lakini bado tatizo lipo. Kwa hiyo, inapendekezwa kwamba juhudi zaidi ichukuliwe ili kuondokana na adha hiyo.

Mheshimiwa Spika, ajira katika Keshi la Polisi hasa kule Visiwani Zanzibar, utaratibu wake unaendeshwa kwa misingi ya kisiasa. Maana shughuli yenewe anakabidhiwa Sheha ambaye naye ni kada wa Chama Tawala. Kwa hiyo, wale wote amba ni vijana, ama wanaotoka upande wa Vyama vya Upinzani au wazee, wao ni kutoka upande wa Vyama vya Upinzani, basi hawapati nafasi ya kuajiriwa. Kwa hiyo, ni vyema Serikali itafute au ilite utaratibu mwengine utakaojali sifa na sio wanachama wa Chama fulani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa Wizara hii kwa kuupa umuhimu wa pekee usalama wa raia wa Tanzania.

Vile vile, nawapongeza Waziri na Naibu wake kwa kupata nyadhifa hizo. Nawatakia kila la heri katika kazi ya kutuhakikishia usalama raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia hoja hii kwa kuangalia upungufu wa Askari katika nchi yetu. Taarifa zinaonyesha kwamba hivi sasa tuna uwiano wa 1:3000 ambapo uwiano wa kimataifa ni 1:400-600.

Pamoja na juhudhi za Serikai za kuongeza Askari nchini, lakini bado idadi hajijatosheleza mahitaji. Hili linasababishwa na uoga wa wananchi wa kujinga na Jeshi hilo kwa kuhofia maisha yao yatakuwa duni mpaka kufa, kwani mazingira ya kazi hayavutii na makazi yao yanatia aibu.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi pia ni tatizo. Vituo vya kazi havina vyombo vya usafiri na wala hawana redio *calls*, mfano halisi ni Kituo cha Kagunga Kigoma Kaskazini, Kituo kilichopo mwambao wa Ziwa Tanganyika tena kipo mpakani. Vile vile, Kituo hicho hakina Mkuu wa Kituo ila yupo anayemkaimu tu. Je, ni lini Serikali itapeleka Mkuu wa Kituo katika Kijiji cha Kagunga na vitendea kazi kama boti kwa ajili ya usafiri na vitendea kazi vingine? Naomba nijibiwe katika majibu ya Wizara jioni.

Mheshimiwa Spika, nadai kujibiwa hilo swali, kwani Kituo hicho ni muhimu sana, kinahudumia Vijiji vingi kama Zashe, Kiziba na Mwamgongo. Hivyo, inabidi kupewa umuhimu wa pekee. Pia, usafiri wa boti ni muhimu kwa wahalifu kwani hutakiwa kubebwa kutoka sehemu/Vijiji tofauti.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Pili wa Bunge hili mwezi Februari, niliuliza swali kuhusu umuhimu wa Wizara hii kuwatafutia vifaa vya kazi vya kukidhi mahitaji ya Polisi na hasa *bullet proof* wakati wakipambana na hawalifu hasa majambazi watumiao silaha. Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa itazingatiwa katika Bajeti hii na alinihakikishia kuwa vifaa vingine pamoja na *bullet proof* vitanunuliwa mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili hiyo na ni kifungu kipi katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linahusu pensheni kwa Askari. Suala hili ni muhimu sana liangaliwe upya kwani linachanganya au utekelezaji wake umepitwa na wakati. Mfano, Askari wa cheo cha *Constable* anaingia kwenye pensheni baada ya miaka 12 ya utumishi wake. Je, Serikali haioni kuwa haimtendei haki Askari mwenye cheo hicho cha *Constable*? Naomba ufanuzi wa kina kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Maaskari wengi siku hizi wanajiendeleza kitaaluma. Lakini cha kushangaza, wanapewa nyota tu na taaluma zao hazitumiki. Mfano mtu ana Shahada ya sheria au *Advanced Diploma* ya Maendeleo ya Jamii, anapewa nyota. Masomo aliyoysoma yanafaa kwa maendeleo ya Jeshi. Serikali haioni kuwa umefika wakati Maaskari wenye taaluma mbalimbali wawekwe katika vitengo mbalimbali kulingana na taaluma zao?

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa vyeo na elimu vinachanganya katika Jeshi la Polisi, mfano mwenye *degree* moja anapenda kuchukua nyota na mwenye *degree* moja, anapenda kuchukua nyota na mwenye Cheti cha *Form Four* ambaye ni *Station Sergeant*, pia anakwenda kuchukua hiyo hiyo nyota.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi, Jeshi halioni kuwa linajichanganya hasa katika kipindi hiki ambacho wasomi wanatakiwa wawe *motivated* zaidi?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la kuo na kuolewa. Askari wa kiume akiwa anaruhusiwa kukaa na mkewe Kambini wakati msichana Polisi akiolewa haruhusiwi kuishi na mumewe katika eneo la Kambi wanaloishi hivyo kulazimika kutafuta makazi nje ya Kambi. Naomba ufanuzi juu ya suala hili. Serikali haioni kuwa inafanya ubaguzi kati ya Askari wa kiume na wa kike?

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huo naomba kuwasilisha nikimkumbusha Mheshimiwa Waziri anipe majibu au atoe ufanuzi kwenye hoja ambazo zimeonyesha utata. Ahsante.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Bajeti ya Wizara hii ya Usalama wa Raia. Awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba nitachangia katika maeneo machache tofauti. Kwanza ni Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba Jeshi la Polisi kuwa na *genda sensitive* kuwa na *balance*. Najua *historically*, Jeshi la Polisi wanaume walikuwa ni wengi. Lakini kwa sasa hivi nina uhakika kuna wanawake waliosoma na wenyе uwezo wa kuliongoza Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata jibu kwamba, *ratio* hapa nchini ipo namna gani na tuna *RPC RCO* na *OCD* wangapi? Kuna wanawake wangapi wenyе vyeo Tanzania nzima? Napenda kutoa pongezi kwa Mkuu wa Polisi katika jitihada zake za kuimarisha usalama wa Taifa hili, lakini hata hivyo bado tuna njia ndefu ya kuimarisha usalama wa raia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la usalama barabarani. Mara nyingi *Police Traffic* wamekuwa tu wakisimamia vyombo vya moto kama magari na pikipiki. Katika barabara kuna waendesha mikokoteni, wananchi wanauza vitu barabarani *especially* Dar es Salaam, barabara ya *Pugu Road accident* zinasababishwa na hawa. Ni jinsi gani *traffic* wanaweza ku-control hawa watu wa mikokoteni? Hata mmachinga akigongwa, anayefunguliwa mashtaka ni mwendesha gari. Wizara itasaidiaje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu silaha, Jeshi la Polisi limekuwa likidhibiti silaha za kisasa. Lakini visu vimekuwa vinauzwa kiholela barabarani na ukizingatia kuna watu wenyе upungufu wa akili na visu vinaweza kutumika katika kutenda uhalifu. Naomba jibu, Wizara ina mpango gani wa kudhibiti uuzaaji holela wa visu Mitaani?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya *IGP* nasikitika kuona Askari *FFU* anaendesha pikipiki, lakini havai *helmet* yake, kuna tatizo gani? Ushahidi ninao kama utahitajika.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la kuendesha gari na wakati dereva amekunywa pombe. Unywaji pombe na ku-*drive* kunaongeza *accidents* nyingi bila sababu. Labda Wizara iangalie na Wizara ya Sheria labda wafute kabisa *drink and drive*.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kinachoongeza ajali barabarani ni wakati dereva anayeendesha gari na kuongea na simu za mkiononi. Hii ni hatari sana na dereva anaweza kujisahau na kusababisha ajali. Ningeshauri dereva lazima atumie *head phone*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni *breakdown*. Kwa kweli magari yanayotumika kuvuta magari Dar es Salaam ni mabovu, inaharibu magari ya watu. Nafikiri ni wakati muafaka sasa Serikali wanunue magari ya kisasa ambayo yatabeba magari hayo badala ya kuyavuta.

Mheshimiwa Spia, napenda kuuliza *ratio* ya Police kwa kila Mtanzania ni ngapi? Inaonekana kama vile Police hawatoshi. Kwa sababu, kwa mfano Askari wa Barabarani wanafanya kazi saa mbili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

Mheshimiwa Spika, kuna *accidents* zinazosababishwa tu na uzembe kwa mfano daladala baada ya saa kumi na mbili zinaendeshwa na *Day worker (tanboy)* ambaa hawana hata *license*; wanajua kabisa hamna Askari wa kuwakamata barabarani. Naomba jibu, Wizara ina mikakati gani kuhusu hili?

Mheshimiwa Spika, motisha kwa wafanyakazi wa Polisi, wafanyakazi katika Wizara hii, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Mfano, kuna Polisi wanaishi uraiani inakuwa ni vigumu sana kwa Polisi hawa kuwakamata wahalifu ukizingatia unaweza kukuta aliyetenda kosa ni mwenye nyumba. Nafikiri ni wakati muafaka kuondoa Polisi uraiani.

Mheshimiwa Spika, naomba jibu, ni lini nyumba za *Police line* Moshi Mjini zitajengwa? Kwa kweli zilizopo ni chakavu na ni ndogo (chache)?

Pia, Polisi waangaliwe maslahi yao, kama mishahara sijui kama wanalipwa kutokana na walivyosoma au la.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu, nikichangia kuhusu Wizara hii, naomba majibu. Baadhi ni vithibiti vyaa mwendo vimeishia wapi? Na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *Traffic* anapokamata gari, naomba jibu la swali hilo. Inakuaje *traffic* anakamata gari labda kwa makosa mabovu halafu *traffic* yule anataka kupanda ndani ya gari lile na saa nyingine unakuta ni mwanamke ndiye aliyekamatwa.

Je, huu ndio utaratibu? Kwa nini asimwandikie *notification* au kama ni *fine* kwa nini wasitoze papo kwa papo? Hii haipendezi, wanaweza kuleta au kuonyesha kuwa rushwa inataka kutendeka.

Mheshimiwa Spika, kuna mfanyabiashara Mjini Moshi aliyemchoma Ndugu Swai mpaka kufa. Mfanyabiashara huyu anaitwa kwa jina la J.J. na P.P. alifutilia kesi ile mbali. Mpaka leo hii mke wa Marehemu hajatendewa haki na mfanyabiashara yule alikimbilia kwa habari za kusikika ametorokea nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, maana huyu mke wa Marehemu ana machungu mpaka leo. Naomba jibu. Je, Serikali/*Interpol* imefikia wapi katika kumkamata J.J.? Niliona katika magazeti *RPC Kilimanjaro* akiliulizia, amefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, ulinzi kwa watalii, kumekuwa na matukio mengi ya watalii kuvamiwa kuporwa bidhaa zao. Hivi majuzi barabara ya Londorossi West Kilimanjaro, watalii wa Kimarekani walivamiwa na kuporwa mali zao. Naomba Serikali itueleze ni mikakati gani ya kuimarisha ulinzi kutoka *Airport to Arusha/Moshi* njia za Landorosi/Machame na kwenye hifadhi zote za wanyama kwa ajili ya ulinzi. Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Nashukuru.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, baadhi ya Vituo vya Polisi Zanzibar, magari ya abiria yanasis mama kwa kupekuliwa katika kutii bango ambalo lipo katika Kituo cha magari ya abiria ili yasisiame kwa kupekuliwa. Ninaomba Wizara inieleze suala hilo ni la kisheria au ni la utaratibu? Kwa Pemba Kituo cha Polisi Mkoani gari inasisi mama Kituo kimoja linapotokea Chakechake. Kituo cha Mtambile gari inasisi mama kutoka Chakechake na kwenda Chakechake, wakati Kituo cha Wete gari haisimami aidha kwa kutoka Chakechake au kwenda Chakechake.

Mheshimiwa Spika, suala hili linaleta usumbufu mkubwa kwa wasafiri kwenye gari hizo. Ninaomba kama ni utaratibu uendeshwe au kama ni sheria, ipo haja ya sheria hiyo iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa tatu wa Bunge lako Tukufu niliuliza swali juu ya mauaji ya mwanafunzi Juma Omar yaliyotokea Jimbo la Mkoani wakati wa uandikishaji wahusika wa mauaji hayo wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa, bado suala liko katika uchunguzi. Je, kutokea wakati huo uchunguzi umefikia wapi? Ieleweke yako mauaji yamefanyika Pemba, lakini washutumiwa wameshachukuliwa hatua za kisheria. Je, iweje ni suala la huyo Juma Omar ndio linalofanyiwa uchunguzi na uchunguzi huo ni wa aina gani?

Ni zaidi ya miaka 30 nimeshuhudia ongezeko la Askari Polisi katika Wilaya yangu ya Mkoani, lakini sijashuhudia ujenzi wa nyumba hata moja ya Askari Kituo cha Mkoani. Hivi sasa kuna Askari anaishi kwenye chumba kimoja mke na watoto wanen. Haya ni maisha gani? Wilaya ya Mkoani iko kwenye Mkoa wa Kusini Pemba ikiwemo Wilaya ya Chakechake. Wilaya ya Chakechake japo nyumba zilizojengwa hazitosh: Je, Wilaya ya Mkoani nyumba za Askari zitajengwa lini?

Mheshimiwa Spika, ili chombo hicho kifanye kazi kitaalamu au kwa uhuru zaidi, lazima kifanye kazi kwa utaratibu wa sheria ambazo zimeaunda Jeshi hilo. Kuna taarifa Wilayani, kuna chombo kinaitwa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Pia kuna taarifa, Kamati hiyo ina uwezo wa kuviajiza vyombo vyaa usalama na ulinzi maagizo mbalimbali yakiwemo kuwakamata watu kwa baadhi ya matokeo kama habari hizo ni kweli zitaashiria Polisi baadhi ya kazi wanazozifanya wanazifanya sio kwa hiari yao bali kwa shinikizo la Kamati. Utaratibu huo sio mzuri. Kama ni kweli, unaweza kuwatia wananchi ndani bila ya hatia. Chombo cha Polisi kiachwe huru kifanye kazi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuna ucheleweshaji mkubwa wa Askari wanapopandishwa cheo kulipwa fedha zao kwa mujibu wa cheo chake. Wizara irekebishe hilo. Askari wanapohamishwa kwenda maeneo mapya ya kazi hucheleva sana mishahara yao kuwafuata, inabidi waifuate katika maeneo walikotoka. Hili ninaomba Wizara irekebishe. Ahsante.

**MHE. YONO S. J. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu, hakuna hata Kituo cha kimoja cha Polisi.

Wananchi wamejaribu kuomba huduma hii muhimu lakini majibu kutoka Wizarani na Mkuu wa Wilaya ya Njombe yanakatisha tamaa, eti wananchi wajenge vituo vyao. Jimbo langu ni kubwa sana na lina watu wengi kuliko majimbo ya Wilaya ya Njombe. Jimbo la Kaskazini kuna Kituo cha Makambako na Jimbo la Kusini lina Kituo cha Polisi Njombe Mjini. Sisi tupo mbali sana na Makao ya Wilaya na Makambako. Tuko mpakani mwa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Magharibi lina Tarafa tatu na Kata tisa. Kata hizo ni Usuka, Mdundu, Wangama, Wanginjombe, Ludunga, Saja, Illembula, Usuka na Imalinyi. Tarafa hizo tatu ni Mdandu, Wanging'ombe na Imalinyi.

Kinachosikitisha, kwa vile Kituo cha Polisi hakipo, Watendaji wa Vijiji na Tarafa wamekuwa Polisi na Mahakimu, kitendo ambacho kinafanya wananchi kunyanyaswa, uonevu, wizi na mauaji na kesi kupotezwa. Naomba Serikali itupatie Kituo angalau kimoja wananchi wasiteseke na majibu niliyopewa, bado sijaridhika.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo, kwa nini Polisi wameweka doria barabarani? Huzuia magari hasa malori na kudai rushwa, kwamba lori likisafiri toka Mwanza hadi Dar es Salaam linaweza kuzuiliwa njiani, mbali na Vituo vya kupima uzito wa magari, zaidi ya mara 50 na wananchi hawa wanakoseshwa biashara kutokana na kucheleweshwa njiani.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Jeshi la Polisi libuni mpango wa muda mrefu kufundisha nidhamu na maadili ya kijeshi kwa nia ya kuboresha utendaji wa Jeshi na kuongeza imani ya wananchi.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Pia niipongeze michango yote iliyotolewa kwenye Bajeti hii.

Pamoja na hivyo, nina michango michache ambayo ningependa Wizara hii iyazingatie. Awali, naiomba Wizara hii nyeti iangalie maslahi ya Askari, yaani mishahara, posho mbalimbali pamoja na kero ya posho ya uhamisho ili Askari hao pamoja na kazi nzito ya kulinda usalama wa Raia, basi Serikali nayo iwakumbuke kwa kuwaboreshea maslahi yao.

Jambo lingine ni suala la mafunzo pamoja vifaa vya kazi. Naomba Serikali iangalie kwa karibu mambo haya hasa wakati huu ambao nchi imekumbwa na wimbi la ujambazi hasa wa kutumia silaha za moto. Ni vyema Serikali ikatoa mafunzo pamoja na kuviboresha vitendea kazi vya kazi Askari hao ili angalau wasiweze kuzidiwa na majambazi kama ambavyo imejitokeza mara kadhaa.

Vilevile, Serikali iimarishe ulinzi katika maeneo nyeti hasa mabenki na maeneo mengine yenye kutoa huduma za kifedha ili kupunguza wimbi la watu kuingia hamu ya kuyafanya ujambazi kutokana na ulinzi haffifu unaokuwepo.

Naendelea kuishauri Serikali kwamba, hivi sasa majambazi wamekuwa wakitafuta maeneo yenye udhaifu (*soft targets*) wa kiulinzi kama vile Visiwani Zanzibar na kwenda kufanya ujambazi bila ya kuwa na hofu. Ndiyo maana ujambazi uliotokea Zanzibar umetokea kwenye maeneo matatu ndani ya siku chache, tena sehemu zote silaha za moto zimetumika. Serikali itafute mbinu za kuwanyima wahalifu nafasi ya kutekeleza unyama wao kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kama majeshi.

Pamoja na mchakato wote huo unaoendelea, Serikali iimarishe usajili wa silaha zote nchini hasa zinazomilikiwa na watu binafsi ili kuweza kutambua mtandao wa majambazi wanaotumia silaha. Silaha hizo zimetokea wapi? Hii itasaidia kuweza kuwanasa wale wote wanaoazimisha silaha za moto ili zikafanyiwe uhalifu.

Namalizia kwa kumtakia kheri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi ngumu iliyo mbele yao. Niwakumbushe kwamba Watanzania wote wanawaangalia wao zaidi katika kuimarisha ulinzi wao wa ndani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na naomba fedha zote walizoomba waidhinishiwe.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Wizara nzima kwa jinsi ambavyo wameianzisha Wizara hii na kwa mafanikio makubwa waliyoyafikia katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama sasa, hakika inaridhisha kila uchao na wananchi wanaendelea kujenga imani katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kuna haja kubwa kwa Jeshi la Polisi kujenga mahusiano na mashirikiano imara zaidi na raia. Hii itasaidia Jeshi letu la Polisi kufaidika na msaada wa wananchi na raia wema walio wengi. Wananchi hawa wanafahamu wahalifu, kwani wanaishi nao lakini kwa kuogopa ama kwa kutokuwa na uhakika wa ulinzi wao pindi watakawataja wahalifu ambaao ni jirani zao, basi huona ni heri wakajilinda kwa ukimya. Mazoea yanaonyesha kuwa siri huvuja na kuwafikia wahalifu ambaao baadaye huwafuata hawa raia wema na kutishia usalama wao.

Kwa kuwa Polisi hakika watakuwa wadadisi zaidi, kama watawashirikisha raia wema katika kupata taarifa na kuwa raia wema wanataka kuwa na uhakika na usalama wao pindi wanapotoa taarifa za majambazi na kwa kuwa simu ya Polisi huwa hajibibi mara nyingi: Je, isingekuwa vyema sasa kwa Jeshi la Polisi kuwa na anuani pepe (*E-mail address*) kwa ajili ya kutunza usiri zaidi na usalama wa watoa taarifa? Anuani pepe hii iandaliwe kwa kila Mkoa na pale pasipo na huduma ya *internet* au barua pepe katika Wilaya, basi ni vyema zaidi anuani pepe hizo zikajulikana.

Lakini pia, kwa ajili ya ufuutiliaji wa ngazi za juu na kama ilivyo desturi nzuri ya Jeshi la Polisi kutoa orodha ya komandi na simu zao, basi pia itolewe orodha ya anuani pepe (*E-mail address*) kwa kufuata komandi pia.

Suala la usalama kwa watoa taarifa kwa utaratibu huu linaweza kutumika hata na *PCB* na Taasisi nyingine zinazotegemea taarifa za raia wema.

Mheshimiwa Spika, wakati naendelea kuipongeza Wizara na Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri na inayoendelea kuboreka, napenda niwaase waliangalie kwa makini zaidi suala la wao kuhusishwa na rushwa, hasa zile rushwa ndogondogo zinazohusisha hasa Askari wa Barabarani. Kwa kweli suala hili linaendelea kutia dosari katika kazi nzuri ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Jeshi la Polisi limekua likipokea misaada ya njenzo za usafiri. Hili ni jambo jema na la kupongeza na kusisitiza kwa walio tayari kuendelea kufanya hivyo. Lakini pia Jeshi nalo litumie vyema nyenzo hizi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kujenga upya Jeshi hili na kuboresha utendaji wao, suala la kuwapatia sare mpya na *friendly* sasa pia ni muhumu sana.

Mheshimiwa Spika, ukiingia katika maduka ya *Shorprite* utawaona walinzi walivyo nadhifu, wanapendeza na pia unajihisi kuwaamini, hofu inakutoka kabisa kwamba wako pale kwa ajili ya usalama wako.

Jambo hili linaendelea kujenga imani na mahusiano ya kuaminiana baina ya wananchi na Polisi waliovaa sare nzuri na za kupendeza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawapongeza kwa kazi nzuri ya Usalama wa Raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara hii ya Usalama wa Raia kwamba, katika juhudi za kuimarisha Ulinzi na Usalama maeneo ya Vijijini, liimarishwe zaidi Jeshi la Sungusungu. Wapo Viongozi wengi na Sungusungu wametiwa ndani kutokana na matatizo wakipambana na wahalifu. Naomba Serikali ifute kesi zao maana zimekuwa na muda mrefu mno.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nzega ni kubwa na kwa kweli inahitaji uhakika wa usafiri. Naomba Kituo cha Polisi kiongezewe gari na Kituo cha Polisi Puge kipewe gari au pikipiki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jengo la Magereza na Mahabusu la Nzega kuwa dogo, nashauri ijengwe sero hapo katika Kituo cha Polisi.

Nawatakia kazi njema.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

Aidha, napenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kizalendo linaloifanya katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa ya amani na utulivu.

Naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii ilioletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba upokee shukrani za dhati kwa utendaji mzuri wa Ndugu zetu wa Polisi. Kwa kweli imeonyesha wazi kuwa wameweza kubadilika na kufanya wananchi warudishe imani kwao. Tunajua binadamu hakamiliki. Naamini wataendelea kufanya kazi zao kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya ili kuendana na awamu hii. Lakini tu sio hivyo, pia kwa kuona jitihada ya Serikali kutambua matatizo yao kuunda Wizara na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninayo mambo mawili. Kwanza kuhusu mtu kubambikizwa kosa, wewe unayebambikwa unapata usumbufu na hatimaye unaonekana huna hatia, kinachofuata unatakiwa kama unataka ufungue mashtaka dhidi ya aliyekuonea. Sasa mimi naona huo ni usumbufu mwengine. Kwa nini basi nchi kwa maana ya Polisi hawachukui nafasi ya kufanya hivyo? Kwani, wao pia wamesumbuliwa, wamepotezewa muda wao na hata kutumia vifaa ambavyo imebidi watumie wakati wa kuendesha kesi. Hii ingesaidia watu kuacha kutumia vibaya Polisi wetu kwa kuwa anayefika kwanza Kituoni ndiye anayesikilizwa.

Pili, napenda kuuliza, kwa nini Polisi huwa wanapangiwa zamu za kuwepo Vituoni na Mitaani hadi usiku? Lakini *traffic* ikifika usiku, wanakuwa hawako

barabarani kwa utaratibu unaofanana na wenzao. Mimi nadhani usiku ndiyo wakati mbaya kwani wanaweza kuwepo madereva walevi, wasio na leseni na pia magari mabovu ndiyo mwanya wao wa kutembea.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoanza kusema, sina mengi kwani mengi yamesemwa juu ya makazi ya Polisi, inaeleweka na tunashukuru hatua zinachulikuwa.

Narudia kuwapongeza na kutegemea hoja zangu zitajibowi wakati wa majumuisho ya Mheshimiwa Waziri. Naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa hotuba yako nzuri yenye ufanuzi wa kina hususan Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nitazungumzia kuhusu Jeshi la Polisi. Napenda kumpongeza *Inspector General* wa Polisi, Kamishna Said Mwema na Maofisa wengine wa Polisi kwa kazi nzuri ya kudhibiti hali ya uhalifu hapa nchini.

Pili, nampongeza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Ndugu Mganga na *Ma-OCD* wote wa Mpwapwa, Dodoma Vijijini, Dodoma Mjini, Kondoa na Kongwa kwa kazi nzuri ya kupambana na uhalifu katika Mkoa na Wilaya zote. Hivi sasa hali ya Ulinzi na Usalama imekuwa nzuri pamoja na kwamba yapo matukio madogo madogo ya hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma linajitahidi kudhibiti ujambazi wa kutumia silaha, utekaji wa magari. Tatizo kubwa ni kukosa vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa kama vile magari, pikipiki na *radio calls*.

Nashauri vitendea kazi viboreshwe katika Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma na Vituo vyote vya Polisi hapa nchini pia wananchi waelimishwe kwamba suala la Ulinzi na Usalama ni la kila mwananchi sio la Jeshi la Polisi na Mgambo.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kwamba Maslahi ya Jeshi la Polisi/Askari Polisi yaboreshwe kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana usiku na mchana.

Pia, Askari Polisi wajengewe nyumba wasikae vibandani. Nyumba za Askari Polisi Mpwapwa zifanyiwe ukarabati kwani, zimechakaa sana.

Vile vile, ajira ya Askari Polisi iangaliwe upya ili kuchukua vijana waaminifu na mafunzo ya Askari Polisi yaboreshwe na hasa katika karne hii ya 21 ya Sayansi na Teknolojia, wafundishwe mbinu za kisasa za kupambana na uhalifu nchini na idadi ya Polisi wanafunzi iongezwe Chuo cha Polisi Moshi ili kuongeza idadi ya Askari Polisi hapa nchini.

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga Chuo cha Upelelezi hapa Dodoma: Je, ujenzi huo utaanza na kukamilika lini? Ujenzi wa Chuo hicho utasaidia kupata Maafisa Upelelezi wengi watakaoharakisha upelelezi wa kesi na kupunguza msongamano wa mahabusu Magerezani.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba magari mabovu yasiruhusiwe na mabasi yasiruhusiwe kusafiri usiku ili kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia kwa kazi nzuri zinazofanywa na Jeshi la Polisi katika kupambana na ujambazi na aina nyininge za uhalifu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya muundo wa Jeshi hilo uliofanywa na Serikali unaelekea kulipa Jeshi hilo nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linakabiliwa na tatizo kubwa sana la makazi ya Askari. Askari wengi wanaishi nje ya maeneo yao na wale wanaoishi kwenye maeneo yao, wanaishi katika mazingira magumu sana. Baadhi wamelazimika kujijengea vibanda vya tope. Hatuwezi kuwategemea Askari wa Polisi watufanyie kazi nzuri wakitokea kwenye mazingira hayo mabaya sana na ambayo hayastahili kwa maisha ya binadamu. Hali ni mbaya zaidi kwa Askari wenyе familia. Wakati sasa umefika kwa Serikali kuchukua hatua madhubuti kuwajengea Askari wa Jeshi la Polisi *barracks* zenyе hadhi na zinazokidhi masharti ya majengo ya kushi binadamu. Kazi hiyo ni sharti ianze mwaka huu na iendelezwe kwa kasi kubwa katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili linahusu ajali za barabarani ambazo zinaua Watanzania wengi na husababisha uharibifu mkubwa wa mali kila mwaka na kwa hiyo, kuliingizia Taifa hasara kubwa sana kila mwaka. Naamini kwamba nyingi ya ajali za barabarani zinazotokea zinafurika na Jeshi la Polisi lingeweza kuzuia nyingi ya ajali hizo. Madereva wengi hawajapata mafunzo ya kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kutosha wa kuendesha magari kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam madereva wengi wa daladala hawana leseni za udereva na waongoza kwa kusababisha ajali za barabarani. Askari wa Polisi wanashindwa nini kufanya ukaguzi wa leseni wa kushtukiza na wa mara kwa mara? Kutokudhibiti uendeshaji wa magari, Polisi wanachangia kuendeleza kuwapo kwa ajali za barabarani.

Tabia za madereva kuendesha magari wakiwa wamelewa ni chanzo kingine cha ajali. Polisi wakiahidi kuwapima madereva ili kuwabaini walevi na kuwaondoa barabarani na kuwachukulia hatua za Sheria. Ahadi hiyo imeishia wapi?

Chanzo kingine cha ajali ni ubovu wa magari yanayoendeshwa kwenye barabara zetu. Mengi ya magari hoyo hayana breki, mengine yana matairi yaliyokwisha na kadhalika.

Pamoja na Ukaguzi wa leseni za udereva, Polisi wanapaswa kukagua magari kuhakikisha kwamba yana ubora wa kuyawezesha kutumiwa barabarani kwa usalama na bila kuchafua mazingira. Wapo Askari wengi wa trafiki, lakini vitendo vyta uvunjaji wa Sheria za barabara vinaendelea bila kudhibitiwa. Wakati umefika kwa Polisi kupambana na ajali za barabarani kwa ujasiri ule ule waliotumia kupambana na ujambazi.

Mheshimiwa Spika, mwendo wa kasi na tabia ya madereva wa magari makubwa kupendelea kusafiri usiku na tabia nyingi zinazochangia wingi wa ajali za barabarani, mambo yote haya yakidhibitiwa ajali za barabarani zitapungua sana na kupunguza hasara zinazotokana na ajali hizo. Jeshi la Polisi lina nafasi kubwa katika kupunguza ajali za barabarani iwapo watatimiza wajibu.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, Kwanza, natoa pongozi kwa Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia kwa hotuba yake na pia kwa uteuzi wake, hususan nampongeza *IGP* na Idara nzima kwa kazi kubwa inayoonekana licha ya matatizo makubwa ya uhalifu ambayo yamejitokeza hivi karibuni.

Pili, mimi naunga mkono hoja ya Wizara hii mpya. Ila jambo moja tu naomba uamuzi wa Mheshimiwa Waziri. Katika Kata yangu ya Kalenga haina Kituo cha Polisi katika Makao yake Makuu. Kituo kiko Ipamba au Tosamaganga ambapo Makao Makuu yako Kalenga ambayo inapakanana na Makao Makuu ya Kata nyingine ya Ulanda. Ukaribu wa Makao ya Kata hizi mbili ina maana kwamba Kituo cha Kalenga kingehudumia Ulanda pia na kwa hiyo, kuua ndege wawili kwa jiwe moja.

Mheshimiwa Spika, Huko nyuma tulikuwa tumethibitisha kuwa Ofisi na angalau nyumba mbili zingepatikana kwa huduma hiyo. Wakati huo huo uhalifu mkubwa, hasa mauaji umekuwa ukitokea kila mara na mara nyingi imekuwa vigumu kuwafikisha wananchi katika vyombo vy a sheria kwa upungufu wa ushahidi.

Mheshimiwa Spika, nimeomba Idara ya Polisi itazame uwezekano wa kuhamisha Kituo kilichopo Ihamba na kukipeleka Kalanga ili kihudumie Kata hizo mbili pamoja na Kata ya Nzili iliyopo jirani. Naahidi ushirikiano wangu.

Mwisho, naunga mkono hoja hii na kwa kweli naitakia Wizara mafaniko yote.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba Kituo cha Polisi Kibaigwa kifunguliwe, yaani pawekwe mawasiliano ya hakika, pajengwe nyumba za Askari na gari ya *patrol* iwe *stationed* pale.

Mheshimiwa Spika, majambazi waligeuza Kibaigwa kichaka chao, fyekeni au chomeni moto hicho kichaka.

Mheshimiwa Spika, napongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri na mabadiliko ya uongozi ngazi ya Wilaya ya Kongwa pia, tunashukuru kwa gari jipya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itafute tiba ya rushwa kwa *Traffic*. Askari hawa ni sugu kwa rushwa ndogo ndogo barabarani.

Wananchi wa Kongwa wako tayari kuanzisha ujenzi wa Vituo vya Polisi Mlali, Pandambili na Songambel. Tunaomba utaratibu na ramani. Hili linatokana na *SACCOS* za maeneo hayo kuporwa na kulipuliwa na majambazi.

Mheshimiwa Spika, kisingizio cha gari la Polisi Kongwa kukosa mafuta (*diesel*) wanaporipotiwa mambo/matukio litazamwe. Je, ni Bajeti ndogo kweli? Kama hivyo ndivyo, utaratibu uliopo wa kuchangisha wanavijiji kwenye tukio ili kupata Sh. 50,000/= ni sawa? Tunaomba, kama ni hivyo wanavijiji wapewe risiti halali.

**SPIKA:** Ahsante, hapo ndio mwisho wa wachangiaji kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo sasa kwa kujibu hoja mbalimbali za Wabunge naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed aanze kujibu kwa dakika 15, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtoha hoja, Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Mwapachu, pale saa 11:30, hadi saa 12:30. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Aidha, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa wazima na afya na kukutana hapa jioni hii. Kabla ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wetu. Pia, nitumie fursa hii kumpongeza kwa kuteulewa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Nitoe pongezi maalum kwa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Aman Karume na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kushika nafasi za juu za uongozi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeze wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge letu hili. Aidha, pongezi maalum ziende kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa kwao kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya familia yangu na kwa niaba ya Wana-CCM wa Kisiwa cha Pemba, napenda nimshukuru sana, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunichagua kuwa Mbunge na hatimaye kunichagua kuwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia. Nataka nimhakikishie yeye Mheshimiwa Rais, Viongozi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba heshima hiyo tutaienzi na tutafanya kazi kama ambavyo yeye anavyotaka tufanye.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuishukuru sana familia yangu, hususan mke wangu, watoto wangu na ndugu zangu kwa kunisaidia sana kwa kunipa moyo katika kutekeleza majukumu yangu. Shukrani maalum ziende kwa Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Harith Mwapachu, ambaye sio tu amenipa ushirikiano makubwa, malezi mazuri na maelekezo katika utendeji wa kazi, lakini kwa ukarimu mkubwa alionao kwetu sisi sote Watendaji wa Wizara hii. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu kwa namna ambavyo wanatusaidia kwa michango mbalimbali, ushauri na maelekezo yao kwa nia njema ya kutekeleza wajibu wetu vizuri. Napenda niwashukuru sana.

Aidha, niwashukuru zaidi wale wote waliochangia kwa maneno hapa mbele na wale waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia katika hotuba za awali za Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na wa Mipango. Wote tunawachukuru sana kwa michango yao mizuri na kwa kweli siku zote michango yao inakuwa dira kwetu ya kufanya kazi zetu.

Siri ya mafanikio yetu ambayo wengi mmetupongeza, yanatokana na michango yenu na maelekezo yenu. Nataka niwahakikishie kwamba sasa tunaichukua michango hiyo kwa kuifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa leo hapa na hasa hasa juu ya hali halisi ya uhalifu na ujambazi nchini, maslahi ya Askari wetu, makazi ya Vituo na Polisi, upungufu na vitendea kazi, Kikosi cha Usalama barabarani, ajali za barabarani, usumbufu wa raia kwa Askri wetu, utaratibu wa ajira na kupanda vyeo katika Jeshi la Polisi, suala zima la pensheni na kiinua mgongo, ulinzi hafifu wa mipakani, madawa ya kulevya na hasa hasa suala la ujambazi katika maziwa na bahari.

Mheshimiwa Spika, ningependa niwahakikishie kwamba Serikali yetu kupitia Jeshi la Polishi, limejitahidi sana kuchukua hatua mbalimbali ya kukabiliana na matatizo haya. Lakini kama mnavyojua, mwanzo mgumu. Hapa ndipo tulipoanzia, nataka niwahakikishie kwamba tutaendelea kufanya vizuri zaidi ya hapo ambapo tumefanya.

Hivi sasa tuna mpango wa miaka kumi, kuanzia mwaka 2003 mpaka 2013. Nia yetu ni kuboresha Jeshi la Polisi kwa kupitia mipango mbalimbali, kwanza katika ujenzi na ukarabati wa nyumba za Askari, ununuzi wa magari, ununuzi wa vifaa vya mawasiliano, vifaa vya upelelezi, ununuzi wa mashua za doria, vifaa vya usalama barabarani, ujenzi na ukarabati wa Ofisi, kuanzisha Maabara ya Uchunguzi na kadhalika. Yote haya nia yetu ni kuyatekeleza.

Lakini kama mnavyojua, hali halisi ya uchumi wa nchi yetu, kwa hiyo, kwa vyovoyote vile, tutakwenda hatua kwa hatua, tumeanza pia mazungumzo na nchi rafiki na

Wahisani wetu kwa nia njema kabisa ili tuweze kufanikisha juhudhi hizi, tuweze kutekeleza wajibu wetu vizuri kwa wananchi. Tunaomba subira yenu Waheshimiwa Wabunge ili tushirikiane tufanye kazi kwa ukamilifu zaidi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naamini Waziri wangu ataaeleza mengi kwa kina na kutoa ufanuzi hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Mimi inanibidi nizungumzie kijumla jumla kutokana na muda. Kwa upande hasa hasa ambao uliwagusa sana Waheshimiwa Wabunge katika maeneo ya ziwa, ni kweli tatizo la ujambazi katika maziwa lipo na limeathiri sana wananchi wa maeneo hayo.

Kuna ujambazi wa kutumia silaha katika maziwa, kuna uvuvi haramu unaofanyika katika maziwa, kuna masuala ya uporaji katika maziwa, kuna masuala ya magendo katika maziwa na mengine mengi ambayo yanaathiri sana shughuli za uvuvi na shughuli nyingine katika maziwa.

Jeshi la Polisi limejjipanga vizuri kwenye suala hilo, japo bado ni tatazo kubwa, lakini ninawahakikishia wananchi wanaishi katika maeneo ya maziwa kwamba tutafanya kila jitihada kupunguza tatizo hilo na ikiwezekana kulimaliza kabisa. Hivi sasa tuna-operation ya pamoja baina yetu na vyombo vya dola na kazi imenza kufanyika vizuri. Lakini nataka niwahakikishie kwamba tutazidisha *speed* yetu, hivi sasa tuko katika suala zima la ukarabati wa vyombo mbalimbali vya baharini hasa zile boti za kwenye maziwa. Tunategemea kutumia zaidi ya bilioni 1.5 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa mwisho wa boti zetu hizi na mara zitakapokuwa zote zimekamilika, basi kazi itafanyika vizuri.

Najua matatizo yanayowakuta katika maeneo hayo, lakini nia yetu ni kuhakikisha tunayaondoa matatizo haya. Aidha, tunafanya kila jitihada kukibadilisha chombo chenyewe cha Jeshi la Wanamaji ili kukijenga vizuri kiuongozi na kufanya mabadiliko makubwa ndani ya Kikosi hicho ili kiweze kufanya kazi zake vizuri zaidi. Naamini, nipe ni muda, tutaona matokeo ya shughuli ambayo tumekusudia kuifanya. Ni shughuli ngumu, lakini nawahakikishieni kwamba tutafanya jitihada hizo.

Tuna nia pia, tukipata uwezo, katika kipindi hiki cha Bajeti hatukuweza kufanikiwa, lakini nia yetu ni kununua boti mpya kumi na tatu. Saba kwenye maziwa na sita kwa ajili ya matumizi ya baharini.

Naomba mfahamu kwamba boti moja ya kwenye ziwa tunahitaji ya Shilingi bilioni tano. Kwa hiyo, kama mnavyojua, hali yetu ni ngumu kwa wakati huu na boti zile za baharini kila boti moja ni Shilingi bilioni kumi. Kwa hiyo, nalo ni tatizo.

Aidha, tuliona umuhimu wa kuwa na helkopta ili kuwahi yanapotokea mambo mbalimbali, lakini tatizo ni hilo ninalolisema la kifedha na helkopta moja inahitaji sio chini ya Shilingi bilioni nane. Kwa hiyo, hali yetu halisi kwa wakati huu ni ngumu, lakini nitaendelea kuzungumza na Serikali tuone kila uwezekano utakaofanyika kwa nia ile ile ya kuwashudumia wananchi. Kuhusuana na suala la Vituo, katika kipindi hiki cha mwaka 2006/2007 tunatarajia kuviendeaza vile vituo ambavyo tumevianzisha.

Hali ni hiyo hiyo, tumetengewa fedha jumla ya Shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya kuvikarabati na kuvimalizia vile ambavyo tumeshavianza. Vituo vyenyewe ambavyo kwa mwaka huu vitapata fursa hiyo ni kama hivi vifuatavyo:-

Kwanza ujenzi wa Kituo cha Mfikiwa tutaendelea nao, *FFU* Finya, Tunguu Zanzibar, Uguja Ukuu, Chuo cha Polisi Zanzibar na kujenga nyumba ya Mkuu wa Polisi Kaskazini Uguja,tutaendelea nao. Kwa upande wa Bara tutaendelea kukamilisha Kituo cha Mwanga, Chamwino, Magu, Tabora, Iringa, Mwanza Sitakishari, Morogoro, Namtumbo, Kondoaa, Mpanda Kunduchi, Kateshi, Babati na Kanda maalum ya Dar es Salaam. Vile vile, katika maeneo mengine tutajitahidi kufanya ukarabati mdogo kwa vile vituo ambavyo sikuvitaja, lakini iko *portion* ambayo tutaitumia kwa kazi hiyo. Tunawaombeni sana subira yenu.

Lipo tatizo la ma-*OCD* na jambo hili limetajwa sana na kadri tunavyopeleka *OCD* mahali, sio *OCD* peke yake kunahitajika makazi, Askari wawepo wa kufanya kazi. Kwa hiyo, nalo ni tatizo sugu, lakini tunalijua umuhimu wake na tumo katika kulipangia mkakati tuone ni namna gani tunaweza kulitatta katika eneo hilo. Pia liko suala ambalo lilizungumzwa sana suala bakshishi na suala la pensheni. Jambo hili liliguswa sana na Wabunge wengi, naamini kwamba uamuvi huu maisha huwa ni chaguo la Askari mwenyewe anapolitumikia Jeshi kwa miaka 12. Tumeliona tatizo hilo ndani ya Jeshi na hivi sasa tunafanya utaratibu ili tuwe na utaratibu mmoja tu wa pensheni ili tuondokane na malalamiko haya yanayojitikeza.

Waheshimiwa Wabunge, lakini lazima tuelewane vizuri kwamba ule uchaguzi wa awali ulikuwa ni wao na Askari ye yote lazima aijue vizuri *PGO*. Kwa hiyo, aijue lipi lina maslahi kwake na lipi halina maslahi kwake. Kwa hiyo, kilichotokea hapo nyuma, kwa vyovyyote vile, nawaombeni sana tusameheane. Kilichobakia sasa tutazame ya mbele ili tufanye kazi yetu vizuri. Ili nisije nikagongewa kengele ya pili, kwa heshima na taadhima nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono hoja hii tuipitishe ili mtupe nafasi ya kwenda kufanya kazi vizuri. Nawahakikishia mtaona namna tutakavyoweza kufanya kazi hiyo. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa kunipa nafasi hii ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kabla ya kujibu hoja, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri na yenye manufaa waliyitoa kwa kuzungumza na kwa kutuandikia. Michango hiyo imetusaidia sana na itatusaidia sana katika utendeji wetu, kwani michango yote ni mizuri yenye nia ya kuboresha utendaji kazi, sio tu kwa upande wa Wizara, lakini zaidi kwa upande wa Jeshi hili la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kipekee kabisa niishukuru sana Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa juhudii zao kubwa wanazochukua bila kuchoka ili kuhakikisha kwamba Wizara yangu na Jeshi la Polisi linapatiwa vitendeja kazi vyakutosha na kuboresha maslahi na mazingira yao katika utendaji kazi wao na ipo mifano mingi ya juhudii zao, lakini muda kwa kweli hautoshi kuweza kutaja yote.

Namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Wilam Kusila na Makamu wake, Mheshimiwa Kepteni Mstaafu, George Mkuchika na Wajumbe wote kwa michango, mawazo na ushauri wao wanaotupa bila kuchoka na napenda kuchukua fursa hii kuwathibitishia kuwa tunazithamini na kuzienzi juhudhi hizo. Kuna mambo kadhaa ambayo wamezungumzia katika taarifa:-

- (i) Kuunda Kitengo Maalum cha Ulinzi wa vyombo vyatofu;
- (ii) Wameshauri kwamba Benki na vyombo vyatofu vikamilishe kanuni za ulinzi;
- (iii) Kuongeza ajira mpya za Askari;
- (iv) Kuajiri wahitimu wa Elimu ya Juu wenye taaluma mbalimbali;
- (v) Kuajiri vijana wanaohitimu kutoka kwenye Jeshi la kujenga Taifa;
- (vi) Kushirikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kujenga makazi ya Askari.
- (vii) Kuongeza boti za kufanya doria.
- (viii) Kufanya Vikao vyatofu ujirani mwema mara kwa mara.
- (ix) Kuendeleza *operation* maalum za Jeshi kwa ushirikiano na nchi jirani.
- (x) Kufanya *operation* ya kumaliza tatizo la mauaji ya imani za kishirikina na
- (xi) Kuchukua hatua za kukomesha tatizo la mapigano baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, nasema haya yote tumeyapokea na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara yangu, kwa michango mizuri aliyoitao. Michango yao pia tunaithamini na tutaifanya kazi kikamilifu, kwani jukumu la ulinzi na usalama si suala la itikadi, ni jukumu la kila mmoja wetu katika kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea kuwa ya amani na utulivu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kama sote tujuavyo, Wizara hii bado ni mpya, yenye takriban miezi sita tu tangu kuundwa hivyo, tunahitaji sana mawazo, ushauri, maoni na mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wadau mbalimbali, hasa kwenu Waheshimiwa Wabunge, ambao ndio wawakilishi wa wananchi. Kama nilivyosema hapo awali, tunathamini sana maoni na ushauri wenu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, waliochangia wakati wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Michango yao ilikuwa ni mizuri, tunaithamini sana na ningependa kuwahakikishia wale wote ambao walichangia katika hotuba hizo kwamba, tumepokea hoja zao na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, ambaye amejitahidi sana kujibu hoja mbalimbali kwa ujumla. Namshukuru sana kwa kazi hiyo nzuri, aliyofanya kwa umakini na ustadi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza hapo awali, kwa kweli itakuwa ni vigumu kuweza kujibu hoja zote ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Nitajaribu kwa jinsi nitakavyoweza kuweza kujibu hoja hizo, lakini kama nitashindwa kuzijibu hapa, ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutazifanyia kazi na tutajibu hoja hizo kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kulikuwa na hoja kutoka Kambi ya Upinzani. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, alikuwa na hoja mbalimbali, nitazungumzia baadhi ya hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa inahu maduhuli ya Serikali, yasiyokusanya yenye thamani ya shilingi 2,708,091,960. Kushindwa kwa sisi kukusanya maduhuli haya ni kutokana na *performance* mbaya ya mashirika yenyewe; TAZARA, TPDC na TRC. Lakini nasema kwamba, baadhi ya maduhuli hayo, yamekwisha fanyiwa kazi na sasa hivi yamekwisha ondolewa katika vitabu vyetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni upotetu wa shilingi 2,913,644,926, hizi zilikuwa *dishonored*, lakini baada ya kuzungumza na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, sasa hivi takwimu hizo haziko katika vitabu vyetu.

Mheshimiwa Spika, pia Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, alizungumzia malipo ya shilingi 176,947,000, hoja za kiasi cha shilingi shilingi 173,363,000 zimehakikiwa na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na hoja husika imekwishafungwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, alizungumzia watumishi wasiochukua mishahara yao na fedha ambazo zilitajwa hapa zilikuwa shilingi 500,636,412, hizi pesa hazikupotea, ni kwamba, baadhi ya watu wameshindwa kuja kuchukua hizo pesa, wengine wamefariki. Kwa hiyo, hizi pesa zimerudishwa katika Wizara ya Fedha, hazikupotea.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Upinzani pia amezungumzia malipo yasiyokuwa na fidia ya Serikali kiasi cha shilingi 999,211,685. Baada ya kupitia vitabu vyetu, pesa

hizi zimekwisha futwa katika vitabu vyetu. Nadhani kwa upande wa hesabu za Wizara na Jeshi la Polisi, hayo yalikuwa ndiyo masuala makubwa.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ambayo alizungumzia Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, ni uduni wa askari. Nadhani Naibu Waziri, ameyazungumzia vizuri na pia katika hotuba yangu, masuala haya tumekwisha yazungumzia kwamba, kutakuwa na Tume ambayo itashughulikia masuala hayo na kwamba, askari watapewa mishahara mizuri na wataongezewa posho. Kwa hiyo, tusubiri mpaka wakati huo.

Mheshimiwa Spika, sasa, baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa na Kambi ya Upinzani, nasema ili kuweza kuokoa muda, basi hayo tutayafanyia kazi na kuweza kuyajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, ni vizuri nikawatambua Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza kuititia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa waliochangia ni Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Dr. George H. Mwakyembe, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Jacob D. Shibili, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Mohamed Juma Habib Mnyaa, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyakwa, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Juma Said Omar na Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni wafuataao: Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Aziza S. Ali, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Bernard K. Membe, Mheshimiwa Brig. Gen. Hasasan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Dr. Samwel J. Malecela, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka,

Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Herbert J. Mtangi na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Juma Suleiman Nhu'nga, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Luca L. Selelii, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Magadalena H. Sakaya, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Omary Ali Mzee na Mheshimiwa Paul P. Kimiti.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Sigfrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Mohamed Rajab Sudi na Mheshimiwa John M. Shibuda. (*Makofii*)

Mhehimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Haji Juma Haji, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Abdallah S. Sumry, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza, nimesema wachangiaji wamekuwa wengi, nitajaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, nyangi ya hoja hizi zinafanana.

Kwanza, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbii, amezungumzia mambo kadhaa, nasema mengi ya haya yanajirudia rudia, kwa hiyo, tutafanya utaratibu wa kuweza kuyajibu kimaandishi. Lakini mambo makubwa ambayo yamejitokeza ni uhusiano mbaya kati ya askari na raia wa Pemba. Sasa hivi nasema tu kwamba, utaratibu wa uanzishaji wa Polisi Kata, unaendelea kutekelezwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na *IGP*, tumetembelea mikoa mbalimbali tukizungumza masuala haya haya ya Polisi Jamii (*Community Police*). Kwa hiyo, ni mategemeo yetu kwamba, baada ya muda si mrefu, kwa kweli hii *concept* ikianza kuenea hapa nchini, tutaweza kudumisha uhusiano baina ya askari pamoja na raia. Kwa hiyo, katika kila Kata tutakuwa na Askari Kata, ambao watakuwa wanashirikiana na askari wenyewe katika masuala ya doria katika kupanga jinsi ya kupambana na uhalifu katika maeneo yao. Kwa hiyo, ni mategemeo yetu kwamba, kwa kufanya hivyo, basi askari hao watakuwa karibu sana na askari wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Idd M. Azzan, amezungumzia juu ya uonevu nje ya maadili ya kazi kama katika Vituo vya Msimbazi, wafanyabiashara kukamatwa ama kupendelewa dhidi ya raia ambao ni wanyonge. Amezungumzia kwamba, kuna matatizo kama hayo katika maeneo ya Kinondoni. Pia amesema kwamba, Kituo cha Magomeni kuwa kidogo, haffi na kwamba ni cha muda mrefu. Nasema haya yote tutayafanya kazi, siyo pengine katika kipindi cha mwaka huu, lakini yatakuwa katika programu yetu ya mwaka 2005 – 2010. Amezungumzia pia kuhusu Kituo cha Kijitonyama kuwa, hakuna nyumba za askari. Hili ni tatizo tulilonalo nchini kote, lakini kama alivyozungumza Naibu Waziri kwamba, tuna mpango wa kujenga Kambi kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya fedha hapa nchini, ikiwa ni pamoja na *Contractors* na mabenki kutoka nje ya nchi, kwa kuanzia tutaanza na Zanzibar pamoja na Dar es salaam. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tuvute subira kuhusu suala hili, lakini mipango madhubuti kwa kweli ipo na tunaiandaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hizi *Night Clubs* bubu kuondolewa, nasema suala hili tutalifanya kazi pamoja na wenzetu wa TAMISEMI, kuona vipi tunaweza kulitatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ali Juma Haji, amezungumzia utaratibu wa bahashishi (*Gratuity and Pension*). Nadhani suala hili nimelizungumzia vizuri katika hotuba yangu, pamoja Naibu Waziri amelizungumzia hili sasa hivi. Kwa hiyo, ni suala ambalo tutalifanya kazi, lakini mwelekeo wetu kwa kweli ni kwamba, lazima tuwe na utaratibu mmoja wa *pension*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fatuma Othman Haji, amezungumzia kwamba, askari wanaoumia kazini na kuuawa wote wana haki ya kibinadamu na vyombo vyahabari vikemee hali hiyo. Nadhani suala hili linaleweka na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hospitali ya Polisi Ziwanu kuwa haina dawa na askari wastaafu wanasmubuka kupata mafao yao, nasema haya yote tutayafanya kazi na kuweza kumjulisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abdallah S. Sumry, alizungumzia vijana wa Tundu, Senga, Kisiwani, Feruzi, Gabesi na Pima, waliotekwa nyara na fedha zao kupelekwa upande wa pili wa Ziwa na hawajaonekana hadi leo, eneo hilo halina Serikali. Tumepokea taarifa hiyo na suala hili tutalifanyia kazi, tutalifuatilia.

Mheshimiwa Gosbert B. Blandes amezungumzia uhaba wa vitendea kazi. Tatizo hili tunalifahamu na tutalifanyia kazi. Maslahi ya Polisi yaboreshwe, tunakubali hilo tutaendelea kuliboresha. Elimu ya Sekondari kwa Aaskari Polisi, nalo pia tumelizingatia na tutaliendeleza. Kuhusu Kituo cha Polisi katika Pori la Kimisi, ushauri huo tumeupokea na tutaufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, amezungumzia kuhusu maslahi ya askari, tutaendelea kuyaboresha kwa mujibu wa taratibu zetu na ikiwabajeti yenye we itakuwa inatosheleza. Amezungumzia juu ya upelelezi kuwa utendaji wake ni duni, nadhani katika *Legal Sector Reform Program*, suala hilo limezingatiwa. Kwa hiyo, kwa kushirikiana sio tu na sisi, lakini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Magereza, pamoja na Mahakama, ikiwa ni pamoja na suala la kusukuma mashauri katika Mahakama zetu, hayo yote tumeyazingatia na tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi. Orodha ni ndefu sana, lakini nitajaribu kwa haraka haraka kuweza kuzitaja hoja hizo na tunasema nini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, amezungumzia kitendo cha Polisi kuzuia magari hasa malori na kudai rushwa. Kwanza, tunatazama huu utaratibu wa kuwa na *Road Blocks*. Nadhani katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha, ziko *Road Blocks* nyingi. Tutaangalia suala hili na kama pia tunaweza kuliweka katika Muswada, kwa sababu nchi nyingine kama Afrika Kusini, sasa hivi katika *Police Act*, suala la kuweka *Road Blocks* ni lazima kuwe kuna afisa maalum, ambaye anatoa idhini. Kwa hiyo na sisi itabidi kwa kweli tutazame zina utaratibu gani kwa sababu zimekuwa kwa kweli ni kero na hasa kwa wafanyabishara, wanasimamishwa simamishwa mara nyingi na hao ndio wanaochangia kwa kiwango kikubwa Pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, alizungumzia mafao tofauti ya bahashishi na *pension*, hili suala tumesha lizungumzia, tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, amezungumzia suala la nyumba. Nasema programu ipo, ni kiasi cha kupata hizo pesa na kuendelea na shughuli hiyo kujenga makambi ya askari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa Askari Polisi, Wizara inaandaa Sera ya Ajira. Kwa hiyo, baada ya muda si mrefu, *IGP* atakuwa amekuja na mapendekezo ya jinsi gani tunaweza kuboresha utaratibu wa ajira katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jacob D. Shibili, amehitaji *OCD Misungwi*. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri, Wilaya nyingi hazina *OCDs* wa kutosha, tuna upungufu wa Maofisa hawa. Lakini tutafanya kila jitihada, kuweza kufanya *Crush Program* ya mafunzo ili tuweze kupata idadi ya kutosha ya maofisa hawa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, amezungumzia uboreshaji wa vitendea kazi, hasa upande wa magari. Nasema katika mwaka huu wa fedha, tutanunua magari 70 kwa vituo vyetu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Wilaya. Lakini kwa kweli mahitaji yetu halisi, kwa jinsi ambavyo sisi tulikuwa tumejipangia, tuna upungufu wa magari 933. Kwa hiyo, jinsi bajeti inavyokuwa kubwa zaidi, basi masuala haya tutaweza kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, pia amezungumzia kwamba, tunahitaji kuwa na helikopta na redio za mawasiliano. Nasema hivi vitendea kazi vyote tunavihitaji. Sasa hivi tuna helikopta moja kubwa na moja ndogo. Tulikuwa tunategemea kwamba, tungeweza kupata helikopta nyingine mbili ikiwa ni pamoja na hizi boti za doria. Boti moja ya doria sasa hivi ni shilingi bilioni kumi. Kwa hiyo, kama unahitaji boti kama mbili au tatu, unazungumzia shilingi bilioni 30 au shilingi bilioni 40. Kwa hiyo, kila itakaporuhusu bajeti yetu, tutafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George M. Lubeleje, amezungumzia ukosefu wa vitendea kazi. Nasema kila tunapopata fedha za kutosha, basi tutaboresha hali hiyo. Pia amezungumzia kuboresha maslahi ya askari, nasema kwa mwaka 2006/2007, zimetengwa shilingi 52,529,327,500, ukilinganisha na pesa za mwaka uliopita zilikuwa ni shilingi 35,322,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mishahara na marupuru ya askari inaendelea kuongezeka kila inapostahili. Kwa hivi sasa tumeshaongeza, kama hotuba yangu inavyosomeka kwamba, posho za askari zimepandishwa kutoka shilingi 28,000 hadi kufikia shilingi 50,000 katika kipindi hiki cha 2005/2006. Kwa hiyo, nia ya Serikali, Wizara na Jeshi la Polisi lenyewe, iko pale pale, kujaribu kuboresha maslahi ya askari wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha mafunzo, nasema hili tumelipokea na Chuo hiki cha Upelelezi cha Dodoma, tumekitengea pesa na tutaanza kukifanyia kazi katika kipindi hiki cha fedha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, alizungumzia ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Kata ya Kalenga. Nasema wakati wa kujenga Kituo cha Polisi Kalenga kwa sasa hivi bado haujafika. Nadhani kwa mwaka ujao, tutaweza kufanya

hivyo. Sasa, hivi katika Wilaya 24, bado hatujawa na *Police Stations*. Kwa hiyo, kufikiria kwamba, unaweza ukajenga tena vituo katika Kata kwa wakati huu, kwa kweli inakuwa ni vigumu. Lakini nasema kwa mwaka ujao wa fedha, pengine tutakuwa na mikakati mizuri zaidi ya kuhakikisha siyo tu kwamba, *Police Stations* katika Wilaya zinajengwa, lakini hata *Police Posts*, mahali ambapo panastahili kujengwa basi tutafanya hivyo.

Pia amezungumzia mafunzo yaboreshwe, hilo tumelizingatia. Kwa kushirikiana na vyombo vingine tudhibiti ujambazi, ni suala ambalo tunalifanya sasa hivi, tunashirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Usalama wa Taifa na operesheni hizi mbalimbali tunazifanya kwa pamoja.

Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, amezungumzia kupandishwa vyeo kwa upendeleo. Suala hili lipo, *IGP* analifanyia kazi na tutakapounda Kamisheni ya Polisi, suala hili tutalizingatia kwa kikamilifu. Pia, ameulizia ni wangapi wamepandishwa vyeo. Kwa sasa hivi hatuna takwimu, lakini tutamwandikia ni watu wangapi katika vyeo mbalimbali wameweza kufaidika na kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Anna M. Komu, amezungumzia kila raia ahusishwe kulinda usalama. Hiyo ndiyo maana ya polisi jamii, ni suala ambalo tumeanza kulifanya kazi. Kwa upande wa Dar es Salaam na kwa upande wa Mbeya nimekwenda. Majuzu nilikuwa Zanzibar, pamoja na *IGP*, kuzungumzia *concept* hii na tutaendelea na suala hili na pia kuliweka katika mafunzo pale CCP Moshi na katika vyuo vyetu vingine vya Zanzibar, pamoja na *Police College* vya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Halima O. Kimbau, anasema wananchi wanatoa taarifa za uongo na kusababisha usumbufu kwa jeshi na raia wengine. Hii ni kweli, pale mwanzoni tulipoanza na utaratibu huu, ambapo *IGP* na Makamanda walitoa hadharani simu zao, kulikuwa na matatizo, lakini sasa hivi utaratibu huo umekuwa wa manufaa makubwa sana kwa polisi.

Karibu asilimia 80 hadi 90 ya matukio ambayo Polisi wanajulishwa na raia wema, tukienda pale *on time*, tunakuta ni kweli. Hivyo hivyo, yaliyotokea Zanzibar yamekuwa ni sahihi. Kwa hiyo, nasema tulikuwa na matatizo pale mwanzoni, lakini sasa hivi tumeweza kuyakabili matatizo hayo vizuri.

Mheshimiwa Yono S. Kevela, anaulizia kuhusu vituo na ofisi katika Kituo cha Njombe Magharibi. Tunasema katika mwaka ujao tutaangalia.

Mheshimiwa Charles N. Keenja amezungumzia makazi kutokuwa mazuri. Tunasema hili suala tunalifahamu na tunaendelea kulifanya kazi. Amezungumzia ajali barabarani na leseni zikaguliwe, madreva walevi wadhibitiwe, magari mabovu yadhibitiwe, taa za kuongoza magari barabarani zidhibitiwe. Hili suala nimezungumzia katika hotuba yangu kwamba, sasa hivi tunatazama Sheria ya *Traffic*. Kwa hiyo, tusubiri mpaka wakati huo tutakapokuja na mapendekezo sahihi.

Mheshimiwa Lucas L. Selelili, amezungumzia kuhusu vitendea kazi na anataka magari sita kwa Wilaya yake ya Nzega. Nasema kwa bahati mbaya, kwa wakati huu hatuna uwezo huo, lakini suala hilo tutalitazama katika bajeti ya mwaka kesho.

Suala la vituo na ofisi, nalo hili nasema tutaendelea kulifanya kazi, hasa katika huu utaratibu ambapo tunazungumza na vyombo vyetu vya fedha nchini na *contractors* kutoka nje, tuone kama tunaweza kujenga ofisi hizo na makambi huko mikoani.

Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, amezungumzia kuhusu vitendea kazi. Hilo ni suala ambalo linaeleweka, nimekwisha zungumzia. Pia, amezungumzia upungufu wa askari kwamba ni wachache Utogi. Tuna tatizo la uhaba wa askari, lakini *IGP* ameshaanza mpango ambao utahakikisha kwamba, tunaongeza idadi ya askari kutoka 2,000 kufikia 4,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, nadhani baada ya muda si mrefu, tutakuwa tuna askari wa kutosha. Pia, amezungumzia kuhusu makazi na kwamba nyumba zijengwe. Nadhani hilo nimekwishalijbu.

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, amezungumzia kuhusu vituo na ofisi na kwamba Kituo cha Kibaigwa kifunguliwe. Kikiwa tayari tutakwenda sote kukifungua kituo hicho. Pia, amezungumzia suala la rushwa upande wa *traffic*, ni kweli kumekuwa na matatizo hayo na ndiyo maana *IGP*, ameanza kuwazungusha zungusha *Regional Traffic Officers*, pamoja na askari wa usalama barabarani. Natumaini baada ya muda si mrefu, suala hili tutakuwa tumelikabili, lakini pia ni kuweka katika mtaala pale kwenye chuo chetu cha Polisi Moshi kwamba, kila askari sasa itabidi ajifundishe utrafiki. Kwa hiyo, wakati wowote unaweza ukawabadilisha.

Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, amezungumzia vituo na ofisi kwamba, ofisi ya *OCD* Utete Rufiji imezeeka ijengwe. Naomba tuzungumze na Mheshimiwa katika bajeti yetu ya mwaka ujao, sasa hivi hatutaweza. Pia, amezungumzia kuhusu makazi, majibu ni hayo hayo. Uhalifu wa magendo udhibitiwe, tumeanza kuyashughulikia haya mambo kwa kushirikiana na *PCB*, Usalama wa Taifa, pamoja na Jeshi la Wananchi, ikiwa ni pamoja na JKT.

Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, naye amezungumzia kuhusu vituo na ofisi na ameomba Kituo cha Lushoto kianze 2006/2007. Katika bajeti ya mwaka huu, tumetenga shilingi bilioni tatu, tutaona uwezekano wa kujenga hicho kituo katika Jimbo la Mheshimiwa Mshangama.

Mheshimiwa Eustace O. Katagira, amezungumzia kuhusu makazi bora na ya kisasa. Majibu ni kama hayo hayo, ambayo nimeyazungumzia. Maslahi, madeni, nayo pia nimekwisha yazungumzia. Bajeti yetu ya mwaka huu wa 2006/2007 imeongezeka kwa asilimia 48.7 ikilinganishwa na mwaka 2005/2006, kwa hiyo, masuala ya posho na mishahara kwa upande wa askari wetu hali haitakuwa mbaya, itakuwa ni nzuri.

Pia, amezungumzia vitendea kazi, magari, pipipiki, simu katika vituo vidogo vya Murogo, Kaisho na Lubewa. Nasema haya kwa mwaka huu wa fedha 2006/2007,

itakuwa ni vigumu, lakini kwa mwaka kesho na kuendelea, suala hili litazungumzika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mkiwa A. Kiwanga, amezungumzia maslahi yaboreshw. Sasa hivi tunasema kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuna Tume ambayo imeundwa. Nadhani baada ya muda si mrefu, hali ya mishahara na posho kwa upande wa askari itakuwa imeboreshwa.

Amezungumzia pia kuhusu vitendea kazi kwamba, idadi ya boti za kasi iongezwe, tutalizingatia suala hilo. Kwa mwaka huu, hatukutenga pesa za kutosha, tumetenga kama shilingi bilioni 1.4 ili kufanya marekebisho na matengenezo ya boti katika Ziwa Nyasa, Tanganyika, pamoja na Victoria. Kuhusu uhamisho wa askari kwamba, wasikae kituo kimoja kwa muda mrefu, hilo tumelizingatia.

Mheshimiwa Michael L. Laizer, amezungumzia kuhusu Kituo cha Longido. Tunaona umuhimu wa kuwa na kituo hicho katika Jimbo lake. Pamoja na kwamba hatukupanga, lakini baada ya mazungumzo yetu pamoja na *IGP*, nadhani tunaweza kutafuta njia ya kuweza kujenga kituo hicho katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Abdallah Vuai Khamis, amezungumzia juu ya ajira za askari, nimekwisha lizungumzia. Pia, amezungumzia vitendea kazi kwamba, ni vichache, nalo hilo nimekwisha lizungumzia.

Limezungumziwa suala la vitendea kazi hasa upande wa magari. Tuna upungufu wa fedha na mahitaji yetu ni makubwa, lakini tutaona mwaka kesho tunaweza tukafanya nini kuweza kuboresha hali hiyo.

Vile vile, suala la kuongeza boti katika *Lake Nyasa*. Sasa hivi pale zipo boti mbili na majuzi nilikuwa Itungi kule Kyela na Mheshimiwa *IGP*. Kinachohitajika hapa ni shilingi milioni 100 ili kuweka *propeller*. Kwa hiyo, baada ya muda si mrefu hizo boti mbili zitakuwa ziko majini zinafanya kazi.

Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, amezungumzia kuhusu mafao tofauti, *gratuity* na suala la pensheni, nimekwisha zungumzia. Kuhusu upungufu wa askari, hilo tunalifahamu. askari ni wachache, lakini jitihada ndiyo hizo kama nilivyoeleza. Amezungumzia kuhusu vitendea kazi, hilo pia nimekwisha lizungumzia, maelezo yake ni hayo hayo. Masuala ya kuwa na *bullet proof vests*, tunatazama.

Mwaka huu hatukuweza kubajeti kwa sababu *vest* moja ni shilingi milioni moja na kitu. Kwa hiyo, ukichukua idadi ya askari tulionao au vikosi ambavyo vinafanya kazi hiyo, inataka uwe na bajeti ya kutosha. Lakini nataka kuwahakikishieni kwamba, hili suala ni muhimu, bajeti ya mwaka kesho itabidi suala hili tulitazame kwa makini.

Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, amezungumzia suala la polisi kujishughulisha na siasa. Katika hotuba yangu nimelizungumzia suala hilo, polisi wanatakiwa wafanye kazi zao *professionally*, wasiwe na mwegamo wa mahali popote

pale. Nadhani tutaendelea kuelimishana juu ya suala hili, tulikuwa kwenye Mfumo wa Chama Kimoja sasa tuko kwenye Mfumo wa Vyama Vingi na tunaendelea vizuri. Kwa hiyo na wao ni lazima tuwape mafunzo ili waweze kufanya kazi zao bila mwegamo wowote.

Kuhusu ubambikaji wa kesi, hili ni suala ambalo tunalo katika sehemu nyingi hasa sehemu za Mara na Shinyanga. Ni kweli, Maofisa wetu wanajihuisha na masuala haya wakati mwingine, lakini *IGP* anafahamu na sisi sote tunalifanyia kazi. Tunaomba tupate taarifa ya askari, ambao mnadhania katika majimbo yetu wanajishughulisha ama wanafanya vitendo hivyo viovu, kwa sababu haya ni makosa ya kijinai.

Mheshimiwa Charles M. Kajege, amezungumzia suala la kubambikiza kesi na kwamba, askari wanashirikiana na watuhumiwa. Majibu ndiyo kama hayo, ni kweli sifichi, kumekuwa na mitandao ndani ya jeshi wakati mwingine, baina ya jeshi, Maofisa wa Jeshi, Askari wa Jeshi na wahalifu.

Kwa hiyo, tumekuwa tunafanya *manpower auditing* katika eneo hilo kuona ni akina nani ambao wanajihuisha na masuala hayo. Kwa hiyo, wale ambao watabainika, sheria itachukua mkondo wake na watashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, ametoa pongezi tu. Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, amezungumzia kuhusu mafao tofauti ya *pension* na *gratuity*. Hilo nimekwisha lizungumzia na Naibu Waziri amelizingumzia. Askari Polisi wanapuza wajibu wao, hilo tunalifanyia kazi, tunalifahamu. Upungufu wa vitendea kazi hilo pia tunalifahamu na tunalifanyia kazi na tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, amezungumzia kuhusu kuangalia upya suala la Sungusungu, kwa kutoa elimu na mipaka ya kazi. Hili litakuja tutakapoandaa *Police Act*. Ni suala ambalo itabidi tulitazame vizuri, kuhusu majukumu ya Polisi ni vitu gani na majukumu ya hawa Askari wa Jadi ni vitu gani. Kwa hiyo, nawaombeni kwa hilo, tuvute subira mpaka wakati huo.

Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, amezungumzia kuhusu Chuo cha Polisi Muheza, wimbi la ujambazi na mauaji Muheza katika siku za karibuni. Nasema hayo ni mapungufu yaliyopo na tutayafanyia kazi. Kuhusu maombi ya gari kwa Kituo cha Amani Muheza, kama nilivyozungumza, mwaka huu tutapata magari 70, kuna upungufu wa magari 933.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira pengine kwa bajeti ya mwaka kesho tunaweza tukafikiria suala hilo. Kuhusu nyumba za askari Muheza, matatizo yetu ni ufinyu wa pesa, lakini kwa *program* za *NSSF*, *NPF* na Mashirika mengine ya kifedha ya ndani na nje katika ujenzi wa kambi hizo, basi kwa wakati muafaka, tunaweza tukalizungumzia suala hilo na kuona kambi hizo zinajengwa.

Mheshimiwa Lucy F. Owenya, amezungumzia kuhusu uwiano kati ya wanaume na wanawake katika nafasi za uongozi. Tutafanya uchambuzi, lakini *IGP* Mwema ni mtu

mwema, nadhani na mimi ni mtu mwema, katika uteuzi wa *RPCs* hivi majuzi ilikuwa ni kazi kweli kutafuta *RPCs* akinamama, ambao wana *qualifications* za kufanya hivyo.

Kwa hiyo, tumekuwa tukiketi kila wakati kuangalia kwamba, nao askari akinamama wanapewa nafasi hiyo. Lakini wakati mwingine napo inakuwa ni mgogoro. Mama Lucy Kibaki, alipokuja pamoja na Mheshimiwa Rais Kibaki, kwa kawaida akinamama ndiyo wanafungua mlango wa Waheshimiwa, lakini Mama Kibaki alisema: “Hapana, nataka mwanaume.” (*Kicheko*)

Mheshimiwa Paul P. Kimiti, amezungumzia ongezeko la idadi ya makachero, jitihada zinafanywa. Amezungumzia pia kuongeza idadi ya wanawake, hoja hiyo tumeizingatia. Majambazi wapigwe picha, hili linafanyika, ikiwa ni pamoja na kuwatafuta wale askari ambao mpaka sasa hivi hatukuweza kuwapata, waliohusika na matukio yale ambayo yalibainishwa na Jaji Kipenka Mussa.

Mheshimiwa Ali Said Salim amezungumzia juu ya kubambikiza kesi, hili nimekwisha lizungumzia. Kuhusu askari kupiga watuhumiwa, atupe tu majina ya watu au askari ambao wamekuwa wakifanya matendo haya na tuweze kuwashughulikia.

Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, ameulizia askari wangapi wamepewa zawadi kutoka Serikalini, tutangaze zawadi hizo. Makao Makuu na kila *RPC* anatoa zawadi, lakini majina ya wananchi huwa hatuyatangazi kwa ajili ya usalama wao. Amezungumzia pia kuhusu matumizi ya simu za mkononi katika kurahisisha ujambazi. Suala hili tunalifanyia kazi, kwa kuzungumza na mamlaka husika kama nilivyozungumza katika hotuba yangu.

Mwisho, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, ametoa pongezi na kusema kwamba, askari wanashirikiana na majambazi. Nasema haya masuala tunayafuutilia kwa karibu sana na kuhakikisha kwamba, mambo haya tunayakomesha katika Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Spika, nasema hoja zimekuwa ni nyingi, imebidi nizipitie kwa haraka haraka, naomba radhi kwa wale ambao sikuweza kujibu hoja zao, watutaarifu na sisi tutafanyia kazi. Lakini la pili, sikuweza kujibu hoja zote hizi kwa ufasaha na kwa kina. Nasema tutaawaandikia Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja wetu kwa maandishi ili muweze kupata majibu ambayo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kabla ya yote na kabla hata sijawahoji, leo ni siku ya 30. Kikao chetu hiki ni cha 30 tangu tumeanza mkutano huu.

Katika hotuba zote zilizotolewa, Waheshimiwa Mawaziri, wamekuwa wakisema watayajibu yote kwa maandishi. Napenda kusema kuwa, mpaka leo hakuna hata mmoja aliyefanya hivyo. Kwa hiyo, tafsiri yangu ni kwamba, wana maana watakuwa wamejibu kufikia Mkutano ujao wa Tano. Kama halina mwisho, basi ahadi hiyo haina maana! Ndiyo, kwa sababu lini sasa zitajibowi?

Kwa hiyo, nasema sasa kwamba, ninavyoamini mimi Waheshimiwa Mawaziri, kwa zile hoja watakazojibu kwa maandishi, maana yake tutazipata kabla ya Mkutano wa Tano. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyoko mbele yetu itaamuliwa baada ya Kamati ya Matumizi, lakini ili tuingie hatua hiyo, kwa Kanuni za Bunge inabidi niwahoji kufikia hatua hiyo.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

### **KAMATI YA MATUMIZI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

##### **Fungu 28 - Wizara ya Usalama wa Raia**

Kif. 1001 – *Administration and General* .... .... Sh. 2,741,497,100/=

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mambo marefu wala mazito, namtoa wasiwasi Mheshimiwa Waziri na ninamtoa wasiwasi kwa sababu leo ni siku yake ya kwanza ya kuanza umri wa miaka 68. Najua jana ilikuwa *birthday* yake. Kwa hiyo, nina masuala mawili, matatu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yote aliyoyatoa hapa, isipokuwa nilipochangia wakati wa Hotuba ya Waziri Mkuu nilizungumzia wale askari wachache, ambao wanatukanisha Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 28, program 10, subvote 1001*, kifungu kidogo 250100, mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Nilitoa maeleo ili kujaribu angalau Jeshi letu liweze kuwa ni Jeshi kama lilivyokuwa miaka 40 iliyopita. Naamini kweli kama maeleo yake aliyosema, *IGP* Mwema ni mtu mzuri na mtu mwema na vile vile sisi Waislam tunasisitizwa kwamba, tunapooa tuoe wake wazuri, tuzae watoto wazuri, tuwape majina mazuri, kama alivyokuwa Saidi Mwema na ndiyo maana kawa mwema.

Sasa, baadhi ya hawa askari wawili au watatu wanaolidhalilisha Jeshi na jinsi lilivyokuwa safi, safu iliyopangwa ni nzuri sana wanafanya kazi vilivyo. Ninaomba utaratibu wa miaka 40 iliyopita, inapotoka ajira ndani ya Jeshi letu, jamani wale Viongozi Wakuu wa Serikali zetu, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wanasiisa, tuwaachie Wakulima na Wafanyakazi. Tatizo la wale vijana wengine wameshashindwa makwao, wanapenya penya kuajiriwa, matokeo yake ndiyo utakuta mambo kama yale yanajitokeza kwa kujiingiza katika ujambazi, wizi wa *exhibit* vituoni, kuacha malindo, kuiba silaha na kutokuwa waangalifu kwa dhamana zao za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, akubaliane na ushauri wangu kwamba, waendelee na hayo.

La pili, nilipochangia kwa maandishi ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Haroub Said Masoud.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Naam!

**SPIKA:** Keti chini. Wakati huu ni wa kutafuta ufanuzi au maelezo kwa Waziri, siyo kutoa ushauri. Kwa hiyo, la kwanza halina maana, umechukua muda bure na una dakika labda zimebaki mbili tu.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazitumia hizo mbili. Nashukuru sana. La pili, nataka ufanuzi. Nilipochangia kwa maandishi nilizungumzia suala la nyumba za askari UNGUJA Ukuu. Hakuna nyumba hata moja, askari wanakaa masafa marefu na niliomba katika fungu kwa sababu ya nyumba za Tunguu. Nashukuru kwamba, Mheshimiwa Waziri, amekubaliana nami na amesema zitajengwa. Kwa hiyo, kwa sababu waungwana wakiombana mambo mema wanapeana na mimi namwomba jambo jema ili anikubalie ujenzi wa nyumba za askari UNGUJA Ukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ukipenda kusema useme, lakini naona mwenzetu amewahisha shughuli zilizoko kwenye Kitabu cha Nne. Nyumba za askari ziko kwenye Kitabu cha Nne, lakini kama una maelezo pengine ya ziada labda.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Kwanza, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwa pongezi zake kwamba, naanza miaka 68, nataka nimhakikishie tu bado niko *active* na wala situmii vikolombwezo. La pili, kuhusu ujenzi kama ulivyo sema, limo ndani ya bajeti. Nilitaka kuthibitisha hilo. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, *vote 28 program 10, subvote 1001 na subvote ndogo 250100, mshahara wa rafiki yangu*. Kwanza kabisa, nataka kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Waziri kwamba, sitamsulubu kwa njia yoyote ile, kwa sababu ni kaka yangu, mtu mzuri. Lakini nazungumzia juu ya Jeshi la Polisi, katika kuchangia kwangu nimeeleza wazi kabisa, kitu kitakacholeta kukosekana kwa amani katika Taifa hili ni askari au polisi kujichanganya na siasa.

Nimetoa ombi kwamba, kuna matendo mengi sana ambayo yamefanywa na polisi Bariadi, badala ya kutengeneza maneno mengi nimewomba Mheshimiwa Waziri, apeleke Tume ikafanye uchunguzi wa hayo mambo ambayo yamefanyika. Hatuwezi kuendelea ambapo Bariadi inakuwa ni mahali pa kuzalisha mahabusu na zaidi ambao wanatokana na Chama cha UDP. Hivi si vizuri na siyo sura nzuri ya Taifa hili. Kwa hiyo, nataka angalau kwa hilo, mengi sitaki kusema kwa sababu nimesema sitaki kumsulubu hata kidogo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is not Parliamentarian, he can not tell me to sit down.*

**MWENYEKITI:** *I agree with you.* Jamani kama mwenzetu anaongea, hata kama hatukubaliani na mawazo, lakini Spika anamlinda mpaka amalize dakika zake. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwa hiyo, naomba kwa unyenyekevu anijibu kama anakubaliana atapeleka watu kuangalia mambo yanayofanyika kule, mimi nitatosheka na nitakaa chini bila maswali zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, polisi kujiingiza katika siasa na kwa lugha aliyoitoa ni kwamba, wanawapa shida watu fulani fulani kule Bariadi.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu hoja ya Mheshimiwa John M. Cheyo, kama ifuatavyo: Inawezekana kwamba tatizo likawepo, kubwa ninalolijua sehemu za Bariadi ni masuala ya ujambazi, fujo ziko pale, lakini hili suala kwamba askari wetu, wanajihusisha ama kujiingiza katika masuala ya siasa, nasema tumelipokea. Kwa kuwa sisi ni watuhumiwa, basi kama kuna kupeleka Tume yoyote ile, basi iwe ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, waweze kulichunguza suala hilo na kutoa ushauri unaopasa. (*Makofi*)

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakwenda kwenye *vote* ya 28, *program* ya 10, *subvote* 1001, kifungu 250100 mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu leo, nimetoa takwimu mbalimbali ambazo baada ya kuzifanya uchunguzi wa kina katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, na kuona upotevu wa fedha nyingi katika Wizara hii, ambazo zingetumika katika mambo mengi tu ya kuinua hali ya askari wetu amba wako katika hali mbaya sana. Mheshimiwa Waziri namshukuru kajitahidi kwa kutoa maelezo ya kina kwa kiasi fulani na ukweli wenyewe mimi nilipokuwepo hapa Bungeni asubuhi, sikupata kuipitia hotuba yake vizuri, wala kusikiliza vizuri, kwa sababu na mimi nilikuwa na jukumu leo. Lakini nilipofika nyumbani, nilikipitia kitabu chake mara tatu, ni hotuba ambayo tukubaliane, iliyojenga matumaini mapya na makubwa kwa Jeshi la Polisi. Hicho kitu nakikubali, isipokuwa sasa, kwa mujibu wa taarifa yako kwamba, tupate majibu haya yote vizuri kwa maandishi zikiwemo hizi takwimu za upotevu wa mabilioni ya shillingi katika Jeshi la Polisi. Mimi ningeomba niwe mtu wa mwanzo kupewa taarifa hii na kupewa namna gani fedha hizi zilipotea au namna gani hazimo katika vitabu. (*Makofi*)

La pili, katika hotuba yangu nilizungumzia suala nyeti ambalo halikugusiwa, usalama wa Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, tena ni usalama wa kiwanja ambacho tumekipa jina la Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Lazima tuheshimu utendaji wote wa Jeshi la Polisi uliopo katika kiwanja kile. Kuna taarifa na tunazo baadhi ya taarifa hizo hata sisi kwamba, kuna baadhi ya askari, ambao vitendo vyao vinakwenda kinyume na taratibu za Jeshi la Polisi, katika uwanja wa ndege na kuingilia hata kazi za watu wengine wanaofanya *immigration* na *customs*. Tukubali kwamba, lile ni eneo nyeti, lidhibitiwe vizuri na kama kuna upungufu wa askari au askari wenye tabia mbovu,

atuelezee mara moja Mheshimiwa Waziri, atafanya nini na hatua gani atazichukua kupitia watendaji wake? (*Makofii*)

La tatu, ninalotaka kulieleza na lilikuwemo ndani ya hotuba ni wafanyabiashara kutokuingiza mikono yao ya kuwapa misaada Jeshi la Polisi. Hivi ni vyombo vyaa sheria, ama tupate misaada baina ya nchi na nchi au hata masharika makubwa ya nje, lakini tusikaribishe mikono ya wafanyabiashara, ambao wanaingiza katika Jeshi lolote la nchi yetu ya Tanzania, kwani litakaribisha mianya ya rushwa na vitendo vingine vinavyokwenda kinyume na sheria. (*Makofii*)

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru ndugu yangu, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, kwa pongezi ambazo amezitoa kwamba, kwa kiwango kikubwa hotuba yetu imeweza kukidhi matakwa yake, namshukuru sana kwa hilo.

Suala la pili, ni hizi takwimu na sisi tumezipata leo na tumejaribu kupiga simu kila mahali na majibu ambayo tumeweza kuyapata ni hayo. Kwa ujumla tunasema kwamba, hakuna pesa zozote ambazo zimepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uthibitisho zaidi na kwa maelezo fasaha zaidi, aniruhusu kupitia kwako, niweze kumwandikia na kufafanua nini kimetokea katika maeneo yote hayo. (*Makofii*)

Suala la tatu kuhusu misaada, ambayo tunaipokea, mimi ndiye mlezi, sasa kama Waheshimiwa Wabunge, hamniamini kuwa mlezi kupokea misaada kama ile, basi sifai kuwa hata katika Wizara ile. Siyo kila mtu ambaye anapokea misaada hiyo na *IGP* inabidi achuje huyu mtu ambaye anatusaidia ni wa namna gain, anakubalika katika Taifa letu, anaheshimika katika Taifa letu, tumekuwa tukifanya hivyo.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, mturuhusu tuendelee na shughuli mpaka tutakapoona kwamba, kuna matatizo. Lakini mwitikio umekuwa ni mzuri, siyo tu wafanyabiashara wakubwa hata wadogo wadogo. Maana nilipokwenda Mbeya, watu walipita kama wako kanisani, huyu anatoa shilingi na kadhalika. Hii ni kujaribu kuhamasisha wananchi na makampuni, ile *sense of ownership* ya ulinzi iweze kujengeka. (*Makofii*)

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwanja wa ndege halikujibiwa.

**SPIKA:** Kuhusu uwanja wa ndege, askari polisi kuchukua nafasi ya *customers* na wengine.

**WAZIRI WA USALAMA WA URAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelipokea. Limenifikia mimi kwa mara ya kwanza, mniwie radhi kwamba, sikuweza kulijibu lakini tutalifanya kazi na tutamjulisha. (*Makofii*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* .... .... .... .... Sh. 379,950,000/=  
Kif. 1003 - *Policy and Planning* .... .... .... .... Sh. 431, 069,900/=  
Kif. 1005 - *Information, Education and Communication* .... .... .... Sh. 220,947,200/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Policy Mainforce* .... .... .... .... Sh. 96,660,438,200/=

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana *vote 28, program 20, subvote 2001, item 261100 - other goods and services not classified above.* Naipongeza sana Serikali kwa kujenga makazi ya polisi pale Magu mwaka 1976. Ni miaka 30 sasa na nawapongeza sana askari wa Magu, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Katika mchango wangu wa maandishi, nilisema kwamba, askari pale Magu hawajapata umeme na umeme uko nyumba ya jirani. Mwaka 2003 tuliandika makisio kwa kusaidiana na *TANESCO*, gharama yake ilikuwa shilingi 1,421,700,000.

Askari wanasiskitika sana kwamba, wanafanya kazi nzuri ya kulinda wananchi na mali zao, lakini wakirudi majumbani kwao jioni wanalala gizani. Anaweza Mheshimiwa Waziri, kuchota hela za *item* hizi shilingi 2,827,000,000 akachoka walau milioni mbili wakawekewa askari wa Magu umeme? Naomba Mheshimiwa Waziri, aseme watawekewa umeme lini askari hawa askari wa Magu, ambao wanafanya kazi nzuri katika makazi yao?

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii au hoja ya Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, nadhani ye ye ana uzoefu alikuwa ni Naibu Waziri wa Fedha, jinsi ya kuchota, tutatumia uzoefu huo kama kutakuwa na uwezekano tutachota tuweze kupeleka umeme pale. (*Makofii*)

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kwa sababu kina *other goods and services not classified*, ndiyo maana nimesema kwamba, uwezekano wa Waziri wa kuchota upo mkubwa, ukizingatia kwamba nyumba hizi zimejengwa miaka 30 iliyopita na askari wanahangaika. Kwa hiyo, haya maombi tuliyoyaleta mwaka 2003, tukapeleka kwa *RPC* na yakaenda Makao Makuu ya Polisi, niliamini kwamba, kama hayakuwekwa kwenye bajeti ya miaka iliyopita, basi angalau mwaka huu yangekuwepo. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Kwa hakika tutashangaa sana, kama inashindikana kutoka fungu kubwa kama hili kupata shilingi 1,400,000,000 ya kuweka umeme kwa polisi Magu!

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2002 - <i>Police Marine</i> . . . . .	Sh. 2,435,560,500/=
Kif. 2003 - <i>Railway Police Division</i> . . . . .	Sh. 271,326,100/=
Kif. 2004 - <i>Police Signals Branch</i> . . . . .	Sh. 5,344,164,600/=
Kif. 2005 - <i>Police Zanzibar</i> . . . . .	Sh. 6,579,798,600/=
Kif. 2006 - <i>Police Airwing</i> . . . . .	Sh. 1,255,735,700/=
Kif. 2007 - <i>TAZARA Police</i> . . . . .	Sh. 302,727,600/=
Kif. 2008 - <i>Field Force Unit</i> . . . . .	Sh. 2,593,014,800/=
Kif. 2009 - <i>Traffic Police</i> . . . . .	Sh. 1,025,848,300/=
Kif. 2010 - <i>Police Airport</i> . . . . .	Sh. 254,311,300/=
Kif. 2011 - <i>Police Dog and Horses</i> . . . . .	Sh. 610,764,500/=
Kif. 3001 - <i>Police College Moshi</i> . . . . .	Sh. 2,937,904,500/=
Kif. 3002 - <i>Police College</i> . . . . .	Sh. 900,212,300/=
Kif. 4001 - <i>Police Vehicle Maintenance</i> . . . . .	Sh. 203,908,800/=
Kif. 5001 - <i>Police Medical Unit</i> . . . . .	Sh. 1,077,222,800/=
Kif. 6001 - <i>Police Building Brigade</i> . . . . .	Sh. 1,651,871,200/=
Kif. 7001 - <i>Criminal Investigation Division</i> . . . . .	Sh. 7,319,613,100/=
Kif. 7002 - <i>Stock Theft Prevention Unit</i> . . . . .	Sh. 357,804,400/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu – 28 – Wizara ya Usalama wa Raia**

Kif. 2001- *Police Main force* . . . . . Sh. 7,153,256,300/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru vote 28, su vote 2001, kifungu kidogo 6302 - *construction of offices and quarters*. Kwa vile kipaumbele cha maendeleo katika nchi yetu kwa sasa tumekuwa tukisema iwe ni maeneo yapembezoni mwa nchi, Wilaya na Mikoa iliyo pembezoni au maeneo ambayo kwa muda mrefu pengine hayakupata maendeleo au yamekuwa nyuma kimaendeleo.

Wilaya ya Ludewa ni mojawapo ya maeneo hayo na Kituo cha Polisi cha Ludewa, pale Mjini kiko katika jengo la kukodisha au kupangisha, ni la zamani na lina hali duni sana, linatia aibu pale Wilayani wakija wageni. Haliridhishi kuwa kituo cha polisi kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Kwa kuwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na alipokuwa anatoa maelekezo na majibu ameonesha kwamba, kituo kile bado hakitajengwa ingawa Halmashauri ilitenga Kiwanja, kipo na kinaendelea kuota majani.

Kwa vile mwaka huu hamna fedha tena licha ya kwamba, tumepeleka bajeti kila mwaka ni shilingi za Tanzania milioni 260 tu, ikiwa ni pamoja na nyumba ya *OC*. Sasa ninachoomba kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa wananchi wa Ludewa wanansikiliza na mimi mwenyewe jiridhishe nafsi yangu, anaweza akaahidi ili iwe *documented* kwamba, Wilaya hii kwa mwaka kesho itapewa kipaumbele kuhakikisha kwamba, Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Ludewa inajengwa? Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Mbunge, huo siyo ufanuzi sasa, unadai ahadi kituo hicho kijengwe mwaka kesho, sasa hiyo ni kinyume na kanuni. Unalo lolote la kutaka maelezo au ufanuzi?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kwamba, maeneo haya yaliyo nyuma na yako mpakani, Wilaya ya Ludewa iko mpakani yanahitaji kuhakikisha kwamba, vituo vyta polisi ni imara. Sasa ufanuzi ni kwamba, kwa nini Wilaya hii haikupewa kipaumbele katika mwaka huu kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Polisi yanajengwa, kama haiwezekani; je, kituo hiki kitajengwa lini? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa umeliwekwa vizuri.

**WAZIRI WA USALAMA WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Profesa Raphael B. Mwalyosi, kama ifuatavyo:-

Kimsingi nakubaliana naye kwa sababu kwa kweli vituo ambavyo viko mpakani, lazima tuvipe kipaumbele. Kwa hiyo, katika kukadiria matumizi ya mwaka kesho kwa upande wa miradi ya maendeleo, tutalifikiria kwa umakini suala hili.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Sub vote* 2001, kifungu kidogo 6107, ambacho kinahusika na ununuzi wa *technical equipments* na kifungu kidogo 6302 - *construction of offices and quarters*. Nilikuwa naomba ufanuzi kama fedha hizi ni pamoja na ujenzi wa ofisi za Kituo cha Polisi cha Kibara, yaani ujenzi wa ofisi na *quarters* za askari, pamoja na ununuzi wa vifaa vyta mawasiliano?

Kwa sababu katika maelezo yangu ya mwanzo niliyowasilisha niliomba maelezo lakini kwa bahati mbaya naona Mheshimiwa Waziri hakuweza kunijibu.

**MWENYEKITI:** Mji gani huo ulioutaja Mwenyekiti hakusikia?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Kituo cha Polisi Kibara kiko katika Mkoa wa Mara.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kuna Kibara na Mwibara?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Kibara ni Makao Makuu ya Mwibara.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Charles M. Kagege, kama ifuatavyo:-

Kwa bahati mbaya katika *estimates* zetu za mwaka huu, hatukupanga kujenga kituo katika jimbo lake katika eneo hilo. Kwa hiyo, naomba tukutane, tuzungumze, tuone ni vipi tunaweza tukasaidiana kwa suala hilo, ni suala ambalo linazungumzika. Vituo vyote hivi ambavyo nimevitaja, vinahitaji lakini kwanza kabisa, ni vituo vyetu ambavyo viko mipakani.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia *vote* 28, *subvote* 2001, *item* 6301, 6302 na 6303. Napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Je, pesa hizi zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea askari zile nyumba za mabati au wana-rehabilitate nyumba zipi kwa sababu askari wengi wanakaa kwenye nyumba za mabati?

Halafu tukija kwenye *item* 3302, naomba niulize, je, fedha hizi zimetengwa pia kushughulikia kujenga nyumba Polisi Kibaha, kwa sababu Kibaha miaka yote imefadhiliwa na Shirika la Elimu Kibaha; je, fedha hizi zimetengwa pia kuwatafutia maeneo yao kama polisi, shirika likibinafsishwa polisi watafanya nini?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri sijui kama umeelewa, shirika likataifishwa, unaweza kuwasaidia kidogo, wasaidieni Waheshimiwa Mawaziri, waweze kujibu hoja zenu.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA**: Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha, limewafadhili polisi, kwa hiyo, nyumba wanazokaa, ofisi wanazokaa wameazimwa na Shirika la Elimu Kibaha.

Je, fedha zimetengwa ili pia kusaidia Polisi Wilaya ya Kibaha na wengine wanatokea hata Mkoa wa Pwani, wako mle mle katika nyumba hizi, kujenga maeneo yao kwa sababu ikitokea bahati mbaya Shirika la Elimu Kibaha likataifishwa mapolisi watakuwa wapi?

**MWENYEKITI**: Likataifishwa au kubinafsishwa?

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, likibinafsishwa samahani.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama kama ifuatavyo: Ni kweli nimetembelea eneo lile, siyo kama Waziri wa Usalama wa Raia, lakini na shughuli zangu mbalimbali pale. Hali yenyewe ilivyo pale si nzuri na ni kweli kwamba, *police station* iko katika mazingira ya shule ya Kibaha.

Sio kituo hiki tu, ni maeneo mengi tu, lakini ikitokea kwamba shule ile ikibinafsishwa, basi tutatafuta njia yoyote ile ya kuweza kutafuta njia mbadala. Lakini tuendelee kuwasiliana kwa pamoja, tuone vipi tunaweza tukatatua suala hilo.

Kuhusu pesa hizi kujenga tena nyumba za askari ambazo ni *full suit*, siyo suti kama niliyovaa mie, za mabati. Kwa kweli kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, hilo suala haliwezekani. Ni lazima tujenge nyumba za kisasa kwa askari wetu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema hoja iliyonismamisha, napenda kuchukua nafasi hii, kuupongeza sana uongozi mpya wa Jeshi la Polisi, chini ya *IGP Saidi Mwema*, ambao wanafanya kazi nzuri sana na nina hakika tukiwaunga mkono, kazi yao itaendelea kuwa nzuri. (*Makofî*)

Nimesimama kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama kwamba, Serikali haina mpango wa kubinafsisha Shirika la Elimu Kibaha. (*Makofî*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *vote ya 28, subvote 2001*, Vifungu vidogo 6302 na 6303. Kile cha kwanza ni *construction of office and quarters Tanzania* na cha pili ni *rehabilitation of police buildings*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi lakini pia wiki iliyopita niilizila swali la nyongeza kwamba, Kituo cha Polisi Vyawa kilichopo Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi ni mionganoni mwa vituo vichakavu sana katika nchi hii na kina zaidi ya miaka 45. Naibu Waziri alipojibu alisema kwamba, kituo hicho kipo kwenye programu ya matengenezo ya miaka kumi.

Sasa kwa sababu sikupata nafasi kusema, miaka kumi Mbozi au Vyawa itakuwa kipindi kipi, nisingeweza kwa sababu tu ya kanuni. Sasa naomba Waziri atueleze kwamba, kituo kiko kwenye programu kwa miaka kumi, lakini tuseme lini hasa ni 2007, 2010, 2013 au namna gani?

Lakini pia hata nyumba zenyewe za askari ambazo ziko takriban tano pale Makao Makuu ya Wilaya, zenyewe pia ni chakavu sana na nyingine askari wanaoishi kwenye nyumba hizo wanalamizika kutengeneza wao wenye, ukiuliza wanasema Serikali wakati mwingine inakosa hata fedha za kutengeneza au kufanya matengenezo madogo madogo ya nyumba hizi.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, atueleze na hili watalifanya lini ili kuwasaidia askari wetu wawewe kuishi katika mazingira ya kufanya kazi? Ahsante sana.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kama ifuatavyo:-

Masuala haya yote ni ya ofisi na hasa kambi za askari. Yote yanatugusa sana na daima mimi pamoja na Naibu Waziri, tukienda kuzungumza na askari, tunafanya jitihada kutembelea kambi za askari.

Hali ni mbaya, hairidhishi hata kidogo na ndiyo maana tuna mikakati hii ya kutafuta wafadhili ama watu ambao wataweza kutukopesha pesa, tuweze kujenga na wakati nateuliwa na Mheshimiwa Rais, aliniuliza namna gani Mheshimiwa Waziri, umeshakwenda Mgulani?

Nikasema sijafika. Nikasema hivi kuna nini, akasema huko lazima uende haraka, tatizo la nyumba kwa askari ni kubwa sana. Nenda ukaone hali ilivyo, nyumba kwanza ni ndogo lakini si hivyo tu, ukiingia ndani ya nyumba hiyo ndogo, unakuta kuna familia mbili zimetenganishwa na shuka. Akaniambia Waziri huoni kwamba, ni kazi hiyo, usiku inakuwaje?

Kwa hiyo, suala hili ni *very serious*, yaani mpaka kiasi Rais anajua masuala kama hayo. Kwa hiyo, yanatugusa kweli kweli, ni lazima tu-*improve working conditions* ya askari wetu ikiwa ni pamoja na vituo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira, tuone katika programu hii ya miaka mitano ijayo, tutaweza kufanya nini. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ninavyomfahamu Mheshimiwa Rais, sidhani kama alimwuliza kwamba, kwa kuwa kuna shuka usiku inakuwaje? Kwa hiyo, nadhani hili ni wazo Waziri alikuwa anawasikitikia tu askari. (*Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 5001 - *Police Medical Unit* .... .... .... .... .... Sh. 200,000,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

## T A A R I F A

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi, limepitisha Makadirio ya Wizara ya Usalama wa Raia, kifungu kwa kifungu bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako liidhinishe makisio hayo kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia*  
*kwa Mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kukumbushana tu ratiba, kesho ni zamu ya Wizara ya Katiba na Sheria, kesho kutwa siku ya Ijumaa ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, halafu tutaendelea sasa kuanzia Jumatatu tarehe 31 Julai, 2007, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, halafu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Hizo ni za siku moja moja na nyingine zitafuatia baada ya hapo.

Tuliigawa hii, lakini nilikuwa nakumbusha hizi za siku chache hizi zinazokuja ili Waheshimiwa Wabunge, muweze kuijandaa.

Kesho asubuhi nitakuwa na safari kuelekea Mkoani Arusha. Nitamwachia Kiti Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti. Lakini Mwenyezi Mungu, akipenda nitaweza kurejea saa tisa na kwa hiyo tutaweza kuwa pamoja jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kwa kuwa shughuli tulizopangwa kwa leo zimeisha, natamka kwamba, naahirisha Bunge hili kabla ya muda wake hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.10 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi*  
*Tarehe 27 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi*)